

**BUNGE LA TANZANIA**

-----

**MAJADILIANO YA BUNGE**

-----

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**Kikao cha Kumi na Saba – Tarehe 29 Aprili, 2019**

*(Bunge lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Katibu

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII):**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezeji wa majukumu ya Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**MHE. YOSEPHER F. KOMBA (K.n.y. MSEMaji MKUU WA KAMBI YA RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA):**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kuweka mezani taarifa Msemaji Mkuu wa Kambi ya Rasmi Upinzani Bungeni wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Maswali, swali la kwanza kwa siku yetu ya leo linaelekezwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI linaulizwa na Mheshimiwa Joram Ismael Hongoli Mbunge wa Lupemba.

Na. 137

**Kufuta Madeni ya Halmashauri ya Miaka ya Nyuma**

**MHE. JORAM I. HONGOLI** aliuliza:-

Madeni ya Halmashauri hususan mikopo ya vijana na wanawake ya miaka ya nyuma kabla ya mwaka 2016 yamekuwa hayalipiki kutokana na Halmashauri nyingi kutokuwa na mapato ya kutosha kuendesha Halmashauri hizo hasa miradi ya maendeleo.

Je, ni kwa nini madeni hayo yasifutwe ili kuondoa hoja za ukaguzi kwenye Halmashauri hizo?

**MWENYEKITI:** Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Waitara.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA  
NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joram Ismael Hongoli, Mbunge wa Lupembe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka za Serikali za Mitaa zimekuwa zikitoa fedha za mikopo kwa ajili ya vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu inayotokana na asilimia kumi ya mapato ya ndani ya Halmashauri kwa kuzingatia maelekezo ya Serikali. Katika kipindi chote cha utekelezaji hakukuwa na sheria kwa ajili ya kusimamia utengaji na utoaji fedha hizo na kusababisha kuwepo kwa changamoto mbalimbali ikiwemo malimbikizo ya fedha ambazo hazikutolewa kwa walengwa katika kipindi husika na kusababisha hoja za ukaguzi kutoka kwa Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutungwa kwa Sheria ya Usimamizi wa Fedha hizo, Ofisi ya Rais, TAMISEMI inakusudia kuyafuta malimbikizo hayo kama ilivyoelekezwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa kazi ya kuhakiki takwimu, kubaini kiasi ambacho kimelimbikizwa katika Halmashauri zote nchini inaendelea na Mara tu itakapokamilika, taratibu za kufuta malimbikizo hayo zitafanyika. Aidha, kwa sasa Ofisi ya Rais, TAMISEMI inazisimamia kwa karibu Halmashauri ili kuhakikisha zinatoa fedha hizo kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hongoli.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nina swali moja la nyongeza. Pamoja na

kwamba Serikali imejibu vizuri, nawapongeza sana; na uamuzi unaokuja wa kufuta madeni ni mzuri sana, nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati hizi fedha zinakopesha huko nyuma, kuna baadhi ya Halmashauri zilipeleka fedha kidogo; pamoja na kwamba hazikupeleka zote, lakini fedha hizi wale waliokopeshwa au vikundi vilikopeshwa vimekuwa vikisuasua sana katika kulipa hizi fedha. Mfano Halmashuri ya Wilaya ya Njombe kabla, tulikuwa Halmashauri moja upande wa Wanging'ombe na Makambako. Baada ya kugawanya hizi Halmashuri, zile fedha zilizokopeshwa kwenye vikundi vya Halmashauri nyingine, kwa mfano, Wanging'ombe na Makambako, imekuwa ni vigumu sana kurejesha na wamekuwa wakisuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini kauli ya Serikali kwa vile vikundi ambavyo vilikopeshwa na sasa wanasuasua kurejesha au hawarejeshi kabisa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Waitara.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nashukuru kwa pongezi ambazo ametoa na kwa hatua ambazo Serikali inachukua kufuta madeni na malimbikizo haya. Naomba nitoe maelekezo kwamba hizi fedha hazikuwa sadaka, wala zawadi. Hii ilikuwa ni mikopo; na dawa ya kukopa ni kulipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaelekeze Wakurugenzi wote nchini walipo na wale Maafisa Ustawi wa Jamii na Mikoa, Wilaya na Kata, vile vikundi ambavyo vilipewa fedha hii ya Serikali kwa ajili ya kujiendeleza na

kuboresha maisha yao, ni muhimu warejeshe fedha hizi na waweke *time frame* baada ya muda fulani fedha irejeshwe. Kwa sababu makusudi ya Serikali ilikuwa, kikundi kimoja kikikopeshwa kikaboresha maisha yake, wakirejesha na wengine zaidi wanaendelea kukopeshwa ili waweze kuyaboresha maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amina Makilagi.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2018 katika bajeti tulipisha sheria kwamba kila Halmashauri ni lazima kutenga 10% ya wanawake na vijana watu wenye ulemavu. Hivi sana ninavyozungumza zipo Halmashauri hapa nchini, ikiwemo Wilaya Butiama hawatoi mikopo kama ambavyo sheria tulivyoipitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua, nini kauli ya Serikali katika kuhakikisha Wakurugenzi wanatekeleza maagizio ya Bunge kutenga 10% ya wanawake, vijana na walemavu ili kusaidia katika vikundi na kuleta tija kwa wanawake, vijana na walemavu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Waitara.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ni kweli kwamba sheria imeshatungwa na kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi ni kwamba huko nyuma hatukuwa na sheria, sasa sheria ipo *in place* inafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwapongeze Wajumbe wa Kamati ya Wizara ya TAMISEMI, walikumbusha Wajumbe, walitoa maelekezo kwenye mikoa na Halmashuri zote nchini na wakatoa masharti kwamba kipindi kijacho,

kama kuna Halmashauri ambayo haijapeleka fedha hizo kwa mujibu wa sheria, hao watapata taabu sana katika Kamati ile wakati wanaleta bajeti yao mwaka ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelekezo ni kwamba kama umekusanya shilingi 100/=, baada ya kuondoa yale makato ya kisheria kabla ya kupeleka zile fedha kwenye makundi muhimu yaliyotajwa, ni lazima 10% ya fedha hiyo ipekewe kwenye vikundi na igawanywe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama Halmashauri ya Butiama haijapeleka fedha, najua walipokuja kwenye Kamati ya Bunge walikuwa wameweka asilimia ndogo karibu 15% au 25% ambayo wakikuwa wamepeleka, lakini tumepata manung'uniko ya hapa na pale; Mheshimiwa Mbunge najua ni mwenyeji mkaazi wa Mkoa wa Mara, naomba nitoe maelekezo tupate taarifa mahsusi kwa Halmashauri ya Butiama kama kweli hawajapata fedha hizi. Mkurugenzi, ikifika kesho saa 7.00 tupate taarifa kama amepeleka fedha kiasi gani; vikundi gani vimepelekewa? Ili tuweze kumaliza jambo hili. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Selasini.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Fedha nyingi hizi zimepotea kwa sababu ya maamuzi ya kisiasa ya kutoa hii mikopo, lakini mwarobaini tumeupata, ni hii sheria tuliyotunga hapa. Ila sasa ni lini Serikali italeta kanuni (najua zimeshaanza kuandaliwa) ambazo zitasimamia ugawaji wa hizi pesa ili kukomesha kabisa ugawaji holela wa hizi fedha na kuwabana hawa Wakurugenzi waweze kuzitoa vizuri?

**MWENYEKITI:** Ahsante jibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Waitara.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Bahati nzuri

Mheshimiwa Selasini ni Mjumbe wa Kamati ya Bunge ya TAMISEMI na Utawala na mojawapo maelekezo ambayo yalitoka kwa Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Selemani Jafo ilikuwa kanuni hizi zitolewe mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe taarifa kwamba kanuni hizi zimeshatolewa, ilitangazwa kwenye gazeti la Serikali, zinasubiri utekelezaji. Kwa hiyo, kimsingi jambo hili limeisha; na mambo yote ambayo Kamati ilielekeza na maoni ya Waheshimiwa Wabunge yamezingatiwa; namna ya kugawanywa, namna ya kusimamiwa na hatua za kinidhamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hata kama kuna vikundi vitakopeshwa fedha, wasipozingatia sheria na kanuni watawajibishwa. Hili ni jambo la kikundi husika ili fedha hii iweze kwenda vizuri kama ambavyo Bunge na Serikali ilikusudia kuboresha maisha ya Watanzania hawa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea. Swali linalofuata bado lipo Ofisi ya Rais, TAMISEMI, linaulizwa na Mheshimiwa Maria Ndilla Kangoye, Mbunge Viti Maalum.

Na. 138

## **Uhaba wa Vyumba vya Upasuaji - Vituo vya Afya Mwanza**

**MHE. MARIA N. KANGOYE** aliuliza:-

Kumekuwa na changamoto kwa baadhi ya vituo vya Afya Mkoani Mwanza kukosa vyumba vya upasuaji:-

Je, ni nini mpango wa Serikali wa kupunguza vifo vinavyotokana na uzazi kwa kucheleweshwa kufanyiwa upasuaji?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maria Ndilla Kangoye, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Mwanza una jumla vya vituo vya kutolea huduma za Afya vya Serikali 272 ikiwepo Hospitali sita, Vituo vya Afya 35 na Zahanati 231. Kwa sasa huduma ya upasuaji wa dharura kwa akina mama inatolewa kwenye Hospitali zote sita na Vituo 10 vya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kupunguza vifo vinavyotokana na uchelewashwaji wa akina mama wakati wa kujifungua kwa kutokufanyiwa upasuaji, mwaka wa fedha 2017/2018 na 2018/2019 Serikali imepeleka kiasi cha shilingi bilioni sita kwa ajili ya ujenzi na upanuzi wa Vituo vya Afya 14 Mkoani Mwanza ambavyo kwa sasa viko katika hatua ya ukamilishaji na hivyo kuna Vituo 11 vya Afya ambavyo vilikuwa havitoi huduma za upasuaji, vitaanza kutoa huduma hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile katika mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali ilipeleka kiasi cha shilingi bilioni tatu Mkoani Mwanza kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali za Wilaya za Ilemela na Buchosa ambazo zitatoa huduma ya upasuaji wa dharura kwa akina mama, hivyo kutanua wigo na kuboresha huduma za upasuaji Mkoani Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kujenga vituo vya kutolea huduma za afya na kuongeza wataalam ili kumaliza tatizo la vifo vya akina mama vinavyotokana na uchelewashaji wa huduma ya upasuaji wakati wa kujifungua.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Maria Kangoye.

**MHE. MARIA N. KANGOYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu hayo kutoka Serikalini, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza:-



Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Ilemela ilifanikisha kuanza ujenzi wa Hospitali ya Wilaya katika Kata ya Buswero na walifanikisha kukamilisha majengo ya *OPD* na vilevile jengo la magonjwa ya dharura. Hata hiyo, kutokana na changamoto zilizokuwa pale, wakaona hapafai kuwa na Hospitali ya Wilaya maeneo yale wakaanzisha ujenzi katika Kata ya Bugogwa:-

Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa majengo yale kuanza kutumika sasa kama Kituo cha Afya, kwa sababu yanakidhi haja hiyo ya kuwa kituo cha afya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, swali langu la pili nianze kwa kuishukuru Serikali kwa kutujengea Kituo cha Afya cha Malya Wilayani Kwimba. Kwa kweli ni kituo kizuri kinatoa huduma kwa wananchi wengi Wilayani humo, lakini kimekuwa na changamoto zifuatazo: hakina Mganga Mkuu na mhusika mkuu pale ni *Clinical Officer*; vile vile hakina mtaalam wa Maabara, hakina chumba cha upasuaji, hakina Daktari wa Akina Mama na Watoto; na bahati nzuri Naibu Waziri, Mheshimiwa Waitara ameshafika katika hiki kituo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, swali langu ni moja: Je, ni lini Serikali itahakikisha kwamba changamoto hizi zinapungua ili tuweze kupunguza vifo vya akina mama na watoto? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kandege.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la kwanza Mheshimiwa Maria anauliza juu ya umuhimu wa eneo ambalo lilikuwa limeshaanza kujengwa Hospitali ya Wilaya lakini ikaonekana kwamba hapafai ni bora kikajengwa kituo cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze kwa dhati. Hata pia Mheshimiwa Angelina Mabula amekuwa akiliongelea suala hili kwa muda mrefu. Ni adhima ya Serikali kuhakiksha kwamba tunaondoa *congestion* katika maeno yote. Kwa hiyo, eneo lile na majengo ambayo yameshajengwa, hakika naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, inafaa kabisa kuwa Kituo cha Afya baada ya maboresho machache ambayo yataenda kukamilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, Mheshimiwa Mbunge pamoja na kwamba amesifia tunashukuru kwa hizo pongenzi kwamba Kituo cha Afya kimeshaanza kufanya kazi nzuri, lakini kinakosa baadhi ya wataalam. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ni azma ya Serikali kwamba yale majengo kwa maana ya vituo vya afya hatujengi ikawa kama picha. Tunataka wataalam wanaohusika ili upasuaji na shughuli zote zinazotakiwa kwenye kituo cha afya ziweze kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Mbunge avute subira. Wakati mwingine kuna wataalam ambao ni lazima wawe *trained*. Kwa mfano, katika upasuaji lazima tuwe na wale watu ambao wanatoa dawa za usingizi na ndiyo maana tumewapeleka kuwa-*train*. Naamini na kituo hicho ambacho anakiongelea kitapata wataalam hao.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Halmashauri ya Mji wa Tarime, kata zote zilikuwa haina kituo cha afya bali walikuwa wanategemea Hospitali ya Mji. Tunashukuru tumepata Kituo cha Nkende ambacho kinaendelea kujengwa; lakini kuna kata nne za pembezoni ambazo zina zahanati tu, kwa maana ya Kata ya Kitale, Kata ya Kanyamanyori na Nanyandoto. Wananchi wa katia ya Kanyamanyori wameamua kuchangishana ili kuendeleza kile kituo cha afya kwa maana kujenga *maternity ward* na maabara:-

Ni lini sasa Serikali itawatia moyo wananchi wale kwa kutoa fedha kuweza kujenga kituo afya cha ili kupunguza vifo vya mama na watoto?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kandege.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepata fursa ya kutembelea Jimbo la Mheshimiwa Mbunge na nikatembelea Hospitali ya Wilaya ambayo mwanzo ilikuwa inahudumia maeneo mengi sana kiasi kwamba kukawa kuna *congestion* kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge mwenyewe anakiri na anashukuru kwamba kimeanza kujengwa kituo cha afya na imebaki hizo kata ambazo yeye amezitaja. Naomba aendelee kuiamini Serikali kwamba kama ambavyo tumeanza kujenga katika hiyo kata kwa kadri bajeti itakavyoruhusu, tumeahidi tutatekeza na katika kata nyingine kwa jinsi bajeti itakavyokuwa inaruhusu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kalanga.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika ziara ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI mwaka 2018 katika Jimbo la Monduli aliahidi kumaliza ujenzi wa Vituo vya Afya vya Nararami na Lemooti.

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake kwa wananchi wa Monduli?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kandege. Ni lini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kama ambavyo katika swali lake ameuliza kwamba Mheshimiwa Waziri wa Nchi TAMISEMI aliahidi juu ya ujenzi kumalizia vituo vya afya viwili katika Jimbo lake, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, hakuna hata siku moja ambayo Mheshimiwa Waziri wa Ofisi ya Rais TAMISEMI alishawahi kuahidi akakosa kutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuvute subira. Kwa muungwana ahadi ni deni, nami nitamkumbusha kwamba kwa Mheshimiwa Kalanga uliahidi kumalizia vituo vya afya hivyo viwili. Kwa kadri fedha itakavyopatikana, hakika naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, hivyo vituo viwili vya afya vitaweza kumaliziwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali linalofuata ambalo linaelekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Madini na linaulizwa na Mheshimiwa Edwin Mgante Sannda, Mbunge wa Kondoa Mjini.

Na. 139

### **Utafiti kuhusu Kiwango cha Madini ya Chokaa Kijiji cha Ausi**

**MHE. EDWIN M. SANNDA** aliuliza:-

Uwepo wa madini ya chokaa umedhihirika katika Kijiji cha Ausia, Kata ya Suruke, Jimbo la Kondoa Mjini, kwa muda mrefu sasa, katika jitihada za kujaribu kunufaika wananchi wamekuwa wakichimba madini haya kienyeji:-

Je, ni lini Serikali itapeleka Wataalam kufanya utafiti kubaini kiwango cha uwepo na ubora wa madini hayo ya chokaa ili wananchi wa maeneo hayo waanze kunufaika sasa na rasilimali hiyo muhimu?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Madini Mheshimiwa Stanslaus Nyongo.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Edwin Mgante Sannda, Mbunge wa Kondoa Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (*GST*) hufanya utafiti wa awali wa madini (*Regional Geological Mapping*) na kuandaa ramani kupitia *QDS* yaani *quarter degree sheet* na taarifa za kijiolojia nchini. Utafiti huo wa awali husaidia kutangaza fursa za uwepo wa madini yanayogunduliwa ili wawekezaji binafsi wa madini wa nje ya nchi waweze kuwekeza katika tafiti za kina na uchimbaji. Hadi kufikia mwaka 1999, *GST* ilifanya utafiti wa Kijiolojia katika Wilaya ya Kondoa na kutengeneza Ramani za Kijiolojia yaani hizo *QDS* zipatazo sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo ikiwemo Kampuni ya *Beak Consultants GmbH* ya Ujerumani na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kati ya mwaka 2013 na 2014 ilifanya utafiti wa awali na kubainisha uwepo wa madini ya chokaa katika Vijiji vya Ausia na Tumbelwa, madini ya *nickel* katika Kijiji cha Ausia, madini ya dhahabu katika Vijiji vya Mpondi, Maji ya Shamba, Birise, Chang'aa, Jogolo, Tumbelo na Forya na madini ya shaba katika Kijiji cha Masange.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itazidi kuiwezesha *GST* na *STAMICO* kuendelea kufanya tafiti za kina kadri itakavyoweza kupata bajeti ya kutosha kama ilivyokwishafanya katika maeneo ya Tanga, Chunya, Katente, Mpanda, Kyerwa na Buhemba ili wananchi wanufaike na rasilimali za madini na kuwawezesha kuongeza kipato, kupunguza umaskini na kuongeza pato la Taifa kwa kulipa kodi stahiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Sannda.

**MHE. EDWIN M. SANNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nipongeze majibu mazuri ya Serikali kutoka kwa Naibu Waziri. Pamoja na majibu mazuri hayo, basi nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, ripoti hii ya utafiti wa awali sisi kama watu wa Ausia na kule Kondoa hatuna, kwa hiyo hata kuweza kujua kuna kiwango cha chokaa kiasi gani imekuwa ni mtihani na ukizingatia kwamba madini haya ni muhimu sana katika kazi za ujenzi, sasa tunataka kujua, ni hatua gani na wao kama Serikali watatusaidia ili twende kwenye utafiti wa kina tuweze kujua madini kiasi gani yapo kule tuendeleo na hatua ya pili ya kupata mwekezaji na hatimaye kuanza kunufaika na uwepo wa madini hayo? Hilo ni la kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ili Mheshimiwa Naibu Waziri akajiridhishe na hali halisi iliyoko pale akifika *site*, je, anaonaje sasa mimi na yeye pamoja na wataalam wake wa Wizara tukaongozana tukaenda *site* tuweze kuharakisha mchakato huu wa wananchi wa Kondoa Mjini waweze kunufaika na madini haya ambayo yanaonekana yako kwa wingi. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Madini, Mheshimiwa Stanslaus Nyongo.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Edwin , Mbunge wa Kondoa Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimshukuru sana Mheshimiwa Sannda kwa kazi nzuri anayoifanya kwa wananchi wa Kondoa, wananchi wa Kondoa nadhani watamtazama tena hapo mwakani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu ni kwamba, alichokisema na majibu yangu ya msingi nilivyosema ni sawa, Wizara yetu kupitia *GST* tunafanya tafiti za kina kupitia zile *QDS* yaani *Quarter degree sheets*, tunafanya kitu wanaita *Geophysical Survey* ambayo inatambua uwepo wa madini

katika maeneo hayo na kwa kweli kwa nchi nzima tuna ramani inayoonyesha uwepo wa madini na kila sehemu ni madini gani yako katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa utafiti wa kina ambayo ni *geochemistry* ambayo inafanywa mara nyingi na mwekezaji mwenyewe. Anakwenda anafanya utafiti wa kina kujua *deposit* iliyopo pale na kama *deposit* hiyo anaona yeye inaweza ikamlipa, ikawa *economical*, sasa hatua ya pili ya kuomba leseni ya uchimbaji, anakuja kuomba kwetu na tunampatia kwa ajili ya uchimbaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba utafiti wa kina umeshaonesha madini katika maeneo niliyoyataja na sasa hivi tunakaribisha wawekezaji wengi waje wawekeze kwa sababu utafiti wa kina unahitaji fedha nyingi.

Kwa hiyo sasa hivi tunaweka mahusiano mazuri na maeneo mbalimbali kwa mfano jana nimepokea ugeni kutoka China, wao wanataka kutusaidia kufanya tafiti za kina kuweza kutambua maeneo na *deposit* zilizopo katika maeneo mbalimbali ili kuweza kuwasaidia wachimbaji kuwapa taarifa za kijijolojia na waweze kwenda kuwekeza maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ameuliza kwamba niko tayari kwenda Kondo na wataalam, mimi nimweleze tu ni kwamba niko tayari, tunaweza tukaenda Kondo na niko tayari muda wote na wataalam wapo, lakini pale panapohitajika tutaweza kubeba timu ya wataalam kwenda nayo, lakini kwa kufika pale na kujionea niko tayari wakati wowote.

**MWENYEKITI:** Mtaambatana pia na Naibu Waziri wa Wizara ya Fedha na Mipango. Mheshimiwa Dkt. Kafumu.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba niishukuru Serikali sana kwa kazi nzuri inayofanya ya kufanya utafiti wa awali ili

kuchora ramani za kijiolojia. Hata hivyo, napenda niikumbushe Serikali kwamba iliahidi kuwasaidia wachimbaji wadogo kwa kuwafanyia utafiti wa kina maana yake *minor exploration* kwa kupitia *STAMICO*. Ni lini basi Serikali itafanya kwa sababu wachimbaji wadogo hawana huo mtaji wa kufanya huo utafiti wa kina kwa ajili ya uchimbaji wakiwemo hao wachimbaji na wanaotafuta madini ya chokaa kule Kondo. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Madini, Mheshimiwa Stanslaus Nyongo.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Kafumu, Mbunge wa Igunga, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa, Serikali ilitoa ahadi kuwasaidia wachimbaji wadogo kufanya tafiti mbalimbali na hasa tafiti za kina, kuweza kujua kuna kiasi gani cha madini katika maeneo mbalimbali na madini tofauti mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanza tu *STAMICO* tayari imekwishanunua mtambo wa ku-*drill* yaani *drilling machine* kwa ajili ya kuweza kufanya tafiti za kina. Mtambo huo kwa kweli tayari upo na tumekwishaanza kufanya tafiti mbalimbali maeneo mbalimbali na niwaase tu wale wachimbaji wadogo ambao wanahitaji huduma hiyo wanaweza sasa hivi wakaleta mahitaji yao au maombi yao katika Shirika letu la Taifa, yaani *STAMICO* kwa ajili ya kufanyiwa hizo *exploration*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tutaendelea kununua mashine mbalimbali ambapo tunaweza sasa tukaendelea kufanya tafiti za kina na kuweza kuwasaidia wachimbaji wadogo kwa sababu tunatambua uchimbaji wao wa kubahatisha ambao unawatia hasara, wengine wanapoteza fedha nyingi kwa sababu ya kwenda



kubahatisha. Uchimbaji wa kubahatisha unasababisha umaskini mkubwa. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na swali linaloifuata, linaulizwa na Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mbunge wa Viti Maalum, lakini linaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Maftaha Nachuma.

Na. 140

**Kufungia Saloon Zinazotoa Huduma ya Kubandika Kucha na Kope**

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA (K.n.y. MHE. RUKIA AHMED KASSIM)** aliluliza:-

Kuna baadhi ya wanawake wameathirika sana na matumizi ya dawa za kuongeza makalio pamoja na matumizi ya kope na kucha bandia:-

Je, Serikali ipo tayari kufungia *saloon* zote pamoja na kuwachukulia hatua kali wale wote wanaotoa huduma hii?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa kwa niaba Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi, Mheshimiwa Dkt. Mwinyi.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA (K.n.y. WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Mamlaka ya Chakula na Dawa imekuwa ikidhibiti ubora, usalama na ufanisi wa bidhaa za chakula, dawa, vipodozi, vifaa na

vitendanishi kupitia mifumo yake ya usajili, ukaguzi na ufuatiliaji wa ubora na usalama wa bidhaa husika zinapokuwa kwenye soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufuatilia ubora na usalama, *TFDA* imeweka mfumo wa kupokea taarifa kutoka kwa watumiaji na watendaji wa afya juu ya ubora na madhara yatokanayo na matumizi ya bidhaa za chakula, dawa, vipodozi, vifaa na vitendanishi. Taarifa hizo hupokelewa kupitia fomu maalum pamoja na mfumo wa kielektroniki wa upokeaji wa taarifa za madhara ya bidhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa za ubora na madhara ya chakula, dawa, vipodozi, vifaa na vitendanishi ni muhimu kwani huzisaidia Mamlaka za Udhhibiti Duniani ikiwemo *TFDA* katika kuchukua hatua mbalimbali kuhusiana na bidhaa inapokuwa kwenye soko mfano kuiondoa kwenye soko, kuifutia usajili au kubadili matumizi ya bidhaa husika. Katika mwaka wa fedha wa 2017/2018, *TFDA* ilipokea kutoka kwa watumiaji na watendaji wa afya taarifa 238 za madhara yaliyohisiwa kusababishwa na matumizi ya dawa ambapo tathmini zilionesha kuwa ni salama na zinafaa kuendelea kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, *TFDA* haijawahi kupokea taarifa za madhara kuhusiana na kucha za kubandika. Kutokana na kukosekana kwa takwimu hizo, Serikali haioni sababu ya kufunga *saloon* zote wala kuwachukulia hatua wanaotoa huduma hii bali Wizara kupitia *TFDA* itaendelea kutoa elimu kwa watumiaji pamoja na kuwahamasisha watendaji wa afya umuhimu wa kutoa taarifa za ubora na madhara yatokanayo na matumizi ya bidhaa za chakula, dawa, vipodozi, vifaa, vitendanishi na vipodozi zikiwemo kucha za kubandika ili kuiepusha jamii kutokana na athari za kiafya zinazoweza kujitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia inatoa wito kwa watumiaji wa vipodozi kuzingatia masharti na maelekezo ya utumiaji sahihi wa vipodozi hivyo na kutoa taarifa pindi

athari za matumizi ya vipodozi na vifaa vya urembo zinapojitokeza. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Nachuma.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza imeelezwa kwamba *TFDA* ndiyo Mamlaka ambayo inashughulikia chakula na dawa, lakini kwa hali ya uhalisia *TFDA* yenyewe *capacity* yake ni ndogo sana ya kuweza kupima vinasaba vyote Tanzania nzima kwa sababu Ofisi yao Kuu iko pale Dar es Salaam na wana vifaa vichache sana.

**MWENYEKITI:** Uliza swali.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu, je, ni lini Serikali itaiongezea vifaa *TFDA* iweze kufanya kazi yake sawasawa nchi nzima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kuna dawa pia ambazo inasemekana na wataalam wa afya, kwamba zinapelekea kuharibu miili ya binadamu na hasa zile dawa za kufanya rangi ya watu weusi iweze kuwa nyeupe, je, Serikali imechukua hatua gani mpaka hivi sasa ili kuwafanya Watanzania wengi wanaotumia dawa hizi wasiweze kupata madhara?

**MWENYEKITI:** Ahsante. (*Makofi*)

Majibu kwa maswali hayo kwa niaba Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Mwinyi.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA (K.n.y. WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Maftaha kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka nimhakikishie kwamba uwezo wa *TFDA* sio mdogo kama anavyodhani, Taasisi hii ni kubwa, ina Maabara ya kisasa sana pale Dar es Salaam lakini pia imeanza kujenga uwezo Kikanda na sio kwamba wanafanya kazi Dar es Salaam peke yake, wako katika Kanda mbalimbali katika nchi yetu, na wana maabara inayotembea, (*mobile lab*) kwa maana hiyo nadhani uwezo wao ni mzuri na wataendelea kuuboresha ili kuweza kufika nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili la dawa ambazo zinasababisha au tunazilita hizi dawa za kujichubua, ili watu wabadilike rangi zao, hili napenda nimwarifu Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu, kwamba *TFDA* imekuwa ikichukua hatua mara nyingi sana. Dawa nyingi sana zimeshaondolewa kwenye soko zenye madhara haya na hizi mara nyingi ni dawa ambazo zina maada inayoitwa *steroid* ambazo kwa kweli zinaharibu ngozi na zinaweza kusababisha madhara makubwa, zimekuwa zikiondolewa na wahusika wamekuwa wakipigwa faini na kwa maana hiyo sasa hivi kuna udhibiti mzuri sana wa dawa zinazosababisha madhara haya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Goodluck Mlinga.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kumekuwa na wimbi kubwa la ongezeko la matumizi ya dawa za nguvu za kiume, enzi zenu nakumbuka kulikuwa na *mkuyati*, lakini sasa hivi, kuna *super moringe*, *mundende*, *super gafina*, *gasosi mix*, *super shafti*, *sado power*, amsha mzuka, Kongo *dust* na hii Kongo *dust* imeonesha kuwa mafanikio makubwa. Je, Serikali imeshafanya utafiti nini kinasababisha tatizo hili la watu kutokuwa na nguvu za kiume kupelekea kutumia sana hizi dawa?

**MWENYEKITI:** Wewe una uzoefu mkubwa sana, ehhe? Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA (K.n.y. WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WAZEE NA WATOTO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mlinga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu zinazopelekea kupungua kwa nguvu za kiume ni nyingi, ikiwemo magonjwa mbalimbali kama vile kisukari, msongo wa mawazo na kadhalika, kwa hiyo kuna sababu nyingi zinazopelekea matatizo haya na ndio maana watu wengi wamekuwa wakitafuta ufumbuzi wa tatizo hilo. Ninachoweza kusema hapa ni kwamba ziko dawa zenye maada ambazo sio za kikemikali, ambazo ni bora zaidi zitumike kuliko kemikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili kama nilivyosema awali *TFDA* wanao uwezo wa kubaini ni dawa gani ambazo zinasababisha madhara na zile ambazo zinasababisha hakuna budi kutolewa taarifa mapema ili ziweze kuondolewa kwenye soko, lakini tunatambua kwamba sasa hivi kuna dawa zilizopitishwa na Mamlaka za Udhhibiti ambazo zinauzwa kihalali kabisa za kuweza kuongeza nguvu za kiume na ambazo hazijaripotiwa kuwa kuna matatizo kama ya athari zinazopelekea kutokana na matumizi ya dawa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wetu ni kwamba wanaotaka kutumia dawa hizi waendeleo kutumia zile ambazo zimethibitishwa kitaalam na wasitumie zile ambazo hazina uthibitisho ili wasiweze kupata madhara.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan Lyimo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na wimbi kubwa la wanaume na vijana kutumia dawa za kuongeza nguvu za kiume, sasa hivi kuna baadhi wanatumia dawa za kukuza maumbile ya kiume, nataka kujua nini madhara yake na ni kwa nini wanafanya hivi? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Mwinyi.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA (K.n.y. WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Susan Lyimo kama ifuatavyo:-

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Sikilizeni basi majibu mazuri hayoo.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA (K.n.y. WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na taarifa nyingi za dawa zinazoweza kukuza maumbile na wito wangu ni kwamba, watu waendeleo kuhakikisha kwamba hawatumii dawa yoyote ambayo haijasajiliwa, haijathibitishwa kitaalamu kwa sababu inaweza ikasababisha madhara na wale ambao wanatoa taarifa hizi bila ya uthibitisho kwa kweli wanafanya kosa na wanatakiwa wachukuliwe hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa nilizokuwa nazo ni kwamba hakuna dawa yoyote ambayo kitaalam imethibitishwa na imepewa kibali kwa ajili ya matumizi kama hayo. Kwa hivyo nawaomba Watanzania wawe makini wanapotaka kununua dawa kama hizi kwa sababu zinaweza zikawa zina madhara. Tungependa wananchi watoe taarifa endapo wamewahi kutumia na wamepata madhara yoyote ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haji.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ningependa kujua kwa sababu haya maumbile ya wanawake wanaokuza makalio ni vitu ambavyo vimeongezeka sana nchini. Je, kuna madhara gani, wanayoyapata wanaume pindi wakishirikiana na wanawake wanaoongeza makalio. *(Kicheko)*

**WABUNGE FULANI:** Aaaaa.

**MWENYEKITI:** Hilo swali, hawezi akalijua yeye madhara hayo.

Waheshimiwa tunaendelea, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Susan Limbweni Kiwanga, Mbunge wa Mlimba na linaelekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Maji, kwa niaba yake Mheshimiwa Devotha Minja.

Na.141

### **Fedha za Mradi wa Maji-Mlimba**

**MHE. DEVOTHA M. MINJA (K.n.y. MHE. SUSAN L. KIWANGA)** aliuliza:-

Mji Mdogo wa Mlimba unazungukwa na Kata za Chisano, Kalengakelo na Kamwene na zina jumla ya wakazi wasioupungua elfu hamsini na nane ambapo hawana maji kwa matumizi ya nyumbani na kunywa; na kwa kuwa kuna chanzo kikubwa cha maji na Mhandisi wa Halmashauri ameshaleta andiko la mradi wa maji:-

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha za mradi huo ili wananchi hao wapate maji ya kunywa safi na salama?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Naibu Waziri, Wizara ya Maji, Mheshimiwa Aweso.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Susan Limbweni Kiwanga, Mbunge wa Mlimba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto ya maji kutotosheleza wakazi wa Kata za Mlimba, Chisano, Kalengakelo na Kamwene waliopo katika Jimbo la Mlimba, Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero kwa kushirikiana na Wizara ya Maji imesanifu mradi mkubwa wa maji ambao

utahudumia wakazi zaidi ya 29,713. Mradi huu utakapokamilika utatatua kero ya maji katika kata zilizotajwa hapo juu ikiwemo Mlimba kwa kuondoa mgao wa maji kabisa.

Andiko la mradi huu linafanyiwa kazi na Wizara ya Maji ili Serikali iweze kutafuta fedha zaidi ya shilingi bilioni 4.5 kuweza kufanikisha ujenzi wa mradi huu ambao umeonekana kuwa suluhisho la maji katika Jimbo la Mlimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika jitihada hizo za kuwapatia wananchi wa Jimbo la Mlimba huduma ya maji safi na salama, Serikali kupitia program ya maji inaendelelea na ujenzi wa mradi wa maji wa Kata za Chita/ Ching'anda a Mbingu/Vigaeni. Pia imekamilisha ujenzi wa miradi ya maji saba katika Vijiji vya Tangamyika, Masagati, Matema, Kamwene, Viwanja Sitini, Mlimba A na B, Namwawala na Idete.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Minja.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nimesikiliza majibu ya Naibu Waziri na kwa kuwa Serikali imepokea andiko hilo, naamini kwamba italichukulia kwa uzito ili kunusuru wananchi hususan akina mama katika Kata za Mlimba na kata za jirani na Jimbo la Mlimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, mkandarasi aliyemaliza Mradi wa Maji Msolwa - Kilombero ambaye hajalipwa fedha zake na Serikali lakini amekubali kuendelea kufanya ujenzi katika Mradi wa Mbingu. Je, Serikali ipo tayari kumlipa fedha zake za awali alizozilimbikiza na anaidai Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kulikuwepo na mpango wa kuongeza kina katika bwawa la Mindu Manispaa ya Morogoro kutokana na maji yaliyopo kutotosheleza wananchi wa Manispaa ya Morogoro. Kwa miaka mitatu sasa Serikali imesambaza mabomba katika



Kata za Kiega A na B, Kihonda, Mkundi, je, ni lini itapeleka maji kwa wananchi hao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa maswali hayo Naibu Waziri, Wizara ya Maji, Mheshimiwa Aweso.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge. Mimi nilipata nafasi ya kufika katika jimbo lake lakini kubwa ambalo tumeona tuna changamoto kubwa pale Mlimba lakini tumefanya jitihada ya uchimbaji wa visima lakini bado kumekuwa na changamoto. Tumeona haja sasa ya kutafuta chanzo cha kutosheleza kuhakikisha wananchi wa Mlimba wanapata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusu fedha anazodai mkandarasi anayetokeleza mradi wa maji, tunashukuru sana Wizara ya Fedha ilitupatia kiasi cha shilingi bilioni 44 kwa ajili ya malipo ya wakandarasi. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge sisi kama Wizara ya Maji hatutokuwa kikwazo kumlipa fedha zake kwa wakati ili aendelee kutekeleza mradi na wananchi waweze kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala zima la maji Manispaa ya Morogoro, kiukweli Morogoro Mjini kuna changamoto ya maji na hii yote imetokana na sababu tu ya ongezeko la watu na hata shughuli mbalimbali za kiuchumi.

Sisi kama Wizara ya Maji tumefanya jitihada kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha kufanya mazungumzo na Serikali ya Ufaransa kwa ajili ya uwekezaji wa fedha kwa maana ya utekelezaji wa miradi ya maji inategemeana na fedha. Zaidi ya Euro milioni 70 zitakazopatikana zitawekezwa katika Mji ule wa Morogoro ili kuhakikisha tunaongeza kina cha Bwawa la Mindu ili wananchi wa Morogoro waweze kupata maji safi, salama na yenye kutosheleza. Sisi kama Wizara ya Maji tutafanya jitihada za haraka ili jambo hili

liweze kutekelezeka na wananchi wa Morogoro waweze kunufaika na huduma hii muhimu. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mboni.

**MHE. MBONI M. MHITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mradi wa Maji Handeni pamoja Korogwe yaani *Handeni Trank Main* ambao tuliahidiwa kuwemo katika miradi ya miji 28 ambayo inategemea fedha kutoka Serikali ya India na naamini kwamba fedha hizo tayari zimepatikana. Je, ni lini Serikali itaanza kutekeleza mradi huu ili wananchi wa Jimbo la Handeni Vijijini waweze kupata maji safi na salama? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Naibu Waziri, Wizara ya Maji, Mheshimiwa Aweso.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge, dada yangu Mboni amekuwa mpiganaji mkubwa sana hususani katika suala zima la maji katika Jimbo lake la Handeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tulipata nafasi ya kutembelea katika jimbo lake na tumeona kabisa hii changamoto. Ndiyo maana Wizara yetu ya Maji tukaona katika miji hiyo 28 ambayo inatakiwa ipatiwe maji haraka ni mmojawapo ni Jimbo lake la Handeni. Nataka nimhakikishie sasa hivi tupo katika hatua ya kumpata Mhandishi Mshauri na mkadarasi ndani ya mwezi Septemba atakuwa amekwishapatikana na miradi hii itatekelezwa katika maeneo yote ili kuhakikisha tunamtua mwanamama ndoo kichwani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Flatei

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri amefika Jimbo la Mbuli Vijijini na ameona changamoto iliyopo hapo inayofanana na Jimbo la Mlimba. Mheshimiwa Naibu Waziri aliahidi kisima kichimbwe Hyadom na tumeomba shilingi milioni 80 na akaahidi itatumwa. Je, ni lini sasa atatupatia fedha za kuchimba kisima pale Hyadom?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Naibu Waziri, Wizara ya Maji, Mheshimiwa Aweso.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri sana anayofanya katika jimbo lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilifika pale Hyadom tumeona kuna mradi mkubwa lakini katika kuhakikisha tunawaongezea chanzo kwa maana ya uzalishaji tukaona kuna haja ya uchimbaji wa kisima. Sisi tuna Wakala wa Uchimbaji Visima *(DDCA)*, kwa hiyo, niwaagize wachimbe kisima kile haraka ili wananchi wa Hyadom waweze kupata ongezeko la maji na waweze kupata huduma hii muhimu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea Waheshimiwa, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Musa Rashid Ntimizi, Mbunge wa Igagula na linaelekezwa kwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Na. 142

### **Hitaji la Mawasiliano ya Simu - Kata ya Mmale**

**MHE. MUSA R. NTIMIZI** alliluliza:-

Kata ya Mmale haina mawasiliano kabisa ya simu:-

Je ni lini Serikali itawapatia wananchi hao mawasiliano kwa kuweka minara ya mawasiliano katika kata hiyo?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Eng. Nditiye.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Musa Rashid Ntimizi, Mbunge wa Igalula, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Uyui, zaidi ya wakazi 66,056 wamefikishiwa huduma za mawasiliano katika Kata za Kizengi, Loya, Lutende, Mabama na Miswaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo, bado kuna changamoto za upatikanaji wa huduma za mawasiliano katika Kata ya Mmale. Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote itaviainisha vijiji vya Kata ya Mmale iliyopo katika Jimbo la Igalula kwa kufanya tathmini ya mahitaji kwa ajili ya kuvifikishia huduma ya mawasiliano na kuvijumuisha katika orodha ya miradi itakayoingia katika zabuni zinazotarajiwa kutangazwa ifikapo mwezi ujao wa tano.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ntimizi.

**MHE. MUSA R. NTIMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya kutia matumaini ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kama nakumbuka Wizara iliahidi kutoa orodha ya vijiji vyote vitakavyotagazwa na kufunga minara katika majimbo yetu nchi nzima. Swali langu ni lini orodha hii tutapatiwa Waheshimiwa Wabunge ili tuwe na nafasi ya kushauri yale maeneo ambayo tunadhani ni muhimu zaidi kupata mawasiliano? Hapo ikiwemo na Bariadi katika Jimbo unalotoka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, maeneo mengi *service provider* hawa wanapenda kujazana katika maeneo ya *centers* tu, wanakimbia kupeleka minara katika maeneo ya vijiji vyetu ambako ndiyo kuna shida kubwa ya mawasiliano na *population* ni kubwa sana. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwalazimisha *service providers* kwenda kuweka minara katika maeneo yetu ya vijijini ili wananchi wetu waweze kupata mawasiliano?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa maswali hayo Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDIYIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Musa Rashid Ntimizi, Mbunge wa Igalula, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa jinsi anavyoshughulika kuhakikisha jimbo lake wananchi wanapata huduma ya mawasiliano. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine wote kwamba Serikali inahakikisha kwamba mawasiliano yanapatikana kwa uhakika katika majimbo yote nchi nzima. Hivi navyozungumza nimekwishazungumza tena mara nyingine kwamba tumefikia asilimia 94 ya wananchi kuwasiliana na tutahakikisha kabla ya mwaka ujao kuisha asilimia 100 ya wananchi wa Tanzania wanapata mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la kwanza, Mheshimiwa Mbunge orodha ya mwanzo nitaitoa kesho ya vijiji zaidi ya 600 ambavyo tunategemea kupeleka minara ya mawasiliano kwa ajili ya wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili anataka kujua kwa nini watoa huduma wanarundikana sehemu moja. Kama nilivyowahi kuzungumza hapo awali hawa watoa huduma za mawasiliano ni wafanyabiashara na mfanyabiashara kawaida anatafuta sehemu ambako

atapata biashara nzuri, hawawezi kupeleka sehemu ambako hakuna mvuto au ambako wakiwekeza pesa yao haitarudi. Ndiyo maana Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote imekuwa ikitoa ruzuku kwa haya makampuni waweze kupeleka mawasiliano mpaka vijijini ambako kabisa wananchi hawawezi kununua huduma za mawasiliano kwa jinsi ambavyo watoa huduma wanataka. Ndiyo maana sasa tumeanzisha Mfuko wa Wawasiliano kwa Wote ili uweze kuziba hilo *gap* na kufanya wananchi waweze kuwasiliana nchi nzima.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mnzava.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kama ilivyo lgalula kumekuwa na changamoto kubwa ya mawasiliano kwenye Jimbo la Korogwe Vijijini hususan kwenye Kata za Kizara, Makumba, Kalalani, Mkalamo, Elewa na Lutindi na Mheshimiwa Naibu Waziri anafahamu changamoto hizi. Ni lini Serikali itatoa utatuzi wa changamoto hizi zinazowakabili watu wa Korogwe Vijijini?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Naibu Waziri Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Eng. Ntitiye, ni lini mtafika huko?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikiri kwamba nilishatembelea Korogwe Vijijini na hilo eneo alilolitaja Mheshimiwa Mbunge nililiona, ni kweli kwamba kuna mnara wa mawasiliano lakini hauna nguvu ya kutosha. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba nitatuma wataalam kwanza wakaongeze nguvu kwenye hicho kijiji cha kwanza alichokitaja halafu na nitatoa orodha nyingine kesho aangalie vijiji vingine ambavyo tumeviorodhesha kwa ajili ya kuimarisha mawasiliano maeneo hayo.

**MWENYEKITI:** Haya nione sasa Ludewa na kwenyewe Mheshimiwa Ngalawa.

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo Igalula, Jimbo la Ludewa lina eneo kubwa sana ambalo halina mawasiliano ya simu. Hivi karibuni imejengwa minara katika Tarafa ya Mwambao lakini minara ile toka ilipowashwa imeongea kwa siku tatu tu. Sasa nimuulize Mheshimiwa Waziri kuna tatizo gani minara imejengwa imewashwa siku mbili na baada ya hapo mawasiliano hakuna pamoja na ujenzi wa Kijiji cha Ibumi?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Naibu Waziri Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa *Engineer* Nditaye.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Deo Ngalawa, Mbunge wa Ludewa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekwishatembelea Kata ya Mwambao ambayo iko mwambao wa Ziwa Nyasa na nimekwishavitembelea vijiji mbalimbali kuanzia Lupingu, Higa, Makonde ambako kweli kabisa kulikuwa kuna tatizo kubwa sana la mawasiliano. Mheshimiwa Deo ambaye ni mfuatiliaji mkubwa sana wa suala la mawasiliano ni shahidi kwamba ndani ya miezi mitano toka nimetembelea eneo hilo tumekwishaweka minara tisa (9) ya mawasiliano kwa ajili ya wananchi wa eneo la Mwambao. Minara mitatu (3) ambayo sasa hivi haifanyi kazi ilipata hitilafu kidogo na hivi sasa tunapozungumza tumetuma wataalam kutoka Halotel wanakwenda kurekebisha hitilafu hiyo ili wananchi waweze kuendelea kupata mawasiliano.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kiwelu.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba niulize swali kwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Rombo limekuwa na tatizo kubwa sana la mawasiliano hasa katika kata zilizoko mpakani na ukanda wa juu na Mbunge wa Jimbo hili amekuwa akiuliza maswali mara kwa mara. Je, ni lini tatizo hili litamalizika katika Jimbo hilo la Rombo?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Naibu Waziri Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Eng. Nditiye.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba siyo Jimbo la Rombo tu maeneo ya mpakani ni karibu majimbo yote ambayo yako mipakani Tanzania kuna tatizo la mwingiliano wa mawasiliano ya simu kutoka nchi jirani. Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imekwishawaagiza watoa huduma kwanza kwenda kuongea na majirani zao watoa huduma wa nchi jirani kurekebisha changamoto iliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kulikuwa na utaratibu ambao wenzetu nchi jirani walikuwa wameukiuka ambapo tunaendelea kuufanyia kazi. Sasa hivi eneo la Rombo wako Vodacom na Halotel kwa ajili ya kurekebisha tatizo hil. Eneo la Musoma (Tarime) tumewapeleka Airtel na Tigo kwa ajili ya kurekebisha tatizo hilo. Maeneo ya Bukoba na Kigoma tumewapeleka tena watoa huduma wengine kwa ajili ya kurekebisha tatizo hilo.



**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Ignas Alyce Malocha, Mbunge wa Kwela bado linaelekezwa kwa Wizara hiyo hiyo ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Na. 143

### **Barabara ya Kibaoni – Kasansa - Muze - Kamsamba**

**MHE. IGNAS A. MALOCHA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya maandalizi ya awali ya upembuzi yakinifu kwa ajili ya kuweka lami barabara muhimu ya Kibaoni-Kasansa-Muze-Kilyamatundu-Kamsamba kutokea Mlowo; ambayo inaunganisha mikoa mitatu ya Katavi, Rukwa na Songwe?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Eng. Nditiye.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibiwa swali la Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanza kutekeleza mipango ya ujenzi wa barabara ya Kibaoni- Majimoto-Kisansa-Muze-Kilyamatundu- Kamsamba hadi Mlowo yenye urefu wa kilometa 149 kwa kuanza na ujenzi wa daraja la Momba ambalo limekamilika hivi karibuni. Daraja hili limekuwa kikwazo kikubwa cha mawasiliano kati ya wananchi wa Mikoa ya Katavi, Rukwa na Songwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa barabara hii katika mwaka wa fedha 2018/2019, jumla ya shilingi milioni 200 zilitengwa kwa ajili ya upembuzi yakinifu

wa barabara ya Kibaoni-Majimoto-Inyonga ikiwa ni sehemu ya barabara ya Kibaoni-Kasansa-Muze-Kilyamatundu-Kamsamba hadi Mlowo. Aidha, katika mwaka wa fedha 2019/2020, fedha zimeombwa kwa ajili ya kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Ntendo-Muze-Kilyamatundu ikiwa pia ni sehemu ya barabara ya Kibaoni -Kasansa-Muze-Kilyamatundu-Kamsamba hadi Mlowo. Mara baada ya kukamilika upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na maandalizi ya nyaraka za zabuni za gharama ya ujenzi kujulikana Serikali itatafuta fedha za kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara hii.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Malocha.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza kabisa, naipongeza Serikali kwa ujenzi wa daraja, imekuwa ni faraja kubwa kwa kweli kwa wananchi, tunaipongeza sana Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu hayo, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, Kwa kuwa Serikali inatambua umuhimu mkubwa wa barabara hiyo na imekubali kuanza kutenga fedha kwa ajili ya usanifu kwa maana ya kuweka lami lakini bado katika barabara hiyo yapo maeneo korofi ambayo yanasababisha magari kukwama wakati wa masika. Je, kwa nini Serikali isitenge fedha za kutosha kutatua tatizo hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kipande cha barabara ya Ntendo - Muze chenye kilometa 37.07 ni barabara inayotegemewa na wananchi wa Bonde la Ziwa Rukwa katika kupeleka mazao Mji wa Sumbawanga; na kwa kuwa barabara hiyo ina changamoto nyingi sana ya kukwamisha magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2017/2018 Serikali ilitenga fedha kwa ajili ya kuweka lami kilometa 2 jambo ambalo linaweza likachukua miaka 18 kumaliza barabara hiyo. Kwa nini Serikali isiongeze fedha zaidi kuhakikisha barabara ile inakamilika ili kutoa huduma kwa wananchi?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDIYIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majibu yangu ya mwanzo nimeeleza tu kwamba kwenye mwaka huu wa fedha 2019/2020 tutakuja kuliomba Bunge lako Tukufu litupitishie bajeti yetu ili tuweze kutatua changamoto mbalimbali za barabara zetu hapa nchini ambazo zina mtandao mrefu sana na ambao kwa ujumla kabisa tayari upembuzi yakinifu ulishafanyika na tunaendelea na usanifu wa kina kwa maeneo mbalimbali. Kwa hiyo, jibu lake la kwanza ni kweli kwamba mwaka huu tutatenga fedha nyingi kwa maeneo korofi ambayo yako kwenye barabara niliyoitaja hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kwenye barabara ya Ntendo – Muze kwanza kuna milima mikali sana, na kwa kweli barabara ile ni mbovu na ina changamoto na ndiyo barabara ambayo tunategemea kupata mazao mengi kutoka maeneo hayo. Kuna fedha ambayo tumetenga kupitia *TANROAD* kwa ajili kwenda kurekebisha maeneo korofi ili barabara iweze kupitika mwaka mzima. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Kikwembe.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kunipatia nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa barabara hii ya kutoka Kibaoni mpaka Mlowo imekuwa ikitajwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi na pia imekuwa ikitajwa kwenye kila bajeti inayopitishwa na Bunge hili. Je, kutokana na majibu aliyotoa Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba, barabara imekwisha fanyiwa upembuzi yakinifu? Hivyo basi wanatafuta fedha ili kuja kuiwekea lami.

Je, Serikali haioni sasa kwamba ni hasara kuifanyia barabara upembuzi yakinifu na baadaye kuja kuitafutia

fedha kwa ajili ya kuweka lami jambo ambalo utasababisha tena kuja kufanya upembuzi yakinifu mwingine?

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa *Engineer* Nditije kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi kabisa Serikali ikishafanya upembuzi yakinifu na ikafanya usanifu wa kina huwa hakuna gharama tena ya kurudia zoezi hilo kwa miaka ijayo hata miaka sita, lakini baada ya hapo ndiyo unaweza kufanya tena *feasibility study* upya baada ya kujiridhisha kwamba kuna mazingira ya kijiografia yaliyosababisha eneo hilo kubadilika, lakini ni ndani ya miaka mitano tunakuwa tumeshaanza kufanya utekelezaji wa miradi mbalimbali baada ya upembuzi yakinifu. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Silinde.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwa niaba ya wananchi wa Momba na wananchi wa Kwela kwa ndugu yangu Malocha tunashukuru sana kwa ujenzi wa daraja bora kabisa ambalo nafikiri wananchi tutakavyo kwenda kulizindua wataona kazi ambayo tumeifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, daraja hili ni muunganisho wa hiyo Mikoa mitatu ya Katavi, Rukwa na Songwe lakini barabara inayozungumzwa inatokea kwenye Jimbo la Malocha inapitia Jimbo langu halafu inakwenda mpaka katika halmashauri ya Wilaya ya Mbozi. Ni barabara ndefu zaidi ya kilomita mia mbili na kitu, na barabara hii inajumuiya ya watu wasiopungua zaidi ya 150000. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachoomba ni *commitment* ya Serikali ni lini itakwenda kuanza ujenzi ili wananchi hawa sasa wapate barabara ya lami kama

ambavyo ahadi ya Mheshimiwa Rais Kikwete na ahadi ya Mheshimiwa Rais Dkt. Magufu itekelezwe kabla ya kumaliza mwaka huu wa uchaguzi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Nditaye, Naibu Waziri, Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Ni lini, ni lini, ni lini.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli eneo lile lina watu wengi lakini kwa kweli ni eneo la kimkakati kwa sababu kuna uzalishaji mzuri sana wa mazao mbalimbali ambayo yanasaidia kwenye uchumi wa nchi. Kama nilivyozungumza hapa awali tunaleta bajeti yetu hivi karibuni, tunaliomba sana Bunge lako Tukutu litupitishie bajeti yetu halafu tuanze ujenzi baada ya kupata fedha mara moja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mulugo.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Tunayo barabara ya kutoka Mbalizi kwenda Wilaya ya Songwe, Mbalizi ni Mkoa wa Mbeya na Songwe ni Mkoa wa Songwe na *TANROADS* Mbeya, *TANROADS* Songwe tayari kuna mgawanyiko wa kugawana hiyo barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Ilani na kwenye agizo la Mheshimiwa Rais barabara hiyo yenye kilometa 91 na ilishafanyiwa tayari upembuzi kilometa 56 kutoka Mbalizi mpaka Galula ili iweze kupata lami, lakini mpaka leo kupo kimya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iniambie ni lini watafanya upembuzi yakinifu ili tuweze kupata lami kutoka Mbalizi mpaka Mkwajuni? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge amekiri kabisa kwamba kuna kipande cha barabara kutoka Mbalizi mpaka Songwe ambacho upande mmoja tayari umekwisha fanyiwa upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tunatafuta fedha hivi karibuni *TANROADS* upande mwingine wa pili wataanza kufanya upembuzi yakinifu ili tuwe na upembuzi yakinifu wa jumla wa kilomita 91 kwa ajili ya kuingiza kwenye mipango ya kuanza kufanya utekelezaji wa kujenga kwa kiwango cha lami.

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Amina Saleh Molel, Mbunge wa Viti Maalum linaelekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii.

Na. 144

### **Mpango wa Kenya ambao ni tishio kwa Hifadhi ya Serengeti**

**MHE. AMINA S. MOLLEL** aliuliza:-

Kuna taarifa kwamba nchi ya Kenya inatarajia kutekeleza mpango wa kujenga mabwawa makubwa kwa ajili ya uzalishaji umeme. Kwa kuwa ujenzi huo unatishia ustawi wa uwepo wa Hifadhi ya Taifa Serengeti. Je, Serikali ya Tanzania inachukua hatua gani kuhusu mpango huo?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Saleh Mollel, Mbunge wa Viti Maluum kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2016 Serikali ilipata taarifa ya mpango wa ujenzi wa mabwawa ya umeme uliopangwa kutekelezwa na Serikali ya Kenya. Wizara ilifanya uchunguzi wa madhara yatahayosababishwa na miradi hiyo katika Hifadhi ya Taifa Serengeti kwa kukusanya takwimu za mtiririko wa maji na kulinganisha na mahitaji halisi ya miradi iliyotarajiwa. Uchunguzi ulibaini kuwa utekelezaji wa miradi hiyo, ungesababisha athari kubwa ya kiikolojia ya Serengeti kwani takwimu zilizotumiwa na wataalam wa nchini Kenya kuhalalisha mradi huo hazikuwa sahihi. Miongoni mwa athari hizo ni pamoja na kuhatarisha ustawi wa maisha ya viumbe hai kutokana na ukosefu wa maji katika Mto Mara wakati wa kiangazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya Mto Mara yanajadiliwa na Tume ya kuratibu Bonde la Ziwa Victoria (*Lake Victoria Basin Commission*) chini ya Wizara ya Mambo Nchi za Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Aidha, majadiliano mbalimbali kuhusu hatima ya Mto Mara au miradi inayoathiri maji ya Mto Mara ikiwemo ujenzi wa Bwawa la Umeme la Ewaso, Ngiro nchini Kenya yanaendelea kujadiliwa katika mpango wa Bonde la Mto Mara uliosainiwa mwezi Septemba, 2016 chini ya Wizara ya Maji. Katika pango huo suala la athari za ujenzi mabwawa kwa maliasili zitakazoathirika kutokana miradi itakayofanyika nchini Kenya na Tanzania limejadiliwa na mapendekezo kutolewa kuhusu namna ya kukabiliana na matumizi yenye utata.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mollel.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, namshukuru pia Naibu Waziri kwa majibu mazuri na kwa kuwa Serikali sasa imekiri taarifa hizi, na tunafahamu kwamba siyo kila jambo linalojadiliwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki zinakubaliana na tumeshaona kwamba ni tatizo. Je, Serikali inachukua tahadhari gani ili basi jambo hili lisije kutokea kwa sababu litakuwa na madhara makubwa?

Pili, iwapo Serikali ya Kenya itasimama kutekeleza mradi huo; Je, ni madhara gani makubwa ambayo yanatarajiwa hasa kiikolojia na athari zake katika mzunguko wa wanyama, yaani *Wild West Movement*? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Constatine Kanyasu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimpongeze sana kwa swali lake zuri sana, kimsingi uhai wa Mto Mara ndiyo uhai wa Hifadhi ya Serengeti, na ikolojia ya Serengeti inaanzia katika hifadhi zilizoko nchini Kenya. Kwa hiyo, uwepo wa Mto Mara na uhai wa uhifadhi wa Serengeti ni kitu ambacho sisi kama Wizara tunakitilia kipaumbele sana, kwa hiyo, nampongeza sana kwa maswali yake mazuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la kwanza; Je, Serikali inachukua tahadhari gani tumewaelekeza *TANAPA* kuanza kufuatilia kwa karibu mienendo yoyote ile ambayo inaweza ikapelekea utekelezaji wa mpango huu, na kwa kuwa tunaamini kwamba sisi Serengeti ni Mbuga yetu ambayo tunaitegemea, pia tumewaelekeza kuangalia kama inawezekana kujenga mabwawa ya kuhifadhi maji ili pale utekelezaji wa miradi hii itakapofanyika wanyama wasije wakaathirika kwa ukame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, ni madhara gani makubwa yanayotegemewa ni kwamba kimsingi wanyama tunaowaona Serengeti wengi katika msimu wao wa mwaka mzima huwa wanatembea katika nchi hizi mbili. Kwa hiyo, *Wild West Movement* ambayo huwa inatokea Tanzania, huwa inapita mpaka Maasai Mara. Kwa hiyo, iwapo ikolojia hii itaharibiwa, maana yake ni kwamba wanyama hawa wataacha sasa kuwa wana-*cross border* kuja Tanzania au ku-*cross* kwenda Kenya na matokeo yake utalii huu ambao ni urithi wa dunia unaweza ukaathirika.



**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea. Swali linalifuata linaulizwa na Mheshimiwa Desderius John Mipata, Mbunge wa Nkasi Kusini, bado linaelekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii.

Na. 145

### **Migogoro Kati ya Hifadhi na Vijiji – Jimbo la Nkasi**

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA** aliuliza:-

Hivi karibuni Mheshimiwa Rais alitoa agizo la kutatua migogoro ya vijiji na hifadhi mbalimbali na orodha ya vijiji vyenye migogoro toka Jimbo la Nkasi imefikishwa na kupokelewa na Wizara:-

Je, ni lini migogoro ya vijiji vya Kasapa, King’ombe, Mlambo, China, Nkomanchindo na vinginevyo vilivyoondoshwa vitapatiwa ufumbuzi?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Desderius John Mipata, Mbunge wa Nkasi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mheshimiwa Mbunge anavyofahamu, utatuzi wa migogoro iliyopo katika vijiji vyote nchini na hifadhi vikiwemo vijiji Kisapa, King’ombe, Mlambo, China na Nkomanchindo umetolewa maelekezo na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yangu kwamba mara utekelezaji wa maelekezo hayo utakapokamilika, ufumbuzi wa migogoro hiyo utakuwa umepatikana. Nitoe rai kwa wananchi kuacha kuvamia maeneo mapya ya hifadhi wakati huu, wakati migogoro huo unasubiri yanatafutwa ufumbuzi.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mipata.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa majibu haya yaliyotolewa na Serikali lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Mnamo mwezi wa pili mwaka huu wahifadhi wa *Rwafi Game Reserve*, walifyeka mazao ya wananchi wa kijiji cha King'ombe zaidi ya hekari 359 za mazao mbalimbali. Wakati wanafyeka agizo la Mheshimiwa Rais lilikuwa limekwishatolewa na sasa wananchi hawa hawana chakula. Je, Wizara ipo tayari kufidia chakula hicho walichofyeka? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili chakula ni uhai na moja kati ya hitaji la msingi la maisha kwanini Wizara inafikiria kwamba kufyeka ni kusuluhisha migogoro inayojitokeza badala ya kutafuta suluhisho lingine? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, majibu kwa maswali hayo mawili Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Maliasili na Utalii.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimpongeze kwa sababu amekuwa akitoa ushirikiano mkubwa sana katika kutetea wananchi wanaoishi kando kando na maeneo ya hifadhi. Lakini taarifa kwamba mwezi wa pili mwaka 2019 askari wa *Rwafi Game Reserve* walifyeka mazao kwenye hekari 359, ndiyo nazisikia leo na iwapo ni kweli kwamba taarifa hizi zipo na zimefika katika Wizara yangu, basi Wizara itachukuwa hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili Mheshimiwa Mbunge anataka kufahamu kwamba kufyeka mazao ndiyo suluhu ya migogoro hii lakini pia athari zake kubwa kwa wananchi ambao watakosa chakula. Mheshimiwa Rais alikwisha toa maelekezo na askari wetu wote wanajua katika hifadhi zetu zote za Taifa ni marufuku kufyeka mazao ya wakulima kwa sababu mazao mengi ni ya muda mfupi na iwapo hili linaendelea kutokea naomba Mheshimiwa Mbunge tuwasiliane ili tuweze kuchukuwa hatua. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Ruth Mollel na Mheshimiwa Njalu Silanga ajiandae.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Migogoro kati ya wananchi na hifadhi zetu ni ya muda mrefu kwanza ni-*declare interest* kwamba nilikuwa kwenye Bodi ya TANAPA, na wakati ule walitayarisha ramani ambayo wameainisha maeneo ambayo wanaweza kuwaachia wananchi na maeneo ambayo watawatoa wananchi kwa kuwapa fidia kwa sababu ya ikolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni kwanini Serikali haitumi hiyo ramani ya TANAPA ambayo walishaitayarisha kuweza kutoa suluhu ya hii migogoro kati ya wananchi na hifadhi ambayo imekuwa inaendelea kwa muda mrefu.

**MWENYEKITI:** Ahsante, jibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Maliasili na Utalii.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba migogoro hii ya maeneo ya hifadhi na vijiji imekuwepo kwa muda mrefu, na nadhani kama Mheshimiwa Mbunge anafahamu, wakati Mheshimiwa Rais anatoa maelekezo ya kutokuviondoa vijiji 366 ambavyo vinapakana na hifadhi. Vijiji hivi havikuwa vimeanza migogoro miaka ya hivi karibuni vingine vipo vimesajiliwa tangu miaka ya 70.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Tume Maalumm iliyoundwa na Serikali kupitia jambo, hili imegundua kuna vitongoji zaidi ya 800 ambayo vina migogoro pamoja na hifadhi zetu za taifa. Kwa hiyo, nimuombe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba ushauri wake huu wa kutumia ramani ambayo ilipendekezwa na watu wa TANAPA tumeupokea, lakini pia tuendelee kusubiri maelekezo ya Tume Maalum iliyoundwa kumaliza kabisa migogoro hii ya hifadhi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Njalu.

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Pamoja na Serikali kuendelea kutatua mgogoro wa hifadhi, uko mgogoro mkubwa kando kando ya mapori yetu wanyama wakali tembo kusababisha vifo kwenye maeneo ya Mwalali, Kuyu na Matongo. Serikali ina mkakati gani sasa kutatua mgogoro mkubwa huu kwa sababu tembo wanaendelea kuzaliana, na wanaleta madhara makubwa katika maeneo yetu? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Kanyasu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nikiri kwamba baada ya Serikali kungeza juhudi za ulinzi wa hifadhi na kudhibiti majangili, limekuwepo tatizo la wanyama wengi sasa kuanza kuvamia maeneo ya vijiji na maeneo mengi ambayo taarifa tumezipokea ni kwamba, wanyama kama tembo na wanyama wengine wamevamia mashamba na kuna maeneo ambayo wamesababisha vifo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ambayo Wizara imechukua, kwanza tumeimarisha kikosi chetu cha ulinzi lakini tunaelekea sasa kuanzisha vituo maalum kwa ajili ya ulinzi kwenye kanda. Katika maelekezo ambayo tumeyatoa, maeneo mbalimbali tuliyokwenda tumezielekeza halmashauri zote ambazo zinapakana na maeneo ya hifadhi kuhakikisha kwamba katika maombi yao ya watumishi wanaajiri Maafisa Wanyamapori ambao wataweza kufika kwenye maeneo yenye migogoro kabla sisi askari wetu hawajafika.

**MWENYEKITI:** Wageni walipo Bungeni asubuhi hii, wageni walipo Jukwaa la Mheshimiwa Spika, tuna wageni 33 wa Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako, Mbunge, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia ambao ni viongozi wa Wizara hiyo na Taasisi zilizo chini yake wakiongozwa na Dkt. Leonard Akwilapo, Katibu Mkuu pamoja na Prof. James

Mdoe, Naibu Katibu Mkuu; Dkt. Ave-maria Semakafu, Naibu Katibu Mkuu; Prof. John Kondoro, Mwenyekiti wa Bodi ya *NACTE*; Profesa William Anangisye, Mwenyekiti wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu na Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. (*Makofi*)

Yupo pia Profesa Makenya Maboko, Mwenyekiti wa Bodi ya *COSTECH*; tunae pia Profesa Bernadeta Killian, Mwenyekiti wa Bodi ya Tanzania *Institute of Education (TIE)*; Prof. Jacob Mtabaji, Mwenyekiti wa Bodi ya *TCU*; Profesa Maurice Mbagao, Mwenyekiti wa Bodi ya *TEA*; Ndugu Peter Maduki, Mwenyekiti wa Bodi ya *VETA*.

Wageni wengine ni Dkt. Lyabwene Mtahabwa, Kamishina wa Elimu; Profesa Raphael Chibunda, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (*SUA*); Profesa Faustine Bee, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha (*UDOM*); Profesa Evaristo Liwa, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Ardhi; Profesa Andrea Pembe, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha *MUHAS*; Profesa Lughano Kusikula, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Mzumbe. Prof. Elifas Bisanda, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania; Profesa Emmanuel Luoga, Makamu Mkuu wa Chuo na Taasisi ya Nelson Mandela Sayansi na Teknolojia.

Wengine ni Prof. Lesakit Mellau, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere; Ndugu Abdu-Razak Badru, Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu; Dkt. Charles Musonde, Katibu Mtendaji *NECTA*; na pia tunaye Profesa Charles Kihampa, Katibu Mtendaji – *TCU*, wameambatana na viongozi na Maafisa wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo.

Kundi la kwanza ni *Development Partners* wakiongozwa na Mwenyekiti Ndugu John Lusingu. Wengine ni Zebedayo Kyomo – Canada, Ndugu Pantalee Kapich – *UNICEF*, Ndugu Helena Reutesward – *SIDA Sweden*, Faith Shayo – *UNESCO*, Mathus Nkaiga – Mwakilishi wa *World Bank* nchini na Ndugu Christine Djondo – *Co-Chair*.

Kundi la pili tuna Shehe Khamis Ally; halafu tuna *Teachers Union* wakiwakilishwa na Ndugu Prosper Lubuva.

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako, ambao ni familia yake kutoka Jijini Dar es Salaam; Ndugu Dajos Alimosa na Ndugu Benjamin Ndalichako. (*Makofi*)

Tuna wageni wengine 26 wa Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako ambao ni viongozi wa Serikali ya Wanachuo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (*DARUSO*) wakiongozwa na Ndugu Amradi Mlowola. Karibuni sana wageni wetu wa kundi hilo. (*Makofi*)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge tuna wageni wanane wa Mheshimiwa Goodluck Mlinga kutoka Shirika la *Women Action Towards Economic Development* wakiongozwa na Ndugu Maria Matui. Karibuni sana.

Tuna wageni 24 wa Mheshimiwa Japhary Michael ambao ni Waheshimiwa Madiwani na viongozi wa CHADEMA kutoka Manispaa ya Moshi, wakiongozwa na Mheshimiwa Mstahiki Meya Raymond Mboya. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tuna wageni sita wa Mheshimiwa Joseph Selasini, ambaye ni Katibu wa CHADEMA Kata ya Makiidi, kule Rombo, Kilimanjaro Ndugu Felix Mtenga. (*Makofi*)

Tuna wageni 64 wa Mheshimiwa Suzan Lyimo ambao ni wanafunzi wa Udaktari kutoka Chuo cha *St. Joseph* cha Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Semeni Muyenjwa. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tuna wageni wawili wa Mheshimiwa Khadija Nassir, ambao ni wapiga kura wake kutoka Kusini Unguja, Ndugu Almira Hamad na Ndugu Shadida Aley. Karibuni sana.

Wageni watatu wa Mheshimiwa Zainab Katimba, ambao ni jamaa zake kutoka Mkoani Kigoma; Diwani wa Kata ya Mwanga Kusini Mheshimiwa Mussa Maulid, Ndugu Alhaj Yusuf Juma na Ndugu Ezelia Joseph. (*Makofi*)

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Phillip Mulugo kutoka Umoja wa Shule Binafsi (*TAMONGSCO*) kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania wakiongozwa na Katibu wa chama hicho, Ndugu Shukrani Gideon. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, ambaye ni mdogo wake kutoka Jijini Mbeya, Ndugu Yohana Mwabulili. (*Makofi*)

Wageni waliopo Bungeni kwa ajili ya mafunzo; tunao wanafunzi 109 na walimu 10 kutoka Shule ya Sekondari Dodoma ambao wamekuja kujifunza jinsi Bunge linavyoendesha shughuli zake. Karibuni sana wanafunzi na Walimu wetu. (*Makofi*)

Tangazo; Matokeo ya mechi za Bunge *Sports Club*. Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* Mheshimiwa William Ngeleja anapenda kuwajulisha hayo yaliyowasibu kwamba tarehe 26 Aprili, majuzi, siku ya Muungano timu ya soka ya *Bunge Sports Club* ilitoa jasho timu ya Baraza la Wawakilishi. Mechi hiyo ilichezeshwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa Majaliwa akisaidiwa na washika bendera (*linesmen*) Mheshimiwa Job Ndugai, Spika wa Bunge na Mheshimiwa Zuberi Maulid, Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

Matokeo yalikuwa sare; kufungana magoli matatu kwa matatu na magoli ya *Bunge Sports Club* yalifungwa na kocha mchezaji Mheshimiwa Venance Mwamoto na Mheshimiwa Cosato Chumi. Nyota wa mchezo alikuwa ni Mheshimiwa Hamza Hassan, Kapteni wa Timu ya Baraza la Wawakilishi. (*Makofi*)

Jana kulikuwa na michezo ya timu ya *Netball* ya *Bunge Sports Club* ya *Bunge Queens* iliyoifunga *UDOM*

magoli 15 kwa tatu. Timu ya Soka, *Ndugai Boys* walienda sare magoli matatu kwa matatu na *UDOM*. Mgeni Rasmi katika michezo hiyo alikuwa Mheshimiwa Mama Salma Kikwete. Magoli ya *Bunge Queens* yalifungwa na Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Ester Matiko na Mheshimiwa Anna Lupembe. Nyota wa mchezo huo alikuwa ni Mheshimiwa Grace Kiwelu. Kwa hiyo, hawa watatu nitawahitaji sana leo jioni baada ya kusitisha shughuli za Bunge nikawape pongezi. *(Makofi)*

Kwa upande wa magoli ya soka, yalifungwa na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, magoli mawili na Mheshimiwa Pascal Haonga; goli moja na nyota wa mchezo alikuwa golikipa wetu mahiri Mheshimiwa Dkt. Dismas Ndumbaro. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mwenyekiti anawashukuru sana Waheshimiwa Maspika wetu, Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Wabunge wote na wananchi ambao walipata nafasi ya kufika na kuunga mkono timu zetu.

Waheshimiwa Wabunge, mtaona leo Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano hayupo hapa; na kwa mujibu wa Kanuni zetu, kama hayupo nafasi hiyo huwa inashikiliwa na kiongozi mwingine. Leo nataka niwajulishe kwa kipindi ambacho Mheshimiwa Waziri Mkuu hatakuwa na sisi hapa Bungeni, shughuli hiyo itafanywa na Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. *(Makofi)*

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Hukwenda Mbeya? Au wewe unatoka Iringa, kweli.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natoka Iringa.

**MWENYEKITI:** Haya, mwongozo Mheshimiwa Mch. Msigwa.



## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nimesimama kwa Kanuni ya 64(f) ambayo pamoja na mambo mengine...

**MWENYEKITI:** Kanuni ya 64!

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

**MWENYEKITI:** Aaah, hapana bwana. Wewe ni Mbunge mzoefu sana.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 64(1)(f). Kanuni (f) inasema, hatamsema vibaya; imeeleza mambo mengine lakini inasema; hatamsema vibaya au kutoa lugha za matusi...

**MWENYEKITI:** Tuvumiliane tu Mheshimiwa. Nitakuvumilia useme, lakini mnanisumbua sana kwa sababu mwongozo, wote sasa tumejifunza unaombewa kupitia Kanuni ipi?

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Mwongozo kwa Kanuni ya 68(7).

**MWENYEKITI:** Kanuni ya 64 ina masuala yanayokatazwa na Kanuni zetu kufanyika humu Bungeni. Sasa leo hapa nini kimetokea? Endelea, lakini mnielewe.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekusikiliza, nimekuelewa vizuri. Nimezingatia hiyo Kanuni ya 68(7) lakini nikisoma pamoja na 64(f) mambo ambayo yamekatazwa kuzungumzwa ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani akihitimisha hoja yake alisimama ndani ya Bunge na kuwaambia Watanzania kuwa hajawahi kuona mtu mwongo kama *CAG*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili siyo tu linaondoa mamlaka ya Bunge na kulifanya Bunge lisiwe na nguvu tusipofanya kazi yake inapopaswa, lakini jambo hili ni kinyume kabisa na Katiba kwa sababu CAG anafanya kazi kwa mujibu wa Katiba. Kwa mujibu wa Katiba yetu, CAG sio mtu, ni Taasisi; na CAG sio *thief catcher*, kazi yake siyo kukamata wezi. Kazi ya CAG akishaleta taarifa Bungeni ambaye ni jicho letu, anahakikisha hizi Kamati tulizoziweka zenyewe ndiyo zinakwena ku-*verify*. Katibu Mkuu ndiyo ana-*verify* anatoa majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha Waziri wa Mambo ya Ndani kusimama hadharani siyo tu amelishalisha Bunge, amemdhallilisha na CAG na anamfanya asifanye kazi yake inavyapaswa ili sisi tuweze kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako, Bunge letu limekuwa likilaumiwa kwamba ni Bunge dhaifu linavyoingiliwa hivi: Je, hii ni haki kwa Waziri wa Serikali kusimama hadharani na kumwita CAG ni mwongo katika hesabu ambazo kwanza CAG alishazifunga? Kama Serikali ina shida, inatakiwa iende ikajibu kwenye Kamati yetu ya PAC.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Bunge letu liwe imara, lizidi kuheshimiwa nchini, lionekane lina nguvu, naomba utoe mwongozo wako ili tuweke vitu sawa, tusiharibu mambo kikatiba kwa mujibu wa Katiba ya nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Nasimama kwa shingo upande kabisa. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, naendelea kuisitiza, tuzingatia Kanuni zetu. Hilo ambalo umeliombea mwongozo ambao nasema haupo, sijaomba mwongozo rasmi hapo kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7), lakini kwa vile ni suala ambalo umelisemea kwa nguvu sana, nasema hivi, Kanuni zetu zinaelekeza namna ya taarifa zinazowasilishwa Bungeni

ikiwepo Taarifa ya CAG zinavyoweza kushughulikiwa na Taarifa ya CAG tayari imeshawasilishwa Bungeni.

Kwa mujibu wa Kanuni zetu, siku ile niliwakumbusha, wengine mligunaguna, nikawaambia ikishawasilishwa mezani kwa mujibu wa Kanuni zetu, inaenda kwenye Kamati zetu husika mbili, yaani PAC na LAAC. Juzi Mheshimiwa Spika, akalifafanua vizuri suala hili kwamba hata wale ambao wana haki, maana *document* ikishawasilishwa mezani, inakuwa *available* kwenye *public domain*, inapatikana kwa Umma wanaweza wakasema waliyonayo. Walisema, kama wana kitu cha maana wataenda kuisaidia Kamati husika.

Huo ndiyo utaratibu ambao ningependa sana ufuatwe. Hiyo inajumuisha pia Wizara husika ambazo zitakuwa zimeguswa na Ripoti ya CAG, maana na wenyewe watatoa majibu yao, wataenda kujieleza mbele ya Kamati hiyo. Kama majibu yataridhisha, watasema sawa na hoja hiyo itakuwa imefungwa.

Kwa hiyo, nataka nisisitize kwamba tuzingatie tu kanuni zetu. Hili najumuisha pia na upande wa Serikali kwamba lazima tutambue kwamba tunaongozwa na Kanuni na taarifa zetu pia zinazowasilishwa mbele ya Kamati husika tuna-*process* ya kwenda kuyasema yale ambayo tunaamini yanapaswa yakasemwe huko.

Sasa mengine yaliyosemwa *last week* mimi sitaki kufika huko. Wataenda kuthibitisha kama ni kweli au siyo kweli watakapofika mbele ya Kamati husika.

Katibu.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, haya.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) jambo ambalo

limetokea Bungeni mapema ambalo Mheshimiwa Msigwa amesema, ni kutaka kuomba Mwongozo wako ili kuweka mambo sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe ile mimi nilikuwa nimewasilisha hoja ya Hotuba ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na katika hoja ile, Waheshimiwa Wabunge walipewa fursa ya kutoa michango yao kwa kusema ama kwa maandishi. Katika michango waliyoitoa, hususan Wabunge wa upande wa Upinzani walikuwa wakitaka mtoa hoja, yaani mimi Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi niwape majibu kuhusiana na Taarifa ya CAG kwamba kuna ufisadi Jeshi la Polisi wa sare hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama mtoa hoja, baada ya kusikiliza hoja zote za Wabunge, Kanuni zinanitaka sasa katika kuhitimisha nitoe majibu yale ambayo walikuwa wanataka nitoe. Kwa hiyo, mimi nilikuwa nawajibu Waheshimiwa Wabunge hoja zao. Katika kuwajibu hoja zao ambazo walikuwa wanasema kwenye hoja yao kwamba kuna sare hewa Jeshi la Polisi, ndiyo nikawaeleza bayana bila kuficha kwamba Jeshi la Polisi halijawahi kuwa na manunuzi hewa na kwamba sare hizo zimejaa kwenye makontena na maghala ya Polisi; na nikasema bayana kwamba Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, kaa tu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** ... na hapo ndiyo nilisema CAG ni mwongo na kweli ni mwongo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Hapana, kaa chini. Waheshimiwa Wabunge, nikisimama, mnajua maana yake.

Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, mwongozo wangu, narudia tena, tuzingatie Kanuni za Bunge. (*Makofi*)

Ukweli wa suala hilo utaenda kufahamika mbele ye Kamati husika. Naomba tusiyawahishe mambo, tusiwe *judgmental*, wewe umeshafunga hoja yako, imeshamalizika, *process* inayofuata ni ile niliyoeleza kwa mujibu wa kanuni za Bunge, yote yataenda kuwekwa vizuri huko kwenye kamati. (*Makofi*)

Niambie aliyesema kuhusu utaratibu, unanihusu mimi, nakuruhusu sasa kuhusu utaratibu.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasimama Kuhusu Utaratibu kwenye jambo ambalo umeshalitolea mwongozo. Kwa sababu anaendelea kusema *CAG* ni mwongo....

**MWENYEKITI:** Basi kaa chini.

Katibu!

**NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI:**

### HOJA ZA SERIKALI

#### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 - Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

**MWENYEKITI:** Ahsante, mtoa hoja. Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako, una muda usiozidi saa moja kuwasilisha hoja yako, karibu.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kufuatia taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu, likubali kupokea na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka 2018/2019.

Aidha, naliomba Bunge lako lijadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kwa kuniwezesha kusimama tena mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka 2019/2020. Napenda kumpongeza kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa uongozi wake makini uliotukuka na kwa ujasiri alionao katika kufanya maamuzi yenye tija kwa maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa kwa uongozi wao thabiti na kwa miongozo mbalimbali wanayoitoa ambayo imeendelea kuwa chachu katika kuboresha utendaji wa Serikali ya Awamu ya Tano. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuongoza vyema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Spika wa Bunge, Mheshimiwa Job Yustino Ndugai na Naibu Spika Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu kwa kulingoza Bunge hili kwa busara, hekima na kwa weledi wa hali ya juu. Nawapongeza pia Wenyeviti wa Bunge kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuongoza kwa ufanisi mijadala ndani ya Bunge letu Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa shukrani za dhati kabisa kwa Kamati ya Kudumu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii inayoongozwa na Mwenyekiti Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Juma Nkamia kwa kuendelea kutoa ushirikiano mkubwa kabisa kwa Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru pia kwa dhati familia yangu kwa kuendelea kunipa ushirikiano wa dhati unaoniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya Kitaifa kwa utulivu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sasa naomba nitoe taarifa ya utelekezaji wa kazi za Wizara kwa mwaka 2018/2019 na nitaanza na kuelezea bajeti iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2018/2019 Bunge lako Tukufu liliidhinisha jumla ya shilingi 1,407,136,481,000.00 kwa ajili ya Fungu 46 - Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Fungu namba 18 la Tume ya *UNESCO*. Kati ya fedha hizo kiasi cha shilingi 1,406,469,626,000.00 kilikuwa ni kwa Fungu 46 ambapo shilingi 476,500,224,000.00 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya Kawaida na shilingi 929,969,402,000.00 zilikuwa ni za miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nijielekeze kwenye maduhuli ya Fungu 46, Wizara ilikadiria kukusanya jumla ya shilingi 460,011,442,840.89. Hadi kufikia tarehe 15 Aprili, 2019, Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya shilingi 360,108,828,063.37 sawa na asilimia 78.3 ya makadirio. Naomba nichukue nafasi hii kuzipongeza Taasisi zilizofikia malengo na kutoa wito kwa Taasisi ambazo bado hazijafikia malengo kuongeza kasi ya kukusanya maduhuli ili tuweze kufikia malengo tunapofunga mwaka Juni, 30, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Matumizi ya Kawaida hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2019, Wizara ilikuwa imepokea Jumla ya shilingi 348,485,307,415.38 ambayo ni sawa na asilimia 73.1 ya bajeti ya Matumizi ya Kawaida na

katika Matumizi ya Miradi ya Maendeleo, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2019, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi 597,341,693,915.11 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, ambayo ni sawa na asilimia 64.2 ya bajeti iliyotengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi kuishukuru sana Serikali ya Awamu ya Tano, ambayo ikiahidi inatekeleza. Ukiangalia upatikanaji wa fedha ni kwa kiwango cha hali ya juu kabisa na na naamini kwamba, mpaka kufunga mwaka mwezi Juni, fedha ambazo zimebaki zitaendelea kutolewa, naishukuru sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nijielekeze kwenye Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa mwaka 2018/2019 na nitaomba nianzie na usimamizi wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Wizara imeendelea kuimarisha utoaji wa mafunzo katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Katika mwaka 2018/2019, Serikali imeendelea na ukarabati wa awamu ya kwanza unaohusisha Vyuo 20 vya Rubondo, Gera, Munguri, Chisalu, Newala, Kilwa Masoko, Ikwiriri, Mtawanya, Handeni, Mto wa Mbu, Urambo, Kasulu, Tarime, Ilula, Muhukuru, Sofi, Chilala, Kiwanda, Malampaka na Karumo. Ukarabati uko katika hatua ya umalizaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maandalizi ya awamu ya pili ya ukarabati imeanza mwezi huu wa Aprili, 2019 na inahusisha Vyuo 20 vya Ngara, Msinga, Kisangwa, Mamtukuna, Malya, Same, Sengerema, Ifakara, Kilosa, Kihinga, Msaginya, Mputa, Nandembo, Bariadi (kwako Mheshimiwa Mwenyekiti), Masasi, Sikonge, Chala, Kibondo na Katumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya tatu ambayo ukarabati wake utanza mwezi Juni, 2019, utahusisha Vyuo vya Bigwa, Nzovwe, Mwanva, Ulembwe, Njombe, Mbinga, Singida, Tango, Mwanhala, Nzega, Kisarawe, Arnautoglu, Musoma na Buhangija.



Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendeleza Sayansi, Teknolojia na Ubunifu, Wizara imeandaa rasimu ya mapitio ya Sera ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu, na imekamisha maandiko ya utekelezaji wa Mradi wa *EASTRIP* ambao unalenga kuanzisha Vituo vya Umahiri katika Ufundi katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam kwa Kampasi za Dar es Salaam na Mwanza, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji na Chuo cha Ufundi Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Mradi wa Kukuza Stadi za Kazi na Ujuzi, Wizara imejengea uwezo Taasisi 16 za mafunzo kwa kutoa ruzuku yenye thamani ya shilingi 3,481,702,271.95.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Ithibati na Uthibiti wa Shule, Wizara imesajili jumla ya shule 363 kati ya shule shule 378 zilizomba usajili na imehuisha Mwongozo wa Usajili wa Shule kukidhi mahitaji ya jamii ya sasa. Aidha, hadi kufikia Machi, 2019, Wizara ilikuwa imefanya ufuatiliaji katika Asasi 6,966 sawa na asilimia 61.3 ya lengo na ufuatiliaji unaendelea kwa kasi . Tunaamini asilimia hii itaendelea kupanda mpaka tutakapofikia mwisho wa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usimamizi wa Elimumsingi; katika kusimamia Elimu ya Msingi na Sekondari, Wizara imetoa Waraka wa Elimu unaohusu Utaratibu wa Uundaji na Uendeshaji wa Kamati na Bodi za Shule na Waraka wa Elimu unaohusu Utaratibu wa Kukariri Darasa kwa Wanafunzi wa Shule za Msingi na Sekondari. Imeandaa zana za kuwezesha Walimu kuwabaini wanafunzi wenye vipaji na kuweka mipango ya kuwaendeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usimamizi wa Elimu Maalum; Wizara imeendelea kusimamia utoaji wa Elimu Maalum ili kuhakikisha watoto wote wanapata elimu iliyo bora na katika mwaka 2018/2019, imeandaa Mkakati wa Taifa wa Elimu Jumuishi wa mwaka 2018 - 2021 ili kuwawezesha wadau wa elimu kuimarisha utoaji wa elimu bora kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usimamizi wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi; Wizara imeratibu upatikanaji wa vifaa vya kisasa na vya kutosha kabisa vyenye thamani ya Shilingi bilioni 15 kwa ajili ya Chuo cha Ufundi cha Arusha na vifaa hivyo vimeshapokelewa na tayari vimefungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usimamizi wa Elimu ya Juu; Wizara imeratibu *scholarship* za masomo nje ya nchi ambapo, wanafunzi 153 wa Kitanzania wamepata fursa hizo. Pia imeratibu *scholarship* za Jumuiya ya Madola, China na Hungary kwa mwaka 2019/2020 na kwa sasa mamlaka husika zinaendelea na taratibu za uteuzi kwa kuzingatia vigezo na masharti yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usimamizi wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu; Wizara imeandaa na kuzindua Mwongozo wa kutambua na kuendeleza Ugunduzi, Ubunifu na Maarifa Asilia nchini, imeandaa na kuendesha Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu kwa lengo la kuwatambua na kuwaendeleza wabunifu na wagunduzi mahiri hapa nchini. Imekagua utekelezaji wa miradi saba inayotumia teknolojia ya nyuklia katika Sekta za Maji, Afya, Kilimo na Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali Watu wa Wizara; Wizara imeendelea kuimarisha udhibiti na usimamizi wa Rasilimali na katika kufanya hivyo imekagua malipo ya mishahara ili kubaini uhalali wa watumishi na kuondoa uwezekano wa kulipa mishahara kwa wafanyakazi hewa. Imekagua utekelezaji wa mikataba 22 na imeendelea na ukaguzi maalumu katika Chuo cha Ualimu Ilonga na Patandi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nijielekeze katika Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara ya Elimu na kutokana na muda sitaweza kueleza kazi kubwa na nzuri ambazo zimefanywa na Taasisi hizo zote kwa urefu wake, lakini naomba hotuba yangu yote iingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya utekelezaji wa kazi za Taasisi na Vyuho vya Elimu ya Juu ambavyo vinawajibika katika kufanikisha katika utoaji wa elimu bora nchini pamoja na kuendeleza sayansi, teknolojia na ubunifu yanapatikana katika ukurasa wa 29 hadi ukurasa wa 101 wa kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naendelea kusema kazi iliyofanyika ni kubwa na ningepomba Waheshimiwa Wabunge wapitie hotuba yangu waone kazi nzuri ambayo Serikali imefanya. Naomba nieleze tu kwa kifupi baadhi ya kazi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na Taasisi ya Elimu Tanzania, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Taasisi ya Elimu Tanzania imetekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Imeandika na kusambaza jumla ya nakala 391,949 za vitabu vya somo la *English* Kidato cha Kwanza na cha Pili;

(ii) Imesambaza vitabu vya kiada nakala 6,286,476 kwa wanafunzi wa Darasa la Nne;

(iii) Imesambaza nakala 7,835,697 za aina 25 za vitabu vya Hadithi kwa ajili ya Darasa la Kwanza na la Pili na hapa lengo letu ni kujenga umahiri wa watoto wa darasa la kwanza na la pili kusoma kwa kasi inayokusudiwa.

(iv) Vilevile Taasisi imeanza kurusha hewani kipindi cha Vikaragosi (*Cartoons*) ambacho kinaitwa Nyota Njema kupitia *Television* ya Taifa *TBC* kwa ajili ya kukuza stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu.

(v) Pia taasisi imeandaa Maktaba Mtandao itakayorahisisha usambazaji wa machapisho mbalimbali ya Taasisi; na

(vi) Imeboresha mihtasari ya masomo ya michepuo ya Ufundi, Kilimo na Sayansi Kimu kwa lengo la kuimarisha ufundishaji wa masomo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze sasa kwenye Baraza la Mitihani:-

(i) Baraza hili limeendelea na kazi yake ya upimaji na uendeshaji wa mitihani ya Taifa katika ngazi mbalimbali; na

(ii) Vilevile limenunuja mashine sita za kisasa zinazotumika kuandaa na kuchapa mitihani na vyeti vya wahitimu na hii kwa kweli imeongeza sana ufanisi katika utendaji wa Baraza letu la Mitihani la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu; Wakala huu, pamoja na majukumu mengi yaliyofanyika, umetoa Mafunzo kwa Walimu 1,545 wa Darasa la Kwanza na la Pili kuhusu kuimarisha Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima imekamilisha rasimu ya Mkakati wa Kitaifa wa Kisomo na elimu kwa umma unaolenga kuleta ufanisi katika utekelezaji wa programu za kisomo hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania; Bodi ya Huduma za Maktaba imewezesha upatikanaji wa vitabu 41,964 na imetoa ushauri wa kitaalam kuhusu uendeshaji wa Maktaba katika Wilaya za Sikonge, Tunduma, Mpwapwa, Hai na Nachingwea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi; Mamlaka hii imetekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Imeanza ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi vya Mikoa ya Rukwa na Geita;

(ii) Imekamilisha manunuzi kwa ajili ya Ujenzi wa Chuo cha Mkoa wa Simiyu;

(iii) Inaendelea na mchakato wa kumpata Mkandarasi mwingine ili kuendelea na ujenzi wa VETA Mkoa wa Njombe baada ya Mkandarasi wa awali aliyekuwa amepewa kazi kushindwa kufanya kazi hiyo; Wizara imefuta mkataba wake kwa hiyo tunakamilisha upatikanaji wa mkandarasi mwingine.

(iv) Imekamilisha matayarisho ya eneo kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi Mkoa wa Kagera ambapo ujenzi utaanza rasmi tarehe Mosi, Julai 2019, kwa msaada wa Serikali ya Watu wa China;

(v) Imekamilisha ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya Namtumbo na ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli, ambaye alizindua rasmi chuo hicho mnamo tarehe 5 Aprili, 2019.

(vi) VETA inaendelea na ujenzi na ukarabati wa Vyuo vya Ufundi Stadi katika wilaya mbalimbali ikiwa ni pamoja na Wilaya ya Ileje, Nkasi, Muleba, Urambo, Makete, Karagwe pamoja na Chato; na

(vii) Imekamilisjha maandalizi ya michoro na zabuni kwa ajili ya ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi vya Wilaya ya Kilindi na Korogwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Baraza la Taifa la Ufundi, Baraza limetoa mafuzo juu ya mitaala inayozingatia umahiri kwa wakufunzi 256 na limekagua ubora wa Rasilimali watu katika vyuo 26 na limefanya tathmini ya ulinganifu wa tuzo 180.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Elimu Tanzania, Mamlaka hii imeendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa nyumba 60 za Walimu, madarasa 252 na mabweni 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu; Bodi imepanga na kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi 424,758,636,617 kwa wanafunzi 122,754 na kati ya wanafunzi hao wanufaika 41,234 ni wa mwaka wa kwanza na wanufaika 81,520 ni wanaondelea na masomo. Hadi kufikia tarehe tarehe 15 Aprili, 2019, Bodi ya Mikopo ilikuwa imekusanya mikopo iliyoiva yenye thamani ya shilingi 128,076,510,388 ambayo ni sawa na na asilimia 81 ya lengo la makusanyo ya Shilingi Biloni 157.7 kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nijielekeze kwenye Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania; Tume hii:-

(i) Imeratibu udahili kwa wanafunzi waliojiunga na masomo kwa mwaka 2018/2019;

(ii) Imefanya ukaguzi kwa vyuo 21 kwa lengo la kuhakiki ubora wake; na

(iii) Imefanya Maonyesho ya 13 ya Elimu ya Juu ambayo yalikusisha jumla ya Taasisi 75 za ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (*COSTECH*); katika kipindi cha mwaka 2018/2019, Tume hii:-

(i) Imeendelea kufadhili na kusimamia miradi ya utafiti yenye thamani ya shilingi Biloni 3.581;

(ii) Imewawezesha wabunifu 30 jumla ya Shilingi Biloni moja na milioni 24 ili kuendeleza ubunifu wao;

(iii) Imeanzisha na kufadhili vituo atamizi 17 vilivyogharimu kiasi cha Shilingi milioni 740.9 kwa ajili ya kukuza na kuendeleza ubunifu;

(iv) Imewajengea uwezo watafiti 57 kutoka Vitengo vya Utafiti vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Taasisi ya Utafiti wa Afya ya Zanzibar;

(v) Imeendelea na ujenzi na ukarabati wa Maabara za Taasisi za Utafiti wa Mifugo za Tanga na Uyole na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi ya *SOTA* Musoma; na

(vi) Imetoa fedha kiasi cha Sh.1,771,953,960 kwa ajili ya miradi mipya minane ya ukarabati wa miundombinu ya utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Nguvu za Atomiki. Tume imekamilisha ujenzi wa maabara kwa ajili ya kupima mionzi. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu mimi ninapoendelea na kazi ya kutoa hotuba kwenye Bunge, Mheshimiwa Waziri Mkuu yuko Arusha akiwa anaizindua maabara hiyo ambayo itaongeza ufanisi wa kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume imesajili vituo vipya 101 kwa ajili ya kuanza kutumia vyanzo vya mionzi; imepima wafanyakazi 1,663 kutoka katika vituo 376 na ilipima jumla ya sampuli 12,628 ambazo zote zilibainika ziko salama hazikuwa na mionzi hatarishi. Vilevile Tume ya Nguvu za Atomiki imefungua Ofisi ya Kanda ya Ziwa Jijini Mwanza na Ofisi nyingine ndogo saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nijielekeze katika Chuo Kikuu cha Dar es Salam. Chuo hiki kimefanya miradi ya utafiti 135; kimetoa machapisho 381 katika majarida mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa; na kimenunua nakala 6,927 za vitabu zenye thamani ya Sh.1,078,000,000 ambavyo vimewekwa kwenye maktaba mpya na ya kisasa kabisa ambayo ina uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,500 kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chuo pia kimeendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa tano la Ofisi za Serikali ya Wanafunzi na Mshauri wa Wanafunzi na kimeanza ukarabati mkubwa wa mabweni Na. 2 na Na. 5 kwa gharama ya shilingi 4,900,000,000 ambao utaongeza nafasi za wanachuo 800. Tunaendelea kuimarisha mazingira ya vijana wetu kupata elimu ya juu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo. Katika kipindi cha mwaka 2018/2019, chuo kimeshirikiana na wadau mbalimbali katika kutoa mafunzo kwa wakulima na wafugaji wapatao 3,250 kwa lengo la kuongeza tija katika sekta ya kilimo na mifugo. Chuo pia kimeendelea na tafiti za miradi 28 mipya; kimetoa mafunzo ya uwelewa wa matumizi ya panya katika kugundua ugonjwa wa kifua kikuu kwa watumishi wa afya 264; na kimeendelea na ujenzi wa maabara mtambuka yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,600 kwa wakati mmoja. Vievile kimefanya ukarabati wa miundombinu mbalimbali ikijumuisha hospitali pekee ya Rufaa ya Wanyama ya Taifa iliyopo katika Ndaki ya Tiba ya Mifugo na Sayansi za Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili. Chuo hiki kimeendelea na ujenzi wa Kituo Mahiri cha Magonjwa ya Moyo na Mishipa (*Center of Excellence in Cardiovascular Sciences*) ambao upo katika hatua ya umaliziaji. Pia kimeanzisha miradi mipya ya kitafiti 35 na kimeendelea kufanya tafiti zenye manufaa katika kuboresha huduma za afya hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Ardhi. Chuo kimepitia na kuboresha mitaala 32 na kuandaa rasimu za mitaala mipya 15; kimefanya tafiti katika miradi 76 kwenye maeneo ya usimamizi wa ardhi na kimetoa huduma 48 za ushauri wa kitaalam katika matumizi bora ya ardhi, upimaji na tathimini, usanifu majengo na ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu Dodoma. Chuo kimetoa huduma 11 za ushauri kwenye sekta za elimu, biashara, uwekezaji, *TEHAMA* na afya; kimegharamia masomo kwa watumishi 422 ambapo watumishi 284 wanasoma Shahada ya Uzamivu. Tumedhamiria na tunatekeleza kwa vitendo suala la kukabiliana na changamoto za upungufu wa Wahadhiri katika vyuo vyetu vikuu. Aidha, chuo kimeongeza idadi ya tafiti kutoka 27 hadi kufikia 37.



Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nijielekeze Chuo Kikuu Mzumbe. Chuo kimeendelea na ujenzi wa jengo la utawala na madarasa katika Kampasi ya Mbeya na tunategemea Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ataenda kuweka jiwe la msingi katika ujenzi huu mnamo tarehe 1 Mei, 2019. Chuo pia kimefadhili jumla ya watumishi 28 wa Shahada ya Uzamivu na watumishi 18 wa Shahada za Uzamili; kimetoa mafunzo ya ujasilliamali kwa wadau mbalimbali wapatao 400 ili kuwawezesha kuinua kipato na kujiongezea uchumi wao. Vilevile chuo kimeendelea na ujenzi wa hosteli nne katika Kampasi Kuu zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,024. Niseme tu kuwa uwekezaji tunaofanya katika Chuo Kikuu cha Mzumbe haijawahi kutokea tangu mwaka 1972 kuwa na uwekezaji mkubwa wa namna hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi. Chuo kimeendelea kuwajengea uwezo viongozi, wanachama na watendaji wa Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo Vijijini pamoja na Vyama vya Ushirika wa Mazao. Pia kimeratibu mafunzo kuhusu elimu ya ushirika, ambapo jumla ya walengwa 3,179 walinufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Chuo kimeendesha warsha ya utafiti kwa Maprofesa 12 iliyolenga kubuni miradi mikubwa kwa ajili ya chuo. Pia kimepata Kigoda cha *UNESCO* katika Elimu ya Ualimu na uendeshaji mitaala. Nawapongeza sana Chuo Kikuu Huria kwa heshima hiyo ya kupata Kigoda cha *UNESCO*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius Nyerere cha Sayansi na Teknolojia. Chuo kimeendesha mafunzo kwa wakulima 455 kuhusu mbinu bora za kilimo na kimefadhili watumishi wanne wa Shahada za Uzamivu katika Taasisi ya Sayansi ya Teknolojia ya Nelson Mandela Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam. Chuo hiki kinaendelea na awamu ya

pili ya ujenzi wa jengo la utawala na ofisi za wafanyakazi ambao upo katika hatua nzuri na nashukuru Kamati ya Bunge hii ilikuwa ni mojawapo ya sehemu ambazo walipitia na wameona kazi nzuri inayofanywa na Serikali. Pia kimefanya jumla ya tafiti 12 na kimefanya kongamano la kitaifa kuhusu utokomezaji wa ukatili dhidi ya wanawake na watoto hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa. Chuo hiki kimegharimia masomo kwa watumishi 98; kimekamilisha tafiti saba endelevu na kimekamilisha ujenzi wa ukumbi wa mihadhara wenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,209 kwa wakati mmoja na ofisi 14 zenye uwezo wa kuchukua Wahadhiri 28.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha ufundi Arusha. Chuo kinajenga jengo la ghorofa tatu lenye maabara, ofisi na madarasa ambalo litaongeza udahili katika chuo hiki kwa wanafunzi 1,000. Pia kinaendelea na ujenzi wa kituo cha kupima mitambo midogo midogo ya kufua umeme kutokana na maji; ujenzi wa kituo kipya cha KIKULETWA cha kuzalisha umeme wa megawati 107 na kituo hiki kitatumika kama Kituo cha Mafunzo kwa Vijana kuhusu namna ya kuzalisha umeme. Chuo pia kinaendelea na kazi ya ujenzi wa miundombinu Oljoro kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo ya kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere. Chuo kimekamilisha na kuandaa gharama za ujenzi wa maktaba katika Kampasi ya Kivukoni na hosteli katika Kampasi ya Zanzibar. Vilevile kimekamilisha ujenzi wa jengo la mihadhara lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 324 kwa wakati mmoja na jengo hili limejengwa kwa kutumia mapato ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia, Mbeya. Chuo kimeunda gari dogo kwa ajili ya kubeba mizigo midogo midogo kwa lengo la kurahisisha kazi za uvunaji kwa wakulima; kimefanya ukarabati wa miundombinu ya Kampasi Rukwa ili kuiwezesha kuanza

kudahili wanafunzi wapya 200 katika fani ya Ufundi Mchundo kwa mwaka wa masomo 2019/2020. Vilevile chuo kinaendelea na ujenzi wa maktaba yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,500 kwa wakati mmoja. Ni maktaba kubwa ya kisasa na ya kipekee kabisa na tunategemea Mheshimiwa Rais ataenda kuiwekea jive la msingi mnamo tarehe 1 Mei, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie Taasisi ya Teknolojia, Dar es Salaam. Taasisi hii imewezesha wafanyakazi 57 kwenda masomoni na imeandaa mtaala kufundishia teknolojia ya bidhaa za ngozi katika ngazi ya Stashahada. Tunataka kuwajengea uwezo wakulima wetu katika kuongeza thamani ya bidhaa za ngozi. Kwa hiyo, naamini kwamba mtaala huu utakuwa na manufaa makubwa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie Taasisi ya Sayansi ya Teknolojia ya Nelson Mandela. Taasisi hii inaendelea kutekeleza miradi 33 ya utafiti na miradi hiyo imejikita katika maeneo ya kilimo na usalama wa chakula na inawezesha ufadhili wa wanafunzi katika fani mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nijielekeze katika utekeleji wa miradi ya maendeleo na utekelezaji huu unapatikana katika ukurasa wa 102 - 115 wa kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo. Programu hii inalenga kuimarisha ubora wa elimu nchini na katika mwaka 2018/2019, programu hii imewezesha ujenzi wa miundombinu katika shule 504, shule za msingi 219 na shule za sekondari 285 ambapo jumla ya fedha kiasi cha Sh.56,500,000,000 zilitumwa kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 938, mabweni 210, matundu ya vyoo 2,141, nyumba za walimu 39 ambazo ni *two in one*, kwa hiyo, zinaweza zinaweza zikaweka walimu 78, mabwalo 76 na huduma za maji katika shule kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kupitia Mradi wa Lipa Kulingana na Matokeo (*EP4R*), Wizara imeratibu ununuzi wa magari 20 kwa ajili ya vyuo vya ualimu na umeratibu ujenzi wa ofisi mpya 100 kwa ajili ya Wadhibiti Ubora wa Shule. Niruhusu hapa niweke msisitizo, Serikali imedhamiria kabisa kuboresha udhibiti ubora wa shule na kama ambavyo mnafahamu tuligawa magari 45 kwa ajili ya Wadhibiti Ubora wa Shule, tunakwenda kujenga ofisi 100 na nyingine zaidi tutazijenga katika mwaka wa fedha unaokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia mradi wa Lipa Kulingana na Matokeo, Serikali imejenga Shule ya Sekondari Maalum katika Chuo cha Ualimu cha Patandi, kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum ambayo ina uwezo wa kuchukua wanafunzi 640. Vilevile kupitia mradi huu tumegharimia mafunzo kwa wana taaluma 68 kwa lengo la kuongeza idadi wa Wahadhiri hapa nchi na hawa wote wanafanya masomo ya Uzamivu, kasoro wawili ndiyo wanafanya Uzamili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nijielekeze kwenye Programu ya Maendeleo ya Elimu Msingi. Programu hii inalenga katika kuimarisha stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu kwa ajili ya watoto wenye umri wa miaka mitano mpaka 13 walio ndani na nje ya mfumo rasmi. Mpango huu unafadhiliwa na Mfuko wa Ushirika wa Kimataifa wa Elimu (*Global Partnership in Education*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2018/2019 mradi umewezesha shughuli zifuatazo: Ukamilishaji wa mafunzo kwa walimu 402 wa Elimu Maalum Darasa la Kwanza mpaka la Nne na ukamilishaji wa mafunzo kwa walimu wa nyongeza 1,598 wanaofundisha Darasa la Kwanza hadi la Pili. Mradi huu katika mwaka huu wa fedha ulikuwa katika hatua ya kumalizia *phase one* na nafurahi kuliharifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali yetu iliandika andiko kwa ajili ya kuomba *phase two* ya mradi huu na *Global Partnership in Education* imeweza kuridhia mwanzoni mwa mwezi Aprili kiasi cha dola za Marekani milioni 90 kwa

awamu ya pili. Kwa hiyo, katika hotuba yangu nitaeleza kwa kirefu zaidi kazi kubwa ambayo itaendelea kufanywa na Mfuko huu wa *Global Partnership in Education*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie Mradi wa Kuimarisha Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi. Kupitia mradi huu tumefanya ukarabati katika Vyuo vya Ualimu vya Dakawa, Mpwapwa, Kleruu, Marangu, Tabora na Butimba na ukarabati huo umegharimu kiasi cha Sh. 5,450,000,000. Ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi vya Mikoa vya Simiyu kupitia mradi huu umegharimu kiasi cha Sh. 24,500,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie Mradi wa Ukarabati wa Vyuo vya Ufundi vya Ualimu ambao unagharimiwa na Serikali ya Canada kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania. Mradi huu unalenga kuinua ubora wa elimu ya ualimu na kuwawezesha Watanzania wengi zaidi kupata fursa za kujunga na mafunzo ya ualimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2018/2019 tumeendelea na ujenzi katika Chuo cha Ualimu cha Mpuguso, Shinyanga, Ndala na Kitangali. Nafurahi kwamba Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mnamo tarehe 3 Februari aliweza kufika katika Chuo cha Ualimu Kitangali na kuweka jiwe la msingi na tunategemea kesho tarehe 30 Aprili, atakwenda katika Chuo cha Mpuguso kuweka jiwe la msingi. Thamani ya mradi huu ni Sh.36,000,000,000, kwa hiyo, Serikali inafanya kazi kweli kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie Mradi wa Kuimarisha Mafunzo ya Elimu ya Ualimu. Kupitia mradi huo, Wizara imewezesha vyuo kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia ikiwa ni pamoja na vifaa vya maabara; imenunua na kusambaza *computer* 300 na *projector* 100 kwa ajili ya vyuo vya ualimu kuimarisha ufundishaji wa TEHAMA; imeendelea na taratibu za ununuzi wa *computer* nyingine 480, *UPS* 480, *photocopy heavy duty machine* 35 kwa ajili ya vyuo vyote vya ualimu nchini na *Laptops* 43 kwa ajili ya kuimarisha matumizi ya TEHAMA

katika vyuo vya ualimu hapa nchini. Mradi pia unaendelea na manunuzi ya vifaa kwa ajili ya wanafunzi na wakufunzi wenye mahitaji maalumu na imeandaa miongozo 22 kwa ajili ya mafunzo kazini. Pia mradi umeanza ujenzi wa Chuo cha Ualimu Kabanga na unaendesha mafunzo kazini kwa walimu 397 wa Hisabati kutoka katika Halmashauri zenye ufaulu wa chini katika somo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Elimu wa Kukuza Stadi za Kazi na Ujuzi. Mradi huu umegharimia awamu ya kwanza ya ukarabati katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, ambavyo nimeshavitaja wenye thamani ya Sh.8,777,000,000; umegharimia kiasi cha shilingi bilioni 1.5 za ujenzi wa hosteli kwa ajili wanafunzi wa kike katika Chuo Kikuu cha Ardhi. Vilevile maandalizi ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Dodoma yameanza ambapo kiasi cha shilingi bilioni 18 zimetengwa kwa ajili ya kujenga Chuo Kikuu hapa Dodoma cha kisasa na cha kipekee kuonesha kwamba Serikali sasa rasmi iko Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nijielekeze katika Fungu 18 - Tume ya *UNESCO*. Katika mwaka 2018/2019, Tume imetekeleza kazi ya kuratibu ushiriki wa Watanzania kwenye Mkutano Mkuu wa *UNESCO* na imeratibu mkutano wa Tume za Taifa kwenye nchi za Afrika Mashariki uliofanyika hapa nchini Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2018/2019, sasa naomba nielezee mpango wa bajeti kwa mwaka 2019/2020 na nitaanza na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Katika mwaka wa 2019/2020, Wizara itaendelea kukamilisha ukarabati katika Vyuo vyote vya Maendeleo ya Wananchi 34 ambavyo vitakuwa vimebakia na itaongeza udahili baada ya kukamilisha ukarabati huo kutoka wanafunzi 5,520 hadi kufikia wanafunzi 10,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ithibati ya Shule za Msingi na Sekondari. Katika mwaka 2019/2020, Wizara itafanya kazi ya ufuatiliaji wa Vyuo vya Walimu 137 vikiwemo 35 vya Serikali

na 102 na visivyo vya Serikali. Pia itaanzisha mfumo wa kielektroniki wa ithibati za shule ili kuongeza ufanisi katika usajili wa shule; itafuatilia shule zilizosajiliwa kwa masharti ili kukamilisha miundombinu na hapa naomba niweke msisitizo, niombe Waheshimiwa Wabunge tunapokuwa tunaomba Wizara itoe usajili wakati mwingine mnapokuja na ahadi kwamba mtakamilisha. Naomba niwakumbushe kuwa muungwana ni vitendo, mnapoahidi mtekeleze, tutakuja kuangalia wale tuliowapa usajili kwa masharti kama mmetekeleza masharti. Pia Wizara itafanya ufuatiliaji katika shule 200 zisizo za Serikali ili kuhakiki sifa za kitaaluma na kitaalam za walimu wa kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie udhibiti ubora wa shule na vyo vya walimu. Wizara itatoa mafunzo ya awali kwa Wadhibiti Ubora wa Shule 200 ili kuwajengea uwezo wa kusimamia elimu na itaanza ujenzi wa ofisi 100 za Udhibiti Ubora wa Shule na itafanya ukarabati wa ofisi 40 za Udhibiti wa Shule zilizopo. Tunategemea kufungua ofisi mpya za Udhibiti wa Shule katika Wilaya za Kyerwa, Kakonko, Nanyamba, Madaba na Nsimbo na lengo letu ni kusogeza huduma za ufuatiliaji wa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usimamizi wa Elimu Msingi. Katika kusimamia Elimu ya Msingi na Sekondari, Wizara itatekeleza yafuatayo, itafanya ufuatiliaji na tathimini ya mafanikio na changamoto katika vituo shikizi. Vituo shikizi wakati mwingine vimekuwa vikiichafua Serikali, mtu anapiga picha kituo cha ajabu ajabu wanaonesha kwamba ni shule ya Serikali, tunakwenda kufuatilia vituo vyote shikizi ili tuweze kutoa Mwongozo thabiti wa namna gani vituo hivyo vinapaswa kuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tutawajengea uwezo walimu 300 wa shule za sekondari ili kuimarisha utoaji wa huduma ya ushauri nasaha kwa wanafunzi na hasa watoto wa kike ambao wakati mwingine wamekuwa wahanga wa matukio mbalimbali. Kwa hiyo, tunataka kuhakikisha katika shule zetu za sekondari kuwe na mfumo imara katika

kuhakikisha kwamba vijana wanapata huduma ya ushauri na unasihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Wizara itafanya ufuatiliaji na tathmini kwa Shule za Ufundi, Kilimo, Sayansi Kimu, Biashara na Michezo kwa lengo la kuboresha shule hizo. Kama ambavyo tumekwishaongea, Serikali inataka kuhakikisha kwamba shule hizo zinaendelea kutoa mafunzo katika michepuo hiyo kwa kiwango cha hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie suala la Elimu Maalum. Kwa kuzingatia kuwa elimu ni haki ya msingi ya kila Mtanzania, Wizara itaendelea kusimamia utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum kwa kununua vifaa visaidizi na kutoa mafunzo kwa walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Elimu ya Juu; katika kusimamia elimu ya juu, Wizara itafuatilia maendeleo ya udahili, uandikishaji na utoaji mikopo kwa wanafunzi katika Taasisi za elimu ya juu na itaendelea na zoezi la kuratibu *scholarship* zinazotolewa na nchi rafiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usimamizi wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu; Wizara itaendesha mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na ubunifu ili kuwabaini wabunifu mahiri na kuwandeleza na itakamilisha mwongozo wa Kitaifa wa kuanzisha na kuendesha vituo vya teknolojia na ubunifu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nijielekeze katika Taasisi zilizo chini ya Wizara; kazi zilizopangwa kufanywa na Taasisi zilizo chini ya Wizara zimeainishwa katika ukurasa wa 134 hadi ukurasa wa 194 wa kitabu cha hotuba yangu. Naomba nielezee kwa uchache kazi zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania; katika mwaka 2019/2020, Tume itafanya tathmini ya *program* 200 za masomo mbalimbali zilizowasilishwa na vyuo kwa lengo la kuzisajili.



Mheshimiwa Mwenyekiti, mamlaka ya elimu na mafunzo ya Ufundi Stadi; katika mwaka 2019/2020, mamlaka itatekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Itajenga Karakana katika Vyuo vya mafundi stadi katika Mikoa ya Lindi, Pwani na Manyara pamoja Chuo cha TEHAMA cha Kipawa kilichopo Dar es salaam;

(ii) Itajenga Karakana ya mitambo mizito katika Chuo cha Ufundi Stadi cha Mwanza ili kukidhi hitaji la makapuni ya migodi ya Geita, Ulyankulu pamoja na *North Mara*;

(iii) Itejenga Bweni la wasichana lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 200 katika chuo cha mafunzo ya ufundi stadi ya Mkoa wa Mbeya ili kuongeza udahili wa wasichana katika mafunzo ya ufundi stadi;

(iv) Itajenga nyumba 10 za watumishi wa Chuo cha mafundi stadi cha Ulyankulu;

(v) Itanunua nyumba 10 za watumishi wa chuo cha mafunzo ya ufundi stadi-Manyara na;

(vi) Itajenga Karakana katika Chuo cha Ualimu cha mafunzo ya ufundi stadi-Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya elimu Tanzania; mamlaka imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuwezesha ujenzi wa madarasa 75, nyumba za walimu 20 na Mabweni 16 na;

(ii) Kuwezesha umaliziaji wa shughuli za ukarabati katika shule kongwe nne za Mwenge, Msalato, Ngaza na Mzumbe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu; Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya juu katika mwaka 2019/2020 imepanga kutoa

mikopo kwa wanafunzi 128,285 ambalo litakuwa ni ongezeko la asilimia 4.5 ukilinganisha na mwaka 2018/2019 na kati ya Wanafunzi hao, wanafunzi 45,485 watakuwa ni wa Mwaka wa kwanza ikilinganishwa na wanafunzi 41,234 wa mwaka wa kwanza waliopata mkopo katika mwaka huu. Kwa hiyo, kutakuwa na ongezeko la wanafunzi wa mwaka wa kwanza watakaopata mkopo kwa asilimia 10.3. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Bodi ya Mikopo imepanga kukusanya bilioni 221.5 kutoka kwa wanufaika wa mikopo ambao mikopo yao imeiva na hili ni ongezeko la asilimia 40.5 ukilinganisha na lengo la kukusanya milioni 157.7 katika Mwaka 2018/2019. Lakini pia Bodi ya mikopo itaanzisha na kuimarisha Ofisi mbili za Kanda katika Mikoa ya Mbeya na Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Elimu Tanzania; Taasisi ya Elimu Tanzania itaendelea na kazi yake ya kuandaa machapisho mbalimbali ya elimu na itaandaa muhutasari wa lugha ya Kichina kwa kidato cha Tano na cha Sita ambayo lugha hii sasa inaanza kufundishwa katika shule za sekondari. Lakini pia itaandaa mtaala na muhtasari wa somo la Kiswahili kwa shule za msingi za nchi ya Afrika ya Kusini na nchi ya Sudan Kusini pamoja na nchi nyingine yoyote ambayo itaomba nchi yetu iwasaidie katika kukuza lugha fasaha na adimu ya Kiswahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Taifa la Mitihani; Baraza la Mitihani litaendelea na jukumu lake la upimaji na uendeshaji wa mitihani ya Taifa katika ngazi mbalimbali hapa nchini. Wakala wa maendeleo ya uongozi wa elimu utatoa mafunzo ya uongozi na uendeshaji wa elimu kwa Wakuu wa shule 2554 na utaendesha mafunzo ya usimamizi wa elimu kwa Maafisa elimu 380 na kuendesha mafunzo kwa Maafisa elimu Kata 3996 kuhusu uongozi na uratibu wa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Elimu ya Watu wazima; Taasisi ya Elimu ya Watu wazima itaendelea na

jukumu lake na kuhakikisha inatoa elimu nje ya mfumo rasmi kwa watu ambao wako nje ya mfumo wa elimu lakini pia na kwa watu wazima. Katika Mwaka 2019/2020, Taasisi itaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ikiwa ni pamoja na mradi wa elimu ya sekondari kwa wasichana walio nje ya sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2019/2020, mradi huu kwa ajili ya wasichana walio nje ya sekondari tumeuboresha zaidi ili kuhakikisha kwamba vijana wetu hatuwapotezi na hasa watoto wa kike wanaoacha shule wawe na mahali ambapo wanaweza kusoma katika mazingira ambayo yako *flexible* zaidi. Lakini pia itaendelea na mpango wa elimu changamani kwa vijana walio nje ya shule na mradi wa kuwezesha vijana na watu wazima kielimu na mradi wa kuwezesha vijana katika kuongeza thamani ya mazao ya samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya huduma za Maktaba; Bodi ya huduma za Maktaba itatoa ushauri wa kitaalam katika vituo 100 juu ya uanzishaji, upangaji na uendeshaji wa Maktaba na itajenga maktaba ya Chuo cha Ukutubi-Bagamoyo na pampja na Maktaba za Mikoa ya Singida na Shinyanga na itapanua Maktaba ya Mkoa wa Dodoma na kukarabati Maktaba za Mikoa ya Iringa, Rukwa, Tabora na Ruvuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Sayansi na Teknolojia; Tume imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(a) Kubaini na kugharamia miradi minane mipya ya utafiti yenye lengo la kutatua matatizo ya wananchi.

(b) Kuratibu uendeshaji wa mashindano ya Kitaifa ya Sayansi na kufungasha na kusambaza matokeo ya utafiti kwa walaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya nguvu za *Atomic* Tanzania; Tume itaendelea kukagua vituo vyenye vyanzo 500 ili kubaini hali ya usalama, itaendelea na upimaji wa

viwango vya mionzi kwa wafanyakazi 1600, itaendelea na ujenzi wa Maabara ya Tume Awamu ya II, inayozinduliwa leo ni Awamu ya I. Tunatengeneza Awamu ya II ambayo itaendelea kuboresha huduma ya utoaji mionzi na kuongeza mapato na hapa kwa kifupi tu nichomekee kwamba hii Maabara ya Tume ya nguvu ya *Atomic* ni ya kipekee katika Ukanda wa Afrika kwa hiyo, tunategemea hata nchi nyingine zitakuwa zinaleta vyanzo vya vya mionzi kpmwa katika Maabara yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume itaanza pia ujenzi wa Maabara za Kanda katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza na Zanzibar na itafunga Ofisi za Tume katika Kanda ya Kati katika Mkoa wa Dodoma na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini katika Mkoa wa Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vya elimu ya juu; Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kitaanza ujenzi wa Ndaki ya Tiba za afya katika *Campus* ya Mbeya, kitakamilisha jengo jipya la kituo cha afya cha Chuo, kitaanza awamu ya kwanza ya ujenzi wa jengo la idara ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakuza uchumi lakini ukienda Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, idara ya uchumi pale haina ule mvuto unaostahili kwahiyo Serikali ya Awamu ya Tano inayoboresha uchumi imedhamiria na tunakwenda kujenga jengo la Idara ya Uchumi la kisasa kabisa.

Mheshimiwa mwenyekiti, itakarabati mabweni ya wanafunzi, barabara za ndani na nyumba za Wahadhiri, itaanza ujenzi wa jengo la ofisi na vyumba vya madarasa ya shule kuu ya Waandishi wa Habari pamoja na kuanza ujenzi wa jengo la Taasisi ya Sayansi za Bahari lililopo Buyuni-Zanzibar. Itafanya ukarabati mkubwa wa Karakana ya Wahandisi umeme, maji, mitambo na uashi kwa gaharama ya bilioni 1.5. Karakana hizi hazijafanyiwa ukarabati kwa muda mrefu, Serikali ya Awamu ya Tano iko kazini tumetoa bilioni 1.5 tunakwenda kuziboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Sokoine kitafanya tafiri 40 kuboresha uzalishaji wa mazao ya kilimo, mifugo na misitu pamoja na uvuvi na kitatoa elimu ya ushauri kwa wakulima 2500, kitajenga kumbi mbili za mihadhara zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1000 kila ukumbi na ukumbi wa mikutano wenye uwezo wa kuchukua watu 1000 kwa wakati mmoja. Kitaendelea na ujenzi wa *hostel* yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 700 na kitaandaa na kuboresha shamba darasa la chuo na ningeomba Waheshimiwa Wabunge mnapokuwa mnapita kwenye njia zenu tembeeleni pale katika Chuo chetu Kikuu cha kilimo kinapendeza. Mashamba darasa yako vizuri na wameweka mazao mazuri yanapendeza kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi-Muhimbili; chuo kitatekeleza yafuatayo:-

(a) Kitaanzisha tafiti mpya tano.

(b) Kitaimarisha miundombinu ya tafiti kwa kukamilisha kituo cha umahiri wa magonjwa ya moyo na mishipa yaani *center of excellence in cardiovascular sciences* katika *campus* ya Mloganzila.

(c) Kitafanya ukarabati katia kituo cha kufundishia na tafiti cha Bagamoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Ardhi kitatoa huduma za ushauri wa kitaalam kwa jamii kuhusu matumizi bora ya ardhi, upimaji na tathmini na kitaanza ujenzi wa jengo la usanifu wa majengo na hilo ni jengo la usanifu kweli kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Ardhi kitajenga jengo la madarasa, mfumo wa maji taka na kitakarabati *hostel* mbili za wanafunzi zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 256.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu Dodoma kitatoa mafunzo kwa watumishi 550, kitajenga nyumba za

watumishi kwa ajili ya familia 30 pamoja a nyumba tatu za viongozi yaani Makamu Mkuu wa Chuo na Manaibu wake wawili, kitajenga jengo kwa ajili ya huduma za mionzi katika hospitali ya chuo ili kuongeza wigo wa huduma za matibabu na kitakarabati majengo ya Ofisi, makazi, Mabweni, madarasa pamoja na miundombinu mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Ushirika-Moshi kitajenga Maktaba yenye uwezo wa kuchukua wasomaji 2500 kwa wakati mmoja na Chuo Kikuu huria kitajenga jengo la Makao Makuu Dodoma na majengo ya Ofisi za watumishi katika Mikoa ya Geita, Simiyu, Kigoma, Manyara na Lindi. Aidha, kitajenga ukumbi wa mitihani katika Mkoa wa Morogoro, kitafuatilia upatikanaji wa hatimiliki kwa ajili ya viwanja katika Mikoa ya Mara, Katavi, Dodoma, Lindi, Ruvuma, Kagera na Njombe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Mwalimu Nyerere kitaanza kuendesha *course* za muda mfupi katika kilimo, biashara na ujasiriamali kwa wakulima, wafugaji, wavuvi na vikundi vya wajasiriamali vya vijana na wakina Mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Sayansi na teknolojia-Mbeya kitaendelea kukamilisha jengo la Maktaba ili kukidhi mahitaji ya huduma za Maktaba kwa wanafunzi na wahadhiri, kitakamilisha taratibu za kusajili *campus* ya Rukwa ili ianze kutoa mafunzo na kitaanza kutoa mafunzo ya shahada ya ualimu wa ufundi na stahhada ya uzalimili ya ualimu wa ufundi ili kukidhi mahitaji ya walimu wa ufundi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na uhaba wa walimu wa mafunzo ya ufundi stadi kwa hiyo Chuo hiki cha Sayansi na teknolojia cha Mbeya kitakuwa pia kinashirikiana na chuo cha *Kleruu* pamoja na Chuo cha Ufundi cha Ualimu cha Mtwara kwa lengo la kuhakikisha kwamba tunaziba hilo pengo la ualimu wa ufundi. Lakini pia kitaanza ujenzi wa ukumbi wa mihadhara wenye uwezo wakuchukua wanafunzi 300.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya teknolojia ya Dar es Salaam itaanza kutekeleza Awamu ya II ya mradi unaofadhiliwa na Serikali ya Italy ambao unajikita katika kuanzisha vituo vya ujasiriamali, ubunifu na usambazaji wa teknolojia. Itaanza utekelezaji wa mradi wa *EASTRIP* ambao una lengo la kuanzisha kituo cha umahiri cha kikanda katika TEHAMA na uchakataji wa ngozi na mradi huu unafadhiliwa kwa mkopo wa Benki ya Dunia. Itaendelea kushiriki katika kutekeleza miradi minne mikubwa ya kubiasharisha bunifu zilizotokana na tafiti zenye lengo la kutatua matatizo ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Nelson Mandela itaendelea na miradi 33 ya kitafiti na ubunifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka 2019; *program* ya lipa kulingana na mtokeo imetenga kiasi cha shilingi bilioni 94,600,000,000 kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(a) Kugharamia magari 75 ya kuimarisha udhibiti ubora wa shule na vyuo vya ualimu. Kwa hiyo suala la udhibiti wa ubora, Serikali imeamua tumalizane na changamoto zilizopo moja kwa moja. Lakini pia Awamu ya I tulikuwa tunajenga Ofisi 100 za udhibiti ubora, katika awamu hii tutajenga ofisi 55 za udhibiti ubora wa shule ili kuimarisha mazingira ya utendaji kazi na tutatoa motisha kwa shule za msingi na sekondari 400 zitakazoongeza kiwango cha ufaulu katika mtihani wa Taifa wa darasa la saba na kidato cha nne;

(b) Tutatoa motisha kwa halmashauri 184 kutokana na utekelezaji wa vigezo vilivyokubalika na tutanunua Magari matano madogo na Malori mawili kwa ajili ya Baraza la mitihani kwa ajili ya kuimarisha utendaji wa Baraza la mitihani;

(c) Tutawezesha ujenzi wa shule mpya na ya kisasa ya sekondari katika Mkoa wa Dodoma itakayochukua wanafunzi wa kidato cha kwanza mpaka cha sita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa kukuza ujuzi na stadi; mradi hu umetengewa kiasi cha shilingi bilioni 56,556,726,386 ambao utaendeleza kazi ya ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi katika ngazi mbalimbali, ukarabati wa vyuo vya maendeleo ya wananchi na kuvinunulia vifaa, kuendelea kujengea uwezo Wizara na Taasisi zinazosimamia ubora wa vyuo vikuu na vyuo vya ufundi wa mafundi stadi na ujenzi wa Chuo cha ufundi stadi-Dodoma ambacho kitajengwa katika Kitongoji cha Nala, tayari tumekwishapata ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa kuimarisha elimu na ufundi wa mafunzo stadi; mradi huu umetengewa kiasi cha shilingi bilioni 72,855,000,000 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi na huduma vya Mikoa na kuimarisha mafunzo ya ufundi stadi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa kuimarisha stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu; mradi huu umepata fedha mpya kutoka kwa wafadhili wetu (*Global partnership in education*) kiasi cha shilingi za Marekani dola milioni 90 takribani sawa na shilingi bilioni 200 za Kitanzania na tutakwenda kuimarisha vituo vya walimu na tutaandaa mwongozo kwa ajili ya waratibu wa vituo vya walimu, kuwajengea uwezo waratibu wa vituo na kuweza kufanya ufuatiliaji wa tathmini, kuimarisha ukusanyaji wa takwimu kwa ajili ya mradi wa kuimarisha stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu, kuwezesha uandaaji, uchapaji na usambazi wa vitabu pamoja na kiongozi cha Mwalimu kwa masomo yote ya darasa la sita mpaka la saba, kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum pamoja na walimu ambao wanafundisha wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa kuimarisha mafunzo ya elimu ya ualimu (*Teacher education support program-TESP*); mradi huu umetengewa kiasi cha shilingi bilioni 20,300,000,000 na utakwenda kutekeleza shughuli zifuatazo:-



(a) Kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia vikiwemo vifaa vya Maabara na vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalum kwa ajili ya vyuo vya ualimu.

(b) Kununua vitabu vya rejea vya kielektroniki kwa ajili ya vyuo vya ualimu pamoja na kusambaza vifaa vya TEHAMA.

(c) Kuendelea na ujenzi wa Chuo cha ualimu Kabanga.

(d) Kutoa mfunzo ya program ya wakufunzi kwa wakufunzi 1300 wa vyuo vya ualimu.

(e) Kutoa mafunzo ya TEHAMA na teknolojia saidizi kwa wakufunzi 150 wenye mahitaji maalum na kutoa mafunzo kwa walimu 300 wa shule za msingi na sekondari kuhusu lugha za alama na mbinu sahihi za ufundishaji kwa wanafunzi viziwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukishuhudia wanafunzi wa sekondari, wanafunzi viziwi ufaulu wao umekuwa siyo mzuri kwahiy Serikali inafuatilia na inachukua hatua za kuhakikisha kwamba tunakabiliana na changamoto hiyo kwa kuboresha ufundishaji wa lugha za alama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa ukaratabati wa Vyuo vya Ualimu; mradi huu umetengewa kiasi cha shilingi bilioni 7,295,917,000 kwa ajili ya kuendelea na kukamilisha ujenzi katika vyuo vya walimu vya Shinyanga, Mpuguso, Ndala na Kitangali.

Mradi wa huduma za maji, elimu ya afya na usafi wa mazingira shuleni; mradi huu umetengewa shilingi bilioni 6,948,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya maji na vyoo katika shule za msingi 220 ili kuimarisha mazingira ya kufundishia pamoja na kutoa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa ubora wa elimu sekondari; mradi huu umetengewa shilingi bilioni 80,818,000,000 kwa ajili ya kuendeleza shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na ununuzi wa mashine kwa jili ya Taasisi ya elimu na kuboresha ununuzi wa vifaa kwa ajili ya kufundishia na kujifunzia na kutoa mafunzo kwa walimu jumuiishi pamoja na vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalum na mafunzo kazini kwa walimu ambapo tunatarajia kutoa mafunzo kwa walimu takribani 10000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Taifa ya *UNESCO*; katika mwaka 2018/2019, Tume ya Taifa ya *UNESCO* itaendelea kushirikiana na Wizara, Taasisi na watu binafsi na wadau wengine katika kuboresha masuala ya elimu, sayansi, utamaduni habari na mawasiliano. Kwa kumalizia naomba nitoe shukurani:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutambua mchango mkubwa wa viongozi wenzangu katika kutekeleza na kufanikisha majukumu ya Wizara na kipekee kabisa namshukuru kwa dhati Mheshimiwa William Tate Ole Nasha, Mbunge wa Ngorongoro na Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa ushirikiano mkubwa anaonipa katika kusimamia Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Katibu Mkuu wa Wizara, Dkt. Leonard Akwilapo, Manaibu Katibu Prof. James Mdoe na Dkt. Ave Maria Semakafu, Kamishina wa elimu, Wakurugenzi, Wakuu wa Idara na Wakuu wa Vitengo, Wenyeviti wa Bodi na Mabaraza yaliyo chini ya Wizara na Watumishi wote wa Wizara kwa ushirikiano mkubwa kabisa ambao wananipa na hakika mtajionea kwenye kitabu changu cha hotuba. Haya yote yasingewezekana bila ushirikiano wanaonipatia, ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuwashukuru viongozi wa wafanyakazi, watumishi wa Wizara na Taasisi zake, wanafunzi na wadau wote wa elimu nchini kwa ushirikiano wao katika kuendeleza sekta ya Elimu, Sayansi,

Tekonolijia na Ubinifu. Ninatambua na kuthamini mchango wenu na nitaendelea kupokea ushauri na maoni mnayoyatoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kutoa shukurani za dhati kabisa na za kipekee kwa wamiliki wa vyuo, shule na Taasisi binafsi ambao hakika wamekuwa wakishirikiana nami, wamekuwa wakishirikiana na Serikali katika kuhakikisha kwamba Serikali inafikia malengo yake katika sekta ya elimu.

Napenda pia kuwashukuru washirika wa maendeleo na wadau wa elimu ambao wamechangia kufanikisha mipango ya elimu na kwa kuwa siyo rahisi kuwataja wote, niruhusu niwataje wachache. Napenda kushukuru Serikali za nchi zifuatazo; Algeria, Brazil, Canada, China, Cuba, Denmark, Ethiopia, Finland, Hungary, India, Italia, Japan, Korea ya Kusini, Marekani, Mauritius, Misri, Morocco, Msumbiji, Norway, Pakistan, Sweden, Thailand, Ubelgiji, Ufaransa, Uingereza, Ujerumani, Urusi, Uswisi na Uturuki. Aidha, napenda kutoa shukurani za dhati kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuyashukuru kwa dhati kabisa baadhi ya Mashirika ambayo kwa kweli yamechangia katika kufanikisha malengo ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Napenda kuishukuru Benki ya Dunia, Umoja wa Nchi za Ulaya, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Jumuiya ya Madola, *Global Partnership in Education, British Council, Commonwealth Secretariat, Dfid, UNDP, UNICEF, USAID, UNESCO, JICA, SIDA, KOICA, EQPT, HDIF, DAAD, IUCEA, TEN/ MET CAFED, CSSC, BAKWATYA, FEMINA, KTO Water Aid na Plan International.* (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukurani hiyo sasa kwa heshima kubwa naomba niwasilishe maombi ya

fedha. Ili kuwezesha utekelezaji wa malengo ya Wizara kwa mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Fungu 46 inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 1,386,508,723,272/=, ambapo shilingi 523,788,923,012/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 450,356,645,000/= ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 73,432,278,000/= ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zinazombwa shilingi bilioni 436 ni kwa ajili ya matumizi ya Wakala na Taasisi zilizo chini ya Wizara na kati ya fedha hizo shilingi 388,346,298,000/= ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 48,084,000,000/= ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya maendeleo shilingi 862,719,800,260/= zinaombwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo shilingi bilioni 583,415 ni fedha za ndani na shilingi 279,305,800,000/= ni fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Tume ya *UNESCO* Fungu 18, Wizara inaomba jumla ya shilingi 2,156,017,000/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida na kati ya fedha hizo shilingi 623,724,000/= ni za mishahara na shilingi 1,532,293,000/= ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa kwa heshima na unyenyekevu mkubwa kabisa naomba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Bajeti ya Mafungu yote mawili, yaani Fungu 16 na Fungu 18 na Fungu 46 yenye jumla ya kiasi cha shilingi 1,388,664,740,270/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia kabisa, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwako wewe na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.  
*(Makofi)*

**HOTUBA YA WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA  
MHESHIMIWA PROF. JOYCE LAZARO NDALICHAKO (MB)  
AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI  
YA FEDHA KWA MWAKA 2019/20 - KAMA ILIVYOWASILISHWA  
MEZANI**

**A. UTANGULIZI**

**1. Mheshimiwa Spika**, kufuatia taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu, likubali kupokea na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka 2018/19. Aidha, naliomba Bunge lako lijadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2019/20.

**2. Mheshimiwa Spika**, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kwa kuniwezesha tena kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka 2019/20. Napenda kumpongeza kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa uongozi wake makini uliotukuka na kwa ujasiri alionao katika kufanya maamuzi yete tija kwa maendeleo ya Taifa letu.

**3. Mheshimiwa Spika**, napenda kumpongeza Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) kwa uongozi wao thabiti na kwa miongozo mbalimbali wanayoitoa ambayo imeendelea kuwa chachu katika kuboresha utendaji wa Serikali ya Awamu ya Tano. Pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuongoza vyema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

**4. Mheshimiwa Spika**, naomba nikupongeze kwa dhati wewe Spika wa Bunge, Mheshimiwa Job Yustino Ndugai na Naibu Spika Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu kwa kuliongoza Bunge hili kwa busara, hekima na kwa

weledi wa hali ya juu. Nawapongeza pia Wenyeviti wa Bunge kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuongoza kwa ufanisi mijadala ndani ya Bunge letu.

**5. Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba (Mb) na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Juma Nkamia (Mb) kwa kuendelea kutoa ushirikiano mzuri katika Wizara yangu. Maoni na ushauri ambao wamekuwa wakiutoa katika Sekta ya Elimu yameendelea kufanikisha dhamira ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kutoa elimu bora katika ngazi zote. Ninawashukuru kwa uchambuzi wa kina wa Bajeti hii ya mwaka 2019/20.

**6. Mheshimiwa Spika**, nitumie fursa hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waheshimiwa Mawaziri waliotangulia kuwasilisha hoja zao katika Bunge lako tukufu, ambazo zimetoa tathmini ya ujumla kuhusu utekelezaji wa kazi za Serikali kwa mwaka 2018/19 na mwelekeo wa shughuli za Serikali kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20.

**7. Mheshimiwa Spika**, ninaishukuru familia yangu kwa kuendelea kunipa ushirikiano wa dhati katika kutekeleza majukumu yangu ya Kitaifa.

**8. Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo ya utangulizi sasa naomba nitoe taarifa ya utekelezaji wa kazi za Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2018/19 na Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2019/20.

**B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA 2018/19**

**Bajeti Iliyoidhinishwa Katika Mwaka 2018/19**

**9. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/19 Wizara yangu iliidhinishwa Jumla ya **Shilingi 1,407,136,481,000.00** katika mafungu mawili tofauti yaani Fungu 46 (Wizara ya Elimu,

Sayansi na Teknolojia) na Fungu 18 (Tume ya Taifa ya UNESCO) ambalo nitaeleza utekelezaji wake baada ya Fungu 46.

### **Bajeti iliyoidhinishwa kwa Fungu 46 (Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia)**

**10. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2018/19 Bunge lako Tukufu liliidhinisha kiasi cha **Shilingi 1,406,469,626,000.00** kwa Fungu 46 ambapo **Shilingi 476,500,224,000.00** zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya Kawaida na **Shilingi 929,969,402,000.00** zilikuwa ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

### **Ukusanyaji wa maduhuli kwa Mwaka 2018/19**

**11. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/19, Wizara ilikadiriwa kukusanya jumla ya **Shilingi 460,011,442,840.89** ambapo kiasi cha **Shilingi 16,916,628,402.59** zilipangwa kukusanywa na Idara na Vitengo, na **Shilingi 443,094,814,438.30** zilipangwa kukusanywa na Taasisi zilizo chini ya Wizara. Hadi kufikia tarehe 15 Aprili, 2019, Wizara imekusanya **Shilingi 360,108,828,063.37** sawa na asilimia **78.3** ya makadirio. Kiasi kikubwa cha maduhuli kilitokana na malipo ya ada na huduma mbalimbali za kielimu zilizotolewa na Idara na Taasisi zilizo chini ya Wizara.

**12. Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua nafasi hii kuwaagiza Wakuu wote wa Idara na Taasisi zote zilizo chini ya Wizara yangu kuhakikisha wanaendelea kukusanya maduhuli waliyopanga kukusanya kwa kipindi kilichobakia cha Mwaka wa Fedha 2019/20 ili kufika malengo yaliyowekwa.

### **Matumizi ya Kawaida**

**13. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2019, Wizara imepokea Jumla ya **Shilingi 348,485,307,415.38** kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambazo ni sawa na asilimia **73.1** ya bajeti ya fedha za Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 289,045,655,805.77** ni Mishahara sawa na asilimia **71.1** ya bajeti ya Mishahara.

## Matumizi ya Miradi ya Maendeleo

**14. Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2019, Wizara ilipokea jumla ya **Shilingi 597,341,693,915.11** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, kiasi hiki ni sawa na asilimia **64.2** ya bajeti iliyotengwa.

## TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2018/19

**15. Mheshimiwa Spika**, sasa naomba nitoe taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa mwaka 2018/19 na malengo ya Utekelezaji kwa mwaka 2019/20.

## Kuendeleza Elimu msingi kwa Kutoa Ithibati ya Mafunzo ya Ualimu na Maendeleo ya Kitaalamu ya Walimu

**16. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuimarisha shughuli za ithibati ya mafunzo ya Ualimu ambapo katika mwaka 2018/19 Wizara imetekeleza kazi zifuatazo:

(i) imedahili wanachuo 5,842 waliojiunga na mafunzo ya Elimu ya Ualimu kwa ngazi ya Astashahada na Stashahada kwa lengo la kukidhi mahitaji ya walimu nchini;

(ii) imewezesha utoaji wa mafunzo kwa vitendo (Block Teaching Practice - BTP) kwa wanachuo 20,157 wa ngazi ya Astashahada na Stashahada katika Vyuo vya Ualimu 35 vya Serikali kwa lengo la kuoanisha nadharia na vitendo ili kuzalisha walimu wenye sifa stahiki;

(iii) imegharamia chakula kwa wanachuo 20,157 katika Vyuo vya Ualimu 35 vya Serikali;

(iv) imetoa mafunzo kwa wakufunzi wawezeshaji 80 kutoka Vyuo vya Ualimu 40 vikiwemo Vyuo 35 vya Serikali na Vyuo 5 visivyo vya Serikali. Lengo la mafunzo haya ni kuwajengea uwezo wa kufuatilia ufanisi wa Taaluma kwa kuzingatia Kiunzi kipya cha Uthibiti Ubora wa Shule katika Vyuo vya Ualimu; na



(v) imeandaa rasimu ya Kiunzi cha Mafunzo Endelevu Kazini kwa Walimu (Teachers' Continuous Professional Development Framework). Kiunzi hiki kitakuwa nyenzo ya kuwaendeleza walimu kitaaluma na kitalaamu ili kuongeza ufanisi katika ufundishaji na ujifunzaji.

### **Kusimamia Uendelezaji wa Mafunzo Katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi - (Folk Development Colleges - FDCs)**

**17. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuimarisha utoaji wa mafunzo katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ambapo katika mwaka 2018/19 inaendelea na ukarabati wa awamu ya kwanza unaohusisha Vyuo 20 vya Rubondo, Gera, Munguri, Chisalu, Newala, Kilwa Masoko, Ikwiriri, Mtawanya, Handeni, Mto wa Mbu, Urambo, Kasulu, Tarime, Ilula, Muhukuru, Sofi, Chilala, Kiwanda, Malampaka na Karumo. Ukarabati huo upo katika hatua za umalizaji. Aidha, maandalizi ya awamu ya pili ya ujenzi na ukarabati yameanza mwezi Aprili, 2019 na inahusisha Vyuo 20 vya Ngara, Msingi, Msinga, Kisangwa, Mamtukuna, Malya, Same, Sengerema, Ifakara, Kilosa, Kihinga, Msaginya, Mputa, Nandembo, Bariadi, Masasi, Sikonge, Chala, Kibondo na Katumba. Vyuo 14 vilivyobaki vitaanza kufanyiwa ukarabati katika awamu ya tatu inayotarajiwa kuanza mwezi Juni, 2019. Vyuo hivyo ni Bigwa, Nzovwe, Mwanva, Ulembwe, Njombe, Mbinga, Singida, Tango, Mwanhala, Nzega, Kisarawe, Arnautoglu, Musoma na Buhangija.

**18. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/19, Wizara imedahili jumla ya Wanachuo 5,520 katika Vyuo 54 vya Maendeleo ya Wananchi. Kozi zinazotolewa katika vyuo hivi ni pamoja na Upishi, Kilimo na Ufugaji, Ufundi Umeme wa Majumbani, Ufugaji Samaki na Nyuki, Ususi na Ufumaji, Usindikaji wa Vyakula, Umakenika, Kompyuta, Uselemala, Uashi, Utengenezaji Mapambo, Ujasiriamali, Uendeshaji Hoteli na Umeme wa Magari. Aidha, mafunzo ya uelewa ambayo ni Kiswahili, Kiingereza, Uraia, Utamaduni, Uchumi/Hesabu, Afya ya Jamii, (Usafi na Hifadhi ya Mazingira, Utunzaji wa

watoto, utunzaji wa nyumba, Uzazi wa Mpango na huduma ya kwanza), Sayansi, Kilimo na Vikundi vya Kujitegemea.

**Kutunga na Kutekeleza Sera za Elimu, Utafiti, Huduma za Maktaba, Sayansi, Teknolojia, Ubunifu na Uendelezaji wa Mafunzo ya Ufundi**

**19. Mheshimiwa Spika**, katika kuendeleza Sayansi, Teknolojia na Ubunifu, Wizara kwa mwaka 2018/19 imetekeleza kazi zifuatazo:

(i) imeendelea kupokea maoni kuhusu maeneo yanayohitaji kuboreshwa katika Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 kwa lengo la kufanya mapitio ya Sera hiyo ili iendane na hali halisi ya sasa;

(ii) imeandaa rasimu ya mapitio ya Sera ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu;

(iii) imetafsiri katika lugha ya Kiswahili Sera zifuatazo:

(a) Sera ya Taifa ya Baioteknolojia ya mwaka 2010;

(b) Sera ya Taifa ya Utafiti na

Maendeleo ya mwaka 2010; na

(c) Sera ya Taifa ya Teknolojia ya Nyuklia ya mwaka 2013.

Lengo la kufanya tafsiri ni kuwezesha wadau wengi zaidi kuzielewa kirahisi sera hizo.

(iv) imekamilisha maandiko ya utekelezaji wa Mkataba wa mradi wa *East Africa Skills for Transformation and Regional Intergration Project* (EASTRIP) kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha. Mradi huu unalenga kuanzisha Vituo vya Umahiri katika ufundi katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (Kampasi za Dar es Salaam na Mwanza), Chuo cha Taifa cha Usafirishaji na Chuo cha Ufundi Arusha. Utekelezaji wa mradi

huu unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha wa 2019/20;

(v) inaendelea na mapitio ya Mradi wa *Secondary Education Quality Improvement Program* (SEQUIP) unaotarajiwa kugharamiwa kwa fedha za mkopo kutoka Benki ya Dunia; na

(vi) imeandaa Muundo wa Utumishi wa Bodi ya Kitaalamu ya Walimu ambao utawasilishwa Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ili kupata idhini ya kujaza nafasi za watumishi kwa ajili ya kuanza kutekeleza shughuli za Bodi.

### **Kuainisha Mahitaji ya Nchi Katika Ujuzi na Kuuendeleza**

**20. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha 2018/19 Wizara kupitia Mradi wa Kukuza Stadi za Kazi na Ujuzi (Education and Skills for Productive Jobs - ESPJ) imejengea uwezo Taasisi 16 za mafunzo ili ziboreshe na kutoa mafunzo kulingana na vipaumbele vya Serikali katika shughuli za kuzalisha na kukuza uchumi. Aidha, ESPJ kupitia mfuko wa *Skills Development Fund* (SDF) unaosimamiwa na Mamlaka ya Elimu Tanzania umetoa ruzuku ya jumla ya **Shilingi 3,481,702,271.95**. Ruzuku hiyo itanufaisha jumla ya programu 29 na jumla ya Watanzania 4,483 wanatarajiwa kupata mafunzo mbalimbali ya ujuzi na stadi za kazi katika Taasisi hizo.

### **Kusimamia Ithibati na Uthibiti Ubora wa Shule na Vyuo vya Ualimu Ithibati ya Shule na Vyuo vya Ualimu**

**21. Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza jukumu la kusimamia Sera na kuongeza upatikanaji wa fursa za Elimu na Mafunzo, katika mwaka 2018/19 Wizara imetekeleza yafuatayo:

(i) imesajili jumla ya shule 363 sawa na asilimia 96 ya shule 378 zilizoomba usajili. Mchanganuo wa shule hizo ni kama ifuatavyo: Awali Pekee 19 (zisizo za serikali); Awali na Msingi

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

213 (Serikali 58, zisizo za serikali 155) na Sekondari 131 (za serikali 89 na zisizo za serikali 42);

(ii) imetoa vibali vya ujenzi kwa shule 93 sawa na asilimia 61 ya shule 152 zilizoomba (Shule za Awali pekee 14, Awali na Msingi 55, na Sekondari 24);

(iii) imetoa vibali 52 vya kutumia majengo ya shule sawa na asilimia 63 ya maombi 82 yaliyowasilishwa (Shule za Awali pekee 05, Msingi 33, Sekondari 11 na Vyuo vya Ualimu 03);

(iv) imetoa vibali vya kuongeza mikondo kwa shule 12 zilizokidhi vigezo, kati ya hizo shule za Awali na Msingi zilikuwa 07 na Sekondari 05;

(v) imetoa vibali vya kuongeza tahasusi kwa shule za Sekondari 40 kati ya 43 sawa na asilimia 93 ya shule zilizotuma maombi;

(vi) imetoa kibali cha kubadili matumizi ya Chuo cha Ualimu cha Mt. Alberto kilichopo Musoma kuwa Shule ya Sekondari;

(vii) imetoa uthibitisho kwa wamiliki na Mameneja wa shule 172 kati ya 219 walioomba sawa na asilimia 79 ya maombi. Kati yao, wamiliki wa shule za Awali Pekee 10, shule za Msingi 135, shule za Sekondari 25 na Vyuo vya Ualimu 02. Aidha, vibali vya kuanzisha huduma ya bwani vilitolewa kwa shule zote 96 zilizoomba ambapo Shule 46 zilikuwa za Msingi na Shule 50 zilikuwa za Sekondari;

(viii) imehuisha Mwongozo wa Usajili wa Shule ili kukidhi mahitaji ya jamii kwa wakati uliopo, hususan ukubwa wa eneo la kujenga shule, pamoja na kuongeza uwazi kuhusu masuala mbalimbali ya taratibu zausajili, uendeshaji na usimamizi wa shule; na

(ix) imetoa leseni kwa walimu 347 waliotimiza vigezo kati ya 485 walioomba. Maombi hayo yalijumuisha walimu 466

wa Kigeni na 19 Watanzania ambapo waliopata Leseni ni 328 wa kigeni na Watanzania wote 19.

### **Uthibiti Ubora wa Shule na Vyuo vya Ualimu**

**22. Mheshimiwa Spika**, Wizara ina jukumu la kuthibiti Ubora wa Shule na Vyuo vya Ualimu. Hadi kufikia Machi, 2019 imetekeleza kazi zifuatazo;

(i) imefanya tathmini ya jumla katika Asasi 6,966 sawa na asilimia 61.5 ya lengo la Asasi 11,327 na kutoa ushauri na mapendekezo kwa ajili ya kuboresha ufundishaji na ujifunzaji ili kutoa elimu bora kwa Watanzania;

(ii) imefanya ufuatiliaji wa shule 61 zikiwemo za Msingi 23 na Sekondari 38 zilizopewa usajili kwa masharti ya kukamilisha miundombinu. Wamiliki wa shule ambazo hazijakamilisha masharti ya usajili walihimizwa kukamilisha miundombinu ya shule zao ili kukidhi vigezo na masharti ya usajili; na

(iii) imefanya ufuatiliaji wa shule za Sekondari 1,371 zinazotoa huduma ya bweni kwa lengo la kubaini kama Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya uendeshaji wa shule za bweni inazingatiwa na kutoa ushauri kwa wamiliki wa shule kuhusu namna ya kuanzisha na kutoa huduma hizo za bweni.

### **Usimamizi wa Elimumsingi**

**23. Mheshimiwa Spika**, katika kusimamia Elimu ya Msingi na Sekondari, katika mwaka 2018/19 Wizara imetekeleza yafuatayo:

(i) imeratibu mashindano ya Uandishi wa Insha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi zilizo Kusini mwa Bara la Afrika (SADC) kwa wanafunzi wa Shule za Sekondari. Mwanafunzi **Innocent Benedict Shirima wa Kidato cha Nne kutoka shule ya Sekondari Moshi** alishika nafasi ya kwanza kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki;

(ii) imechambua nyaraka mbalimbali za Elimu na kutoa Waraka wa Elimu Namba 1 wa mwaka 2018 unaohusu utaratibu wa uundaji na uendeshaji wa Kamati na Bodi za Shule na Waraka wa Elimu Namba 2 wa mwaka 2018 unaohusu utaratibu wa kukariri darasa kwa wanafunzi wa Elimu ya Msingi na Sekondari; na

(iii) imeandaa zana na taratibu ili kuwawezesha walimu kuwabaini wanafunzi wenye vipawa na vipaji na kuweka mipango ya kuwaendeleza kwenye ngazi za Elimu ya Awali, Msingi na Sekondari.

### **Usimamizi wa Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi**

**24. Mheshimiwa Spika**, katika kusimamia utoaji wa Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi Wizara kwa mwaka 2018/19 imetekeleza kazi zifuatazo:

(i) imeandaa na kuzindua Mpangowa Elimu Changamani (Intergrated Programme for Out of School Adolescents - IPOSA) na mpango mkakati wa utekelezaji kwa kushirikiana na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW) na Ofisi ya Rais – TAMISEMI. Mpango huu utaimarisha utoaji wa Elimu Nje ya Mfumo Rasmi kwa vijana wenye umri kuanzia miaka 14 hadi 17; na

(ii) imefanya mapitio na kuboresha vijitabu vinne (4) (*Primers*) kwa ajili ya Kilimo Bora cha Chai, Pamba, Mahindi na Kijitabu cha Maendeleo, vinavyotumiwa na wanakisomo katika vikundi vya Elimu ya Watu Wazima.

### **Usimamizi wa Masuala Mtambuka katika Elimu**

**25. Mheshimiwa Spika**, katika kusimamia utoaji wa Elimu ya Masuala Mtambuka kwa mwaka wa fedha 2018/19 Wizara imeendesha mafunzo ya Stadi za Malezi na Unasihi shuleni yaliyotolewa kwa washiriki 175. Lengo la mafunzo hayo ni kuimarisha usimamizi na kuboresha utoaji wa huduma ya malezi, ushauri na unasihi shuleni.

## Usimamizi wa Elimu Maalum

**26. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/19 Wizara imeendelea kusimamia utoaji wa Elimu Maalum ili kuhakikisha watoto wote wanapata elimu iliyo bora kwa kutekeleza kazi zifuatazo:

(i) imeandaa Mkakati wa Taifa wa Elimu Jumuishi wa mwaka 2018 - 2021 pamoja na mpango wa utekelezaji wake ili kuwawezesha wadau wa elimu kuchangia upatikanaji wa fursa na utoaji wa elimu bora kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum nchini. Mkakati na Mpango wa Utekelezaji wake vipo katika hatua ya uchapaji;

(ii) imeratibu utungaji, usimamizi na usahihishaji wa mitihani ya upimaji kwa wanafunzi viziwi 157 wakiwemo 84 wa kidato cha Pili na 73 wa kidato cha Nne. Upimaji huo ulifanyika katika shule za sekondari za Iringa Wasichana, Malangali, Njombe Viziwi, Kazima na Moshi Ufundi kwa lengo la kubaini changamoto za ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi viziwi nchini;

(iii) imetoa mafunzo kwa walimu 402 wanaofundisha wanafunzi wenye mahitaji maalum ambapo walimu 84 wanafundisha wanafunziwasioona, 118 wanafundisha wanafunzi viziwi na 200 wanafundisha wanafunzi wenye ulemavu wa akili na usonji. Lengo la mafunzo hayo ni kuimarisha uwezo wa walimu kufundisha wanafunzi wenye mahitaji maalum.

## Usimamizi wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi

**27. Mheshimiwa Spika**, katika kuratibu jukumu la uendelezaji wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi katika mwaka 2018/19 Wizara imetekeleza kazi zifuatazo:

(i) imegharamia chakula cha Wanachuo 5,520 katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 54;

(ii) imegharamia chakula cha wanafunzi 366 wa mwaka wa kwanza na wa pili kwa mwaka 2018/19 katika Chuo cha Ufundi Arusha (ATC);

(iii) imeratibu upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa Chuo cha Ufundi Arusha (ATC) ambapo vifaa vipya vya kisasa vinavyogharimu kiasi cha **Shilingi** bilioni 15 vimenunuliwa. Ufungaji wa mashine hizo umekamilika katika karakana tano (5), ambazo ni karakana za Mitambo, Magari, Umeme, Uchomeleaji na Useremala.

(iv) imeratibu ukarabati na upanuzi wa karakana tano (05). Kukamilika kwa ukarabati na ufungaji wa vifaa vipya vya kisasa kutatoa fursa kwa wanafunzi wengi zaidi kudahiliwa na kupata ujuzi unaoendana na teknolojia ya kisasa;

(v) imeratibu upatikanaji wa mtaalamu elekezi kwa ajili ya *Capacity Building on Labour market surveys/student tracer studies and employer satisfaction surveys*. Lengo ni kuwezesha ubainishaji wa mahitaji ya soko la ajira na kufanya mapitio ya Mitaala. Kazi hii ipo kwenye hatua za manunuzi; na

(vi) Imetafsiri Mitaala itakayotumika na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kutoka lugha ya kiingereza kwenda kwenye lugha ya Kiswahili kwa lengo la kurahisisha uelewa wa maarifa yatolewayo kwa vijana.

## **Usimamizi na Uendelezaji wa Elimu ya Juu**

**28. Mheshimiwa Spika**, katika usimamizi na uendelezaji wa Elimu ya Juu nchini, Wizara kwa mwaka wa fedha 2018/19 imetekeleza kazi zifuatazo:

(i) imeratibu skolashipu za masomo nje ya nchi kwa mwaka 2018/19 ambapo, wanafunzi 159 wa Kitanzania wamefanikiwa kupata fursa za masomo na kati yao wanafunzi 97 walipata nafasi za masomo nchini China, Uingereza 03, Hungary 23, Misri 06, Morocco 05, Urusi 12 na Algeria 13.



(ii) imeratibu skolashipu za Jumuiya ya Madola, China na Hungary kwa mwaka 2019/20 na kwa sasa mamlaka husika zinaendelea na taratibu za uteuzi kwa kuzingatia vigezo na masharti yao. Wizara pia imetoa matangazo ya nafasi za masomo nchini Morocco, Misri, Ethiopia, Pakistani, Brazil, Mauritius, Thailand, Uturuki, Malaysi, Korea Kusini na Marekani kwa lengo la kutoa fursa za Elimu ya Juu kwa vijana wa Kitanzania;

(iii) imefadhili wanafunzi 5 raia wa China kusoma Lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam;

(iv) imeendelea kufuatilia utendaji wa miradi minne (4) inayoratibiwa na Vituo vya Umahiri vya Afrika katika Kanda ya Afrika Mashariki na Kusini iliyopo Chuo Kikuu Cha Sokoine cha Kilimo (SUA) na Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST) ili kuhakikisha malengo ya uanzishwaji wa vituo hivyo yanafikiwa katika kutoa elimu bora ya Uzamili na Uzamivu na kujenga ushirikiano wa kimataifa katika maeneo ya kipaumbele kikanda; na

(v) imeendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa mradi wa *Education and Skills for Productive Jobs* (ESPJ) unaolenga Kukuza Stadi za Kazi na Ujuzi.

**29. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kushirikiana na Mashirika na Taasisi mbalimbali katika kufadhili wanafunzi wa Elimu ya Juu kama ifuatavyo: Benki ya Taifa ya Biashara wanafunzi 19 - Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam – DUCE, wanafunzi 18 wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wamepata ufadhili kutoka Benki ya Barclays, Mo Dewji Foundation wanafunzi (29), Tertiary Education Scholarship Trust wanafunzi (30), DAFI/UNHCR (Ujerumani) wanafunzi (4) na Help to Help Sweden wanafunzi (21).

### **Usimamizi wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu**

**30. Mheshimiwa Spika**, katika kutambua, kujenga, kukuza na kuendeleza ubunifu kwa Watanzania katika Nyanja za Sayansi, Teknolojia na Ubunifu, Wizara kwa mwaka wa fedha 2018/19 imetekeleza kazi zifuatazo:

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

- (i) imegharamia chakula kwa wanafunzi 692 waliosajiliwa ngazi ya Stashahada katika mwaka wa masomo 2018/19 katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT);
- (ii) imegharamia mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi 403 wa mwaka wa kwanza na wa pili kwa mwaka 2018/19 katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam;
- (iii) imegharamia mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi 264 waliosajiliwa ngazi ya Stashahada kwa mwaka wa kwanza na wa pili kwa mwaka wa masomo 2018/19 katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya;
- (iv) imegharamia chakula kwa wanafunzi 603 waliosajiliwa ngazi ya Stashahada katika mwaka wa masomo 2018/19 katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya;
- (v) imeandaa na kuzindua Mwongozo wa kutambua na kuendeleza Ugunduzi, Ubunifu na Maarifa Asilia nchini ili kujenga na kukuza hamasa ya matumizi ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu katika shughuli za jamii na maendeleo na hivyo kuongeza mchango wake katika uchumi;
- (vi) imeandaa na kuendesha Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu kwa lengo la kuwatambua na kuwaendeleza wabunifu na wagunduzi mahiri. Mashindano yalikusisha wabunifu kutoka makundi ya Shule za Sekondari, Sekta isiyo Rasmi, Vyuho vya Ufundi Stadi, Vyuho vya Ufundi, Vyuho Vikuu pamoja na Taasisi za Utafiti na Maendeleo. Jumla ya wabunifu 415 walijitokeza ambapo, kati yao wabunifu mahiri 60 (10 kutoka katika kila kundi) walipatikana na kushiriki kilele cha mashindano. Hatimaye wabunifu watatu mahiri kwa kila kundi walipatikana na kupewa tuzo. Aidha, ubunifu wao utaendelezwa;
- (vii) imekusanya taarifa na kutambua teknolojia 165 zilizozalishwa nchini kwa lengo la kupata takwimu zitakazotumika kutengeneza kanzi- data ya teknolojia zinazoweza kutumika kutatua changamoto kwenye jamii na kuchangia katika ujenzi wa uchumi wa viwanda nchini;

(viii) imekagua na kutathmini utekelezaji wa miradi saba (7) inayotumia teknolojia ya nyuklia katika Sekta za Maji, Afya, Kilimo na Mifugo kwa ufadhili wa Shirika la Nguvu za Atomiki Duniani (IAEA) na kubaini kuwa utekelezaji wake unafanyika kulingana na makubaliano; na

(ix) imeshiriki Mkutano Mkuu wa 62 wa Shirika la Nguvu za Atomiki Duniani uliofanyika mwezi Septemba, 2018 jijini Vienna, Austria ambapo katika Mkutano huo miradi mipya mitano (5) itakayotumia teknolojia ya nyuklia ilipitishwa na imepata ufadhili.

### **Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali Watu**

**31. Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza jukumu la kusimamia na kuendeleza Rasilimali Watu, kwa mwaka 2018/19 Wizara imetekeleza yafuatayo:

(i) imeratibu na kusimamia ujenzi wa Ofisi za Wizara kwenye Mji wa Serikali Mtumba ambapo ujenzi umekamilika;

(ii) imeandaa Orodha ya Kazi na Maelezo ya Kazi kulingana na Muundo na Mgawanyo wa Majukumu ya Wizara ulioidhinishwa mwezi Julai, 2018. Orodha hii imesaidia Wizara kupata mahitaji kamili ya watumishi na kubainisha majukumu ya kila mtumishi kwa lengo la kuboresha utendaji wa Wizara;

(iii) imeandaa Mpango wa Mafunzo wa Miaka Mitatu (3) 2018/21 ambapo katika mwaka wa fedha 2018/19 watumishi 571 wameshiriki mafunzo ya muda mfupi na watumishi 43 wanapata mafunzo ya muda mrefu. ambayo yatawasaidia kuboresha utendaji kazi wao;

(iv) imeandaa, kuratibu na kutoa mafunzo mbalimbali ya kuwajengea uwezo watumishi. Watumishi 50 walipatiwa mafunzo ya Huduma kwa Wateja na Utunzaji wa Kumbukumbu; Watumishi 88 walipata mafunzo ya Uboreshaji wa utendaji kazi na usimamizi wa kumbukumbu na Watumishi 89 walipata mafunzo elekezi na kupewa

kiapo cha uadilifu katika utumishi wa umma na utunzaji siri serikalini;

(v) Watumishi 77 wanaotarajiwa kustaafu walipatiwa mafunzo ya kujiandaa kustaafu kazi ili kupunguza changamoto zinazowapata wastaafu mara utumishi wao unapofikia ukomo; na

(vi) imekamilisha uandaaji na uwekaji wa mfumo kwa ajili ya kuboresha utaratibu wa utunzaji wa kumbukumbu kwa njia ya kielektroniki katika masijala. Mfumo huu utarahisisha utendaji kazi na upatikanaji wa majalada.

### **Usimamizi wa Rasilimali za Wizara**

**32. Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha udhibiti na usimamizi wa rasilimali za Wizara, katika mwaka 2018/19 Wizara imetekeleza kazi zifuatazo:

(i) imekagua malipo ya mishahara (payroll) kuanzia mwezi Desemba, 2017 hadi Juni, 2018 kwa watumishi wa Wizara ili kubaini endapo watumishi wanaolipwa mishahara ni watumishi halali;

(ii) imekagua utekelezaji wa taratibu za ununuzi na usimamizi wa mikataba 22 ili kuhakikisha kuwa mikataba hiyo inatekelezwa kwa kuzingatia Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2011 na kanuni zake za mwaka 2013;

(iii) imefanya ukaguzi wa matumizi ya fedha katika miradi ifuatayo:

(a) Mradi wa kuimarisha Ufundishaji na Ujifunzaji wa Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (Literacy and Numeracy Education Support- LANES) ambapo jumla ya Mikoa 10, Halmashauri 18 na Ofisi 4 za Uthibiti Ubora wa Shule zilizopelekewa fedha za utekelezaji wa kazi za mradi wa LANES ilikaguliwa;

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

(b) mradi wa Kukuza Stadi za Kazi na Ujuzi kwa ajili ya shughuli za kuzalisha na kukuza uchumi (ESPJ);

(c) Mradi wa Ujenzi wa Vyuo vya Ualimu (Upgrading Teachers College-UTC);

(d) mradi wa Kuimarisha Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi na Elimu ya Ualimu (Support to Technical Vocational Education and Training and Teachers Education - STVET -TE);

(e) programu ya Lipa Kulingana na Matokeo katika Sekta ya Elimu (Education Program for Results- EP4R) kwa fedha za ujenzi wa shule ya sekondari ya wanafunzi wenye mahitaji maalum zilizopelekwa Chuo cha Ualimu Patandi na fedha za ujenzi wa Chuo cha Ualimu Murutunguru;

(f) miradi miwili (2) ya Vituo vya umahiri (ACE II) inayotekelezwa na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo. Miradi hiyo ni: *Innovative Rodent Pest Management and Biosensor Technology Development* (IRPM and BTM) na *Southern African Centre for Infectious Diseases Surveillance - (SACIDS)*; na

(g) miradi miwili (2) ya Vituo vya umahiri (ACEII) inayotekelezwa na Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela. Miradi hiyo ni: *Centre for Water Infrastructure and Sustainable Energy Future* (WISE FUTURE); na *Centre for Research, Agriculture Advancement, Teaching Excellence and Sustainability in Food and Nutritional Security* (CREATES). Lengo ni kuona kama matumizi ya fedha yanaendana na malengo ya mradi.

(iv) imekagua Taasisi tano (5) zilizopelekwa fedha za utekelezaji wa kazi za mradi wa kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK). Taasisi hizo ni: Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM), Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA), Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania (BOHUMATA) na Mtandao wa Elimu Tanzania - (TEN/ MET);

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

(v) imekagua taasisi tatu (3) zilizopelekewa fedha za utekelezaji wa kazi za mradi wa ESPJ ambazo ni: Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), *Tanzania Private Sectors Foundation (TPSF)*, na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU);

(vi) imekagua vifaa na kemikali za maabara zilionunuliwa katika Vyuo vya Ualimu kumi (10) kupitia mradi wa STVET -TE na EP4R ili kubaini endapo taratibu za manunuzi zilizingatiwa na vifaa hivyo vimefika kama ilivyokusudiwa;

(vii) imefanya uhakiki wa wanafunzi waliokuwa wakinufaika na Programu ya Ujuzi Vocha (Trainee Vouchers Scheme) inayotekelezwa na Bodi ya Mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) kupitia mradi wa ESPJ ambao ulifanyika katika Vyuo saba (7);

(viii) imefanya ukaguzi maalumu katika Chuo cha Ualimu llonga na Patandi kuhusiana na ujenzi wa Vyuo hivyo; na

(ix) imefanya ukaguzi wa matumizi ya Fedha za Wizara ili kubaini endapo matumizi yanayofanywa yamezingatia Sheria ya Fedha ya mwaka 2001 na Kanuni zake za mwaka 2004 pamoja na Miongozo mbalimbali iliyowekwa na Serikali.

**SHUGHULI ZILIZOFANYWA NA TAASISI NA MASHIRIKA YALIYOPO CHINI YA WIZARA YA ELIMU KWA MWAKA 2018/19**

**Taasisi ya Elimu Tanzania**

**33. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2018/19, Taasisi ya Elimu Tanzania imetekeleza kazi zifuatazo:

(i) imeandika vitabu vya kiada vya masomo ya Historia na Jiografia kwa Kidato cha 1 - 4, pamoja na masomo ya Sayansi (Biology, Chemistry, Physics na Basic Mathematics) na Kiswahili kwa Kidato cha 5 - 6;

(ii) imeandika, kuchapa na kusambaza jumla ya nakala 391,949 za vitabu vya somo la *English* Kidato cha Kwanza na cha Pili zilizogawiwa kwa uwiano wa kitabu kimoja kwa

wanafunzi watatu (1:3). Nakala hizi zimesambazwa katika Halmashauri zote za Tanzania Bara;

(iii) imekamilisha uandishi, uchapaji na usambazaji wa aina nane (8) za vitabu vya kiada vya wanafunzi wa Darasa la Tano kwa masomo ya Kiswahili, Hisabati, *English*, Uraia na Maadili, Maarifa ya Jamii, Stadi za Kazi, Sayansi na Teknolojia na *French* kwa kuzingatia mtaala wa mwaka 2015. Jumla ya nakala zilizosambazwa ni 2,933,791 kwa uwiano wa kitabu kimoja kwa wanafunzi watatu (1:3). Aidha, jumla ya nakala 281,148 za Kiongozi cha Mwalimu kwa masomo hayo vimesambazwa katika Halmashauri za Mikoa yote ya Tanzania Bara. Vitabu na viongozi hivi vitasaidia kuongeza ubora wa ufundishaji wa masomo husika kwa darasa husika;

(iv) imeandaa vitabu vya kiada kwa ajili ya wanafunzi wenye uoni hafifu na wasioona wa Darasa la Tatu na Nne ambavyo vimeandaliwa katika mfumo wa maandishi makubwa (large print), nukta nundu (braille) na Mchoro mguso (embossed drawing) ili kuwawezesha wanafunzi hao kusoma masomo yao kirahisi. Vitabu hivi kwa sasa vipo katika hatua ya usambazaji;

(v) imeandika Kiongozi cha Mwalimu kwa masomo 5 (Kuhesabu, Kuandika, Kusoma, Afya na Mazingira, na Sanaa na Michezo) ya Darasa la Kwanza na la Pili na aina saba (7) za Kiongozi cha Mwalimu kwa Darasa la Tatu. Vitabu hivyo vitamsaidia mwalimu kufundisha mada zilizokusudiwa kwa ufanisi zaidi;

(vi) imekamilisha usambazaji wa vitabu vya kiada nakala 6,286,476 kwa wanafunzi wa Darasa la Nne katika uwiano wa kitabu kimoja kwa mwanafunzi mmoja (1:1) kwa masomo ya Hisabati, *English*, Uraia na Maadili, Maarifa ya Jamii, Stadi za Kazi, Sayansi na Teknolojia na *French* katika Halmashauri zote za Tanzania Bara;

(vii) imesambaza katika Halmashauri zote nakala 7,835,697 za aina 25 ya vitabu vya Hadithi kwa Darasa la Kwanza na la Pili katika uwiano wa kitabu kimoja

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

wanafunzi watatu (1:3) ambavyo vitasaidia kumjengea mwanafunzi umahiri wa kusoma kwa kasi inayokusudiwa

(viii) imeandika Mwongozo wa uandishi na tathmini ya vitabu vya ziada na kuhuisha Mwongozo wa uandishi na tathimini ya vitabu vya kiada. Miongozo hii itasaidia waandishi binafsi na serikali kuandika vitabu vyenye ubora zaidi;

(ix) imeandika mwongozo wa uandaaji na tathmini ya maudhui ya kielektroniki. Mwongozo huu utasaidia katika upatikanaji wa maudhui ya kielektroniki yenye ubora na hivyo kuongeza matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji;

(x) imeandaa Mwongozo wa Kitaifa wa Mtaala (National Curriculum Framework) ambao utakuwa unaongoza zoezi la kuandaa na kuhuisha Mitaala nchini kwa ngazi za Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Mafunzo ya Ualimu;

(xi) imefanya tathmini ya miswada ya machapisho 188 ya vitabu vya ziada ili yaweze kupatiwa ithibati ambapo Miswada 33 ilipata ithibati. Miswada 155 bado inaendelea kufanyiwa maboresho ili iweze kufikia kiwango kinachotakiwa;

(xii) imeanza kurusha hewani kipindi cha Vikaragosi (*Cartoons*) kupitia TBC (siku ya Jumamosi na Jumapili kuanzia saa 4 asubuhi) – Kipindi cha watoto kitiwacho Nyota Njema kwa ajili ya kukuza stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa wanafunzi wa Darasa la Kwanza na la Pili;

(xiii) imeandaa Maktaba Mtandao (TIE - online library) itakayowezesha usambazaji wa machapisho mbalimbali ya Taasisi ikiwemo vitabu kwa wadau wa elimu kwa uharaka. Maktaba hiyo ilizinduliwa tarehe 30 Machi, 2019;

(xiv) imehuisha mtaala na mihtasari ya mafunzo ya Ualimu Tarajali (Pre- service) wa Astashahada ya Elimu Maalumu. Mihtasari hii itawezesha ufundishaji na ujifunzaji wa Elimu Maalumu kuwa rafiki;



## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

(xv) imeandaa Mwongozo wa utekelezaji wa mafunzo ya Ualimu ya Stashahada ya miaka mitatu ya masomo ya Sayansi na Biashara;

(xvi) imeboresha mihtasari ya masomo ya michepuo (Ufundi, Kilimo na Sayansi Kimu) Kidato cha Kwanza hadi cha Nne. Mihtasari hii itawezesha kuandaa wahitimu watakaokuwa na ujuzi zaidi katika fani husika;

(xvii) imeandaa Moduli za Mafunzo kazini kwa Walimu wa Elimu ya Awali, Darasa la Kwanza na la Pili. Moduli hizi zipo hatua ya uchapaji. Moduli hizi zinalenga kukuza uwezo wa walimu wa kufundisha stadi za KKK;

(xviii) imetoa mafunzo ya ujasiriamali kwa wakufunzi wa Vyuo vyote vya Serikali vya Ualimu. Mafunzo haya yatasaidia Wakufunzi kutoa elimu sahihi ya ujasiriamali kwa Walimu tarajali na Walimu hao watatoa elimu hii kwa wanafunzi wa shule za Msingi na Sekondari;

(xix) imeandika vitabu vya kiada aina sita (6) na vya hadithi aina 12 kwa Elimu ya Awali kwa shule zinazotumia Kiswahili kama lugha ya kufundishia. Vitabu hivi vipo katika hatua ya uchapaji;

(xx) imeandika vitabu vya kiada aina sita (6) kwa shule za Awali na aina 9 kwa Darasa la I mpaka la III kwa shule zinazotumia Kiingereza kama lugha ya kufundishia. Vitabu hivi vipo hatua ya uchapaji; na

(xxi) imeandika Kiongozi cha Mwalimu kwa masomo 6 (Kuhesabu, Kuwasiliana, Kushirikiana, Kutunza Mazingira, Kutunza Afya, Michezo na Sanaa) vya Elimu ya Awali.

### **Baraza la Mitihani la Tanzania**

**34. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2018/19, Baraza la Mitihani la Tanzania limetekeleza kazi zifuatazo:

(i) limekamilisha uchapaji, usafirishaji na usahihishaji wa Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne (SFNA) 2018 ambao ulifanyika tarehe 22 hadi 23 Novemba 2018. Jumla ya watahiniwa 1,302,461 walifanyiwa upimaji huo kati ya 1,362,642 waliokuwa wamesajiliwa;

(ii) limekamilisha uchapaji, usafirishaji na usahihishaji wa Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili (FTNA) 2018 ambao ulifanyika tarehe 12 hadi 23 Novemba 2018. Jumla ya watahiniwa 506,235 walifanyiwa upimaji huo kati ya 545,077 waliokuwa wamesajiliwa;

(iii) limekamilisha uchapaji, usafirishaji na usahihishaji wa Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi (PSLE) 2018 ambao ulifanyika tarehe 05 hadi 06 Septemba, 2018. Jumla ya watahiniwa 944,218 walifanya mtihani huo kati ya 957,904 waliokuwa wamesajiliwa;

(iv) limekamilisha uchapaji, usafirishaji na usahihishaji wa mitihani ya Kidato cha Nne (CSEE) na Maarifa (QT). Jumla ya watahiniwa 414,197 walifanya mtihani huo kati ya 426,988 waliokuwa wamesajiliwa. Aidha, jumla ya watahiniwa 12,237 walifanya mtihani wa Maarifa kati ya 14,344 waliokuwa wamesajiliwa; limekamilisha usajili wa watahiniwa wa Kidato cha Sita (ACSEE) na Ualimu 2019 ambapo jumla ya watahiniwa 87,169 wa Kidato cha Sita na 11,824 wa Ualimu wanatarajia kufanya mitihani hiyo kuanzia tarehe 06 hadi 23 Mei, 2019; na

(v) limenunua mashine 6 za kisasa zinazotumika kuandaa na kuchapa mitihani na vyeti vya wahitimu.

### **Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM)**

**35. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2018/19, Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM) umetekeleza majukumu yafuatayo:

(i) umedahili jumla ya wanachuo 2,431 ambapo, kati yao wanachuo 1,890 ni wa kozi ya Stashahada ya Uongozi na

Usimamizi wa Elimu (DEMA) na Wanachuo 541 kwa kozi ya Stashahada ya Ukaguzi wa Shule;

(ii) umedahili walimu wakuu 482 (99%) kati ya 486 walioomba kwa ajili ya Astashahada ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu (CELMA) kutoka Mikoa ya Iringa, Mbeya, Songwe na Njombe. Lengo ni kuwajengea uwezo Walimu wa Shule za Msingi katika masuala ya Uongozi wa Elimu. Walimu Wakuu waliopata mafunzo wanatoka katika Wilaya za Kyela, Chunya, Iringa, Ludewa, Wanging'ombe na Songwe;

(iii) umeboresha Mtaala wa Mafunzo ya Uongozi kwa kuongezea masomo ya kufundishia ya Hisabati, Sayansi na Maarifa ya Jamii katika ngazi ya Elimu ya Msingi ili kuwapa wahitimu maarifa na mbinu za kufundisha masomo hayo;

(iv) umetoa Mafunzo kwa Walimu 1,545 wa Darasa la Kwanza na la Pili kuhusu Stadi za KKK kwa Mikoa mitano (5) ya Tanzania Bara ambayo ni Dar es Salaam, Geita, Mwanza, Tanga na Morogoro ili kuwajengea uwezo walimu na kuongeza idadi ya walimu wenye uwezo wa kufundisha stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) katika Shule za Msingi;

(v) umefanya utafiti wa majaribio kwa lengo la kupima nyenzo zitakazotumika katika tafiti na kubainisha maeneo muhimu katika kuimarisha usimamizi na uongozi wa shule, Uthibiti wa Elimu pamoja na stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu;

(vi) umeweka mfumo wa *e-library* na mfumo maalumu wa kutambua vitabu (KOHA) kwa ajili ya kuwawezesha watumiaji wa Maktaba kupata huduma kwa urahisi mahali popote nje ya jengo la Maktaba na ndani ya majengo ya Wakala;

(vii) umefadhili mafunzo kwa Watumishi wanne (4) katika ngazi ya Shahada ya Uzamivu kwa lengo la kuwajengea uwezo ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi;

(viii) umekarabati bwani lenye uwezo wa kulaza wanachuo 200, hivyo, kupunguza changamoto ya malazi kwa wanachuo; na

(ix) unaendelea kukamilisha ukarabati wa ukumbi wa chakula wenye uwezo wa kuhudumia wanachuo 176 kwa wakati mmoja ili kuboresha mazingira ya kutolea huduma ya chakula kwa wanafunzi.

### **Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW)**

**36. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2018/19 Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima imetekeleza yafuatayo:

(i) imedahili jumla ya wanafunzi 2,642 (Wanaume 1,075, Wanawake 1,567) wa Astashahada, Stashahada, na Shahada katika kampasi za Dar es Salaam, WAMO - Morogoro na Luchelele – Mwanza;

(ii) imekamilisha rasimu ya Mkakati wa Kitaifa wa Kisomo na Elimu kwa Umma (National Literacy and Mass Education Strategy). Kukamilika kwa rasimu ya mkakati huu kutasaidia kuleta ufanisi katika utekelezaji wa programu za kisomo;

(iii) imekamilisha uwekaji wa mtandao wa TEHAMA (Local Area Network- LAN) kwenye jengo la TEWW Makao Makuu ambao utaongeza ubora wa ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi na jamii yote ya TEWW;

(iv) imepanua Maktaba ya Makao Makuu ili kuiwezesha kuhudumia wanafunzi 160 kwa wakati mmoja ikilinganishwa na wanafunzi 80 waliokuwa wanaweza kuhudumia hapo awali; na

(v) imetekeleza miradi mbalimbali ya Elimu ya Watu Wazima kwa kushirikiana na wadau, kama ifuatavyo:

(a) Mradi wa Elimu ya Sekondari kwa Wasichana walio nje ya Shule yaani *Secondary Education for Out of School Adolescent Girls* (SEOSAG). Walengwa ni wasichana

waliokatisha masomo kwa sababu mbalimbali ikiwemo kupata mimba za utotoni. Mradi unatekelezwa kwa majaribio katika Halmashauri mbili za Mkoa wa Tanga, ambazo ni Halmashauri ya Wilaya ya Tanga Mjini na Korogwe. Takribani wasichana 700 wamesajiliwa;

(b) Mpango wa Elimu Changamanikwa Vijana walio nje ya Shule yaani *Integrated Program for Out of School Adolescents* (IPOSA). Mpango una maeneo makuu manne ya ujifunzaji yaani Stadi za kisomo; Stadi za ufundi wa awali; Stadi za maisha na Ujasiriamali. Mpango unatekelezwa katika mikoa minane, ambayo ni Dar es Salaam, Tabora, Dodoma, Kigoma, Njombe, Iringa, Mbeya na Songwe ambapo kwa kuanzia, jumla ya vijana na watu wazima 10,000 wanatarajiwa kufikiwa ifikapo Juni, 2021 jumla ya Vijana na Watu Wazima 3,238 wameandikishwa hadi sasa. Kati ya hao Wanaume ni 1,798 na Wanawake ni 1,440;

(c) Mradi wa kuwawezesha kielimu wasichana wenye umri wa miaka 14-24 (Empowering Girls through Education) unaolenga kuwawezesha wasichana walio nje ya mfumo rasmi wa shule kupata fursa ya elimu. Ni mpango unaotekelezwa katika Mikoa ya Arusha, Kigoma na Mwanza. Aidha, mpango huu unatekelezwa kwa kutumia TEHAMA ili kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji; na

(d) Mradi wa majaribio wa kuwawezesha vijana katika kuongeza thamani mazao ya samaki, unaofanyika katika Mkoa wa Mwanza katika kampasi ya Luchelele.

## **Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania**

**37. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2018/19, Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania imetekeleza kazi zifuatazo:

(i) imewezesha upatikanaji wa vitabu 41,964 ambapo, vitabu 770 vimepatikana kwa mujibu wa Sheria ya Bunge Namba 6 ya mwaka 1975 iliyoanzisha Bodi ya Huduma za Maktaba na vitabu 41,194 vimepatikana kwa ufadhili.

Aidha, jumla ya magazeti 15,916 yalinunuliwa na majarida 1,547 yamepatikana kwa ufadhili. Upatikanaji wa machapisho haya umesaidia kuongeza uelewa kwa jamii kuhusiana na masuala mbalimbali katika sekta za elimu, siasa na uchumi;

(ii) imetoa ushauri wa kitaalamu kuhusiana na masuala ya uanzishaji na uendeshaji wa Maktaba katika Wilaya tano (5) ambazo ni Sikonge, Tunduma, Mpwapwa, Hai –na Nachingwea. Aidha, imetoa ushauri kwa shule za msingi 26, sekondari nne (4) na vituo vya jamii (community centers) vinne (4). Lengo ni kuhakikisha kuwa Maktaba zote zinazoanzishwa kwa kuzingatia vigezo na masharti husika; na

(iii) imedahili jumla ya wanafunzi 720 katika Chuo cha Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka (SLADS) kwa mchanganuo ufuatao: *NTA* Ngazi ya 4 wanafunzi 231, *NTA* Ngazi ya 5 wanafunzi 234 na *NTA* Ngazi ya 6 wanafunzi 255.

### **Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi - VETA**

**38. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2018/19, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi - VETA imetekeleza kazi zifuatazo:

(i) imeanza ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi na Huduma (RVTSs) vya mikoa ya Rukwa na Geita, ambapo ujenzi uko katika hatua mbalimbali za utekelezaji;

(ii) inakamilisha hatua za mwisho za manunuzi kwa ajili ya kupata Mkandarasi wa Ujenzi wa Chuo cha Mkoa wa Simiyu;

(iii) inaendelea na ujenzi wa chuo cha ufundi stadi cha Wilaya ya Chato, ambapo ujenzi umefika asilimia arobaini na nane (48) na unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2019;

(iv) inaendelea na mchakato wa kumpata Mkandarasi ili kuendelea na ujenzi wa VETA Mkoa wa Njombe baada ya Mkandarasi wa awali kusimamishwa;

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

(v) imekamilisha matayarisho ya eneo la ujenzi wa mradi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Mkoa wa Kagera ambao utatekelezwa kuanzia Julai 2019 kwa msaada wa Serikali ya Watu wa China. Mkandarasi *Shanxi Construction Company* kutoka Jamhuri ya Watu wa China ndiye atakayefanya kazi ya ujenzi;

(vi) imekamilisha ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya Namtumbo. Chuo hicho kilizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mnamo tarehe 5 Aprili, 2019;

(vii) imekamilisha maandalizi ya michoro na zabuni kwa ajili ya ujenzi wa vyuo viwili (2) vya Ufundi Stadi vya wilaya ya Kilindi na Karagwe kwa lengo la kuongeza udahili na kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Ujenzi unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha wa 2019/2020;

(viii) imeendelea na kazi ya ukarabati na upanuzi wa chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya Karagwe, kwa lengo la kuongeza udahili na kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia;

(ix) imekamilisha ujenzi wa karakana ya kisasa ya Useremala katika Chuo cha Ufundi Stadi na Huduma cha Mkoa wa Dodoma, ambapo majengo yaliyokamilika yalikabidhiwa rasmi kwa VETA tarehe 22 Machi, 2019. Taratibu za ununuzi na ufungaji wa Mitambo na Vifaa zinaendelea kufanyika;

(x) imekamilisha ujenzi wa karakana za Useremala, Umeme wa Magari na Jengo la utawala katika Chuo cha Ufundi Stadi na Huduma cha Mkoa wa Morogoro – Kihonda;

(xi) inaendelea na ujenzi wa mabweni mawili (2) na nyumba mbili (2) za wafanyakazi katika Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya Makete. Mradi huu unalenga kuongeza nafasi za bweni kwa wasichana na kuboresha makazi ya wafanyakazi ili kuongeza motisha;

## NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

(xii) imekamilisha ujenzi wa karakana ya Ushonaji katika chuo cha Ufundi Stadi na Huduma cha Mkoa wa Pwani;

(xiii) inaendelea na ujenzi wa mabweni mawili katika chuo cha Ualimu wa Ufundi Stadi cha Morogoro;

(xiv) imekamilisha utafiti wa kubaini mahitaji ya ujuzi na utaalamu katika sekta mbili (2) za mafunzo ambazo ni viwanda na utalii na ukarimu. Utafiti huu utasaidia kuboresha Mitaala ya fani mbalimbali katika sekta husika ili kukidhi mahitaji ya soko;

(xv) imedahili wanafunzi 222,683 katika mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi katika Vyuo vya Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini, ambapo wanafunzi wa kike ni 75,349 (sawa na asilimia 34);

(xvi) imesajili Vyuo 603, kati ya hivyo 71 vimepatiwa usajili wa kudumu na ithibati, na 532 vimepatiwa usajili wa awali;

(xvii) imetoa mafunzo ya *Microteaching* kwa walimu wa ufundi stadi 89; kati yao 38 ni wenye Stashahada na 51 wenye vyeti vya ufundi. Mafunzo hayo yataboresha ujuzi wa Walimu wa Ufundi Stadi ili kuendana na mabadiliko ya kiteknolojia;

(xviii) inaendelea na umaliziaji wa majengo na ununuzi wa vifaa kwa ajili ya kuanzisha Vyuo vya Ufundi Stadi katika Wilaya za Ileje, Nkasi, Urambo, Newala, Muleba, Kasulu DC, Itilima, Ngorongoro na Babati; na

(xix) inaendelea na taratibu za kupata ardhi na hatimiliki kwa ajili ya ujenzi wa vyuo vya Ufundi Stadi ya Wilaya za Kongwa, Ruangwa, Nyasa na Kasulu TC.

### **Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi**

**39. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2018/19, Baraza limetekeleza kazi zifuatazo:



*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

(i) limekagua Vyuo 29 na kutoa usajili kwa Vyuo 26 vya Elimu ya Ufundi; Idara 35 zimetambuliwa ili kuweka usawa katika utoaji wa elimu na mafunzo ya ufundi bora kwa ngazi zote na Vyuo vitano (5) vimekaguliwa kuhakiki ubora wa taaluma kulingana na vigezo vya Baraza;

(ii) limefanya tathmini na kutoa ithibati kwa Vyuo 179 ili viweze kutoa mafunzo ya ufundi yenye ubora;

(iii) limefuatilia Vyuo 265 na kufanya tathmini ya ubora wa mafunzo yanayotolewa. Vyuo ambavyo havikukidhi vigezo vya utoaji wa mafunzo vilizuliwa kudahili wanafunzi ili kuvipa nafasi ya kurekebisha mapungufu yaliyobainika. Aidha, Vyuo 255 vilipatiwa ushauri juu ya namna ya kuboresha utoaji wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi;

(iv) limehakiki Mitaala 38 inayozingatia umahiri ambapo mtaala mmoja (1) wa fani ya Maendeleo ya Jamii ngazi ya Nne hadi ya Sita (NTA Level 4 - 6) umehuishwa. Aidha, ukusanyaji wa maoni ya wadau kwa ajili ya kuhuisha Mitaala mitano (5) unaendelea;

(v) imehakiki na kutoa ithibati kwa Mitaala 9 ya kitaifa inayokuzwa na mamlaka nyingine ikiwa ni pamoja na Wizara ya Afya, Kilimo, Mifugo, Uvuvi, Mambo ya Ndani, na Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala Bora. Lengo ni kuhakikisha kuwa Mafunzo yanayotolewa yanakidhi soko la sasa na baadaye;

(vi) limeratibu na kuhakiki udahili wa Wanafunzi 158,819 (Wanaume 83,836 na Wanawake 74,983) katika ngazi ya Astashahada ya Awali (Basic), Astashahada na Stashahada ambapo fani za Sayansi na Teknolojia shirikishi ni 26,278, Ualimu ni 1,776, Afya na Sayansi ni 13,748 na Biashara, Utalii na Mipango ni 117,017;

(vii) limefanya tathmini ya vyeti 13,634 vilivyopokelewa kwa ajili ya kutoa namba ya uthibitisho (Award Verification Number) kwa ajili ya uthibitisho ili kudhibiti uendeshaji wa mafunzo bila kufuata kanuni na sheria zilizowekwa na Baraza;

(viii) limefanya ufuatiliaji katika Vyuo 12 ambavyo vimebainika kukiuka taratibu na kanuni zilizowekwa na Baraza ili kudhibiti uendeshaji wa mafunzo bila kufuata kanuni na sheria zilizowekwa na Baraza;

(ix) limetoa mafunzo juu ya Mitaala inayozingatia umahiri kwa wakufunzi 256 wa Vyuo vya Elimu ya Ufundi. Mafunzo haya yatasaidia wahitimu katika Vyuo vya ufundi kupata ujuzi uliokusudiwa;

(x) limekagua ubora wa rasilimali watu na kufanya uhakiki kwa kufuata muundo wa mgawanyo wa majukumu na muundo wa maendeleo ya utumishi kwa wakufunzi (*Harmonized Scheme of Services*) katika Vyuo 26 kwa lengo la kuhakikisha kuwa Vyuo hivi vina wakufunzi wenye sifa kulingana na kozi zinazotolewa;

(xi) limefanya tathmini na ulinganifu kwa Tuzo 180 ili kudhibiti viwango vya Elimu ya Ufundi nchini;

(xii) limeandaa vitabu 13 vya mwongozo wa matumizi ya mifumo ili kurahisisha utumiaji wa mifumo hiyo na kurahisisha utendaji;

(xiii) limefanya utafiti kwa lengo la kubaini upungufu wa ujuzi uliopo katika kufanikisha dhamira ya Serikali ya kujenga Uchumi wa Viwanda; na

(xiv) limeunganisha mifumo ya TEHAMA kwa njia ya Programu yenye kuwezesha Mifumo iliyotengenezwa kwa lugha mbalimbali kuweza kuwasiliana (*Application Programming Interface* (API) ili kuiwezesha OR- TAMISEMI kupata taarifa za waombaji wa ajira katika kada mbalimbali kutoka kwenye kanzidata ya Baraza.

## Mamlaka ya Elimu Tanzania

**40. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2018/19, Mamlaka imetekeleza kazi zifuatazo:

(i) imeendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa nyumba 60 za walimu katika shule za sekondari 15 ambao uko katika hatua mbalimbali za ujenzi. Ujenzi katika shule 11 zilizopo Mabira (Kyerwa), Kalenge (Uvinza), Mnacho (Ruangwa), Matambarare (Ruangwa), Tegeruka (Musoma), Lupaso (Masasi), Makonde (Njombe), Matipwili (Chalinze), Milundikwa (Nkasi), Monica Mbega (Nyasa) na Matumbo (Singida), Ikobe (Mbogwe), Bunduki (Mvomero), Kongolo (Magu) na Bushiri (Pangani);

(ii) imeendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa madarasa 252 katika shule za Msingi 84; na

(iii) imeendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa mabweni 12, katika shule za sekondari 11.

### **Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu**

**41. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2018/19, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu imetekeleza kazi zifuatazo:

(i) imehuisha na kutoa Mwongozo wa maombi ya mikopo kwa Lugha ya Kiswahili na Kiingereza ambao ulisambazwa kwa njia mbalimbali zikiwemo magazeti, tovuti, redio na runinga ili kuelimisha waombaji;

(ii) imepanga na kutoa mikopo yenye thamani ya **Shilingi 424,758,636,617.00** kwa wanafunzi 122,754; kati yao wanufaika 41,234 ni wa mwaka wa kwanza na 81,520 ni wanafunzi wanaoendelea na masomo;

(iii) imetoa ruzuku ya **Shilingi 2,994,628,875** kwa wanafunzi 893 wapya wa Vyuo vya ndani ya nchi na wanafunzi 13 wanaoendelea na masomo kupitia udhamini wa Serikali ya Ujerumani (DAAD Scholarships);

(iv) imekusanya mikopo iliyoiva yenye thamani ya **Shilingi 128,076,510,388.48** hadi tarehe 15 Aprili, 2019. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 81.2 ya lengo la makusanyo ambalo ni **Shilingi Bilioni 157.7**;

(v) imetambua na kutoa hati za madai kwa wadaiwa wapya 14,627 wa mikopo (ambayo ni asilimia 47 ya lengo la kubaini wadaiwa 31,000), kufanya ukaguzi kwa waajiri wapatao 2,698 kati ya lengo la waajiri 3,426;

(vi) imetekeleza kampeni mbili (2) zilizohusu utambuzi wa wanufaika na wajibu wa waajiri katika mkoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Kigoma, Zanzibar, Dodoma, Singida, Mbeya na Arusha;

(vii) imetoa elimu kuhusu vigezo, wajibu wa wanufaika na waajiri kupitia katika maonesho ya Sabasaba, ya Vyuo Vikuu, mikutano ya wanafunzi, vyombo vya habari na mitandao ya kijamii; na

(viii) imetekeleza awamu ya kwanza ya maboresho ya mifumo ya TEHAMA kwa kubuni na kufanya majaribio, moduli za maombi na uchambuzi, ulipaji, na urejeshaji wa mikopo pamoja na kuunganisha mifumo ya malipo ya ndani na mifumo ya kielektroniki wa malipo ya Serikali (GePG).

## **Tume ya Vyuo Vikuu**

**42. Mheshimiwa Spika**, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania katika mwaka wa fedha 2018/19 imetekeleza yafuatayo:

(i) imeratibu udahili wa wanafunzi waliotaka kujiunga na masomo kwa mwaka 2018/19;

(ii) imefanya mapitio na kuboresha Mwongozo wa udahili kwa mwaka wa masomo 2018/19 ngazi ya shahada na kuhuisha uwezo wa Vyuo kuchukua wanafunzi kwa kila programu kulingana na vigezo vilivyopo;

(iii) imeandaa, imechapisha na kusambaza vipeperushi 5,000 vya masuala ya udahili;

(iv) imefanya mkutano maalumu na wakuu wa Taasisi za Elimu ya juu kuhusu maboresho katika mfumo wa udahili wa

Tume na mambo ya kuzingatia kwa vyuo vyote kwa mwaka wa masomo 2018/19;

**43. Mheshimiwa Spika;** katika Uthibiti wa Ubora wa Elimu ya Juu, Tume imetekeleza yafuatayo:

(i) imefanya mapitio ya miongozo inayotumika katika usimamizi na uthibiti ubora katika Elimu ya Juu na kufanya maboresho. Maboresho hayo yalipitiwa na wadau wa Elimu ya Juu katika mkutano maalumu uliohudhuriwa na wakuu wa taasisi za Elimu ya Juu kwa lengo la kupata maoni ya kuhuisha mwongozo wa uthibiti ubora na ithibati. Maoni yanafanyiwa kazi na wataalamu kabla ya Tume haijaidhinisha miongozo hiyo kwa kutumika ifikapo Juni 2019. Kazi hii imekamilika kwa kiwango cha asilimia 80;

(ii) imefanya ukaguzi wa kawaida na kushitukiza kwa vyuo **21** kwa lengo la kuhakiki ubora. Baadhi ya Vyuo hivyo vilibainika kuwa na mapungufu kadhaa yanayoathiri utoaji wa elimu bora. Tume imeendelea kuvishauri na kuelekeza vyuo hivyo kurekebisha mapungufu hayo kwa mujibu wa Sheria na Taratibu zilizopo;

(iii) Tume ilipokea maombi 280 ya Mitaala mbalimbali ya masomo kutoka Vyuo Vikuu nchini kwa lengo la kuitathmini na kuiidhinisha. Hadi kufikia tarehe 15 Aprili 2019 Mitaala 164 ilikuwa imeshaidhinishwa, Mitaala 63 ipo kwenye hatua ya kuidhinishwa baada kukamilisha uchambuzi na Mitaala 53 iliyobaki ipo katika hatua mbalimbali za uchambuzi;

(iv) imepokea maombi ya kutathmini na kutambua tuzo 1,716 za ngazi mbalimbali zilizotolewa katika Vyuo vya Elimu ya Juu nje ya nchi. Kati ya hizo, tuzo 723 zilitambuliwa na zingine zilirudishwa kwa wahusika kwa kukosa nyaraka muhimu za utambuzi kulingana na Mwongozo;

(v) imefanya maboresho ya mfumo wa kukusanya taarifa unaojulikana kama *Universities Information*

*Management System* (UIMS) ili kurahisisha ukusanyaji na utoaji wa taarifa mbalimbali toka Vyuo Vikuu. Mfumo huo umeunganishwa na mfumo ya Vyuo vya Elimu ya Juu ili kukusanya na kupata taarifa kwa wakati. Pia mfumo huu umeunganishwa na mfumo wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia unaojulikana kama 'ESMIS' ili kuwezesha kupata taarifa mbalimbali za vyuo bila kupitia vyuoni;

(vi) imetoa mafunzo kwa mameneja wa kanzidata na maafisa udahili wa Vyuo 82 vya Elimu ya Juu kuhusu matumizi ya mfumo wa mfumo wa ukusanyaji na utoaji wa taarifa;

(vii) imeshiriki katika mikutano na makongamano yaliyofanyika nchini Rwanda, Uganda, Senegal na Kenya yanayohusu usimamizi na uthibiti ubora katika Elimu ya Juu. Tume imejifunza na kubadilishana uzoefu kuhusu usimamizi, uthibiti na ithibati mbalimbali katika Elimu ya Juu;

(viii) imefanya maonesho ya 13 ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia katika viwanja vya Mnazi Mmoja, Dar es Salaam. Jumla ya taasisi 75 za ndani na nje ya nchi zilishiriki vikiwemo Vyuo Vikuu, Taasisi za Utafiti, Taasisi chini ya Wizara, Taasisi za Serikali na Taasisi Binafsi zinazojihusha na masuala ya Elimu ya Juu. Maonesho hayo yameweza kuongeza uelewa mpana wa huduma zinazotolewa hususani programu za masomo vyuoni, tafiti, ushauri pamoja na huduma nyinginezo za Elimu ya Juu; na

(ix) imeratibu uhamisho wa ndani wa Wanafunzi 2,707 kutoka Chuo kimoja kwenda Vyuo vingine. Uhamisho ulihusisha vyuo vinane vilivyokuwa na changamoto katika utoaji wa elimu bora.

## **Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia – COSTECH**

**44. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2018/19 Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia – COSTECH imetekeleza kazi zifuatazo:

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

(i) imeendelea kuelimisha umma kuhusu matumizi ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu katika shughuli za kiuchumi na kijamii kwa kuchapisha makala 112 katika magazeti mbalimbali kama vile *Daily News, Guardian, Citizen, Nipashe, Mwananchi, Habari Leo* na *Mtanzania*. Aidha, imerusha vipindi vya redio sita katika vituo vya redio za TBC Taifa, *Clouds FM, East Africa*, na vipindi vya televisheni 11 katika vituo vya *TBC 1, Clouds TV, East Africa, Star TV, Azam TV, TV 1*; na kuandaa makala za televisheni tatu ambazo zimewekwa katika mitandao ya kijamii;

(ii) imetoa mafunzo kwa washiriki 20 wakiwemo wasimamizi wa masuala ya Bioteknolojia katika taasisi na Wizara mbalimbali kwa lengo la kuwaongezea ujuzi, maarifa na uwezo kuhusu kanuni za usalama wa mazingira na taratibu za uendeshaji wa masuala yanayohusu Bioteknolojia.

(iii) imeendesha warsha iliyohusisha wadau 33 kuhusu teknolojia na usalama wa Bioteknolojia mjini Unguja, Zanzibar ili kukuza ufahamu wa usimamiaji wa kanuni zinazoongoza Bioteknolojia pamoja na kuwajengea uwezo wasimamizi wa kuandaa sheria itakayoongoza teknolojia hiyo maalum kwa Zanzibar;

(iv) imejenga uwezo kwa watafiti kutoka Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST), Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) na Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) katika masuala ya hakimiliki dhihini (Intellectual Property Right) kwa lengo la kuwawezesha kulinda na kunufaika na matokeo ya utafiti wao;

(v) imeendelea kufadhili na kusimamia miradi ya utafiti katika maeneo ya vipaumbele vya kitaifa katika sekta za Viwanda, TEHAMA, Kilimo, Afya, Mazingira na Maliasili yenye thamani ya shilingi Bilioni 3.581;

(vi) imewawezesha wabunifu 30 jumla ya **Shilingi Bilioni 1.24** ili kuendeleza ubunifu wao;

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

(vii) imeanzisha na kufadhili vituo atamizi 17 kiasi cha **Shilingi milioni 740.9** kwa ajili ya kukuza na kuendeleza ubunifu na hivyo kuongeza fursa za ajira na kiuchumi;

(viii) imetoa mafunzo kwa taasisi na Vyuo Vikuu 50 Tanzania Bara na Visiwani juu ya ukusanyaji wa takwimu zinazohusiana na sayansi, teknolojia na ubunifu;

(ix) imewajengea uwezo watafiti 57 kutoka katika vitengo vya utafiti katika idara mbalimbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Taasisi inayoratibu Utafiti wa Afya ya Zanzibar (Zanzibar Health Research Institute) kwa lengo la kuwezesha kufanya na kuratibu tafiti zinazolenga kutatua changamoto mbalimbali katika jamii;

(x) kwa kushirikiana na East Africa Science and Technology Commission (EASTECO) iliratibu mkutano ulioshirikisha watafiti nchini kuibua viupaumbele vya utafiti kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ambavyo vitatoa Mwongozo kwa watafiti katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na kuainisha Vipaumbele muhimu vya utafiti;

(xi) imeendelea na ujenzi na ukarabati wa maabara za utafiti wa Taasisi za Utafiti wa Mifugo Tanga (TALIRI - Tanga), Taasisi za Utafiti wa Mifugo Uyole (TALIRI - Uyole) na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi (TAFIRI – Sota, Musoma);

(xii) imetoa fedha **Shilingi 1,771,953,960.00** kwa ajili ya miradi mipya minane (8) ya ukarabati wa miundombinu ya utafiti katika Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR), Chuo Kikuu cha Sokoine cha kilimo, Taasisi ya Utafiti na Mafunzo ya Tengeru (HORTI Tengeru), TALIRI- Mpwapa, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS) na Taasisi ya Chanjo za Mifugo Kibaha (TVI). Lengo la ukarabati huu ni kuboresha miundombinu ya utafiti ili kufanya matokeo ya utafiti yawe na ubora zaidi;

(xiii) imeendeleza miradi minne ya utafiti kwa lengo la kubiashirishwa kwa kupewa ufadhili wa **Shilingi milioni 65**



kwa kila mradi; miradi hiyo ni Udhibiti wa maambukizi ya bakteria kwa kutumia bakteria wengine; mfumo wa kuchuja maji; matumizi ya TEHAMA kwenye uvuvi; na matumizi ya dawa za mitishamba;

(xiv) imefadhili miradi minne ya utafiti (Commissioned Research) iliyotokana na maombi maalumu kutoka katika taasisi za TAFIRI, Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) na Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda (TIRDO) kwa lengo la kutatua changamoto zilizojitokeza katika sekta ya uvuvi na nishati. Aidha, Tume imefadhili miradi miwili yenye thamani ya **Shilingi milioni 860** inayoratibiwa na Tume ya Mipango ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar; na

(xv) imefadhili watafiti sita kwa gharama ya **Shilingi 420,000,000** katika mafunzo baada ya Shahada ya Uzamivu (Post Doc) kwa lengo la kuongeza Rasilimali watu katika nyanja za Kilimo, afya na Maliasili.

#### **Tume ya Nguvu za Atomiki**

**45. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2018/19 Tume ya Nguvu za Atomiki imetekeleza yafuatayo:

(i) imepokea na kutathmini maombi 360 ya leseni za kutumia, kumiliki, kusafirisha na kuingiza nchini vyanzo vya mionzi ambapo leseni 351 sawa na asilimia 97.5 zimetolewa na maombi tisa (9) yasiyokidhi vigezo yamekataliwa;

(ii) imekagua migodi ya chini ya ardhi (underground mine) sita (6) ambayo ni *Geita Gold Mine, North Mara Gold Mine, Bulyankulu Gold Mine, Tanzanite One Limited, Stamigold Company Limited* na *Buzwagi Gold Mine* na kubaini kuwa ipo salama na haina madhara ya mionzi kwa mazingira na wafanyakazi;

(iii) imekagua na kuhakiki vituo 590 vya vyanzo vya mionzi nchi nzima ambapo ukaguzi huo ulibaini kuwa vituo 421 vilikuwa vinaendeshwa kwa kufuata taratibu husika. Aidha, vituo 67 vya vyanzo vya mionzi vilikuwa vinafanya kazi bila kusajiliwa na vituo 102 vilikuwa vinatumia vyanzo vya

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

mionzi bila kufuata utaratibu wa kiusalama ambapo vituo 40 vimekwishatimiza masharti na hivyo kuruhusiwa kuendelea na kazi zake;

(iv) imesajili vituo vipya 101 kwa ajili ya kuanza kutumia vyanzo vya mionzi. Hivyo, hadi kufikia tarehe 15 Aprili 2019 vituo vya mionzi vilivyosajiliwa ni 900;

(v) imepima wafanyakazi 1,663 kwenye vituo 376 sehemu mbalimbali nchini. Upimaji huo ulibaini kuwa katika vituo vyote viwango vya mionzi vilikuwa kati ya 0.1 mSv hadi 3.4 mSv ambavyo ni salama kwa binadamu;

(vi) ilisafirisha vyanzo vya mionzi viwili (2) vilivyokwisha muda wa matumizi kutoka Wakala wa Barabara na Shule ya Kimataifa ya Tanganyika na kuhifadhiwa katika jengo maalumu la kutunzia mabaki ya vyanzo vya mionzi jijini Arusha kwa lengo la kuzuia madhara yanayoweza kutokea kutokana na vyanzo hivyo;

(vii) ilipima Sampuli 12,628 na kutoa vibali 12,628 vilivyojumuisha sampuli za vyakula 12,069, mbolea 172, Sigara 155 na matumizi mengine kama chakula cha mifugo 232. Sampuli zote zilizopimwa hazikuwa na mionzi hatarishi na hivyo kuwa salama kwa matumizi yaliyokusudiwa;

(viii) imeendelea kuratibu miradi saba (7) ya kitaifa na kushiriki katika miradi 40 ya kikanda ambayo inatekelezwa kwa ushirikiano na Shirika la Nguvu za Atomu Duniani. Miradi hii itawezesha nchi kuimarisha matumizi ya sayansi na teknolojia ya nyuklia;

(ix) imefungua ofisi ya kanda ya ziwa jijini Mwanza na ofisi zingine ndogo saba (7) katika maeneo ya Kigoma, Pemba, Mtwara (Mtambaswala na Kilambo), Kagera (Kabanga), Songwe (Kasumulu) na Uwanja wa ndege wa Kilimanjaro (KIA) hivyo kuifanya TAEC kuwa na jumla ya ofisi 22 nchini. Lengo ni kuthibiti matumizi salama ya mionzi na kuwasogezea wananchi huduma karibu;

(x) ilinunua vifaa 17 kwa ajili ya ofisi za mipakani kwa thamani ya **Shilingi 146,068,945.14**. Viwili kati ya hivi ni kwa ajili ya kuthibiti ubora wa machine za tiba ya mionzi (quality control kits) na vingine 15 kwa ajili ya kuthibiti matumizi salama ya mionzi ya bidhaa mbalimbali zinazoingia na kutoka nje na nchi;

(xi) imeendelea kujitangaza kwa kutumia maonesho ya Sabasaba, Nanenane, sherehe za Mapinduzi ya Zanzibar na vipindi ya Televisheni na Redio pamoja na mitandao ya jamii. Hadi kufikia tarehe 2 Aprili 2019, TAEC ilishiriki katika maonesho matatu (3), jumla ya vipindi 45 vya redio na 24 vya runinga vilirushwa hewani. Aidha, vipeperushi na vijarida 4,922 vilisambazwa kwa lengo la kuongeza uelewa juu ya kazi zinazofanywa na Tume;

(xii) iliandaa mkutano wa Kanda ya Afrika wa IAEA ambapo washiriki 46 kutoka nchi 42 za Afrika walihudhuria. Mkutano huo ulipitia utekelezaji wa malengo ya miradi na kuweka mikakati ya kuwezesha sayansi na teknolojia ya nyuklia kuchangia kwenye maendeleo ya Taifa; na

(xiii) Iliendesha mafunzo maalum ikishirikiana na IAEA kwa vyombo vya usalama kwa ajili ya kusimamia ulinzi na usalama wakati wa mashindano ya mpira wa miguu kwa vijana chini ya umri wa miaka 17 yaliyofanyika Jijini Dar es Salaam mwezi wa Aprili 2019.

## **Chuo Kikuu cha Dar es Salaam**

**46. Mheshimiwa Spika**, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika kipindi cha mwaka 2018/19 kimeteteleza yafuatayo:

(i) kimedahili jumla ya wanafunzi 26,640 ambapo kati yao wa Astashahada ni 494 (Wanaume 297 na Wanawake 197); Stashahada 478 (Wanaume 334 na Wanawake 144), Shahada ya kwanza 24,026 (Wanaume 14,497 na Wanawake 9,529), Stashahada ya Uzamili 95 (Wanaume 47 na Wanawake 48); Shahada ya Uzamili 1,282

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

(Wanaume 756 na Wanawake 526) na Shahada ya Uzamivu 265 (Wanaume 178 na Wanawake 87) katika Kampasi Kuu ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Aidha, kwa Kampasi ya Mbeya, Chuo kimedahili wanafunzi 1,146;

(ii) kimefanya miradi ya utafiti 135 katika maeneo ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu, TEHAMA na Maendeleo ya Viwanda; Elimu, Kilimo, Afya, na Usalama wa Chakula; Utawala Bora, Sera na Uzalishaji Viwandani; Jinsia, Maendeleo ya Taaluma, Utungaji wa Sera na matumizi ya Sera; Historia, Utamaduni, Lugha, Uhifadhi na Utalii Endelevu, Mali Asilia, na Mazingira, Sheria na Maendeleo Jumuishi ya Taifa. Miradi ya tafiti hizo imesaidia: (a) kupunguza tatizo la walimu katika Vyuo Vikuu vya Tanzania kwa kudhamini jumla ya watanzania 140 katika ngazi za masomo ya Uzamivu (66), Uzamili (45), *Postdoc* 17 na mafunzo ya muda mfupi (12); na (b) kuanzisha Programu nne (4) za Uzamivu na nne (4) za Uzamili;

(iii) kimetoa machapisho 381 katika majarida mbalimbali ya kitaifa na kimataifa. Hili ni sawa na ongezeko la majarida 27 ikilinganishwa na majarida 354 ya mwaka 2017/2018;

(iv) kimeongeza majarida yanayokidhi viwango vya kimataifa kutoka majarida tisa (9) kufikia majarida kumi na moja (11) ambayo yanapatikana kwa njia ya mtandao;

(v) kimekamilisha ujenzi wa Maktaba yenye hadhi ya Kimataifa ya kwanza na ya aina yake kujengwa katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati na kuzinduliwa rasmi na Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 27 Novemba, 2018. Maktaba hiyo ina uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,100 kwa wakati mmoja, ina ukumbi wa mkutano unaochukuwa watu 580 kwa wakati mmoja na kituo cha Utamaduni wa Kichina chenye Ofisi 5 na madarasa 10 yenye kubeba wanafunzi 550;

(vi) kimenunua nakala 6,927 za vitabu vyenye thamani ya **Shilingi 1,078,000,000** ambavyo vimewekwa kwenye Maktaba hiyo mpya. Aidha, mashubaka na samani kwa ajili ya kuhifadha vitabu hivyo vimetolewa kwa msaada wa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China; na

(vii) kimenunua na kuongeza vifaa katika Kituo cha Afya cha Chuo ili kuboresha mazingira ya kutolea huduma ya afya.

**47. Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kazi zifuatazo zimetokelezwa:

(i) kuendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa tano la wanafunzi la kujisomea, kupumzika, kufanya michezo ya ndani, migahawa, maduka ya vitabu na ofisi za Serikali ya Wanafunzi na Mshauri wa Wanafunzi;

(ii) kuanza ukarabati mkubwa wa mabweni Namba 2 na Namba 5 kwa gharama ya **Shilingi** bilioni 4.9 ambao unatarajia kukamilika ifikapo mwezi Agosti 2019. Kukamilika kwa mradi huu kutaongeza nafasi 800 za makazi ya wanachuo; na

(iii) kuendelea na ujenzi wa mfumo mpya wa maji katika Kampasi ya Mwalimu Nyerere Mlimani, ambapo inahusisha kuweka upya mabomba makubwa mapya na kujenga tenki kubwa la kuhifadhi maji na mashine kubwa nne za kusukuma maji. Mradi huu unategemewa kumaliza tatizo la maji chuoni na unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Agosti 2019.

#### **Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA)**

**48. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2018/19, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kimetokeleza yafuatayo:

(i) kimedahili jumla wanafunzi wapya 5,023 ambapo kati yao Astashahada ni 45, Stashahada 257 na Shahada 4,526.

Aidha, wanafunzi wa Shahada za uzamili 182, Stashahada ya uzamili 6 na shahada ya uzamivu 07 walidahiliwa. Idadi ya wanafunzi wote imeongezeka kufikia 11,266 kutoka 9,775 sawa na ongezeko la asilimia 15.3;

(ii) kimeshirikiana na wadau mbalimbali kutoa mafunzo kwa wakulima na wafugaji wapatao 3,250 kutoka manispaa ya Morogoro, wilaya za Mvomero, Kilosa, Tunduru na Iringa kwa lengo la kuongeza tija katika sekta ya kilimo;

(iii) kimeendelea na tafiti za miradi 28 mipya na kufanya jumla ya miradi kufika 119 kutoka 91 sawa na ongezeko la asilimia 30.8;

(iv) kimetoa mafunzo ya uelewa wa matumizi ya panyakugundua ugonjwa wa katika kifua kikuu kwa watumishi wa afya 264 yaliyojumuisha waratibu wa ugonjwa wa kifua kikuu, wauguzi, madaktari wa binadamu na wataalamu wa maabara kutoka katika hospitali 60 kutoka mikoa ya Dar es salaam na Dodoma;

(v) kimeingia mikataba mipya ya ushirikiano na taasisi 7 ili kuongeza mahusiano kwa lengo la kujenga uwezo wa wafanyakazi na wanafunzi katika kufanya tafiti za kisayansi na kilimo na hatimaye kuongeza uzalishaji na tija kwa wananchi;

(vi) kimejenga nyumba vitalu (greenhouses) 56, kati ya hizo 55 zimejengwa kwa kushirikiana na *Private Agricultural Sector Support (PASS) Trust* kwa ajili ya kufundisha na kuandaa vijana kujiajiri kupitia kituo atamizi (Incubation centre), na nyumba kitalu kimoja imejengwa kwa fedha kutoka serikalini kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa lengo la kuongeza miundo mbinu ya uzalishaji na mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi;

(vii) kinaendelea na ujenzi wa maabara mtambuka yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,600 kwa wakati mmoja. Maabara hii itapunguza changamoto ya vyumba vya

maabara chuoni. Aidha awamu ya kwanza ya utekelezaji imefikia asilimia 50%. Mradi huu unajengwa kwa fedha za ndani na unatarajiwa kukamilika mwezi July, 2019;

(viii) kimefanya ukarabati wa miundombinuikijumuisha: mbalimbali

a) ukarabati wa jumla ya mabweni 5 ya wanafunzi, kati ya hayo, mabweni 3 (Unit one) yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 222 yapo Kampasi ya Solomon Mahlangu, na mabweni 2 ya Nicholaus Kuhanga yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 924 yapo kampasi kuu. Ukarabati huo umeboresha mazingira ya malazi ya wanafunzi;

b) kimefanya ukarabati wa hosteli moja (1) iliyopo Taasisi ya Elimu ya Kujiendeleza kwa ajili ya wanafunzi wa kigeni yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 16 kwa wakati mmoja. Ukarabati huu umeongeza uwezo wa Chuo kuwapatia malazi wanafunzi wa kigeni 16; na

c) kimefanya Ukarabati wa Hospitali pekee ya rufaa ya Wanyama ya Taifa iliyopo katika Ndaki ya Tiba ya Mifugo na Sayansi za Afya, kwa lengo la kuongeza ufanisi wa kutoa huduma bora za matibabu ya wanyama na hivyo kuongeza uzalishaji na tija katika sekta ya Mifugo na Afya ya Jamii.

### **Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili**

**49. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2018/19, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili kimeteteleza yafuatayo:

(i) kimedahili jumla ya wanafunzi 1,139 wakiwemo wanafunzi 739 wa Shahada ya kwanza (Wanaume 523 na Wanawake 216) na wanafunzi 400 wa Shahada ya Uzamili (Wanaume 222 na Wanawake 178) ambapo idadi ya wanafunzi imeongezeka hadi kufikia 4,209 kutoka 3,642 na sawa na ongezeko la asilimia 15.6;

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

(ii) kimeongeza usajili wa wanafunzi katika mfumo wa TEHAMA (E-learning platform) kutoka wanafunzi 213 katika mwaka 2017/18 hadi kufikia 715 sawa na ongezeko la asilimia 70.21;

(iii) kimekamilisha utengenezaji wa vigezo vya kupima uadilifu kwa wanafunzi (Professionalism assessment tools) kwa Shahada ya kwanza ya udaktari wa tiba na pia kukamilisha Mwongozo wa utahini;

(iv) kimetoa mafunzo kwa walimu vinara 20 na kuwezesha wanafunzi 227 wa Shahada ya Uzamili kwa mafunzo mafupi ili kuleta weledi katika fani ya udaktari bingwa; (v) kimeandaa mfumo wa kuboresha huduma kwa wagonjwa (Patient Centered Service Strategy) unaotumika katika hospitali ya rufaa ya tiba na kufundishia Mloganzila;

(vi) kimekamilisha mpango wa uzalishaji mali katika hospitali ya Tiba na Kufundishia ya Mloganzila (*Business Plan*) ambao unatekelezwa baada ya kupitishwa na Baraza la Chuo, tarehe 10 Agosti, 2018;

(vii) kimeongeza uwiano wa wanafunzi wa kike kutoka asilimia 35 mwaka 2017/18 hadi kufikia asilimia 38.2 mwaka 2018/19;

(viii) kimeendelea na ujenzi wa Kituo Mahiri cha Magonjwa ya Moyo na Mishipa ya Damu (Centre of Excellence in Cardiovascular Sciences) ambao upo katika umaliziaji na utakamilika mwezi Mei 2019. Lengo la kituo hiki ni kuboresha utafiti na huduma za matibabu ya magonjwa ya moyo;

(ix) kimetoa mafunzo katika uandishi wa miradi kwa watafiti kupitia msaada kwa ushirikino na Nchi ya Sweden ili kuongeza uwezo wa kuandika maandiko ya miradi yanayoweza kushindana kitaifa na kimataifa;

(x) kimeanzisha miradi mipya ya kitafiti 35 kutoka katika Skuli tano na kukifanya Chuo kuwa na miradi ya kitafiti 104 kutoka 69 ya mwaka 2017/2018;



## NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

(xi) kimefanya Mkutano wa 6 wa kitaaluma MUHAS unaojulikana kama *Scientific Conference* uliohudhuriwa na watafiti 418 ambapo mada 164 ziliwasilishwa; na

(xii) kimeendelea kufanya tafiti zenye manufaa katika uboreshaji wa huduma za afya nchini ikiwemo;

a) kutoa idadi ya makundi maalum yenye hatari ya kupata maambukizi ya virusi vya UKIMWI ili kusaidia Serikali kuandaa mpango wa kupunguza maambukizi:

b) kufanya majaribio ya chanjo ya virusi vya UKIMWI kwa hatua ya pili (HIV DNA- Prime Phase II) ambayo imekuwa na mafanikio makubwa. Maandalizi ya majaribio zaidi yatasaidia kufikia hatua ya tatu na ya mwisho (Phase III);

c) kufanya majaribio ya dawa mbadala ya kuzuia malaria kwa akina mama wajawazito wasioweza kutumia dawa ya sasa;

d) kufanya utafiti na kusaidia kutengenezwa kwa mpango wa kwanza wa matibabu ya saratani nchini (Cancer Treatment Guidelines) utakaozinduliwa mnamo mwezi Mei 2019;

e) kufanya utafiti kuhusu Kifua Kikuu sugu (TB Drug Resistance) na kutoa matokeo yanayosaidia kuboresha miongozo ya matibabu; na

f) kufanya tafiti za magonjwa ambukizi yatokanayo na vimelea aina ya bakteria zilizopelekea kuboresha mpango wa dawa sugu (Bacterial Resistance Guidelines).

### Chuo Kikuu cha Ardhi

**50. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2018/19, Chuo Kikuu cha Ardhi kimetekeleza yafuatayo:

(i) kimedahili jumla ya wanafunzi 4,135 wanawake 1,752 na wanaume 2,383 katika ngazi za Stashahada 11

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

(Wanaume 7 na Wanawake 4); Shahada 3,862 (Wanaume 2,189 na wanawake 1,673); Uzamili 195 (Wanaume 130 na wanawake 65) na Uzamivu 67 (wanaume 56 na Wanaume 11);

(ii) kimefadhili mafunzo ya Shahada ya Uzamivu kwa watumishi wanataaluma 12 (Wanaume 10 na Wanawake 2) na Shahada ya Uzamili 6 (Wanaume 4 na Wanawake 2) ili kuongeza idadi wa Wahadhiri nchini. Aidha, kimegharamia mafunzo ya watumishi waendeshaji watatu (3) Wanaume wawili (2) na Mwanamke mmoja (1) wa Shahada ya Uzamili;

(iii) kimepitia na kuboresha Mitaala 32 na kuandaa rasimu ya Mitaala mipya 15. Hii itasaidia Mitaala kutumika kutoa mafunzoyanayoendana na mahitaji halisi ya soko;

(iv) kimefanya tafiti katika miradi 76 kwenye maeneo ya usimamizi wa Ardhi, kujikinga na maafa, utunzaji wa mazingira na majenzi. Matokeo ya tafiti hizi yataatumika kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabili jamii katika matumizi bora ya ardhi, kujikinga na maafa, utunzaji wa mazingira na majengo;

(v) kimetoa huduma 48 za ushauri wa kitaalamu katika matumizi bora ya Ardhi, upimaji na tathmini, usanifu majengo na ujenzi. Miongoni mwa huduma hizo ni ujenzi wa Mahakama kwa kutumia teknolojia ya gharama nafuu katika Wilaya 16, ambapo tayari majengo yamekamilika katika Wilaya za Geita, Njombe, Lindi, Simiyu, Katavi, Bukombe, Bunda, Ruangwa, Chato, Rungwe, Sikonge, Kilwa, Kasulu, Kondoa, Longido na Kilindi;

(vi) kimeandaa jumla ya machapisho 12 katika maeneo ya usimamizi wa ardhi na mazingira, makazi na majengo kwa ajili ya kutumiwa na jamii katika kuongeza maarifa yatakayotatua changamoto mbalimbali;

(vii) kimetoa huduma za jamii kwa kufanya upembuzi yakinifu, usanifu na kuandaa michoro ya ujenzi

wa viwanja vya michezo Jijini Dodoma hivyo kusaidia Serikali kupunguza gharama za maandalizi ya awali ya mradi; na

(viii) kimetoa mafunzo katika maeneo mbalimbali yakiwemo maeneo ya matumizi bora ya Ardhi kwa Jiji la Dar es Salaam katika maeneo yanayoathirika na mafuriko; Mafunzo ya kukabilliana na athari za mafuriko kwa wananchi wanaokaa kandokando ya mto Kizinga Wilaya ya Temeke; mafunzo ya kuvuna maji ya mvua kwa wakazi wa Goba wanaoishi kandokando ya mto Mbezi, Wilaya ya Ubungo; na mafunzo ya kutengeneza *Biogas* na *Briequettes* kwa wakazi 20 wa Bagamoyo. Lengo la mafunzo hayo ni kupunguza athari zinazotokana na uharibifu wa mazingira.

**51. Mheshimiwa Spika**, katika uboreshaji wa mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji chuo kimeendelea na ukamilishaji wa Jengo la Ardhi (Lands Building) ambalo litakiongezea chuo nafasi za madarasa kwa wanafunzi 2,980 na ofisi 125. Ujenzi wa jengo hilo unafanyika kwa awamu mbalimbali kama ifuatavyo:

a) sehemu ya Wing "A" ujenzi wake umekamilika na kuwezesha upatikanaji wa nafasi za kukaa wanafunzi 1,580 na ofisi 25; na

b) sehemu ya Wing "B" ujenzi unaendelea na utakamilika mwezi Agosti 2019, na itakapokamilika itawezesha kuchukua wanafunzi 320 na nafasi 198 za ofisi; na

c) ujenzi wa Wing 'C' uko katika hatua za mwisho za ukamilishwaji; kukamilika kwa ujenzi wa Wing "C" kutaongeza vyumba vya madarasa vyenye jumla ya nafasi za kutumiwa na wanafunzi 700.

### **Chuo Kikuu cha Dodoma**

**52. Mheshimiwa Spika**, Chuo Kikuu cha Dodoma katika kipindi cha mwaka 2018/19 kimetekeleza yafuatayo:

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

- (i) kimedahili wanafunzi wapya 11,221 ambapo wa Shahada ya kwanza walikuwa 9,756, Stashahada 924 na Astashahada 175. Aidha, jumla ya wanafunzi wapya 351 walidahiliwa katika Shahada za Juu ambapo Shahada ya Uzamili ni 302 na Shahada ya Uzamivu ni 49;
- (ii) kimetoa huduma 11 za ushauri katika maeneo ya Elimu, Biashara, Uwekezaji, TEHAMA na Afya;
- (iii) kimegharamia masomo kwa watumishi 422 katika ngazi za Shahada ya Uzamivu (284), Uzamili (95), Shahada ya Kwanza (24), na Stashahada na Astashahada (19) kwa lengo la kuboresha utendaji kwenye taasisi; na
- (iv) kimeongeza idadi ya tafiti hadi 37 kutoka tafiti 27 za mwaka 2017/2018. Tafiti hizo zitasaidia kutatua changamoto katika jamii.

### **Chuo Kikuu Mzumbe**

**53. Mheshimiwa Spika**, Chuo Kikuu Mzumbe katika kipindi cha mwaka 2018/19 kimetekeleza yafuatayo:

- (i) kimedahili wanafunzi wapya 5,103 ambapo wanaume ni 2,619 na wanawake ni 2,484. Kati ya wanafunzi hao wapya, Astashahada ni 392, Stashahada ni 708, Shahada ni 3,294, Shahada ya Uzamili ni 690 na Shahada ya Uzamivu ni 19;
- (ii) kimeendelea kutekeleza miradi ya utafiti sita (6), kupata miradi minne (4) mipya kwa njia ya ushindani na kufanya jumla ya miradi inayoendelea chuoni kuwa 10;
- (iii) kimetoa ushauri wa kitaalamu na kozi fupi 41 katika maeneo ya Menejimenti, Uongozi, Biashara na Sayansi ya Jamii;
- (iv) kimeendelea na ujenzi wa jengo la utawala na madarasa katika Kampasi ya Mbeya ambao umekamilika kwa asilimia 70;

(v) kimeendelea kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi katika eneo la Iwambi, Kampasi ya Mbeya ambapo hatua iliyofikiwa ni ya kumpata Mshauri Elekezi;

(vi) kimeboresha huduma za TEHAMA kwa kuanzisha mfumo wa kupokea maombi na udahili wa wanachuo. Pia Chuo kinaendelea kutengeneza mfumo wa usimamizi wa taarifa za kitaaluma (Academic Records Management System - MU-ARMS) kwa lengo la kuboresha mawasiliano;

(vii) kimefadhili jumla ya watumishi 28 wanaosoma Shahada ya Uzamivu na watumishi 18 katika masomo ya Shahada ya Uzamili, ambapo watumishi wapya waliojiunga na masomo ya Shahada ya Uzamivu ni 13 na Shahada ya Uzamili ni 11; lengo ni kuongeza idadi ya wahadhiri; na

(viii) kimetoa mafunzo ya Ujasiriamali kwa wadau mbalimbali wapatao 400 kutoka manispaa ya Morogoro na Wilaya ya Mvomero ili kuwawezesha kuinua vipato vyao kiuchumi.

**54. Mheshimiwa Spika**, katika uboreshaji wa mazingira ya kufundishia na kujifunzia chuo kimeendelea na ujenzi wa Hosteli nne (4) katika Kampasi Kuu Morogoro zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,024 ambapo ujenzi wake umefikia asilimia 15 na unatarajiwa kukamilika Oktoba, 2019. Pia kimefanya ukarabati mkubwa wa mabweni mawili (2) na kufanya jumla ya mabweni yaliyokarabatiwa kuwa sita (6). Kukamilika kwa miradi hiyo kutapunguza changamoto ya upungufu wa mabweni kwa asilimia 25.

### **Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi**

**55. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2018/19 Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi kimeteteleza yafuatayo:

(i) kimesajili jumla ya wanafunzi 5,044 kati ya wanafunzi 4,386 waliotarajiwa sawa na ongezeko la asilimia 15; kati yao wanawake ni 2,320 (46%) na wanaume ni 2,724 (54%)

katika ngazi mbalimbali kama ifuatavyo; Astashahada 740; Stashahada 1,046; Shahada ya kwanza 2,988; Stashahada ya Uzamili 30; Shahada ya Uzamili 200 na Shahada ya Uzamivu 40;

(ii) kinaendelea na zoezi la uandaaji wa programu mpya saba (7); nne (4) za Shahada za Uzamili na tatu (3) za Shahada ya kwanza ili kupanua wigo wa programu katika fani mbalimbali na kuwezesha kuongezeka kwa udahili wa wanafunzi;

(iii) kimeandaa maandiko ya tafiti sita (6) kwa ajili ya ufadhili kutoka nje ya Chuo. Maandiko haya yapo katika maeneoya Elimu, Afya, Ushirika, Biashara na Ujasiriamali;

(iv) kimeratibu zoezi la uchapishaji wa Jarida la Utafiti la *Journal of Co-operative and Business Studies Vol. 2* yenye jumla ya tafiti tisa na *Vol. 3* yenye jumla ya tafiti 10 zinazolenga kubaini matatizo ya ushirika na mbinu za kutatua changamoto za kiushirika;

(v) kimekarabati kafeteria, eneo la mapokezi katika kituo cha Mikutano cha Ushirika na kuboresha mazingira ya ukumbi wa mikutano wa Baraza la Chuo kwa kununua viti 26 na meza ili kuwezesha utoaji wa huduma bora kwa wadau mbalimbali na pia kusaidia katika ukuzaji wa mapato ya Chuo;

(vi) kimeandaa na kurusha vipindi 38 vya redio ili kuhimiza wadau kujifunza masuala ya ushirika. Vipindi hivi vimerushwa kupitia Shirika la Utangazaji Tanzania (Tanzania Broadcasting Corporation – TBC);

(vii) kinaendelea kuwajengea uwezo viongozi, wanachama na watendaji wa vyama vya ushirika vya akiba na mikopo vijijini (RUSACCOS) pamoja na vyama vya ushirika wa mazao (AMCOS) na msingi katika maeneo ya uongozi na usimamizi, usimamizi wa fedha na mikopo, masoko, uwekezaji na uandaaji wa mipango biashara kupitia programu ya *Marketing Infrastructure, Value*

*addition and Rural Finance Support* (MIVARF). Programu hii inahusisha vyama vya akiba na mikopo 101 pamoja na vyama vya ushirika wa mazao vya msingi 66. Lengo la programu hii ni kuimarisha vyama vya ushirika na kuvifanya vijijendeshe kwa tija; na

(viii) kimeratibu mafunzo katika Ofisi za Chuo Mikoani. Mafunzo mbalimbali kuhusu Elimu ya Ushirika yalitolewa kwa wadau katika ofisi hizo ambapo jumla ya walengwa 3,179 walitufika.

### **Chuo Kikuu Huria cha Tanzania**

**56. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2018/19, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kimeteteleza yafuatayo:

(i) kimesajili jumla ya wanafunzi 11,535 ambapo wanafunzi 5,532 ni wa Shahada ya Kwanza, 4,165 ni kozi zisizo za Shahada (Non-Degree) 1,766 wa Uzamili na wa Uzamivu 72;

(ii) kimeendesha warsha ya utafiti kwa Maprofesa 12 wa Chuo iliyolenga kubuni miradi mikubwa na kimeandika maandiko mawili (Research Proposal) ya kuomba fedha za utafiti;

(iii) kimefanya mafunzo kwa wanataaluma 30 ili kuwajengea uwezo katika kutumia programu mbalimbali za kompyuta kama *Statistical Package for the Social Sciences* (SPSS) na INVIVO katika kuchakata taarifa za kiutafiti;

(iv) kimeendesha mafunzo ya kutumia mfumo wa kujifunzia (*Electronic Learning Management System*) na mfumo wa matokeo ya wanafunzi (*Students Register Information System*) kwa wanafunzi 174 kupitia Taasisi yake ya Teknolojia za Elimu na Menejimenti katika vituo 11 vya Mikoa ya Arusha, Mbeya, Zanzibar, Kigoma, Morogoro, Iringa, Mwanza, Dodoma, Mtwara, Kagera na Dar es Salaam;

(v) kimeratibu mfumo wa kujifunzia na mifumo ya Maktaba katika Vyuo vya Ualimu vya Monduli na Tabora kupitia Taasisi yake ya Teknolojia za Elimu na Menejimenti kwa ufadhili wa UNESCO chini ya mradi wa *China Funds in Trust*. Kupitia Program hii jumla ya watumishi 16 walipatiwa mafunzo ambayo yatawawezesha kusimamia mafunzo ya TEHAMA katika Vyuo vya Ualimu; na

(vi) kimefanikiwa kupata Kigoda cha UNESCO katika Elimu ya Ualimu na uendelezaji Mitaala. Kigoda hicho kitawezesha kukitangaza Chuo na kuvutia wafadhili kwenye Elimu Sayansi, Utamaduni na Teknolojia.

### **Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius K. Nyerere cha Sayansi ya Kilimo na Teknolojia**

**57. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2018/19, Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius K. Nyerere Cha Sayansi ya Kilimo na Teknolojia katika kimetekeleza yafuatayo:

(i) kimeanza mchakato kwa ajili ya kupata Hati-Miliki ya Ardhi ya sehemu ya Chuo yenye ukubwa wa takribani ekari 650, na tayari maombi yamepelekwa katika Ofisi ya Ardhi Kanda ya Simiyu;

(ii) kimeendesha mafunzo kwa wakulima 455 kuhusu mbinu bora za kilimo. Aidha, ekari saba (7) zimelimwa mazao mbalimbali kwa ajili ya mashamba darasa;

(iii) kimeandika maandiko ya kuomba fedha (Project proposal) na kuwasilishwa katika taasisi za TEA na COSTECH pamoja na wahisani mbalimbali akiwemo *International Development Research Center (IDRC)*, Ubalozi wa Canada na Benki ya Dunia; na

(iv) kimefadhili watumishi wanne (4) wa Shahada ya Uzamili katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela Arusha (NM-AIST) kupitia mradi wa *CREATES*.



## Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam

**58. Mheshimiwa Spika,** Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam katika kipindi cha mwaka 2018/19 kimetekeleza yafuatayo:

(i) kimedahili wanafunzi 1,818 (sawa na asilimia 87 ya lengo) wakiwemo 528 wa fani ya Sayansi (sawa na asilimia 75 ya lengo);

(ii) kimeandaa rasimu 6 za Mitaala ya Stashahada, Shahada, na Shahada za Uzamili;

(iii) kimekamilisha uwekaji wa miundombinu ya TEHAMA katika Shule za Mazoezi;

(iv) kinaendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa jengo la utawala na ofisi za wafanyakazi na utafiti ambapo mradi upo katika hatua za umaliziaji na mkandarasi anatarajiwa kukabidhi jengo mwezi Juni, 2019;

(v) kimefanya jumla ya tafiti 12 ambapo tafiti nane (8) ni mwendelezo wa tafiti zilizokuwa zinaendelea na tafiti nne (4) ni mpya;

(vi) kimewezesha Wanataaluma 120 kusimamia mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi 3,947 wa mwaka wa kwanza na wa pili na hivyo kuufanya ufundishaji na ujifunzaji kuwa wa vitendo badala ya nadharia pekee;

(vii) kimenunua vifaa vya kufundishia na kujifunzia vya wanafunzi wenye mahitaji maalum, ambavyo vinakiwezesha Chuo kutoa elimu jumuishi; na

(viii) kimefanya kongamano moja la Kitaifa linalohusu 'utokomezaji wa ukatili dhidi ya wanawake na watoto nchini Tanzania.' Kongamano hili limesaidia kujenga uelewa kwa wanajamii kuhusu kuwapo kwa ukatili dhidi ya wanawake na watoto, madhara yake na namna ya kukabiliana nao. Aidha, kongamano hili limesaidia katika kuifahamisha jamii mikakati mbalimbali inayochukuliwa na

Serikali ya Awamu ya Tano katika kukabiliana na ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

### **Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa**

**59. Mheshimiwa Spika,** Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa katika kipindi cha mwaka 2018/19 kimeteteleza yafuatayo:

(i) kimedahili jumla ya wanafunzi 6,808 wa Shahada ya kwanza sawa na asilimia 127 ya lengo; kati yao wanaume ni 4,416 sawa na asilimia 65 na wanawake ni 2,392 sawa na asilimia 35;

(ii) kimenunua jumla ya vitabu 887 ili kuboresha huduma ya maktaba pamoja na ufungaji wa kamera 13 kwa ajili ya ulinzi na usalama wa Vitabu ndani ya eneo la Maktaba. Aidha, chuo kimejiunga kwenye Umoja wa Maktaba na Taasisi za Tafiti nchini ili kuboresha huduma ya vitabu, machapisho na majarida kwa njia ya kieletroniki;

(iii) kimeanzisha Shahada mpya mbili (2) za Uzamili; *Master of Science with Education* (Biology and Chemistry Streams) na *Master of Arts with Education – Geography Stream*;

(iv) kimeboresha Mitaala ya elimu kwa programu nne (4) za Shahada za awali kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ili iendane na wakati na mahitaji ya soko;

(v) kimegharamia watumishi 98 kwenda masomoni sawa na asilimia 108.9 ya lengo, ambapo wanawake ni 33 na wanaume ni 65; kati yao wanataaluma ni 91 (Wanaume 59 na wanawake 32) na waendeshaji saba (7) (Wanaume 6 na Mwanamke 1);

(vi) kimekamilisha tafiti saba (7) endelevu ikiwemo utafiti wa kutaka kujua kiasi cha hewa ukaa kinachotunzwa katika misitu iliyopo Manispaa ya Iringa. Utafiti huu utahamasisha jamii husika kutunza misitu ili kudhibiti mabadiliko ya tabia nchi;

(vii) kimeanza utekelezaji wa tafiti 9 mpya katiya 6 zilizolengwa kutekelezwa ikiwemo utafutaji wa njia salama na mbadala wa viatilifu katika kuzuia uharibifu wa wadudu wa nyanya. Tafiti hii inategemewa kusaidia kupunguza madhara kwa binadamu na mazingira yatokanayo na utumiaji wa viatilifu;

(viii) kimeshiriki kutoa shauri za kitaalamu (5) zikiwemo ushauri katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kuandika, Kusoma na Kuhesabu (KKK) kwa Walimu wa Shule za Msingi (Darasa la Kwanza na la Pili) kwa Mkoa wa Mara, Kigoma na Katavi;

(ix) kimekamilisha ujenzi wa ukumbi wa mihadhara wenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,209 kwa wakati mmoja na ofisi 14 zenye uwezo wa kuchukua wahadhiri 28 ambao umekabidhiwa tarehe 5 Aprili, 2019 na kuanza kutumika. Aidha, chuo kinaendelea na ujenzi wa maabara za Sayansi zitakazokuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 240 kwa wakati mmoja. Mradi wa ujenzi wa maabara umefikia asilimia 15. Kukamilika kwa mradi huu kutaboresha ujifunzaji kwa vitendo kwa walimu wanafunzi wa masomo ya Sayansi; na

(x) kimetoa jumla ya machapisho 18 katika nyanja mbalimbali za kitaaluma. Aidha, kimeshiriki katika mikutano saba (7) ya kimataifa ambapo jumla ya mada saba (7) zenye ushauri kwa jamii ziliwasilishwa.

## **Chuo cha Ufundi Arusha**

**60. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2018/19, Chuo cha Ufundi Arusha kimetekeleza yafuatayo:

(i) kimesajili jumla ya wanafunzi 2,413, ambapo kati yao wa Stashahada ni 1,986 na Shahada ni 427;

(ii) kimegharamia mafunzo ya muda mrefu kwa jumla ya watumishi 40, ambapo watumishi 15 wapo Shahada ya Uzamivu, watumishi 22 Shahada ya Uzamili na watumishi watatu (3) Shahada ya Kwanza. Lengo ni kuongeza tija ya utendaji kwa watumishi; (iii) kinajenga

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

jengo la ghorofa tatu (3) lenye maabara, madarasa, ofisi, na stoo ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji ambapo ujenzi umefikia asilimia 42. Kukamilika kwa jengo hili kutaongeza udahili wa wanafunzi 1000 sawa na ongezeko la asilimia 41.4 ya usajili wa sasa;

(iv) kinaendelea na ujenzi wa kituo cha kupima mitambo midogo midogo ya kufua umeme kutokana na nguvu ya maji (Micro-Turbines Testing Station). Hatua ya utekelezaji imefikia asilimia 85. Kituo kitakapokamilika kitasaidia wataalam wanaotengeneza *turbines* kuweza kuzijaribu na kujua ukubwa wa vyanzo na *turbine* kwa ajili ya kuzalisha umeme wa maji;

(v) kinaendelea na tafiti mbalimbali ambazo ni pamoja na:

a) matumizi bora ya maji katika Kilimo cha mpunga katika maeneo ya Skimu za Mahande (Mto wa Mbu) na *Lower Moshi* (Kilimanjaro);

b) utafiti wa mradi wa umeme Wilayani Mbulu, ambao unaolenga kuzalisha umeme na kuhudumia vijiji vya Kwermusi na Amoa; na

c) utafiti kuhusu uundaji wa helikopta unaolenga

kuwasaidia wataalam kutengeneza ndege (helikopta) za gharama nafuu na salama.

(vi) kinaendelea na ujenzi wa kituo kipyua cha kuzalisha umeme wa 1.7 MW cha KIKULETWA. Umeme huu utaunganishwa kwenye msongo wa Taifa vile vile Kituo hiki kitatumika kwa mafunzo (Training Factory);

(vii) kinaendelea kukamilisha ujenzi na ukarabati wa majengo ya KIKULETWA; Hatua ya Ukarabati na ujenzi wa miundombinu imefikia asilimia 95 na inatarajiwa kukamilika ifikapo tarehe 31 Desemba, 2019;

(viii) kinaendelea na kazi ya ujenzi wa miundombinu Oljoro kwa awamu ya pili kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo ya kilimo cha umwagiliaji;

(ix) kimetoa mafunzo ya stadi mbalimbali za ujuzi kwa wanafunzi 126 kutoka kaya maskini ambapo Chuo kimeweka utaratibu wa kufuatilia wahitimu hao ili waweze kujajiri na kuajiriwa;

(x) kimepokea jumla ya kompyuta 100, meza 100 na viti 200 ikiwa ni sehemu ya mradi wa “Kutegemeza Elimu ya Ufundi na Ualimu (STVET)”. Katika mradi huo, Chuo kitafunga mtandao wa ndani (Local Area Network) katika majengo yote ya Chuo kutoka kwenye Mkongo wa Taifa ili kuboresha utoaji wa mafunzo kupitia TEHAMA;

(xi) kimetoa ushauri wa kitaalamu kwa *Tanzania National Roads Agency* (TANROADS) katika Mikoa ya Simiyu, Arusha na Singida. Pia wakandarasi mbalimbali wa ndani na nje wanaoshiriki kwenye usanifu na ujenzi wa miradi mbalimbali ya barabara na majengo wameendelea kupata ushauri wa kitaalamu; na

(xii) kimeendelea kutoa ushauri wa kitaalamu kwenye utekelezaji wa mradi wa ufungaji wa *Solar PV* kupitia mradi wa *Sustainable Solar Market Packages* (SSMP) kwa Wakala wa Umeme Vijijini (REA) ikiwa ni pamoja na kuhakiki ubora, ukubwa, viwango na aina ya mitambo inayofungwa na mkandarasi iwapo inakidhi mahitaji. Mradi huu unatekelezwa katika Wilaya za Biharamulo na Bukombe.

### **Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere**

**61. Mheshimiwa Spika**, Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere katika kipindi cha mwaka 2018/19 kimeteteleza yafuatayo:

(i) kimedahili jumla ya wanafunzi 8,981 wakiwemo 7,757 (wanawake 3,636 na wanaume 4,121) wa Kampasi ya Kivukoni na 1,224 (wanawake 707 na wanaume 517) wa Kampasi ya Zanzabar;

(ii) kimegharamia mafunzo ya muda mrefu kwa wanataaluma 12 na wafanyakazi waendeshaji wanne (4). Aidha, kimegharamia wafanyakazi wanataaluma 13 na wafanyakazi waendeshaji 12 kwa ajili ya mafunzo ya muda mfupi ili kuwajengea uwezo zaidi watumishi ili kuongeza ufanisi katika kazi zao;

(iii) kimekamilisha michoro na kuandaa gharama za ujenzi wa maktaba katika kampasi ya Kivukoni na hosteli katika kampasi ya Zanzibar;

(iv) kimekamilisha ujenzi wa jengo la mihadhara lenye uwezo wa kubeba wanafunzi 324 kwa wakati mmoja kwa kutumia mapato ya ndani ya chuo; na

(v) kimenunua vitabu 184 katika fani za Rasilimali watu, Utafiti, Mipango, Elimu, Ujasiriamali, Kiswahili, *English*, Masoko, Fedha, Kodi, Maadili, Hesabu, Manunuzi na Biashara kwa lengo la kuboresha ujifunzaji na ufundishaji.

### **Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya**

**62. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2018/19, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya kimetekeleza yafuatayo:

(i) kimeongeza udahili kufikia wanafunzi 4,630 kutoka 4,209 (ongezeko la asilimia 10), ambapo wanafunzi 2,225 wamesajiliwa katika ngazi ya Stashahada (513 ni wasichana na 1,712 ni wavulana). Pia wanafunzi 2,405 wamesajiliwa ngazi ya Shahada (wasichana 371 na wavulana 2,034);

(ii) kimekamilisha uandaaji wa michoro ya ramani ya jengo la vyumba viwili vya madarasa ambavyo vitakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 600 kwa pamoja na hivyo kuongeza nafasi za kujifunzia na kufundishia. Ujenzi wa jengo hili utakamilika mwezi Julai 2019;

(iii) kimeendelea kutekeleza miradi tisa (9) ya ukarabati wa shule za sekondari, miradi kumi (10) ya ukarabati wa Vyuo

vya Ualimu na miradi mitatu (3) ya ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi;

(iv) kimeunda gari dogo kwa ajili ya kubebea mizigo midogo midogo kwa lengo la kurahisisha kazi za uvunaji kwa wakulima wa viazi. Gari hili linaendelea k u f a n y i w a maboresho kutokana na mapendekezo ya wadau;

(v) kimefanya upembuzi yakinifu juu ya kuandaa mfumo wa kuzalisha gesi kwa kutumia samadi kwa ajili ya matumizi ya kupikia na kuwasha taa katika maeneo ya vijijini na hivyo chuo kutunukiwa cheti na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kutokana na ubunifu huu;

(vi) kimeunda mashine kwa ajili ya kupukuchua nafaka na sasa mashine hiyo ipo katika hatua ya uboreshaji kutokana na maoni ya wadau mbalimbali. Mashine hiyo ikikamilika itapunguza muda unaotumiwa na wakulima wakati wa kupukuchua nafaka mbalimbali;

(vii) kimefanya ukarabati wa miundombinu katika Kampasiya Rukwailikuiwezesha kuanza kudahili wanafunzi wapya 200 katika fani ya ufundi mchundo kwa mwaka wa masomo 2019/2020; na

(viii) kimeendelea na ujenzi wa jengo la Maktaba lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,500 kwa wakati mmoja na hivyo kuboresha mazingira ya kujifunzia kwa wanafunzi. Ujenzi wa jengo hilo umekamilika kwa asilimia 51 ya jengo lote na asilimia 69 ya ujenzi awamu ya kwanza.

### **Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam**

**63. Mheshimiwa Spika**, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam katika kipindi cha mwaka 2018/19 imetekeleza yafuatayo:

(i) imesajili wanafunzi wapya 1,499 ambapo Stashahada ni 905 (Wavulana 718 na Wasichana 187), Shahada ya Kwanza ni 579 (Wavulana 470 na Wasichana 109), Shahada ya Uzamili 15 (Wavulana 15 na Wasichana

0); Lengo limefikwa kwa asilimia 88.2. Jumla ya wanafunzi waliopo kwenye Taasisi imeongezeka kutoka wanafunzi 4,135 mwaka 2017/18 na kufikia wanafunzi 4,257 (Wavulana 3,392 na Wasichana 865) mwaka 2018/19;

(ii) imeendelea kufanya shughuli za kiutafiti na ubunifu kama ifuatavyo:

a) mradi wa utafiti unaoangalia uhusiano wa wadudu na mimeamisitu kwa lengo la kulinda mazingira na kukuza uzalishaji kwenye kilimo katika misitu ya Pwani. Mradi huu unafadhiliwa na *JRS Foundation* ya Marekani;

b) mradi wa ubunifu wenye lengo la kuimarisha matumizi ya ardhi kidogo inayopatikana maeneo ya mijini kuzalisha mazao ya kilimo kama vile mbogamboga. Mradi huu unafadhiliwa na Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania (COSTECH);

c) mradi wa uanzishwaji kituo cha utafiti nishati endelevu kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Uingereza (DfID). Lengo la mradi ni kuanzisha kituo kitakachokuwa kinatafiti nishati endelevu nchini. Mradi huu utachochea shughuli nyingi za kiuchumi hasa zinazotegemea uwepo wa nishati ya umeme kwani mategemeo ya matokeo ya mradi huu ni kugundulika kwa vyanzo vingi vya nishati ya umeme; na

d) mradi wa upanuzi wa jengo la maktaba kwa kutumia utaratibu wa manunuzi wa *Force Account* ambapo kwa sasa tayari asilimia 40% ya vifaa vya ujenzi vimenunuliwa.

(iii) imekamilisha maandalizi ya mtaala ulioidhinishwa na NACTE kwa ajili ya kuanza kutoa mafunzo ya Shahada ya Uhandisi katika Madini; Wanafunzi 65 wanatarajiwa kudahiliwa katika mafunzo hayo kila mwaka kuanzia mwaka wa masomo wa 2019/20; kwa lengo la kupunguza pengo la wahandisi katika sekta ya madini nchini;



(iv) imekamilisha maandalizi ya mtaala ulioidhinishwa na NACTE wa mafunzo ya Shahada ya Uzamili katika Uhandisi wa Nishati Endelevu; Wanafunzi 40 wanatarajiwa kudahiliwa katika mafunzo hayo kila mwaka kuanzia mwaka wa masomo wa 2019/20; Udahili wa wanafunzi hao utasaidia kupunguza mahitaji ya wasimamizi waandamizi wa miradi inayotekelezwa na itakayotekelezwa hapa nchini;

(v) imewezesha wafanyakazi 57 kwenda masomoni katika ngazi mbalimbali ndani na nje nchi wakiwemo walimu 50 na wafanyakazi waendeshaji 7;

(vi) imegharimia mafunzo kwa vitendo (IPT) kwa wanafunzi 366 wa mwaka kwanza na wa pili kwa mwaka wa masomo 2017/18; Mafunzo haya yamesaidia wanafunzi wa Taasisi kupata ujuzi, na uzoefu wa shughuli za uzalishaji viwandani ikiwa ni matakwa ya mtaala;

(vii) imeandaa Mtaala wa kufundisha masomo ya Teknolojia ya bidhaa za ngozi katika ngazi ya Stashahada katika Kampasi ya Mwanza ambayo imehakikiwa na kuidhinishwa na Baraza la Elimu ya Ufundi (NACTE). Kuanza kwa mafunzo haya kutasaidia kuongezeka kwa ajira hasa kwa vijana watakaojikita katika sekta ya ngozi ambayo imekuwa kwa sasa haina mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi hapa nchini; na

(viii) imefanya ukarabati wa jengo moja katika Kampasi ya Myunga lenye madarasa mawili yenye uwezo wa kubeba wafunzi 50 kila moja. Ukarabati huu umesaidia kuanzishwa kwa mafunzo ya ufundi sanifu/stadi (NVA 3) yanayosimamiwa na VETA ambapo kwa kuanzia wanafunzi 20 wamedahiliwa na wanaendelea na masomo.

### **Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST)**

**64. Mheshimiwa Spika**, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela Arusha (NM- AIST) katika kipindi cha mwaka 2018/19 imetekeleza yafuatayo:

(i) imedahili wanafunzi 90 na kufikisha jumla ya wanafunzi 521 kutoka 441 sawa na ongezeko la asilimia 20;

(ii) imeandikamaandiko 23 ya kuomba fedha za utafiti na ufadhili wa wanafunzi kwa lengo la kuongeza udahili na miradi ya utafiti. Hadi kufikia mwisho wa mwezi Machi 2019, jumla ya maandiko manane (8) kati ya 23 yalikuwa yamekubaliwa na wafadhili;

(iii) imeongeza mahusiano na wadau wa ndani na nje ambapo wadau wa kimataifa wameongezeka kutoka 24 hadi kufikia 37 sawa na ongezeko la asilimia 54.2; ukanda wa Afrika Mashariki kutoka 29 hadi 36 sawa na ongezeko la asilimia 24.1; na wa ndani ya nchi wameongezeka kutoka 17 hadi 23 sawa na ongezeko la asilimia 35.5; na

(iv) inaendelea na utekelezaji wa jumla ya miradi ya utafiti 33. Miradi hiyo imejikita katika maeneo yanayohusu kilimo na usalama wa chakula kama vile uzalishaji wa miche bora ya ndizi inayohimili magonjwa ya kitropiki na kuondoa sumu kuvukatika nafaka, maji, nishati, TEHAMA, na maambukizi ya ugonjwa wa kimeta kwa wanyama pori na wanaofugwa. Aidha, miradi hiyo inawezesha pia ufadhili wa wanafunzi katika fani mbalimbali.

## **UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYO CHINI YA WIZARA KWA MWAKA 2018/19**

### **Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu (Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo katika Sekta ya Elimu - EP4R)**

**65. Mheshimiwa Spika**, programu hii inalenga kuimarisha Elimu kwa kuzingatia ubora na usimamizi wa rasilimali fedha na manunuzi ya umma kwa ajili ya mipango ya elimu. Katika mwaka wa fedha 2018/19 Wizara kupitia Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo katika Sekta ya Elimu (EP4R) imetekeleza shughuli zifuatazo:

(i) imewezesha ujenzi wa miundombinu katika shule 504 (msingi 219 na sekondari 285) ambapo jumla ya **Shilingi** bilioni 56.5 zilitumwa katika shule husika kwa mwaka 2018/

19. Ujenzi wa miundombinu unahusisha madarasa 938, mabweni 210, vyoo 2,141, nyumba 39 (2 in 1), mabwalo 76 na huduma za maji katika shule 10 unaendelea katika Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara. Aidha, ujenzi wa shule 4 mpya za Msingi katika Halmashauri za Dodoma Jiji, Masasi Mji, Buhigwe na Chato na ukarabati wa Shule ya Msingi Mwisenge A na B unaendelea;

(ii) imeratibu mchakato wa ukarabati na upanuzi wa Vyuo vinane (8) vya Ualimu ambavyo ni Bustani, Vikindu, Mtwara Kawaida, Mtwara Ufundi, Singa chini, Monduli, Bunda na Katoke ambapo hatua iliyofikiwa ni Bodi ya Zabuni kumthibitisha msimamizi ili aweze kupatiwa mzabuni;

(iii) imeratibu ununuzi wa magari 20 kwa ajili ya Vyuo vya Ualimu;

(iv) imeratibu ujenzi wa ofisi mpya 100 za Uthibiti Ubora wa Shule ili kuboresha mazingira ya utendaji kazi. Ujenzi unatarajiwa kuanza mwezi Juni, 2019, baada ya taratibu za manunuzi kukamilika;

(v) imegharamia ujenzi wa Shule ya Sekondari Maalumu Patandi kwa ajili ya Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 640. Ujenzi wa madarasa nane, Jengo la Utawala, Bwalo na Jiko, Chumba cha Maabara, chumba cha TEHAMA, Maktaba na Bweni moja vimekamilika na tayari wanafunzi wa Kidato cha Kwanza mwaka 2019 wameanza masomo; na

(vi) imegharamia mafunzo ya wanataaluma 68 wakiwemo wa Shahada ya Uzamili wawili (2) na Uzamivu 66 kutoka Vyuo Vikuu vya Umma kwa lengo la kuongeza idadi ya Wahadhiri nchini.

**Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) –  
Kuimarisha Ufundishaji na Ujifunzaji wa Stadi za Kusoma,  
Kuandika na Kuhesabu - KKK**

**66. Mheshimiwa Spika**, programu hii inalenga kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa Stadi za Kusoma, Kuandika na

Kuhesabu (KKK) kwa watoto wenye umri wa miaka 5-13 walio ndani na nje ya mfumo rasmi. Mpango huu unafadhiliwa na Mfuko wa Ushirika wa Kimataifa wa Elimu (*Global Partnership for Education-GPE Fund*). Kwa mwaka wa fedha 2018/19 Wizara kupitia mradi imewezesha utekelezaji wa shughuli zifuatazo:

(i) ukamilishaji wa mafunzo kwa walimu 402 wa Elimu Maalum ambayo yamefanyika katika Vyuo vya Ualimu Morogoro, Butimba na Patandi kwa ajili ya kuwajengea uwezo zaidi walimu katika ufundishaji na ujifunzaji wa Stadi za KKK kwa wanafunzi wasioona na Viziwi wa Darasa la I-IV;

(ii) ukamilishaji Mafunzo kwa walimu wa nyongeza 1,598 wanaofundisha darasa la I na II, kwa ajili ya kuwajengea uwezo katika stadi za ufundishaji na ujifunzaji wa Stadi za KKK;

(iii) ufuatiliaji wa pamoja kwenye Halmashauri za Liwale, Mafia, Magu, Manyoni na Monduli; uliohusisha viongozi waandamizi kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, OR- TAMISEMI, Washirika wa Maendeleo ya Elimu, na wajumbe kutoka Taasisi zisizo za Serikali kwa lengo kubaini changamoto zilizopo katika utekelezaji wa malengo ya elimu;

(iv) kuratibu mkutano wa pamoja wa kutathmini utekelezaji wa Sekta ya Elimu, Sayansi na Teknolojia 2018 (JESR); na

(v) kuhamasisha ushiriki wa jamii katika kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za KKK kupitia Mtandao wa Elimu (TEN-MET).

### **Mradi wa Kuimarisha Elimu ya Ufundi, Mafunzo ya Ufundi Stadi na Elimu ya Ualimu**

**67. Mheshimiwa Spika**, mradi huu umejikita katika kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika Vyuo vya Ualimu pamoja na Mafunzo ya Ufundi Stadi. Kwa mwaka

wa fedha 2018/19, Wizara kupitia mradi huu imewezesha utekelezaji wa shughuli zifuatazo:

(i) kukamilisha maandalizi ya kuanza ukarabati na ujenzi katika Vyuo vya Ualimu sita (6) vya Dakawa, Mpwapwa, Kleruu, Marangu, Tabora na Butimba ambapo **Shilingi 5,450,000,000.00** zimetengwa na Mshauri Elekezi kutoka Chuo Kikuu cha Ardhi amepatikana; na

(ii) kuendelea na ujenzi wa vyuo vya Ufundi Stadi vya Mikoa ya Simiyu, Geita na Rukwa ambapo kiasi cha **Shilingi 24,500,000,000.00** zimetengwa kwa ajili ya ujenzi huo.

**Mradi wa Ukarabati wa Vyuo vya Ualimu (*Upgrading Teachers Colleges - UTC*)**

**68. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania ikishirikiana na Serikali ya Canada. Mradi unalenga kuinua ubora wa Elimu ya Ualimu ili kuwawezesha watanzania wengi kupata fursa za kujiunga na Mafunzo ya Ualimu. Kwa mwaka wa fedha 2018/19 Wizara imetekeleza shughuli zifuatazo:

(i) imeendelea na ujenzi wa Chuo cha Ualimu Mpuguso ambao umehusisha nyumba tatu (3) za ghorofa za walimu kwa ajili ya familia 12, nyumba moja (1) isiyo ya ghorofa ya mwalimu, nyumba mbili (2) za ghorofa kwa ajili ya mabweni ya wanafunzi 304 pamoja na ukarabati wa nyumba moja (1) ya mwalimu kwa awamu ya kwanza. Kwa awamu ya pili, ujenzi umefikia hatua ya umaliziaji ambao umehusisha majengo mawili ya ghorofa yenye vyumba 16 vya madarasa, maktaba, jengo la mihadhara, maabara yenye vyumba viwili na ukarabati wa mabweni;

(ii) imeendelea na mradi wa ujenzi wa Chuo cha Ualimu Shinyanga ambapo kwa awamu ya kwanza umehusisha nyumba moja (1) ya ghorofa ya walimu kwa ajili ya familia nne (4), nyumba 1 ya ghorofa kwa ajili ya mabweni ya wanafunzi 152 na ukarabati wa nyumba za walimu nne (4) na mabweni mawili (2) na vyoo vya wanafunzi matundu tisa (9). Kwa awamu ya pili, majengo yameezekwa

na yapo katika hatua za umaliziaji ambapo ujenzi unahusisha ghorofa mbili (2) zenye madarasa 16 kila moja; bweni moja (1) la ghorofa lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 152; maktaba na jengo la mihadhara; ukarabati wa mabweni awili (2); na bwalo la chakula;

(iii) imeendelea na ujenzi wa Chuo cha Ualimu Kitangali kwa awamu mbili ambapo kwa awamu ya kwanza ujenzi huo unahusisha nyumba 10 za vyumba vitatu (3) kila moja kwa ajili walimu, nyumba moja (1) yenye vyumba vinne (4) ya Mkuu wa Chuo; na Jengo la Mikutano. Awamu ya pili inahusisha ujenzi wa majengo mapya ya nyumba mbili (2) za ghorofa zenye vyumba vya madarasa 16, Maktaba, jengo la mihadhara, na majengo mawili (2) ya ghorofa ya mabweni kwa ajili ya wanafunzi 304. Jiwe la msingi la Majengo hayo liliwekwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na

(iv) imeendelea na mradi wa ujenzi wa awamu ya kwanza katika Chuo cha Ualimu Ndala ambao upo katika hatua ya msingi. Ujenzi huo unahusisha, ujenzi wa nyumba mbili (2) za ghorofa za mabweni kwa ajili ya wanafunzi 304, nyumba mbili (2) za ghorofa za madarasa zenye vyumba 16, Jengo la mihadhara, maktaba, na maabara za fizikia, kemia na baiolojia. Awamu ya pili imeendelea na ujenzi na ukarabati ambao upo katika hatua za umaliziaji. Ujenzi unahusisha nyumba mbili (2) za walimu za vyumba vinne (4) kila mmoja; nyumba tatu (3) za walimu zenye vyumba vitatu (3) kila moja; na Nyumba mbili (2) za ghorofa za walimu kwa ajili ya familia nane (8). Ukarabati unahusisha mabweni mawili (2) pamoja na vyoo viwili vya wanafunzi vyenye matundu 20.

### **Mradi wa Kuimarisha Mafunzo ya Elimu ya Ualimu (Teacher Education Support Program - TESP)**

**69. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unalenga kuimarisha Mafunzo ya Elimu ya Ualimu katika Vyuo 35 vya Ualimu vya Serikali. Kwa mwaka wa fedha 2018/19, Wizara kupitia mradi huu imewezesha utekelezaji wa shughuli zifuatazo:

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

- (i) Ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika Vyuo wa ualimu 35 vya Serikali vikiwemo vifaa vya Maabara za Sayansi kwa Vyuo vya Sayansi ili kuwawezesha wanafunzi kujifunza kwa vitendo;
- (ii) inaendelea na manunuzi ya Vitabu vya Masomo ya Kufundishia na Utaalamu katika elimu ya Ualimu ili kuwawezesha Wakufunzi na Wanafunzi kuwa na rejea za kutosha katika ufundishaji na ujifunzaji;
- (iii) Ununuzi na usambazaji wa Kompyuta za Mezani (Desktop Computers) 300, na *Projector* 100 kwa ajili ya kuimarisha Matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji katika vyuo vya ualimu na vifaa hivyo vimegawiwa katika Vyuo vya Ualimu 18 ambavyo ni; Dakawa, Ilonga, Mandaka, Mhonda, Murutunguru, Mamire, Ndala, Singachini, Shinyanga, Vikindu, Patandi, Tarime, Mpuguso, Sumbawanga, Mpwapwa, Tukuyu, Morogoro na Korogwe;
- (iv) inaendelea na manunuzi ya Kompyuta za Mezani (Desktop Computer) 480, *UPS* 480, *Photocopy* 35 (Heavy Duty) na *Laptops* 43 kwa ajili ya kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji katika vyuo vya Ualimu;
- (v) inaendelea na manunuzi ya vifaa vya Wanafunzi na Wakufunzi ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji kwa Wanafunzi wenye Mahitaji maalumu;
- (vi) imewezesha mapitio ya Mtaala wa Elimu ya Ualimu kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania ili kuwa na Mtaala unaoendana na mahitaji ya sasa;
- (vii) inaendelea na maandalizi ya Mkakati wa Jinsia wa Wizara kupitia Mshauri Elekezi, utakaowezesha utoaji na Usimamizi wa Elimu ya Ualimu kwa kuzingatia usawa wa kijinsia;
- (viii) inaendelea na maandalizi (Design) ya uunganishaji wa Vyuo vya Ualimu katika Mkongo wa Taifa ili kuviwezesha

kuwa na mtandao wa uhakika katika kuwezesha ufundishaji na ujifunzaji kwa kutumia TEHAMA;

(ix) imeandaa miongozo 22 ya mafunzo kazini kwa wakufunzi kwa ajili ya kuimarisha uwezo wao wa kufundisha masomo mbalimbali;

(x) imeanza ujenzi wa Chuo cha Ualimu Kabanga ambapo Mkandarasi ni SUMA JKT na Msimamizi ni *Bureau for Industrial Cooperation (BICO)* – Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa lengo la kuongeza uwezo wa chuo kudahili na pia kuweka mazingira mazuri na rafiki ya Ufundishaji na Ujifunzaji. Kazi ya tathmini ya athari za mazingira katika eneo la ujenzi kwa kumtumia Mshauri Elekezi - Taasisi ya Teknolojia Dar es salaam (DIT) imefanyika ili kukidhi mahitaji ya kisheria na kwa usalama wa majengo na jamii itakayoishi hapo;

(xi) imeendesha mafunzo kazini kwa Walimu 398 (Shule za Msingi 200 na Walimu wa Sekondari 198) wa Hisabati kutoka katika Halmashauri zenye ufaulu wa chini wa somo hilo. Halmashauri zilizohusika kwa shule za Msingi ni Meatu, Simanjiro, Mkalama na Ukerewe; na kwa shule za Sekondari ni: Gairo, Rufiji, Nanyamba, Ruangwa, Momba, Nyasa, Madaba na Korogwe; na

(xii) imekamilisha maandalizi ya Mafunzo kwa Menejimenti za Vyuo vya Ualimu vya Serikali ambapo mafunzo hayo yatatolewa na Taasisi ya Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu - (ADEM) kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kusimamia majukumu yao ya Kitaaluma na Utawala.

### **Mradi wa Elimu na Kukuza Stadi za Kazi na Ujuzi (Education and Skills for Productive Jobs - ESPJ)**

**70. Mheshimiwa Spika**, mradi wa ESPJ unatekelezwa kwa utaratibu wa Lipa Kulingana na Matokeo (Programu for Results - P4R), utekelezaji wa shughuli za mradi katika hatua za mwanzo umejikita katika kukamilisha viashiria vya kutoa fedha (Foundational Disbursement Linked Indicators)



*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

na kuweka Mwongozo wa utekelezaji wa mradi. Katika mwaka wa fedha 2018/19, Wizara kupitia Mradi huu imetekeleza kazi zifuatazo:

(i) imegharimia awamu ya kwanza ya ukarabati na ujenzi katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 20 na jumla ya **Shilingi 8,777,468,088.00** zilitengwa kwa kazi hiyo.

(ii) imegharimia ujenzi wa hosteli ya wanafunzi wa kike katika Chuo Kikuu cha Ardhi (ARU) kwa gharama ya **Shilingi Bilioni 1.5**;

(iii) imeanzisha mabaraza ya kisekta ya kusimamia maarifa (Sectoral Skills Councils) kwa kushirikiana na Taasisi ya TPSF;

(iv) imegharamia zoezi la kutafsiri Mitaala 24 ya fani mbalimbali za ufundi stadi na mihutasari 16 ya masomo mbobezi ya Vyuo vya maendeleo ya Wananchi (NTSC - VETA ngazi za 1-3) kutoka lugha ya Kiingereza kwenda Kiswahili kwa gharama ya **Shilingi 289,502,400.00**;

(v) imewezesha vijana 650 kutoka kaya maskini kupata Mafunzo kwenye Taasisi mbalimbali kulingana na mahitaji yao yaliyoko katika vipaumbele vya Serikali;

(vi) imewezesha na kuratibu zoezi la kuwajengea uwezo wahasibu kutoka Vyuo Vya Maendeleo ya Wananchi 54, Vyuo vya Ualimu 35 na Makao Makuu ya Wizara kuhusiana na malipo kwa kutumia mfumo wa kielektroniki, wakaguzi 16 wa ndani; wataalamu 8 wa TEHAMA kutoka Wizarani, TEA, NACTE, HESLB, VETA na TCU;

(vii) imeandaa, kuratibu na kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo watumishi 304 katika maeneo yafuatayo: huduma kwa wateja na Utunzaji wa Nyaraka (50), kuongeza ufanisi na Utunzaji wa Nyaraka (88), na watumishi 89 Maadili katika Utumishi wa Umma na kupewa kiapo cha uadilifu. Aidha, watumishi 77 wanaotarajiwa kustaafu walipatiwa mafunzo ya kujiandaa kustaafu kazi; na

(viii) imeanza maandalizi ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Dodoma ambapo eneo lenye ukubwa wa ekari 200 limepatikana katika kitongoji cha Nalla na **Shilingi** bilioni 18 zimetengwa kwa ajili hiyo. Ujenzi unatarajia kuanza July 2019.

### **Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni (School Water Sanitation and Hygiene - SWASH):**

**71. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2018/19 Wizara kupitia mradi wa Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni imetoa mafunzo ya Mwongozo wa Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni (School WASH Guideline) kwa Wathibiti Ubora wa Shule wa Halmashauri 63 za mikoa ya Njombe, Ruvuma, Mbeya, Songwe, Rukwa, Katavi, Arusha, Dodoma, Tanga na Kilimanjaro. Mafunzo haya yalilenga kuwajengea uwezo Wathibiti Ubora wa Shule katika kufuatilia, kutathmini na kutoa ushauri kuhusu huduma ya maji, usafi wa mazingira na ujenzi wa miundombinu ya vyoo shuleni.

### **TUME YA TAIFA YA UNESCO (FUNGU 18)**

**72. Mheshimiwa Spika**, baada ya kueleza utekelezaji wa mpango na bajeti kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu 46) naomba sasa nitoe utekelezaji wa Tume ya Taifa ya UNESCO (Fungu 18) kwa mwaka 2018/19.

**73. Mheshimiwa Spika**, Tume ya Taifa ya UNESCO ina jukumu la kuratibu na kutoa ushauri kuhusu Elimu, Sayansi, Habari na Utamaduni katika muktadha wa kimataifa. Aidha, Tume inashiriki katika kutengeneza viwango vya ubora vinavyotakiwa katika Nyanja ya Elimu, Sayansi na Utamaduni kwa kutoa maoni moja kwa moja au kwa kushirikisha wadau kutoa maoni katika maandalizi ya nyaraka mbalimbali kama vile mikataba na makubaliano ya kimataifa.

**74. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/19 Tume ilikadiria kukusanya Maduhuli yenyethamani ya **Shilingi 70,000,000.00**. Hadi kufikia tarehe 15 Aprili, 2019 Tume ilikuwa haijafanikiwa kukusanya maduhuli hayo. Hii ni kutokana na kutofanyika

kwa kazi zilizopangwa kwa ajili ya kukusanya maduhuli katika kipindi husika. Kazi hizo zimepangwa kufanyika mwezi May, 2019 hivyo Tume inatarajia kukusanya fedha hizo kabla ya tarehe 30 Juni 2019.

**75. Mheshimiwa Spika**, makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa mwaka 2018/19 yalikuwa ni **Shilingi 666,855,000.00** (Mishahara **Shilingi 334,562,000.00** na Matumizi Mengineyo **shilingi 332,293,000.00**). Hadi kufikia tarehe 31 Machi 2019 Tume imepokea jumla ya **Shilingi 396,818,000.00** sawa na asilimia **59.5** ya makadirio. Kati ya fedha hizo Mishahara ni **Shilingi 215,897,000.00** sawa na asilimia **64.5** na Matumizi Mengineyo ni **Shilingi 180,921,000.00** sawa na asilimia **54.5** ya makadirio.

**76. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2018/19 Tume imetekeleza kazi zifuatazo:

(i) imekutana na wadau na kujadili namna bora ya kuboresha upatikanaji wa fursa kwa Watanzania kupitia kazi na programu za UNESCO na mashirika mbalimbali ya Kimataifa;

(ii) imeratibu ushiriki wa Tuzo za GAPMIL *Global Media and Information Literacy* kwa wadau wa hapa nchini ili kupata ushiriki katika Tuzo hizi;

(iii) imeratibu na kushiriki katika Tuzo za Mfalme Hamad Bin Isa Al-Khalifa kwenye masuala ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika elimu;

(iv) imetoa fursa ya mafunzo kwa Watumishi wawili kwenye masuala ya maji salama yaliyofanyika nchini Kenya kwa kushirikiana na Ofisi ya Kikanda ya UNESCO;

(v) imeratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano Mkuu wa UNESCO uliofanyikanchini Ghana na Italia pamoja na kutoa mrejesho kwa wadau kuhusu Maazimio yake;

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

(vi) imeshiriki katika Ukaguzi katika Kambi ya Siwandu katika Hifadhi ya *Selous* ili kudhibiti uharibifu wa mazingira;

(vii) imetembelea Hifadhi ya Ngorongoro na kutoa elimu kwa wadau kuhusu mapori tengefufu na namna bora ya kuyaendeleza;

(viii) imekagua mradi wa “Kilwa Kisiwani” kuhusu ujenzi wa ukuta wa kuzuia mawimbi ya bahari yasiweze kuharibu magofu ya Kilwa Kisiwani ili kujiridhisha na ripoti iliyowasilishwa ukaguzi ulithibitisha kuwa fedha iliyotumwa na UNESCO kwa ajili ya ujenzi wa ukuta huo ilitumika kama ilivyokusudiwa;

(ix) imeshiriki kikao katika kupitia Sheria ya Uhifadhi ya Ngorongoro kilichoandaliwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba;

(x) imeandaa Mkutano wa wasimamizi wa vituo ili kujadili utekelezaji wa maazimio na ushauri uliowekwa wenye kuangalia hatari inayoweza kutokea kwenye vituo vye Urithi vilivyopo, na kuandaa kikosi kazi cha kusimamia masuala yaliyopendekezwa;

(xi) imeshiriki kwenye programu ya O3- *Our Rights, Our Lives, Our Future* iliyojikita katika kupunguza maambukizi mapya ya UKIMWI ndoa na mimba za utotoni na unyanyasaji wa kijinsia;

(xii) kupitia sekta ya Utamaduni na Urithi wa Dunia, Tume imefanya Mkutano na wadau wa Mji Mkongwe Zanzibar ili kuboresha mahusiano;

(xiii) imeratibu mradi wa mazingira kupitia Mtandao wa kishule wa UNESCO-ASP Net nchini; na

(xiv) imeratibu Mkutano wa Tume za Taifa kwenye nchi za Afrika Mashariki hapa nchini.

## **C.MPANGO NA BAJETI YA FUNGU 46 KWA MWAKA 2019/20**

**77. Mheshimiwa Spika**, baada ya kueleza utekelezaji wa mafungu yote mawili yaani Fungu 46 na Fungu 18 naomba sasa nielezee Mpango na Bajeti ya Mafungu haya kwa mwaka wa fedha 2019/20.

**78. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/20, Wizara yangu imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

### **Kuendeleza Elimu ya Awali, Msingi na Sekondari kwa Kutoa Ithibati ya Mafunzo ya Ualimu na Maendeleo ya Kitaalamu ya Walimu**

**79. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/20, Wizara itatekeleza kazi zifuatazo:

(i) kudahili jumla ya wanachuo 17,554 katika Vyuo vya Ualimu;

(ii) itagharamia chakula na mafunzo kwa vitendo (Block Teaching Practise - BTP) kwa wanachuo 21,873 kwa Vyuo vya Ualimu vya Serikali 35; na

(iii) itafanya ufuatiliaji kwa Vyuo vya Ualimu 137 (35 vya Serikali na 102 visivyo vya Serikali) ili kubaini uzingatiaji wa Kanuni, Taratibu na Miongozo ya Elimu.

### **Kusimamia Uendelezaji wa Mafunzo Katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi**

**80. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/20, Wizara itaendelea na ukarabati wa Vyuo 34 vya Maendeleo ya Wananchi. Aidha, Wizara itaongeza udahili wa Wanafunzi kutoka 5520 kwa mwaka wa masomo 2018/2019 hadi kufikia 10,000 kwa mwaka wa masomo 2019/20 na itaendelea na ununuzi wa vifaa vipya vya kisasa vya kufundishia na kujifunzia, kwa lengo la kuboresha mazingira ya utoaji wa mafunzo.

## **Kutungua na Kutekeleza Sera za Elimu, Utafiti, Huduma za Maktaba, Sayansi, Teknolojia na Ubunifu**

**81. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2019/20 Wizara itaendelea kusimamia Sera, Sheria na Miongozo katika Sekta ya Elimu ili kuhakikisha kuwa elimu katika ngazi zote inatolewa kwa ubora unaokusudiwa kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itakamilisha mapitio ya Sera ya Sayansi na Teknolojia ya mwaka 1996 ili kuwa na Sera ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu inayoendana na mahitaji ya sasa;

(ii) itafanya tathmini na uchambuzi wa utekelezaji wa Sera ya Nyuklia ili kubaini mafanikio na changamoto kwa lengo la kuzifanyia kazi;

(iii) kutoa ushauri wa kisheria kuhusu Sera, Nyaraka, Miongozo na Mikakati ya Sekta ya Elimu, Sayansi na Teknolojia;

(iv) Kuandaa na kuwasilisha katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali maandalizi ya miswada ya sheria, marekebisho ya sheria na Kanuni zinazoihusu Sekta ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

## **Kuainisha Mahitaji ya Nchi Katika Ujuzi na Kuuendeleza**

**82. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2019/20 Wizara itaendelea kukuza stadi za kazi kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) kukuza vipawa vya walimu na wanafunzi wenye ubunifu kupitia ushirikiano wa karibu na viwanda mbalimbali vinavyotumia ubunifu na teknolojia zinazozalishwa nchini katika kuzalisha bidhaa kwa wingi na kuzitangaza kwenye soko na hivyo kuhamasisha ubunifu;

(ii) kuwezesha Vyuho 30 vya Maendeleo ya Wananchi kutoa maarifa na ujuzi wa Ufundi kwa wanafunzi wa kike walioshindwa kuendelea na masomo ya elimu ya Msingi na Sekondari kwa sababu mbalimbali;

(iii) kuendelea na zoezi la kurasimisha ujuzi kwa wanagenzi 6,243 ambao hawakupitia katika mfumo rasmi wa mafunzo;

(iv) kuboresha stadi za kazi/ujuzi kwa wajasiriamali 3,000 kupitia programu ya Mafunzo ya kukuza Ujasiriamali (*Integrated Training for Entrepreneurship Promotion* (INTEP));

(v) kujenga uwezo kwa walimu wa ufundi stadi ili kuboresha ujuzi wao katika nyanja mbalimbali za kiujuzi; na

(vi) kuendelea kuzijengea uwezo Taasisi za VETA, NACTE, na TCU ili kusimamia Ubora wa Elimu ya Ufundi na Stadi za Kazi.

### **Kusimamia Ithibati na Uthibiti Ubora wa Shule na Vyuo vya Ualimu**

**83. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/20 Wizara itaendelea kusimamia Ithibati ya Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu na Kusimamia Ubora wa Elimu kwa kutekeleza yafuatayo:

#### **Ithibati ya Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu**

**84. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/20 Wizara:

(i) itaanzisha mfumo wa Kielektroniki wa Ithibati ya shule ili kuongeza ufanisi katika usajili wa shule;

(ii) itafuatilia shule zilizosajiliwa kwa masharti ya kukamilisha miundombinu ili kuona zimetimiza masharti waliyopewa;

(iii) itafanya ufuatiliaji katika shule 200 zisizo za Serikali ili kubaini sifa za kitaaluma na kitaalam kwa walimu wa kigeni, kwa lengo la kuhakikisha Sheria za nchi na sifa za walimu zinazingatiwa ipasavyo.

## Uthibiti Ubora wa Shule na Vyuvo vya Ualimu

**85. Mheshimiwa Spika**, katika Uthibiti Ubora wa Shule na Vyuvo vya Ualimu Wizara itatekeleza yafuatayo:

(i) itafanya tathmini ya jumla ya Asasi 5,945 ambazo ni sawa. na asilimia **25** ya Asasi zote zikiwemo shule za Msingi **4,667**; sekondari **1,244**; na Vyuvo vya Ualimu **56**; ili kutoa ushauri na mapendekezo kwa ajili ya kuboresha ufundishaji na ujifunzaji kwa lengo la kutoa elimu bora;

(ii) itatoa mafunzo ya awali kwa Wathibiti Ubora wa Shule wapya 200 ili kuwajengea uwezowa kusimamia kikamilifu ufundishaji wa walimu darasani pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu na kitaaluma kwa Walimu Wakuu wa Shule;

(iii) itaendelea ujenzi wa Ofisi 100 za Uthibiti Ubora wa Shule katika Wilaya mbalimbali na ukarabati wa Ofisi za Uthibiti Ubora wa Shule 40 ili kuboresha mazingira ya kufanyia kazi na kuongeza ufanisi wa utendaji kazi; na

(iv) itafungua Ofisi mpya za Uthibiti Ubora wa Shule tano (5) katika Wilaya za Kyerwa - Kagera, Kakonko - Kigoma, Nanyamba - Mtwara, Madaba - Ruvuma na Nsimbo - Katavi kuongeza ufanisi katika ufuatiliaji wa masuala ya Elimu.

## Usimamizi wa Elimumsingi

**86. Mheshimiwa Spika**, katika kusimamia Elimu ya Awali, Msingi na Sekondari, katika mwaka 2019/20 Wizara itatekeleza yafuatayo:

(i) itafanya ufuatiliaji na tathmini ya mafanikio na changamoto katika vituo shikizi vya shule ili kuandaa mikakati ya kuimarisha Elimu katika Vituo hivyo nchini;

(ii) itaandaa Mwongozo wa uanzishaji na usimamizi wa Maktaba za Vijijini ili kukuza stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK);



## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

- (iii) itawajengea uwezo walimu 300 wa Shule za Sekondari ili kuimarisha stadi za utoaji wa huduma ya ushauri na unasihi kwa wanafunzi kwa lengo la kukabiliana na changamoto zinazowapata wanafunzi wao;
- (iv) itafanya usimamizi na ufuatiliaji wa michezo ya UMITASHUMTA na UMISETA katika ngazi za Mkoa na Taifa ili kuona ubora na viwango vya uendeshaji wa michezo hiyo na hatimaye kuandaa mikakati stahiki;
- (v) itafanya ufuatiliaji na tathmini kuhusu utekelezaji wa nyaraka na miongozo katika Sekta ya Elimu;
- (vi) itafanya ufuatiliaji wa programu za Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi kuhakiki uwepo na ufanisi wa vituo hivyo;
- (vii) itafanya ufuatiliaji na tathmini kwa Shule za Ufundi, Kilimo Sayansikimu, Biashara na Michezo ili kubaini changamoto na kuzitafutia ufumbuzi kwa ajili ya kuboresha Shule hizo;
- (viii) kuandaa Kiunzi cha utambuzi na kutoa tuzo kwa wahitimu wa Programu za Elimu Nje ya Mfumo Rasmi;
- (ix) itaandaa Mwongozo wa Stadi za Maisha kwa kuzingatia Elimu ya UKIMWI na changamoto wanazopata wanafunzi;
- (x) itahuisha Mwongozo wa Mafunzo ya Malezi na Unasihi kwa walimu na wakufunzi wa Vyuo vya Ualimu ili kuimarisha huduma ya malezi shuleni; na
- (xi) itaimarisha utoaji wa Elimurika ambayo huhusisha watoto wa rika moja, Elimu ya Afya ya Uzazi na Stadi za maisha kwa kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miongozo.

### **Usimamizi wa Elimu Maalum**

**87. Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia kuwa Elimu ni haki ya msingi kwa kila Mtanzania, Wizara kwa mwaka 2019/20

itaendelea kuimarisha utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum kwa kutekeleza yafuatayo:

- (i) kuvijengea uwezo Vyuo vya Elimu ya Ufundi Stadi na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ili kuimarisha upatikanaji wa fursa za elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi na stadi kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum;
- (ii) kutoa mafunzo kuhusu matumizi ya lugha ya Alama ya Tanzania kwa walimu 500 wanaofundisha katika shule za msingi na sekondari ili kuinua ubora wa Elimu kwa wanafunzi viziwi;
- (iii) kuwajengea uwezo walimu a wakufunzi wenye mahitaji maalum wapatao 150 kuhusu matumizi ya teknolojia saidizi ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji katika ngazi za Elimu ya Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu; na
- (iv) kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa kuwabaini na kuwaandikisha shuleni watoto wenye mahitaji maalum ili kuwapa fursa ya Elimu kwa kuzingatia mahitaji yao katika ujifunzaji.

### **Usimamizi na Uendelezaji wa Elimu ya Juu**

**88. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/20 Wizara imepanga kufanya yafuatayo:

- (i) itafuatilia maendeleo ya udahili, uandikishaji na utoaji wa mikopo kwa wanafunzi katika Taasisi za Elimu ya Juu;
- (ii) itaratibu skolashipu za wanafunzi wa Elimu ya Juu kutoka nchi rafiki;
- (iii) itafadhili wanafunzi 10 raia wa China kusoma Lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam;
- (iv) itafuatilia utendaji wa Vituo vya Umahiri vya Afrika katika Kanda ya Afrika Mashariki na Kusini (African Centre of

Excellence- ACE II), ili kuhakikisha malengo ya uanzishwaji wa vituo hivi yanatekelezwa; na

(v) itaendeleza ufadhili wa masomo ya wanataaluma kutoka Vyuo Vikuu vya Umma katika Shahada za Uzamili na Uzamivu katika Nyanja za Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati.

**Usimamizi wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi 89. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2019/20 Wizara imepanga kutekeleza kazi zifuatazo: -

(i) itawezesha kutoa mafunzo ya muda mrefu ya Ufundi stadi na Elimu ya Wananchi (Folk Education) kwa washiriki 10,000 katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 54;

(ii) itawezesha mafunzo ya muda mfupi na mafunzo nje ya Chuo kwa washiriki 24,000 katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 54;

(iii) itawezesha Usimamizi na Ukaguzi wa shughuli za mafunzo katika Vyuo 54 vya Maendeleo ya Wananchi;

(iv) itawezesha upatikanaji wa Vifaa vya kiufundi vya kufundishia na kujifunzia katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 54;

(v) itawezesha maafisa saba (7) kushiriki mikutano ya ushirikiano wa kikanda na kimataifa kwenye maeneo ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi nje ya Nchi (EAC, SADC, IDEA, UNEVOC, UNESCO, EFE) ili kuwajengea uwezo wa kuratibu na kusimamia Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini;

(vi) itawezesha mkutano wa kimkakati wa wadau wanne (4) katika Mafunzo ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi ili kuwajengea uwezo wa kusimamia na kuratibu mafunzo na uandaaji wa Mitaala ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi;

(vii) itagharamia malipo ya huduma muhimu kwa Vyuo 54 vya Maendeleo ya Wananchi (Umeme, Maji, Huduma za simu, Posta);

(viii) itagharamia mkutano wa mwaka wa wakuu wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 54;

(ix) itagharamia upimaji na upatikanaji wa hati miliki ya maeneo ya Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kote nchini; na

(x) itagharamia chakula katika Vyuo 54 vya Maendeleo ya Wananchi.

### **Usimamizi wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu**

**90. Mheshimiwa Spika**, katika kutambua, kujenga, kukuza na kuendeleza ubunifu kwa Watanzania katika nyanja za Sayansi, Teknolojia na Ubunifu Wizara itafanya yafuatayo:

(i) itaendelea kuibua na kuwatambua wabunifu na wagunduzi nchini kwa kuendesha mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu na kutoa tuzo kwa wabunifu mahiri na kuwaendeleza;

(ii) itakamilisha kuandaa Mwongozo wa Kitaifa wa Kuanzisha na Kuendeleza vituo vya teknolojia na ubunifu nchini;

(iii) itakamilisha mapitio ya vipaumbele vya Taifa katika Utafiti kwa lengo kuvifanya viendane na mahitaji ya sasa;

(iv) itaandaa na kuhuisha kanzi-data ya teknolojia, ubunifu na utafiti unaofanyika nchini kwa lengo la kutambua, kulinda na kuhamasisha matumizi yake katika kutatua changamoto katika jamii;

(v) itaandaa kiunzi cha kuratibu ubunifu na utafiti kwa lengo la kufanya ubunifu na utafiti uwe na mchango katika kutatua changamoto zinazoikabili jamii nchini;

(vi) itasimamia na kuendeleza mchango wa matumizi salama ya teknolojia ya nyuklia katika maendeleo ya Taifa; na

(vii) itaendelea kujenga uelewa wa wananchi katika masuala ya sayansi, teknolojia na ubunifu kupitia vyombo vya habari kwa lengo la kuhamasisha matumizi yake katika kutatua changamotombalimbali kwenye jamii.

### **Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali watu**

**91. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2019/20 Wizara itatekeleza majukumu yafuatayo:

(i) kuandaa na kutekeleza Mpango wa Wizara wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa mahali pa kazi;

(ii) kutoa mafunzo elekezi ya kazi kwa watumishi wa pya na watumishi ambao hawajapatiwa mafunzo hayo ili kuwajengea ufahamu kuhusu Sheria, Kanuni, Taratibu, Miongozo na Maadili ya Kazi katika Utumishi wa Umma;

(iii) kutoa mafunzo na kufanya ufuatiliaji wa utumiaji wa Mfumo wa Wazi wa Mapitio ya Tathmini ya Utendaji Kazi kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi na uwajibikaji wa watumishi;

(iv) kuandaa na kuendesha mafunzo kuhusu mwenendo na maadili katika utumishi wa umma kwa watumishi wa Wizara;

(v) kuendelea kusimamia na kuhakiki rasilimali watu kwa lengo la kuthibitisha uwepo wa watumishi katika maeneo yao ya kazi na endapo sifa walizonazo zinaendana na majukumu wanayoyatekeleza; na

(vi) kuendelea kuboresha mfumo wa mawasiliano wa kupokea, kutunza na kusambaza nyaraka za ofisi kwa lengo la kuleta ufanisi na kuongeza kasi ya mawasiliano ya kiofisi.

## Usimamizi wa Rasilimali za Wizara

**92. Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha udhibiti na usimamizi wa rasilimali za Wizara, kwa mwaka wa fedha 2019/20 Wizara itatekeleza majukumu yafuatayo:

(i) itakagua mifumo na taratibu za ukusanyaji wa maduhuli ili kubaini endapo taratibu zinazingatiwa, mifumo inafuatwa na inajitosheleza na endapo maduhuli yanakusanywa kikamilifu;

(ii) itakagua mifumo ya udhibiti wa matumizi ya Wizara ili kubaini endapo mifumo hiyo inajitosheleza na inafuatwa ili kufikia malengo yaliyokusudiwa;

(iii) itakagua mfumo wa malipo ya mishahara (payroll) ili kubaini endapo watumishi halali ndiyo wanaolipwa mishahara kwa kiwango kinachotakiwa;

(iv) kufanya ukaguzi wa miradi inayotekelezwa na Wizara ili kubaini endapo malengo ya mradi yaliyowekwa yanafikiwa;

(v) ukaguzi wa mali (assets) za Wizara ili kuona kama mali hizo zinatambuliwa na Wizara, zimeingizwa katika daftari la kuhifadhi kumbukumbu (asset register) ya Wizara na kuona kama kuna udhibiti wa mali hizo;

(vi) ukaguzi wa mifumo ya taratibu za manunuzi na usimamizi wa mikataba ili kubaini endapo mifumo hiyo inatekelezwa ipasavyo;

(vii) itawezesha utekelezaji wa vikao vya Kamati ya Ukaguzi ya Wizara;

(viii) kuwezesha utekelezaji wa Vikao vya Kamati ya Kusimamia, Kudhibiti na Kuratibu Mapato na Matumizi ya Serikali; na

(ix) ukaguzi wa rasilimali fedha zinazopelekwa katika taasisi za Wizara ili kubaini kama zimepokelewa, zinaingizwa

kwenye daftari la mapato la taasisi kwa mujibu wa sheria na zinatekeleza kazi zilizokusudiwa.

## **URATIBU WA TAASISI NA WAKALA ZILIZO CHINI YA WIZARA**

**93. Mheshimiwa Spika**, Wizara itaendelea kuratibu shughuli za Taasisi na Wakala inazosisimamia. Kazi zilizopangwa kufanyika mwaka 2019/20 katika Taasisi zilizo chini ya Wizara ni kama ifuatavyo:

### **Tume ya Vyuu Vikuu Tanzania**

**94. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/20, Tume itatekeleza yafuatayo:

(i) kusimamia ubora wa Elimu ya Juu kwa kupitia mifumo na miongozo mbalimbali inayotumika kusimamia Uthibiti na Ithibati ya Elimu ya Juu nchini;

(ii) kukagua Vyuu 15 vya Elimu ya Juu kwa lengo la kuhakiki ubora wa Vyuu hivyo;

(iii) kufanya tathmini kwa programu 200 za masomo mbalimbali katika Vyuu Vikuu nchini kwa lengo la kuzisajili;

(iv) kufanya tathmini na kutambua Tuzo 3,000 za ngazi ya Shahada zilizotolewa katika Vyuu vya Elimu ya Juu vya nchi za nje;

(v) kuboresha Mfumo wa kutumia TEHAMA katika utoaji na ukusanyaji taarifa kutoka Vyuu vya Elimu ya Juu nchini ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa kwa wakati kwa ajili ya mipango na maamuzi ya kisera na kiutendaji;

(vi) kushiriki katika makongamano na mikutano ihusuyo uimarishaji na Uthibiti Ubora wa Elimu ya Juu katika ukanda wa Afrika Mashariki na kimataifa kwa lengo la kuongeza ujuzi na weledi katika kuthibiti ubora wa Elimu ya Juu nchini;

(vii) kuratibu Maonesho ya 14 ya Elimu ya Juu nchini ili kutoa elimu kwa umma kuhusu Vyuo na programu mbalimbali zitolewazo;

(viii) kuratibu udahili wa wanafunzi 85,000 wa mwaka wa kwanza watakaomba kudahiliwa katika Vyuo vya Elimu ya Juu ili kuhakiki kama wanakidhi vigezo vya kudahiliwa katika programu husika; na

(ix) kuwajengea uwezo taasisi tano (TCU, VETA, NACTE, TEA na HESLB) kwa lengo la kuwawezesha kutekeleza majukumu yao ya kusimamia utekelezaji wa mradi wa ESPJ kwa ufanisi.

### **Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi**

**95. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/20 Mamlaka itatekeleza kazi zifuatazo:

(i) itaongeze udahili wa wanafunzi wa kozi ndefu na fupi katika Vyuo vya Ufundi Stadi nchini kutoka wanafunzi 200,000 hadi 370,000 ifikapo Juni,2020;

(ii) itajenga karakana tano katika Vyuo vya mafunzo ya Ufundi Stadi ambapomikoa ya Lindi na Pwani kutajengwa karakana moja kila Mkoa, Manyara karakana mbili na ujenzi wa karakana ya *“Mechatronics”* katika chuo cha TEHAMA-Kipawa, Dar es Salaam;

(iii) itajenga jengo la utawala, uzio na kufanya marekebisho katika bwani moja na madarasa mawili katika Chuo cha Ufundi cha Arusha (ATC);

(iv) itajenga bwani la wasichana lenye uwezo wa kulaza wanafunzi 200 katika Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi cha Mkoa wa Mbeya ili kuongeza udahili kwa wasichana;

(v) itajenga karakana ya mitambo mizito (Heavy Duty Equipment Mechanics) katika Chuo cha Ufundi Stadi cha Mwanza ili kukidhi hitaji la makampuni ya migodi ya Geita, Bulyanhulu na North Mara;



*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

(vi) itajenga nyumba 10 za watumishi wa Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi cha Ulyankulu pamoja na ununuzi wa nyumba 10 za watumishi wa Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi cha Manyara;

(vii) itajenga karakana katika Chuo cha Ualimu wa Mafunzo ya Ufundi Stadi Morogoro (MVTTTC) kwa lengo la kupanua fursa za mafunzo;

(viii) itaongeze ushiriki wa sekta binafsi ili kuwekeza katika utoaji wa mafunzo ya ufundi stadi kwa kukaribisha ushirikiano wao kupitia *Public Private Partnership* -PPP; na

(ix) itawajengea uwezo wamiliki wa Vyuo visivyo vya VETA ili kuimarisha ubora katika utoaji wa mafunzo ya ufundi yenye kulenga umahiri.

**96. Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha na kuboresha njia mbadala za kuwafikia watu wengi ili kupata mafunzo ya ufundi stadi, Mamlaka itatekeleza yafuatayo:

(i) itaanza utekelezaji wa mfumo rasmi wa mafunzo ya Uanagenzi katika Vyuo vitano (5) vya ufundi stadi vya VETA;

(ii) itaendelea na zoezi la kurasimisha ujuzi kwa wanagenzi 6,243 ambao hawakupitia katika mfumo rasmi wa mafunzo;

(iii) itaboresha stadi za kazi/ujuzi kwa wajasiriamali 3,000 kupitia programu ya Mafunzo ya kukuza Ujasiriamali *Intergrated Training for Entrepreneurship Promotion* (INTEP);

(iv) itatekeleza programu ya mafunzo kwa masafa ikiwemo VETA Somo (VSOMO); na

(v) itaboresha ufanisi wa utendaji kazi katika viwanda mbalimbali kwa kushirikiana na Waajiri ambao ni wamiliki wa viwanda hivyo chini ya utaratibu wa Mpango wa Kuimarisha Maarifa (*Skills Enhancement Program* – SEP).

**97. Mheshimiwa Spika**, katika kuongeza ubora wa mfumo wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Mamlaka itatekeleza yafuatayo:

(i) itanunua vifaa vya kisasa kwa Vyuo vitatu vya Ufundi Stadi vya TEHAMA Kipawa-Dar es Salaam, Mtwara na Lindi vilivyoteuliwa kuwa Vyuo vya mfano (Centres of Excellence) katika utoaji wa mafunzo ya sekta ya kipaumbele ya TEHAMA, Mafuta na Gesi;

(ii) itaendelea na uhuishaji Mitaala ya Elimu na Mafunzo kulingana na mahitaji ya soko la ajira;

(iii) itawezesha uandikishaji na usajili wa Vyuo vya Ufundi Stadi sambamba na utoaji ithibati kwa programu za mafunzo stadi zinazofundishwa;

(iv) itaimarisha utahini na utoaji vyeti vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi kwa kutekeleza na kuwajengea ujuzi wa kutahini ujuzi kwa programu zote na katika Vyuo vyote vya ufundi stadi vilivyosajiliwa;

(v) itatekeleza programu atamizi kwa wahitimu wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi ili waweze kujajiriwa au kujajiri; na

(vi) itaimarisha ushirikiano na Makampuni ya Waajiri yapatayo 100 katika Sekta Rasmi, kupitia programu ya mafunzo kuimarisha ujuzi kwa madhumuni ya kuongeza uzalishaji wenye tija viwandani.

**98. Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha uwezesaji wa kifedha kwa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi na kuimarisha vyanzo vya mapato ya ndani, Mamlaka itatekeleza yafuatayo:

(i) itaimarisha shughuli za kuongeza mapato ya ndani pamoja na shughuli za hoteli na kumbi za mikutano zilizopo katika Vyuo vya Ufundi Stadi vya Njiro-Arusha, Dodoma, Mtwara, Mikumi, Tanga na Mwanza;

(ii) itaboresha fani ya uchapishaji na Ujarida katika Chuo cha Ufundi Stadi cha Mkoa wa Dar es Salaam; na

(iii) itaimarisha kikosi cha ujenzi cha Mamlaka.

**99. Mheshimiwa Spika**, katika kuimarishauwezo wa usimamizi wa elimu, utawala na huduma kwa jamii katika ngazi zote, Mamlaka itatekeleza programu ya uboreshaji wa ujuzi wa watumishi katika Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi. Aidha, itatoa mafunzo ya Ualimu wa Ufundi Stadi katika Chuo cha Morogoro kwa walimu 700 katika ngazi ya cheti na stashahada, na itaboresha uwezo wa kitaalamu kwa walimu 700 wa Ufundi Stadi waliohitimu kutoka Tuzo ya Taifa ya Ufundi Stadi Daraja la III hadi Daraja la VI, (*National Vocational Awards Grade III (NVA III)*) hadi *National Technical Award Grade VI (NTA VI)*).

**100. Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha utawala na usimamizi wa Elimu na Mafunzo, Mamlaka itatekeleza yafuatayo:

(i) itaanza ujenzi wa jengo la utawala la VETA Makao Makuu jijini Dodoma, itaboresha utendaji kazi kwa kutekeleza Muundo wa Mamlaka na Scheme of Service mpya na kuajiri watumishi wapya ili kuziba nafasi 491 zilizo wazi;

(ii) itahuisha Sera na miongozo ya usimamizi wa rasilimali watu ili kuimarisha utendaji na kuendana na Sera na miongozo ya Serikali;

(iii) itaimarisha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika utawala na utoaji wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi;

(iv) itatangaza shughuli za Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini kupitia vipindi mbalimbali vya runinga, redio, majarida, magazeti na mitandao ya simu; na

(v) itaboresha utawala na kuimarisha shughuli za ugavi za Mamlaka kwa kutoa mafunzo ya mabadiliko ya sheria ya manunuzi, kununua vitendea kazi stahiki na kuongeza watendaji wenye utaalamu wa ugavi.

## Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi

**101. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2019/20 Baraza litaendelea kuboresha Elimu na Mafunzo ya Ufundi nchini kwa kutekeleza yafuatayo:

- (i) kufuatilia na kutathmini Vyuo 300 vya Elimu ya Ufundi ili kuhakikisha kuwa Mafunzo yanayotolewa yanakidhi viwango vya ubora;
- (ii) kukagua na kutathmini Vyuo vya ufundi 80 kwa ajili ya uhakiki wa usajili wa Vyuo vitakavyokidhi sifa ya kutoa Mafunzo ya Elimu ya Ufundi, pamoja na kutoa miongozo itakayoviwezesha Vyuo kupata ithibati kamili endapo vitakidhi vigezo vilivyowekwa;
- (iii) kuhakiki na kuidhinisha Mitaala 100 na kuhuisha Mitaala sita (6) ya Kitaifa inayozingatia umahiri katika Vyuo vya Elimu ya Ufundi nchini ili kukidhi mahitaji ya soko la ajira; na
- (iv) kuratibu na kuhakiki udahili wa wanafunzi 120,000 katika programu za Astashahada na Stashahada katika Vyuo vya Ufundi.

## Mamlaka ya Elimu Tanzania

**102. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2019/20 Mamlaka imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:

- (i) kuwezesha ujenzi wa madarasa 75 katika shule za Msingi na Sekondari zenye uhaba mkubwa wa madarasa;
- (ii) kuwezesha ujenzi wa nyumba 20 za walimu wa sekondari katika maeneo yasiyofikiwa kwa urahisi ;
- (iii) kuwezesha ujenzi wa mabweni 16 ya wanafunzi wa kike katika shule za sekondari;

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

(iv) kuwezesha umaliziaji wa shughuli za ukarabati wa majengo katika shule kongwe 4 za Sekondari za Serikali za Mwenge, Msalato, Nganza na Mzumbe;

(v) kuwezesha ukarabati wa ofisi za Mamlaka ya Elimu Tanzania zilizopo Mikocheni Dar-es-salaam;

(vi) kuwezesha ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia pamoja na uboreshaji wa miundombinu kakika vyuo vya kati na Vyuo Vikuu 2 vya Zanzibar. Vyuo hivyo ni Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar;

(vii) kuwezesha ukarabati wa shule za msingi 5 katika jiji la Dodoma;

(viii) kuwezesha ujenzi wa vyoo katika shule 10 zenye upungufu mkubwa;

(ix) kuwezesha ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia na ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu kwa shule 10 za msingi na sekondari; na

(x) kuwezesha uratibu, ufuatiliaji na uendeshaji wa shughuli za Mfuko wa Elimu Tanzania.

**Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu**

**103. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/20, Bodi imepanga kutekeleza yafuatayo:

(i) kupanga na kutoa mikopo kwa wanafunzi 128,285, (sawa na ongezeko la asilimia 4.5 ukilinganisha na mwaka uliopita wa 2018/2019) ambapo kati ya hao, wanafunzi 45,485 watakuwa mwaka wa kwanza ikiwa ni ongezeko la asilimia 10.3 ukilinganisha na wanafunzi 41,234 wa mwaka 2018/19;

(ii) kufuatilia fedha inayolipwa ili kuhakikisha kwamba fedha za mikopo zinawafikia kwa wakati wanafunzi stahiki;

- (iii) kutoa mikopo yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 450** ambapo ni ongezeko la asilimia 5.0 ukilinganisha na mwaka 2018/19;
- (iv) kukusanya **Shilingi Bilioni 221.5** kutoka kwa wanufaika ambao mikopo yao imeiva. Hili ni ongezeko la asilimia 40.5 ukilinganisha na lengo la mwaka 2018/19 ambalo ni **Shilingi Bilioni 157.7**;
- (v) kuanzisha na kuimarisha ofisi mbili (2) za kanda katika mikoa ya Mbeya na Mtwara, ili kufikisha jumla ya ofisi sita (6) za kanda, zinazotarajiwa kukusanya **Shilingi Bilioni 30**;
- (vi) kuongeza ufanisi wa utendaji kazi kwa kuendeleza utekelezaji wa mkakati wa uboreshaji wa mifumo ya TEHAMA ili kuunganisha mifumo ya HESLB na ya wadau wengine na hivyo kuwafikia wanufaika wengi walioko katika sekta binafsi, na isiyokuwa rasmi; na
- (vii) kutekeleza kampeni za uelimishaji kuhusu huduma zinazotolewa na Bodiya Mikopo (HESLB), vigezo, utaratibu, wajibu wa wanufaika na waajiri katika urejeshaji wa mikopo.

## Taasisi ya Elimu Tanzania

**104. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2019/20 Taasisi itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) kuandika muhtasari wa lugha ya Kichina kidato cha Tano na Sita ambayo inafundishwa katika shule za Sekondari 16 (zikiwemo shule za sekondari: Zanaki, Benjamini Mkapa, Morogoro, Kilakala, Dodoma, Umonga, Kiwanja cha Ndege, Ilboru, Arusha, Lindi, Pamba, Mkonge, Mbeya, Samora, Old Tanga, na Usagara);
- (ii) kuandaa Mtaala na Muhtasari wa somo la Kiswahili kwa Shule za Msingi na Sekondari za nchi za Afrika ya Kusini na nchi nyingine zitakazowasilisha maombi ikiwemo Sudani Kusini ambapo Ukuzaji wa Lugha ya Kiswahili

ni moja ya vipengele katika Mkataba wa Makubaliano uliosainiwa hivi karibuni kati ya nchi hiyo na Tanzania;

(iii) kuhuisha mtaala wa elimu ya sekondari ili uzingatie mahitaji ya wanafunzi viziwi;

(iv) kuendelea na uandishi wa vitabu vya kiada kwa Darasa la Sita, Saba, Kidato cha Kwanza mpaka cha Sita na moduli kwa ajili ya Elimu ya Ualimu pamoja na kuandaa maudhui ya kielektroniki;

(v) kuchapa vitabu vya kiada vya Darasa la Sita mpaka la Saba, Kidato cha Kwanza mpaka cha Sita na moduli/vitabu vya Elimu ya Ualimu;

(vi) kufanya uhakiki na tathmini ya vitabu vya ziada na maudhui ya kielektroniki;

(vii) kurusha hewani vipindi vya Taasisi ya Elimu Tanzania vyenye kubeba maudhui ya kielektroniki kwa lengo la kukuza stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu;

(viii) kuendesha mafunzo kazini kwa walimu wa shule za Msingi Darasa la V – VII kwa mtaala ulioboreshwa ili kuwajengea uwezo wa kufundisha kuendana na mtaala huo;

(ix) kuendelea kuandika vitabu vya hadithi kwa ajili ya shule za msingi;

(ix) kufanya utafiti katika maeneo ya ufundishaji, ujifunzaji, na mtaala kwa jumla; na

(ix) kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mtaala kwa ngazi za Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu.

## **Baraza la Mitihani la Tanzania**

**105. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/20 Baraza litatekeleza kazi zifuatazo:

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

- (i) litaendesha Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne kwa watahiniwa 1,783,227 wanaotarajiwa kufanya upimaji huo mwezi Novemba, 2019;
- (ii) litaendesha Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa watahiniwa 978,051 wanaotarajiwa kufanya mtihani huo mwezi Septemba, 2019;
- (iii) litaendesha Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili kwa watahiniwa 547,870 wanaotarajiwa kufanya upimaji huo mwezi Novemba, 2019;
- (iv) litaendesha Mtihani wa Kidato cha Nne kwa watahiniwa 450,200 na Mtihani wa Maarifa kwa watahiniwa 15,500 wanaotarajiwa kufanya mitihani hiyo mwezi Novemba, 2019;
- (v) litaendesha Mtihani wa Kidato cha Sita kwa watahiniwa 87,170 wanaotarajiwa kufanya mtihani huo mwezi Mei, 2020;
- (vi) litaendesha Mtihani wa Cheti na Diploma ya Ualimu kwa watahiniwa 11,924 wanaotarajiwa kufanya mtihani huo mwezi Mei, 2020; na
- (vii) litaendesha Upimaji wa Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa sampuli ya wanafunzi 10,400 wa darasa la Pili.

**Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu - ADEM**

**106. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/20, Wakala unatarajia kutekeleza kazi zifuatazo:

- (i) kudahili walimu 2,521 watakaosoma kozi za Stashahada ya Uongozi na Usimamizi wa Elimu na Uthibiti Ubora wa Shule;



*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

- (ii) kudahili Walimu Wakuu wa Shule za Msingi 50 watakaosoma stashahada ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu (CELMA ODL) ili kuwajengea uwezo katika masuala ya Uongozi wa Elimu;
- (iii) kuboresha Mtaala wa Mafunzo ya Stashahada ya Uthibiti Ubora wa Shule ili iendane na matakwa ya Miongozo mbalimbali na mahitaji ya wakati;
- (iv) kutoa mafunzo ya uongozi kwa wakuu wa shule za Msingi 500 kwa lengo la kuimarisha uongozi wa shule;
- (v) Kutoa mafunzo ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu kwa Wakuu wa Shule 2,554;
- (vi) kuendesha mafunzo ya Usimamizi wa Elimu kwa Maafisa Elimu 380 Tanzania Bara kwa lengo la kuboresha utendaji kazi;
- (vii) kuendesha mafunzo kwa Maafisa Elimu Kata 3,996 kuhusu Uongozi na uratibu wa Elimu kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa elimu katika kata zao;
- (viii) kuendesha mafunzo ya Uongozi na Menejimenti kwa Wakuu na Wasaidizi wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 110 kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa taasisi hizo;
- (ix) kutoa mafunzo kwa Washiriki kutoka Vyuo vya Ualimu wapatao 340 juu ya Usimamizi wa Taaluma, Fedha, Manunuzi na Ufuatiliaji na Tathmini kwa lengo la kuimarisha usimamizi na matumizi sahihi ya fedha;
- (x) kufanya tafiti ya tathmini ya Mafunzo ya kozi ya Astashahada ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu (CELMA ODL) kwa Walimu Wakuu wa Shule za Msingi wa Mikoa ya Iringa, Mbeya, Njombe na Songwe;
- (xi) kukarabati jengo la zamani la ADEM na bwalo moja la chakula ili kuongeza idadi ya watakaohudumiwa ndani ya Wakala;

(xii) kugharamia Mafunzo kwa Watumishi watatu (3) katika ngazi ya Shahada ya Uzamivu kwa lengo la kuwajengea uwezo katika kutekeleza majukumu; na

(xiii) kujenga Ofisi sita (6) na kumbi nne (4) za mihadhara katika Kampasi za Bagamoyo, Mbeya na Mwanza.

### **Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima**

**107. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/20 Taasisi itatekeleza kazi zifuatazo:

(i) itaboresha ujifunzaji huria na masafa na kuongeza udahili wa wanafunzi wa elimu ya Sekondari nje ya mfumo rasmi kutoka wanafunzi 12,423 mpaka 13,665;

(ii) itaongeza udahili wa wanafunzi wa programu za Astashahada, Stashahada na Shahada kutoka wanafunzi 2,642 mpaka 3,038 kutokana na kuongezeka kwa miundombinu ya majengo kwenye Vituo vya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima pamoja na kuboresha matumizi ya TEHAMA katika kufundishia na kujifunzia;

(iii) itaboresha utoaji wa Programu za Elimu ya Watu Wazima katika Mikoa 21 kwa kuendelea kuvijengea uwezo vituo vya uratibu vya mikoa;

(iv) itatekeleza mkakati wa kisomo ili kupunguza kiwango cha watu wasiojua kusoma na kuandika nchini;

(v) itajenga na kukarabati miundombinu ya ufundishaji na ujifunzaji katika vituo vitatu (3) vya Bukoba, Moshi, Sumbawanga na Dar es Salaam; na

(vi) itaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya elimu ya watu wazima ikiwemo Mradi wa Elimu ya Sekondari kwa Wasichana walio nje ya shule za Sekondari;

Mpango wa Elimu Changamani kwa Vijana Walio nje ya Shule; Mradi wa kuwawezesha vijana na watu wazima

Kielimu; na Mradi wa kuwezesha vijana katika kuongeza thamani mazao ya samaki.

### **Bodi ya Huduma za Maktaba**

**108. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/20, Bodi itatekeleza kazi zifuatazo:

(i) itatoa mafunzo ya Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka kwa wanafunzi 1,000 kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa wataalamu hao nchini;

(ii) kuimarisha na kuinua ubora wa huduma za Maktaba katika Mikoa 22, ili kupunguza ujinga, umaskini na kuleta uelewa na maendeleo katika jamii zetu;

(iii) itatoa ushauri wa kitaalamu katika vituo 100 juu ya uanzishaji, upangaji na uendeshaji wa Maktaba za shule, Vyuho, taasisi na Halmashauri za Jiji, Manispaa, Miji na Wilaya; na

(iv) itajenga Maktaba ya Chuo cha Ukutubi (SLADS) pamoja na Maktaba za Mikoa ya Singida na Shinyanga. Aidha, itapanua Maktaba ya Dodoma na kukarabati Maktaba za Mikoa ya Iringa, Rukwa, Tabora na Songea.

### **Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia – COSTECH**

**109. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/20 Tume imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:

(i) kubaini na kugharamia Miradi mipya 8 ya Utafiti yenye lengo la kutatua matatizo ya wananchi yaliyopo kwenye vipaumbele vya utafiti vya Taifa kupitia MTUSATE

(ii) kuratibu pamoja na kuchangia uendeshaji wa mashindano ya kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ya mwaka 2020;

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

- (iii) kufungasha na kusambaza matokeo ya tafiti kwa walaji husika ikiwemo wananchi, viongozi na watunga sera;
- (iv) kuboresha mifumo ya ubunifu na kuwaendeleza wabunifu nchini ili waweze kujajiri;
- (v) kubiasharisha matokeo ya utafiti nchini ili ziweze kutumika na kuleta tija kwa maendeleo ya nchi;
- (vi) kuandaa mfumo wa uhawilishaji wa teknolojia kupitia uwekezaji wa nje, pamoja na uhakiki wa teknolojia zinazoibukia;
- (vii) kuandaa miongozo na kuimarisha uwezo wa kusimamia na kuendesha Kongano hapa nchini;
- (viii) kusimamia uanzishwaji wa mifumo na Miongozo mbalimbali ili kuziwezesha taasisi nchini kufanya tafiti zinazotatua matatizo katika jamii na zenye viwango vinavyokubalika kimataifa;
- (ix) kufanya Tathmini na Ufuatiliaji wa Miradi inayofadhiliwa na Tume;
- (x) kuboresha mfumo wa udhibiti na utoaji vibali vya utafiti nchini;
- (xi) kuendesha Mafunzo, Semina, Mijadala, na Mikutano mbalimbali kuhusiana na Sayansi, Teknolojia na Ubunifu; na
- (xii) kuhakikisha huduma za intaneti kwa Taasisi za utafiti kupitia mkongo wa Taifa zinapatikana muda wote ili kuimarisha mawasiliano.

**Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania**

**110. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2019/20, Tume itatekeleza yafuatayo:

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

- (i) itatathmini maombi 500 ya leseni mbalimbali kwa lengo la kuona kama yanakidhi matakwa ya Sheria na Kanuni za Usalama na Kinga ya Mionzi ya mwaka 2004 ikiwa ni makisio ya mwaka kulingana na idadi ya vituo vilivyopo sasa;
- (ii) itaendelea na ukaguzi wa migodi sita ya chini ya ardhi (underground mine) ambayo ni; Geita - Geita, North Mara - Tarime, Bulyankulu - Kahama, Stamigold Tulawaka - Biharamuro, Buzwagi - Kahama na Williamson - Shinyanga. Lengo la ukaguzi huu ni kubaini hali ya usalama wa mionzi kwa wafanyakazi na mazingira;
- (iii) itaendelea kukagua vituo vyenye vyanzo vya mionzi 500 ili kubaini hali ya usalama watumishi na watu wengine;
- (iv) itaendelea na usajili wa vituo vyenye vyanzo vya mionzi vipatavyo 140 na hivyo kufanya jumla ya vituo vilivyosajiliwa kufikia 1,040;
- (v) itaendelea na upimaji wa viwango vya mionzi kwa Wafanyakazi 1,600 nchini kwa lengo la kubaini usalama wao;
- (vi) itaendelea na ujenzi wa maabara ya Tume awamu ya pili ambayo itaboresha utoaji huduma, kuongeza mapato na ufanisi katika utendaji wa kazi za Tume;
- (vii) itaanza ujenzi wa maabara za kanda katika Mikoa ya Dar es Salaam Mwanza na Zanzibar;
- (viii) itaanzisha mradi wa kuhifadhi mazao ya kilimo ikiwemo vyakula viharibikavyo kirahisi kwa kutumia mionzi;
- (ix) itakamilisha upembezi yakinifu wa kuanzisha mradi utakaowezesha kutengeneza madawa ya kuchunguza na kutibu saratani pamoja kinu cha tafiti za kinyuklia;
- (x) itakusanya, kusafirisha na kuhifadhi mabaki ya vyanzo vya mionzi yasiyotumika kutoka vituo vinne na

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

kuyahifadhi katika jengo maalumu (Central Radioactive Waste Management Facility- CRWMF) lililopo Arusha;

(xi) itapima kiasi cha mionzi katika sampuli 16,357 za vyakula na mbolea;

(xii) itaimarisha upimaji wa mionzi kwenye mazingira katika vituo 50 ambavyo vimekuwa vikiendeshwa kwa ushirikiano na Taasisi nyingine;

(xiii) itaendelea kuendesha kituo cha kupima mionzi katika hewa ya anga (Radionuclide Monitoring Station-TZPRN64) kilichopo katika kampasi kuu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam) chini ya mkataba wa kimataifa wa *Comprehensive Nuclear Test-Ban Treaty (CTBT) for Non-Proliferation Test (NPT) of Nuclear Weapons*;

(xiv) itafanya kaguzi kwenye vituo 120 vinavyotoa mionzi isiyoayonishwa (Non-Ionizing Radiation) mfano minara ya simu, redio, runinga, na vifaa vingine vya mionzi ili kubaini usalama wa wakazi wa maeneo husika; na

(xv) itafungua ofisi za Tume katika kanda ya Kati katika Mkoa wa Dodoma na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini katika Mkoa wa Mbeya. Vigezo vinavyotumika kuchagua kanda ni uwepo wa vyanzo vya mionzi.

## **Vyuo vya Elimu ya Juu**

### **Chuo Kikuu cha Dar es Salaam**

**111. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2019/20 Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kitatekeleza yafuatayo:

(i) kuongeza udahili wa wanafunzi wa Shahada za awali kutoka wanafunzi 26,640 hadi 28,821 ambapo wanafunzi wa kike wanatarajiwa kuongezeka kutoka 10,531 hadi 11,584;

(ii) kuongeza idadi ya miradi ya utafiti kutoka 135 hadi 188, machapisho katika majarida ya kitaifa na kimataifa

kutoka 735 hadi 915 na majarida ya kimataifa kutoka 11 hadi 15 na kuyafanya yafikike kwa njia ya mtandao; na

(iii) kuwagharamia wanataaluma 112 kuanza masomo ya Uzamili.

**112. Mheshimiwa Spika**, katika uboreshaji wa miundombinu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kitatekeleza yafuatayo:

(i) kukamilisha awamu ya kwanza na kuanza awamu ya pili ya ujenzi wa kituo cha wanafunzi (*Students' Centre*);

(ii) kuanza ujenzi wa Ndaki ya Tiba za Afya (University of Dar es Salaam- Mbeya College of Health and Allied Sciences-UDSM-MCHAS);

(iii) kupanua bweni la Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa ghorofa mbili zaidi na kuendelea na ujenzi wa Jengo la huduma katika bweni hilo ambalo linahusisha maduka, ATM, *Hair Saloons, Dry cleaner*, mgahawa mdogo na *supermarket*;

(iv) kukamilisha Jengo Jipya la Kituo cha Afya cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa lengo la kuboresha huduma zinazotolewa na kuongeza mapato;

(v) kuanza awamu ya kwanza ya ujenzi wa Jengo la Idara ya Uchumi na ukarabati wa nyumba za walimu; na

(vi) kukarabati mabweni ya wanafunzi, barabara za ndani na kuanza ujenzi wa jengo la ofisi na vyumba vya madarasa ya Shule Kuu ya Waandishi wa Habari pamoja na ujenzi wa Jengo la Taasisi ya Sayansi za Bahari lililopo Buyuni Zanzibar; na

(vii) kufanya ukarabati mkubwa wa karakana za uhandisi umeme, maji, mitambo na uashi ambazo zimedumu kwa miaka 40 bila ukarabati na nyumba za walimu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa gharama **Shilingi Bilioni 1.5**.

## Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo

**113. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/20 chuo kitatekeleza yafuatayo:

(i) kuongeza udahili wa wanafunzi wa mwaka wa kwanza, wakiwemo wanafunzi wa Shahada za Kwanza kutoka 4,526 hadi 4,845, Shahada za Juu (Uzamili na Uzamivu) kutoka 195 hadi kufikia 245. Ongezeko hili ni kutokana na ufadhili wa Mradi wa Vituo vya Umahiri Afrika - II (ACE-II);

(ii) kuanzisha shahada za kwanza nne (4) mpya na shahada za uzamili nne (4), na masomo yasiyo ya shahada katika fani moja (1) ili kuendana na mahitaji ya soko la ajira;

(iii) kufanya tafiti 40 mpya kwa lengo la kuboresha uzalishaji wa mazao ya kilimo, mifugo, misitu na uvuvi ili kuhuisha elimu na uwezo wa wananchi katika kuzalisha mali na malighafi za mazao ya kilimo kwa ajili ya viwanda;

(iv) kuongeza utoaji wa elimu na ushauri kwa wakulima 2,500 kwa kutumia mbinu mbalimbali kama vituo atamizi, mashamba darasa, semina, kozi fupi, runinga na redio ili kuongeza uzalisha na tija na hatimae kupunguza umaskini kwa wananchi;

(v) kuboresha na kuongeza mahusiano na taasisi nyingine ndani na nje ya nchi ili kuleta tija katika tafiti na shughuli mbalimbali za maendeleo;

(vi) kujengea uwezo vitengo vya uzalishaji mali ili kuongeza mapato ya ndani ya Chuo kwa asilimia 32;

(vii) kuboresha mazingira ya kufundishia na kusomea ikiwa ni pamoja na kuongeza kiwango cha upatikanaji wa vitendea kazi na zana bora za kufundishia; na

(viii) kuongeza na kuboresha miundombinu ya mawasiliano pamoja na elimu katika nyanja hiyo kwa watumishi.



**114. Mheshimiwa Spika**, katika uboreshaji wa miundombinu Chuo kitatekeleza yafuatayo:

(i) kitajengakumbimbili(2)zamihadhara zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 kila mmoja, ukumbi mmoja (1) wa mikutano wenye uwezo wa kuchukua watu 1,000 na madarasa manne (4) yenye uwezo wa kuchukua watu 50 kila moja;

(ii) kitaendeleza ujenzi wa hosteli moja (1) Kampasi ya Solomon Mahlangu, yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 700; na maabara mtambuka katika kampasi kuu;

(iii) kitakarabati miundombinu iliyochakaa ambayo ni pamoja na vyumba 17 vya kufundishia Kampasi Kuu na Solomon Mahlangu, mabweni sita (6) kampasi kuu na Solomon Mahlangu, nyumba 30 za watumishi kampasi kuu na Solomon Mahlangu, ofisi na madarasa Kampasi ya Tunduru na barabara za ndani zenye urefu wa kilomita 10 Kampasi kuu ya Solomon Mahlangu;

(iv) kitaandaa na kuboresha Shamba Darasala Chuo (*University Model Farm*) ambapo ekari moja na robo zimepandwa Zabibu, ekari kumi na mbili Miembe, ekari tano Korosho, ekari mbili Mipapai, ekari mbili Mananasi ekari mbili Mipasheni, ekari mbili Michikichi na ekari tatu Minazi;

(v) itaanzisha mafunzo ya udereva wa matrekta na mitambo mingine ya kilimo kwa wanafunzi wa chuo, wakulima, na wadau wengine wa kilimo, pamoja na kulima ekari 350 za shamba la chuo za mazao mbalimbali.

**Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili**

**115. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2019/20 Chuo kitatekeleza yafuatayo:

(i) kitaongeze udahili wa wanafunzi wa Shahada na Stashahada mbalimbali kutoka udahili wa sasa wa wanafunzi 1,139 hadi kufikia wanafunzi 1,998;

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

- (ii) kitafanya tathmini ya Mitaala ya shahada ya udaktari (*tracer study*) ili kubaini mapungufu katika mtaala na utekelezaji wake;
- (iii) kitaongeza idadi ya walimu vinara 10 (Health Professional Educators) kwa kuwafundisha ili waweze kufundisha walimu wengine mbinu mbalimbali na utahini;
- (iv) kitaongeza idadi ya kozi (modules) zitakazokuwa zinatolewa kwa kutumia jukwaa la TEHAMA kwa asilimia 30 kutoka kozi za sasa 40 hadi kufikia kozi 52;
- (v) kitaongeza usajili wa wanafunzi wanaotumia jukwaa la TEHAMA kwa asilimia 20 kutoka wanafunzi 715 hadi kufikia wanafunzi 864;
- (vi) kitaongeza udahili wa wanafunzi wa kike kwa Shahada ya kwanza kutoka asilimia 30 ya sasa hadi kufikia asilimia 40 ili kuleta uwiano wa kijinsia; na
- (vii) kitaimarisha kitengo cha jinsia kwa kukamilisha Sera ya Jinsia.

**116. Mheshimiwa Spika**, katika uboreshwaji wa t a f i t i na ushauri elekezi, Chuo kitatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) kitafanya kongamano la nane (8) la kisayansi (8<sup>th</sup> MUHAS Scientific Conference) na kuboresha semina za kitafiti za ndani ya chuo ili kusambaza matokeo ya tafiti kwa wadau ikiwemo watunga sera za afya;
- (ii) Kitaimarisha makundi ya kitafiti (Research Clusters) na kutoa mafunzo kwa viongozi wa makundi hayo;
- (iii) Kitaanzisha tafiti mpya tano (5) kwa kila kitengo zenye kulenga ktatua matatizo ya kipaumbele kama ilivyoanishwa katika sera za tafiti za chuo na za Taifa;
- (iv) Kitaimarisha miundombinu ya tafiti kwa kukamilisha kituo cha Umahiri wa magonjwa ya moyo na mishipa ya

damu (Center of Excellence in Cardiovascular Sciences) katika kampasi ya Mloganzila na kufanya ukarabati katika kituo cha kufundishia na tafiti cha Bagamoyo (Bagamoyo Training Unit); na

(v) Kitafanya tafiti zinazoendelea ili kuboresha sera na afya bora kwa jamii katika magonjwa ambukizi (kifua kikuu, matumizi ya dawa kinga ya UKIMWI-HIV *pre-exposure prophylaxis*, dawa mbadala za malaria, hatua ya pili ya chanjo ya virusi vya UKIMWI-HIV *DA- prime phase II trial*), magonjwa yasiyoambukizwa (ugunduzi wa saratani ya matiti kwa kutumia *Gene-expert*, namna ya kupima kiasi cha mafuta mwilini, magonjwa ya moyo), na magonjwa yasiyopewa kipaumbele (neglected Tropical Diseases).

**117. Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha mapato ya ndani Chuo kitatekeleza yafuatayo:

(i) kitaboresha ukusanyaji wa mapato katika vyanzo mbalimbali vya chuo kwa kukamilisha kujiunga na kutumia mfumo wa kukusanya mapato wa serikali (Government e-payment Gateway-GePG);

(ii) kitaongeza mapato kwa uwekezaji katika mali zisizohamishika (Fixed assets) ambazo ni kutokana na kodi za pango la *CHPE Building Conference Centre* na Jengo la *Clinical Research Labaratory*; na

(iii) kitaongeza utoaji huduma katika vitengo mbalimbali vya chuo ikiwemo shule ya meno na kuanza mpango wa ujenzi wa Kliniki ya Uporoto (Uporoto Polyclinic).

**Chuo Kikuu cha Ardhi**

**118. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/20 Chuo Kikuu cha Ardhi kitatekeleza yafuatayo:

(i) kitadahili wanafunzi 4,800 wakiwemo wanafunzi 4,500 katika ngazi ya Shahada ya kwanza, 235 katika ngazi ya Shahada ya Uzamili na 15 katika ngazi ya Shahada ya Uzamivu;

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

(ii) kitafanya miradi ya Utafiti 50 zinazolenga kutatua changamoto za jamii hususani katika maeneo ya matumizi bora ya ardhi, utunzaji wa mazingira, kujikinga na maafa, usimamizi bora wa ardhi, makazi na majenzi na sayansi ya jamii. Aidha, Chuo kitaandaa machapisho 150 katika maeneo ya usimamizi wa ardhi na mazingira, makazi na majengo;

(iii) kitatoa mafunzo ya kitaalamu kwa jamii kuhusiana na matumizi bora ya ardhi, kujikinga na majanga, kutengeneza bidhaa kwa kutumia mabaki ya mazao ya kilimo, kutunza kumbukumbu za biashara ndogondogo na utunzaji wa mazingira;

(iv) kitatoa huduma za ushauri wa kitaalamu kwa jamii kuhusu matumizi bora ya ardhi, upimaji na tathmini, usanifu majengo na ujenzi;

(v) kitaendelea kukamilisha ujenzi wa Jengo la Ardhi (Lands Building) pamoja na kuweka samani Maabara (Multi-Purpose Laboratory), mabweni ya wanafunzi, ukumbi wa mdahalo (Multipurpose Pavillion), mifumo ya maji taka, miundombinu ya TEHAMA na kukarabati karakana, madarasa, mabweni ya wanafunzi, bwalo la chakula na nyumba za watumishi;

(vi) kitaanza ujenzi wa jengo la usanifu majengo, kuandaa michoro ya ujenzi wa karakana, bwalo la chakula na kituo cha Afya;

(vii) kitanunua magari matatu (3), genereta moja (1), samani na vifaa vya TEHAMA; na

(viii) kitatoa mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 32; wakiwemo 17 katika ngazi ya Shahada ya Uzamivu na wanane (8) katika ngazi ya Shahada ya Uzamili; wawili (2) katika ngazi ya Shahada ya kwanza na watano (5) katika ngazi ya Stashahada.

## Chuo Kikuu Mzumbe

**119. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2019/20 Chuo kitatekeleza yafuatayo:

(i) kitadahili wanafunzi 5,145 katika programu mbalimbali (Astashahada 396, Stashahada 715, Shahada ya Kwanza 3,327, Shahada ya Uzamili 697 na Shahada ya Uzamivu 10);

(ii) kitaandaa programu mbili za masomo kwa lengo la kuongeza fursa zaidi za masomo;

(iii) kitagharamia watumishi 35 katika masomo ya Shahada ya Uzamivu na 16 katika masomo ya Shahada ya Uzamili;

(iv) kitaandaa machapisho 40 kwenye majarida mbalimbali ya kitaifa na kimataifa na kuandaa jarida la "Uongozi" la Chuo Kikuu Mzumbe kwa lengo la kusambaza matokeo ya tafiti na kazi mbalimbali za kitaaluma ili kuleta maendeleo ya kiuchumi kwa jamii;

(v) kitaandaa mapendekezo 16 ya kazi za utafiti na mapendekezo 37 ya kazi za ushauri wa kitaalamu, kozi fupi na huduma kwa jamii;

(vi) kitaweka samani katika hosteli za wanafunzi Kampasi Kuu eneo la Maekani.

**120. Mheshimiwa Spika,** katika uboreshaji wa miundombinu, chuo kitatekeleza kazi zifuatazo:

(i) kitajenga jengo la madarasa na mfumo wa maji taka Kampasi Kuu ya eneo la Maekani, pamoja na kuweka samanikatika majengo yaliyopo Tegeta Kampasi ya Dar es Salaam;

(ii) kitakarabati hosteli mbili za wanafunzi zenye uwezo wakuchukuwa wanafunzi 256 katika Kampasi ya Mbeya, jengo la Kurugenzi ya Utafiti, Machapisho na Masomo

ya Uzamili na nyumba kumi za watumishi mabweni mawili na jengo la Lumumba *Complex* Kampasi Kuu; na

(iii) kitaandaa Mpango wa matumizi bora ya ardhi katika eneo la Ilemela Mwanza na Kiseriani Arusha.

### **Chuo Kikuu cha Dodoma**

**121. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/20 Chuo kitatekeleza kazi zifuatazo:

(i) kitadahili wanafunzi wapya 12,123 ambapo wanafunzi wa shahada za awali watakuwa 9,774, Stashahada na Astashahada 1,934, Shahada za juu 413 ili kufikia jumla ya wanafunzi 32,079 ambapo wasichana watakuwa asilimia 43;

(ii) kitaajiri jumla ya watumishi wapya 445 ili kukabiliana na uhaba wa watumishi pamoja na ongezeko la wanafunzi chuoni ili kuleta ufanisi wa kazi na ufundishaji wa wanafunzi;

(iii) kitatoa mafunzo kwa watumishi 570 ili kuwajengea uwezo na ufanisi katika utendaji kazi, ambapo watumishi 320 watapatiwa mafunzo ya muda mrefu na 250 mafunzo ya muda mfupi; na

(iv) kitafanya jumla ya tafiti mpya 20, huduma za ushauri (Consultancies) 15, na mahusiano na taasisi nyingine (collaborations) 14 ambazo zitajikita katika maeneo ya afya, elimu, maji, madini, TEHAMA, mazingira, rasilimali asilia, uchumi na maendeleo ya jamii.

**122. Mheshimiwa Spika**, katika uboreshaji wa miundombinu Chuo kitatekeleza kazi zifuatazo:

(i) kitajenga nyumba za watumishi sita (ghorofa 3 zenyekuchukua familia 10 uwezo wakila moja ambapo familia 30 zitaishi humo, nyumba 3 kwa ajili ya Makamu Mkuu wa chuo na manaibu wake wawili) ambapo ujenzi huu utafanyika kwa awamu.

(ii) kitaanza awamu ya kwanza ya ubunifu wa majengo yaliyobaki katika Ndaki tatu (3) (Ndaki ya Sayansi Asilia na Hisabati; Ndaki ya Sayansi za Afya; na Ndaki ya Sayansi za Ardhi) ambazo hazikamilika. Kukamilika kwa Majengo haya, kutasaidia kuongeza idadi ya wanafunzi hivyo kuongeza wigo wa watanzania kupata elimu;

(iii) kitajenga jengo kwa ajili ya huduma za mionzi katika hospitali ya Chuo ili kuongeza wigo wa huduma za matibabu ambazo huduma hizi hazipatikani kwa wingi kwenye Hospitali zilizopo hapa jijini Dodoma; na

(iv) kitakarabati majengo ya ofisi, makazi, mabweni, madarasa pamoja na miundombinu mingine ikiwemo barabara na viwanja vya michezo.

**123. Mheshimiwa Spika**, katika uboreshaji wa ufundishaji na ujifunzaji Chuo kitatekeleza yafuatayo:

(i) kitanunua vitabu kwa ajili ya kuboresha huduma za Maktaba Chuoni, kompyuta 220 kwa ajili ya vyumba vya kompyuta vya wanafunzi; na

(ii) kitanunua magari matano kwa ajili ya kusaidia shughuli za ofisi.

### **Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi**

**124. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/20 Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi kitatekeleza yafuatayo:

(i) kitadahili wanafunzi 5,846 kati yao, wanafunzi wa Astahahada 821, Stashahada 1,134, Shahada ya kwanza 3,690 na Shahada za Uzamili 201;

(ii) kitaandaa programu nne (4) za mafunzo kwa lengo la kupanua wigo wa programu za mafunzo ambazo ni muhimu katika kuongeza ufahamu na uwezo wa wadau katika kusimamia maendeleo ya ushirika nchini;

(iii) kitafanya miradi ya utafiti na kutoa ushauri wakitaalamu pamoja na kuchapa makala mbalimbali kwa kushirikiana na vyuo vingine vya ndani na nje ya nchi kwa lengo la kusambaza elimu inayokidhi mahitaji ya sasa ya jamii ili kupunguza umaskini;

(iv) kitaendelea kutoa na kueneza elimu ya ushirika nje ya Chuo ili kuchochea ari ya maendeleo katika jamii kwa kushirikiana na wadau wengine, hususani Wizara ya Kilimo; Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC); Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO); Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania (TFC) na vyama vya ushirika nchini na katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki;

(v) kitachangia maboresho ya Sheria, Kanuni na uandaaji wa mkakati wa maendeleo ya ushirika nchini kwa kutoa wataalam watakao shirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika nchini na wadau wengine;

(vi) kitaendeleza mafunzo ya wafanyakazi 60, hususani Wahadhiri katika ngazi ya Shahada za Uzamili na Uzamivu;

(vii) kitajenga maktaba yenye uwezo wa kuchukua wasomaji 2,500 kwa wakati mmoja ili kuongeza wigo wa wasomaji na kuboresha mazingira ya kujifunzia; na

(viii) kitaimarisha vyanzo vya mapato ya ndani kwa kuimarisha usimamizi ili kuongeza tija na kuanzisha vingine ili kuongeza mapato ya chuo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

### **Chuo Kikuu Huria cha Tanzania**

**125. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/20, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kitatekeleza yafuatayo:

(i) kitadahili jumla ya wanafunzi 13,100 kati ya hao, wanafunzi 2,000 Astashahada, 3,000 Stashahada, 6,000 Shahada ya kwanza, wanafunzi 2,000 Shahada ya Uzamili na 100 Shahada ya Uzamivu;



(ii) kitaboresha Mitaala ya programu zinazofundishwa ili kuendana na hali halisi ya maendeleo ya kiuchumi na kiteknolojia;

(iii) kitatoa huduma za ushauri wa kitaalamu katiika Nyanja za mazingira, TEHAMA, nishati, kilimo na chakula, uongozi na biashara, maendeleo ya utalii, sheria, uthibiti wa ubora, utawala na maendeleo. Pia itahusisha watu wenye ulemavu na mahitaji maalumu, maliasili, umaskini, utamaduni, haki za binadamu, maendeleo ya watu na mawasiliano;

(iv) kitajenga Jengo la Makao Makuu Dodoma na majengo ya Ofisi za watumishi katika vituo vya mikoa ya Geita, Simiyu, Kigoma, Manyara na Lindi na ukumbi wa mitihani mkoani Morogoro;

(v) kitajenga ngazi za dharura katika jengo lenye ghorofa kumi (ODL Tower) lililopo Makao Makuu ya muda ya Chuo Kinondoni, Dar es Salaam na kukarabati majengo ya Ofisi za vituo vya mikoa ya Mwanza, Mbeya, Shinyanga, Kilimanjaro, Dar es Salaam na Iringa;

(vi) kitajenga uzio katika viwanja vya vituo vya Mtwara, Arusha na Rukwa na kufanya ukarabati wa vituo vya uratibu vya Mafia na Tunduru;

(vii) kitatoa mafunzo kwa watumishi na wanafunzi kwa ajili ya kuongeza ujuzi na matumizi ya TEHAMA na kununua vifaa vya TEHAMA; na

(viii) kitafuatilia upatikanaji wa hati Miliki za viwanja kwa matumizi ya Chuo katika mikoa ya Mara, Katavi, Dodoma, Lindi, Ruvuma, Kagera na Njombe.

### **Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius K. Nyerere cha Sayansi ya Kilimo na Teknolojia**

**126. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2019/20 Chuo kitatekeleza yafuatayo:

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

- (i) kitaanzisha na kuendesha kozi za muda mfupi katika kilimo, biashara na ujasiriamali kwa wakulima, wafugaji, wavuvi, na vikundi vya vijana na akina mama wajasiriamali;
- (ii) kitaandaa maandiko ya tafiti sita (6) kwa ajili ya kutafuta fedha kutoka kwa wahisani mbalimbali na kufanya tafiti nne (4);
- (iii) kitaimarisha shughuli za mafunzo na huduma za ugani kwa jamii za wakulima, wafugaji na wajasiriamali kwa wakulima wadogo wadogo 300 wanaokizunguka chuo;
- (iv) kitafanya ukarabati wa miundombinu katika Kampasi ya Oswald Mang'ombe ili kuruhusu udahili wa wanafunzi 200 katika programu zitakazoanzishwa;
- (v) kitaandaa Mitaala 10 kwa ngazi ya Shahada ya kwanza, kwa ajili ya kupitiwa na kuidhinishwa na TCU;
- (vi) kitakamilisha upatikanaji wa hati ya maeneo ya chuo hususan, Kisangura - Mugumu katika Wilaya ya Serengeti na Kinesi-Wilaya ya Rorya;
- (vii) kitawaendeleza kitaaluma watumishi katika ngazi za Shahada za Uzamili na Uzamivu, ili kukiwezesha Chuo kuwa na wanataaluma waliobobea katika fani tofauti; na
- (viii) kitaajiri watumishi wapya 266 katika kada mbalimbali ili kuwezesha Chuo kuanza kikiwa na watumishi wanaohitajika.

**Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam**

**127. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/20 Chuo kitatekeleza yafuatayo:

- (i) kitadahili wanafunzi wa mwaka wa kwanza 2,400 ambapo 600 ni wa fani ya Sayansi na 1,800 ni wa fani za Sanaa;

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

- (ii) kitagharimia vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi 57 wenye mahitaji maalum pamoja na vifaa vya utafiti kwa wanataaluma;
- (iii) kitawezesha tafiti 20 ikiwa ni pamoja na tafiti za sayansi na teknolojia;
- (iv) kitagharimia uendeshaji wa mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi 3,800;
- (v) kitaandaa Mitaala mitano (5), ambapo miwili ni ya Stashahada, mmoja Stashada ya Uzamili, Shahada za awali na Uzamili;
- (vi) kitagharimia mafunzo kwa watumishi 35 ili kuwajengea uwezo na kuwapa maarifa mapya, ambapo 30 ni wanataaluma na watano (5) ni waendeshaji; (vii) kitaendelea na awamu ya pili yaujenzi wa jengo la utawala hatua ya pili ili kuongeza ofisi za watumishi na vyumba vya utafiti;
- (viii) kitakarabati miundombinu chakavu, ikiwemo mabweni na kumbi za mihadhara ya Chuo na kununua viwezeshi vya umeme mbadala (Solar) ili kupunguza gharama na kuwa na umeme wa uhakika Chuoni pamoja na kuimarisha miundombinu ya TEHAMA, na;

### **Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa**

**128. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/20 Chuo kitatekeleza yafuatayo:

- (i) kitaongeza udahili wa wanafunzi kutoka 6,808 hadi 7,455;
- (ii) kitaboresha ufundishaji wa kiugunduzi na kutumia teknolojia katika ufundishaji na ujifunzaji katika programu zote za elimu kwa kufanya ununuzi wa vifaa vya TEHAMA na kuboresha maktaba ya Chuo;

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

- (iii) kitatoa mafunzo katika programu za elimu katika ngazi zote za elimu ambapo kitarekebisha na kuboresha Mitaala katika programu za elimu na kutekeleza utafiti na uzinduzi wa programu ya elimu ya mazoezi na sayansi ya michezo;
- (iv) kitaboresha na kutoa mafunzo mbalimbali katika programu za kitaaluma na kiweledi katika nyanja za elimu na zisizo za elimu, pamoja na kuanzisha programu tatu (3) za Shahada, Shahada za Uzamili na Stashahada ya Uzamili;
- (v) kitaimarisha uwezo wa rasilimali watu katika utendaji na utoaji huduma kwa jamii kwa kuimarisha kitengo cha masomo ya uzamili, utafiti na huduma kwa jamii;
- (vi) kitaongeza matokeo yanayotokana na utafiti na ubunifu kutoka machapisho 50 hadi 100;
- (vii) kitagharamia mafunzo kwa watumishi wanataaluma 98 na waendeshaji 12 ya muda mrefu ngazi ya Shahada ya kwanza, Uzamili na Uzamivu; na
- (viii) kitaboresha na kuimarisha miundombinu ya ufundishaji na ujifunzaji kwa kujenga hosteli mbili (2) zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 500 kila moja, na maktaba yenye uwezo wa kuchukuwa wanafunzi 1,000 kwa wakati mmoja na kufanya ukarabati wa majengo ya utawala, ofisi za wanataaluma na barabara za ndani ya Chuo.

## **Chuo cha Ufundi Arusha**

**129. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2019/20 Chuo kitatekeleza yafuatayo:

- (i) kitadahili jumla ya wanafunzi 1,265 wa mwaka wa kwanza kwa Mafunzo ya Ufundi ngazi za Astashahada, Stashahada na Shahada (NTA Level 4-8) na jumla ya wanafunzi 1,000 wa ngazi ya Ufundi Stadi (NVA Level 1-3);

(ii) kitajenga maktaba yenye uwezo wa kuchukua jumla ya wanafunzi 1,000 na bweni la wasichana lenye uwezo wa kulaza wanafunzi 250;

(iii) kitaendelea kutekeleza utafiti wa kuzalisha umeme Wilayani Mbulu chini ya ufadhili wa Wakala wa Umeme Vijijini (REA) ambapo umeme wa kiasi cha KW 70 utazalishwa na utahudumia vijiji viwili vya Kwermusl na Amoa;

(iv) kitaendelea kutafuta mwekezaji mwenza kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha uwekezaji umeme wa 1.7 MW - Kikuleta utakaounganishwa kwenye msongo wa Taifa pamoja na kutumika kwa mafunzo; na

(v) kitaendelea kutoa Ushauri wa Kitaalamu (Consultancy) kuhusu uimara wa udongo, kokoto na lami zinazotumika katika ujenzi wa barabara, ubora wa maji, usanifu wa miradi ya maji na ujenzi wa aina mbalimbali, umeme wa nishati jadidifu.

### **Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere**

**130. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/20 Chuo kitatekeleza yafuatayo:

(i) kitadahili wanafunzi 4,242 katika ngazi ya Astashahada, Stashahada, Shahada ya Kwanza na Shahada ya Uzamili, wanafunzi wa Shahada za Awali 2,173, Stashahada 1,116, Astashahada 953;

(ii) kitafanya tafiti 17 zinazohusu maendeleo ya Uchumi, Elimu, Jinsia na Maendeleo, Taaluma ya Jamii na maadili na Uongozi. Aidha, kitatoa mafunzo na ushauri wa Kitaalamu katika maeneo ya Uongozi na Maadili, Sayansi za Jamii, Jinsia na Ujasiliamali;

(iii) kitagharamia watumishi wanataaluma 14 katika ngazi za Uzamivu na Uzamili ili kupunguza uhaba wa wanataaluma na kuwajengea uwezo zaidi na kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa shughuli zao;

- (iv) kitaanza awamu ya kwanza ya ujenzi wa bweni la wanafunzi katika Kampasi ya Zanzibar litakalo kuwa na uwezo wa kulala wanafunzi 500 kwa pamoja;
- (v) kujenga Maktaba katika Kampasi ya Kivukoni na kufanya ukarabati wa miundombinu chakavu ya maji, umeme, barabara na majengo ya chuo (Madarasa na nyumba za watumishi) kwa lengo la mazingira ya kufundishia na kujifunzia;
- (vi) kitapitia na kuboresha Mitaala ya Chuo na kuwasilisha Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi pamoja na Tume ya Vyuo Vikuu kwa ajili ya kuidhinishwa;
- (vii) kitagharamia ununuaji na ufungaji wa samani katika jengo jipya la mihadhara Kampasi ya Kivukoni; na
- (viii) kitaboresha mfumo wa TEHAMA kwa ajili ya ufundishaji na ujifunzaji.

### **Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya**

**131. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2019/20, Chuo kitatekeleza yafuatayo;

- (i) kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka wanafunzi 4,630 kwa mwaka wa masomo 2018/2019 hadi kufikia wanafunzi 5,000 kwa mwaka wa masomo 2019/2020 ambapo wanafunzi wa Stashahada wakiwa 2,579 na wanafunzi wa Shahada ya kwanza wakiwa 2,421;
- (ii) kufanya tafiti zinazolenga kuongeza ubunifu na kuendelea kutoa ushauri elekezi katika nyanja za sayansi na teknolojia ili kuchochea ukuaji wa uchumi wa viwanda na hivyo kuongeza kasi ya maendeleo katika jamii. Tafiti hizo ni pamoja na utengenezaji wa mkaa kwa kutumia pumba za mpunga na vumbi la mkaa ya mawe na kuunda chombo cha kukaushia tumbaku kwa kutumia umeme wa jua;

(iii) kuendelea na kukamilisha ujenzi wa jengo la Maktaba ili kukidhi mahitaji ya huduma bora za maktaba kwa wanafunzi na wahadhiri;

(iv) kuendelea kuongeza matumizi ya nishati mbadala ili kuwa na vyanzo endelevu vya nishati kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Chuo;

(v) kufanya tathimini ya mali za wananchi katika eneo la Kitalu Na. 2 chenye ukubwa wa hekta 511, kilichopo Mbeya Vijijini ambalo linahitaji kulipiwa fidia ili kutoa nafasi ya kupanua Chuo hapo baadaye;

(vi) kufanya tathimini ya mali za wananchi katika eneo ambalo limeainishwa kuongezwa katika kampasi ya Rukwa ili lifikie ukubwa wa hekta 500;

(vii) kukamilisha taratibu za kusajiri Kampasi ya Rukwa na kuanza kutoa mafunzo katika ngazi ya Stashahada na Shahada ya Kwanza katika Kampasi hiyo na hivyo kuongeza fursa za elimu kwa wananchi;

(viii) kuanza kutoa mafunzo ya Stashahada ya Ualimu wa Ufundi na Stashahada ya Uzamili ya Ualimu wa Ufundi ili kukidhi mahitaji ya Walimu wa Ufundi katika Shule na Vyuo vya Ufundi nchini;

(ix) kuanza ujenzi wa jengo la Chumba cha Mihadhara kitakachokuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 300 kwa wakati mmoja ili kupunguza changamoto ya miundombinu na hivyo kuongeza udahili wa wanafunzi; na

(x) kuendelea kufanya ukarabati wa miundombinu ya majengo ya madarasa, hosteli na nyumba za watumishi ambazo ni chakavu.

### **Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam**

**132. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/20 Taasisi ya Teknolojia Kampasi Kuu ya Dar es Salaam itatekeleza kazi zifuatazo:

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

(i) itadahili wanafunzi wapya 2,000 ikilinganishwa na 1499 waliodahiliwa 2018/19 na kuendelea kuhudumia wanafunzi 3,000 wanaoendelea. Hivyo jumla ya wanafunzi itakuwa 5,000; Ongezeko hili la wanafunzi hasa mafundi sanifu ni kutokana na kuanza utekelezaji wa mradi ya ESTRIP na TELMS II na litasaidia kwa kiasi kikubwa kupata rasilimali watu yenye weledi kwa ajili ya uchumi wa viwanda;

(ii) kuanza kufanya tafiti mpya mbili (2) katika maeneo yafuatayo ya nishati:

a) mradi wa ubunifu wa matumizi ya umeme jua kuvuna maji katika visima virefu kwa ajili ya umwagiliaji kwenye kilimo cha mbogamboga na nyanya utakaofanyika mkoani Morogoro. Mradi huu unafadhiliwa na COSTECH ambapo ubunifu huu utachochea shughuli za kilimo cha umwagiliaji;

b) mradi wa uanzishwaji kituo cha utafiti nishati endelevu kwa ufadhili wa shirika la maendeleo la Uingereza (DfID). Lengo la mradi huu ni kuanzisha kituo kitakachokuwa kinatafiti nishati endelevu;

(iii) itatekeleza miradi 50 ya huduma za ushauri wa kitaalamu kwa jamii kwa lengo la kutatua changamoto na matatizo mbalimbali katika jamii;

(iv) itakamilisha upanuzi wa jengo la Maktaba kwa kutumia mapato ya ndani na kuwawezesha wanafunzi 500 kutumia jengo hilo kwa wakati mmoja;

(v) itaweka samani za ndani na miundombinu ya TEHAMA katika jengo la DIT Teaching Tower kwa lengo la kutatatua changamoto iliyopo ya ukosefu wa samani. Aidha, Mradi huu ukikamilika utaongeza udahili wa wanafunzi 984 kwa mwaka;

(vi) itafanya mapitio ya Mitaala ya programu za StashahadaShahada ili kuingiza dhana naya Mafunzo



Viwandani (*Teaching Factory*) katika Mitaala ya mafunzo ya ufundi; kwa kuzingatia mahitaji halisi ya soko la ajira;

(vii) itaanza matayarisho ya Mitaala ya kozi mpya ya Shahada ya Uhandisi katika Vifaa Tiba (*Bachelor of Engineering in Biomedical Engineering*); na kozi ya Shahada ya Uzamivu katika Teknolojia (*PhD in Technology*);

(viii) itaanza utekelezaji wa mradi wa (*Tanzania Education Labour Market Survey - TELMS*) awamu ya pili unaofadhiliwa na Serikali ya Italia. Mradi huu ni wa miaka mitano(5) na unatarajiwa kuiwezesha Taasisi kujiendesha yenyewe na kuviwezesha Vyuo vingine vitatu Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya, Chuo cha Ufundi Arusha na Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia viweze kujitegemea kwa kuanzisha vituo vya ujasiriamali, ubunifu na usambazaji wa teknolojia na hivyo kuwawezesha wahitimu kujajiri na kuanzisha shughuli zitakazozalisha ajira kwa wengine;

(ix) itaanza utekelezaji wa mradi wa *East Africa Skills for Transformation and Regional Integration Project* (EASTRIP)' wenye lengo la kuanzisha Kituo cha Umahiri cha Kikanda katika TEHAMA na Uchakataji wa Ngozi na Teknolojia za utengenezaji wa bidhaa za Ngozi kwa ufadhili wa Benki ya Dunia. Mradi huu ni wa miaka mitano na unatajiwa kuongeza udahili kwa asilimia 50;

(x) itaendelea kushiriki kutekeleza miradi mikubwa minne (4) ya kubiasharisha bunifu zilizotokana na tafiti zenye lengo la kutatua changamoto za jamii, ikiwemo teknolojia ya taa za kuongozea magari barabarani, kupitia Kampuni ya Taasisi iitwayo *DIT Company Limited*;

(xi) itaendelea kutafuta maeneo kwa ajili ya kuanzisha kampasi mpya mkoa ya Pwani na Jijini Dodoma; Lengo ni kuitikia mahitaji makubwa nchini ya wahandisi na mafundi sanifu kwa kuzingatia dhamira ya Serikali ya uchumi wa viwanda;

(xii) itaanzisha mikataba mipya mitano (5) ya ushirikiano na taasisi na wadau wa maendeleo wa ndani na nje ya nchi katika kukuza uwezo wa kufanya utafiti na kuboresha ufundishaji ili kuunga mkono azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuifanya nchi yetu kuwa ya uchumi wa viwanda; na

(xiii) itaendelea kushiriki katika kusimamia kuwatambua mchakato wana kuwaendeleza wabunifu wa Taasisi na kitaifa.

**133. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2019/20 Taasisi ya Teknolojia Kampasi ya Mwanza itatekeleza kazi zifuatazo:

(i) itaongeza udahili wa wanafunzi katika kozi ya Teknolojia ya Bidhaa za Ngozi ngazi ya Stashahada kutoka watatu (3) hivi sasa hadi kufikia wanafunzi 50;

(ii) itaanza utekelezaji wa mradi wa TELMS awamu ya pili. Kazi kubwa ya mradi itakayofanyika ni kuboresha miundombinu ya Kampasi na ujenzi wa jengo la kufundishia kwa ajili ya kutoa mafunzo ya bidhaa zinazotokana na ngozi; na

(iii) itaendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wajasiriamali katika teknolojia ya ngozi hasa ujuzi wa kutengeneza viatu vya ngozi, mipira, mikanda, mikoba ya wanawake na nyinginezo. Mafunzo haya yatasaidia kuongeza thamani ya ngozi na kuchochea shughuli nyingi za kiuchumi katika sekta ya ngozi, kupunguza umaskini na kuongeza ajira kwa vijana na wanawake.

**134. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2019/20 Taasisi ya Teknolojia Kampasi ya Myunga – Songwe itatekeleza kazi zifuatazo:

(i) itaongeza udahili kutoka wanafunzi 20 kwa sasa hadi 100 mwaka 2019/20 katika utoaji wa mafunzo ya ufundi sanifu/stadi (NVA 3) yanayosimamiwa na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA);

(ii) itaandaa Mitaala ya mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya stashahada katika Uhandisi wa Ujenzi na Madini; na

(iii) itaanza utekelezaji wa mradi wa TELMS awamu ya pili ambapo kazi kuu ya mradi itakayofanyika ni kuboresha miundombinu ya Kampasi mpya ikiwepo pia kujenga jengo la ghorofa tano (5) la kufundishia na hivyo kuongeza udahili katika Kampasi ya Myunga Songwe kwa zaidi ya wanafunzi 400.

### **Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela Arusha**

**135. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/20 Taasisi itatekeleza yafuatayo:

(i) itadahili wanafunzi 145; Shahada ya Uzamili 100 na Uzamivu 45;

(ii) itaandaa na kuzirasimisha taratibu za ndani na nje ambazo ni sera ya utafutaji rasilimali na uwezekaji, sera ya utafiti na ubunifu na sera ya hatimiliki kwa ajili ya utafutaji na upatikanaji wa rasilimali fedha;

(iii) itahamasisha upatikanaji wa fedha kutoka vyanzo mbalimbali vya kitafiti kwa ajili ya ufadhili wa wanafunzi kwa kuandika maandiko yapatayo 48.;

(iv) itaongeza idadi ya uhusiano; kwa wadau wa kimataifa kutoka 33 hadi 36, kwa wadau wa kanda ya Afrika Mashariki kutoka 34 hadi 37 na kwa wadau wa ndani ya nchi kutoka 21 hadi 25;

(v) itasimamia kwa ufanisi shughuli za uendeshaji na utawala kwa kulipa kwa wakati gharama mbalimbali za uendeshaji kwa uwazi, weledi na ubunifu wa kupunguza gharama;

(vi) itaanza ujenzi wa bweni la wanafunzi 500 ifikapo Juni 2020 kwa lengo la kuongeza nafasi za malazi ya wanafunzi;

(vii) itaendelea kutekeleza Miradi 33 ya kitafiti na ubunifu kwa kufadhili wanafunzi na kulipa gharama za kiutafiti kwa wanafunzi na wanataaluma ili kuendelea na kuzalisha bunifu mbalimbali; na

(viii) itaratibu shughuli za utafiti na ubunifu na kuwa na angalau bunifu mbili kwenda hatua ya atamizi.

## **MALENGO YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO MWAKA 2019/20**

### **Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu (Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo katika Sekta ya Elimu- EP4R)**

**136. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo katika Elimu (EP4R) kwa mwaka 2019/20 imetenga kiasi cha **Shilingi 94,600,000,000.00** kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) kugharamia ununuzi wa magari 65 kwa ajili kuimarisha Uthibiti Ubora wa Shule;

(ii) kujenga Ofisi 55 za Wathibiti Ubora wa Shule ili kuimarisha mazingira ya utendaji kazi;

(iii) kununua Magari 10 kwa ajili ya Vyuho vya Ualimu;

(iv) kutoa motisha kwa Shule za Msingi na Sekondari 400 zilizoongeza kiwango cha ufaulu katika Mitihani ya Taifa ya Darasa la Saba na Kidato cha Nne, 2018;

(v) kutoa motisha kwa Halmashauri 184 kutokana na utekelezaji wa vigezo vilivyokubalika kati ya Serikali na Wafadhili wa Programu;

- (vi) kuimarisha mfumo wa Takwimu za Wizara ili kupata takwimu kwa usahihi na kwa wakati na kuwezesha kufanya maamuzi sahihi na kuandaa mipango yenye tija;
- (vii) kununua magari matano (5) aina ya Landcruiser hardtop na malori mawili (2) kwa ajili ya Baraza la Mithani la Taifa - NECTA ili kuimarisha utendaji kazi wa Baraza;
- (viii) kuwajengea uwezo Watumishi wa Wizara kwa lengo la kuboresha utendaji kazi wao;
- (ix) kuwezesha ukaguzi wa nje wa Programu na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mradi; na
- (x) kuwezesha ujenzi wa shule mpya ya Sekondari ya Mfano mkoani Dodoma itakayochukua wanafunzi wa Kidato cha 1 - 6.

### **Mradi wa Elimu na Kukuza Stadi za Kazi na Ujuzi (Education and Skills for Productive Jobs - ESPJ)**

**137. Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Mradi wa Elimu na Kukuza Stadi za Kazi na Ujuzi (Education and Skills for Productive Jobs – ESPJ) kwa mwaka 2019/20 imetenga kiasi cha Shilingi **56,556,728,386.00** kwa ajili kutekeleza shughuli zifuatazo:

- (i) kusimamia uundwaji wa Baraza la Kitaifa la Ujuzi ili kusimamia shughuli za Mabaraza ya Kisekta;
- (ii) kuendelea na utekelezaji wa Mfuko wa Kukuza Stadi za Kazi kwa kutoa ruzuku kwenye taasisi za mafunzo kwa njia ya ushindani;
- (iii) kuanza ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi (VETA) katika katika halmashauri za Ruangwa, Kongwa, Kasulu TC na Nyasa;

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

- (iv) kugharamia ukarabati wa Vyuo vya Wananchi na kuvinunulia vifaa vya kufundishia na kujifunzia;
- (v) kuendelea kujengea uwezo Wizara na Taasisi za VETA, NACTE na TCU ili kusimamia ubora wa Elimu ya Vyuo Vikuu na Vyuo vya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi;
- (vi) kuendelea kusaidia utekelezaji wa shughuli za Mabaraza ya Kisekta;
- (vii) kugharamia ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi Kanda ya Kati na kuendelea na ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kumi na nne (14) ili kuimarisha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji;
- (viii) kugharamia mafunzo katika Vyuo vya VETA na Elimu ya Ufundi kwa kutoa mafunzo kwa njia ya Uanagenzi; na
- (ix) kuendelea na ujenzi wa Chuo cha Ufundi Dodoma katika kitongoji cha Nalla, Chuo ambacho kitakuwa na uwezo wa kudahili wanafunzi wa fani mbalimbali za Ufundi wapatao 5,000 kwa wakati mmoja.

**Mradi wa Kuimarisha Elimu ya Ufundi, Mafunzo ya Ufundi Stadi na Elimu ya Ualimu**

**138. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia mradi wa kuimarisha Elimu ya Ufundi, Mafunzo ya Ufundi Stadi na Elimu ya Ualimu kwa mwaka 2019/20 imetenga kiasi cha **Shilingi 72,855,496,000.00** kwa ajili kutekeleza shughuli zifuatazo:

- (i) kuendelea na ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi na huduma (RVTSCs) vya Mikoa ya Geita na Rukwa;
- (ii) kuanza ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi kwa Mikoa ya Simiyu na Njombe ambapo michakato ya kutafuta Wakandarasi inaendelea;
- (iii) kujenga mabweni mawili (2) katika Chuo cha Walimu wa Ufundi Stadi cha Morogoro (MVITC);

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

(iv) kuagiza, kusambaza na kufunga vifaa vya kieletroniki na mawasiliano vya Umeme na Mawasiliano ya simu katika Chuo cha Ufundi Arusha;

(v) kuendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa nne (4) kwa ajili ya madarasa, maabara na ofisi za walimu, Ugavi, pamoja na ufungaji na usambazaji wa vifaa vya LAN katika Chuo cha Ufundi Arusha;

(vi) kuendelea na ujenzi wa Chuo cha Ualimu Dakawa ukihusisha ujenzi wa mabweni mawili yenye uwezo wa kulaza wanachuo 576, Jengo la ghorofa mbili lenye jumla ya madarasa 6 ukumbi wa mikutano (Assembly Hall) ukumbi wa kuchukua watu 1500 na jengo la jiko;

(vii) kujenga nyumba nne (4) za walimu katika Chuo cha Ualimu Marangu ili kuboresha mazingira wanamoishi walimu na hivyo kuwapa motisha ya kufanya kazi kwa juhudi zaidi;

(viii) ununuzi na usimikaji wa samani kwa ajili ya maabara inayojengwa katika Chuo cha Ufundi Arusha;

(ix) kujenga Bweni la ghorofa moja (1), nyumba nane (8) za walimu na ukarabati wa jengo la utawala katika Chuo cha Ualimu Butimba ili kuboresha mazingira ya utoaji elimu;

(x) kujenga maabara ya ghorofa moja (1); bweni la ghorofa moja (1) kwa ajili ya wanafunzi wa kiume 400 na wa kike 176 wa Chuo cha Ualimu Tabora ili kuimarisha mazingira ya utoaji elimu;

(xi) kujenga bwalo la chakula, bweni la ghorofa moja (1) litakalochukua wanafunzi 176 wa kike; maabara ya ghorofa moja (1) na Nyumba mbili (2) za walimu katika Chuo cha Ualimu Mpwapwa ili kuimarisha mazingira ya utoaji elimu;

(xii) kuagiza, kusambaza na kufunga vifaa vya Programu ya Vito na Usonara katika Chuo cha Ufundi Arusha;

(xiii) kuagiza, kusambaza na kufunga vifaa vya *Biomedical* katika Maabara ya Uhandisi ya Ujenzi na Umwagiliaji katika Chuo cha Ufundi Arusha; na

(xiv) kuagiza, kusambaza na kufunga vifaa vya programu katika Maabara ya Uhandisi ya Ujenzi na Umwagiliaji katika Chuo cha Ufundi Arusha.

**Mradi wa Mpango ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) – Kuimarisha Ufundishaji na Ujifunzaji wa Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu - KKK**

**139. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/20, Wizara itaendelea kutekeleza Mpango wa Kukuza Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (Literacy and Numeracy Education Support - LANES) kwa tengeo la **Shilingi 20,445,589,592.00** kwa kufanya yafuatayo:

(i) kuimarisha vituo vya Walimu (TRC) kwa kuandaa Mwongozo kwa ajili ya Waratibu wa Vituo vya Walimu (TRC) ili kuendana na Mkakati wa Mafunzo Kazini kwa walimu kwa lengo la kuwajengea uwezo na kuwaendeleza;

(ii) kuwajengea uwezo waratibu wa TRCs, kutoa mafunzo kwa wawezeshaji pamoja na kuandaa taarifa ili kuwezesha uendeshaji wa vituo vya walimu kwa ufanisi;

(iii) kuwezesha Ufuatiliaji na Tathmini ili kuimarisha ukusanyaji wa takwimu za programu ya LANES zitakazowezesha uendeshaji wa programu kwa ufanisi;

(iv) kuwezesha utekelezaji wa Kiunzi cha Uthibiti Ubora wa Shule na kuwezesha kazi za ufuatiliaji za Wathibiti Ubora wa Shule kwa kugharimia matengenezo ya magari ya Wathibiti Ubora wa Shule pamoja na manunuzi ya mafuta;

(v) kuwezesha uendeshaji wa Kamati za Sekta ya Elimu (ESDC na TWG) kwa lengo la kuimarisha uratibu wa Kisekta;



(vi) kuwezesha uandaaji, uchapaji na usambazaji wa vitabu vya mwanafunzi pamoja na kiongozi cha mwalimu kwa masomo yote kwa wanafunzi wa Darasa la VI na VII;

(vii) kuwezesha uendeshaji na uratibu wa Programu ya LANES na Ukaguzi wa Ndani na Nje wa Programu ya LANES; na

(viii) kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

### **Mradi wa Kuimarisha Mafunzo ya Elimu ya Ualimu (Teacher Education Support Project - TESP)**

**140. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/20, Wizara kupitia Mradi wa Kuimarisha Mafunzo ya Elimu ya Ualimu (TESP) kwa mwaka 2019/20 imetenga kiasi cha **Shilingi 20,300,000,000.00** kwa ajili kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa Vyuo 35 vya Ualimu vya Serikali vikiwemo vifaa vya maabara na vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu ili kuwezesha ufundishaji na ujifunzaji kwa makundi yote;

(ii) kununua vitabu vya Rejea vya Kieletroniki kwa ajili ya Vyuo vya Ualimu 35 vya Serikali pamoja na kusambaza vifaa ikiwemo vya TEHAMA ili kuwezesha Vyuo kuwa na Maktaba zenye rejea za kutosha zinazopatikana kwa njia ya kielektroniki;

(iii) kuwezesha miundombinu ya TEHAMA katika Vyuo vya Ualimu 35, kuviunganisha na Mkongo wa Taifa, kukarabati na kusimika vifaa katika maabara za Sayansi na TEHAMA pamoja na Maktaba ili kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika mawasilisano na ufundishaji na ujifunzaji;

(iv) kuendelea na ujenzi wa Chuo cha Ualimu Kabanga ili kuongeza nafasi za udahili na kuweka mazingira rafiki ya ufundishaji na ujifunzaji;

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

- (v) kuwezesha ufuatiliaji na tathmini ya mradi juu ya shughuli zinazowezesha na mradi ili kubaini changamoto na kuzitafutia ufumbuzi shahiki katika utekelezaji wake;
- (vi) kutoa mafunzo kwa Wawezeshaji wa Kitaifa (Walimu wa Shule za Msingi 120, Walimu wa Sekondari 80 na Wakufunzi wa Vyuo 100) kuhusu Mtaala wa Umahiri (Competence Based Curriculum) ili waze kuwawezesha ipasavyo Wakufunzi, Walimu na Walimu tarajali;
- (vii) kuhuisha Maudhui ya Nyaraka za Mafunzo endelevu kwa Wakufunzi walioko kazini ili kuboresha maudhui na kutoa mafunzo ya TEHAMA kwa Wakufunzi ngazi ya pili ili kuwawezesha kutumia TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji;
- (viii) kutoa mafunzo ya Programu ya Wakufunzi wa Chuo (Teachers Educators Program - TEP) kwa Wakufunzi 1300 wa Vyuo vya Ualimu pamoja na kuwaendeleza Kitaaluma Wakufunzi wa Vyuo;
- (ix) kuwajengea uwezo wa kiutendaji watumish wasio Wakufunzi katika Vyuo vya Ualimu ili waweze kumudu na kutekeleza majukumu yao kikamilifu;
- (x) kufanya ufuatiliaji kwa Wahitimu wa Ualimu katika vyuo ili kuimarisha ufundishaji na kutoa mrejesho utakaoboresha maamuzi ya kiseru;
- (xi) kutoa mafunzo ya TEHAMA na Teknolojia saidizi kwa Wakufunzi/ Walimu 150 wenye mahitaji maalum ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji katika Vyuo na shule;
- (xii) kuanzisha vituo vya kitaalamu vya Hisabati (Mathematics Professional Development Centre) na kuandaa vifaa vya mafunzo kwa ajili ya kuimarisha ufundishaji, ujifunzaji na ufaulu wa somo la Hisabati;
- (xiii) kutoa mafunzo kwa walimu 350 wa Shule za Msingi na walimu 150 wa Sekondari kuhusu Lugha ya Alama na mbinu

sahihi za ufundishaji kwa wanafunzi viziwi ili waweze kujifunza kikamilifu;

(xiv) kuiwezesha Taasisi ya Elimu Tanzania mapitio ya (TET), Mtaala, kukamilishakuchapisha, kudurufu na kusambaza Mitaala na vifaa vya Mitaala katika Vyuo vya Ualimu;

(xv) kuwezesha Mfumo wa Takwimu wa Usimamizi wa Taarifa za Elimu ya Ualimu kuhusiana na BEMIS ili kurahisisha upatikanaji wa takwimu sahihi na kwa wakati;

(xvi) kuwezesha ugharamiaji wa Huduma za Kitaalamu na Ushauri Elekezi katika kazi za Mradi ili kutekeleza kazi hizo kikamilifu;

(xvii) kuwezesha Vikao vya Wadau wa Elimu na Elimu ya Ualimu kwa lengo la kujadili changamoto na kuandaa mapendekezo ya Kisera;

(xviii) kukamilisha uandaaji wa Kionzi cha Umahiri kwa Wakufunzi na Walimu ili kuwa na vigezo bayana vya kutambulisha sifa na vigezo vya kitaalamu; na

(xix) kuwezesha mafunzo ya Hisabati kwa Walimu waliopo Kazini katika Halmashauri 20 zenye ufaulu hafifu nchini ili waweze kuboresha ufundishaji, ujifunzaji na pia ufaulu wa somo hilo.

### **Mradi wa Ukarabati wa Vyuo vya Ualimu (Upgrading Teachers Colleges- UTC)**

**141. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2019/20, Wizara kupitia Mradi wa Ukarabati wa Vyuo vya Ualimu(UTC) imetenga kiasi cha **Shilingi 7,295,917,591.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi na ukarabati wa Vyuo vinne (4) vya Ualimu ambavyo ni Shinyanga, Mpuguso, Ndala na Kitangali.

**Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni (School Water Sanitation and Hygiene - SWASH):**

**142. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2019/20, Wizara kupitia Mradi wa Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni imetenga kiasi cha **Shilingi 6,948,000,000.00** kwa ajili kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) kuwezesha ujenzi wa miundombinu ya Maji na Vyoo katika shule za Msingi 200 ili kuimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunzia;

(ii) kuendelea na utoaji wa mafunzo kuhusu utumiaji wa Mwongozo wa Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni (SWASH) kwa Wathibiti Ubora wa Shule na Waratibu wa SWASH wa Halmashauri ili kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa huduma ya maji, elimu ya afya na usafi wa mazingira shuleni; na

(iii) Kufanya uhakiki na ufuatiliaji wa ujenzi wa miundombinu ya vyoo na maji shuleni kwa kushirikiana na Wizara zinazotekeleza Kampeni ya Kitaifa ya Usafi wa Mazingira ili kubaini changamoto za utekelezaji na kutoa ushauri stahiki.

**Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Sekondari (Secondary Education Quality Improvement Programme - SEQUIP):**

**143. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2019/20, Wizara kupitia mradi wa Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Sekondari (Secondary Education Quality Improvement Programme - SEQUIP), imetenga kiasi cha **Shilingi 30,818,700,000.00** kwa ajili kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) kuwezesha ununuzi wa mashine za uchapaji kwa ajili ya Taasisi ya Elimu Tanzania kwa lengo la kuwezesha upatikanaji wa vitabu vya kutosha na kuinua ubora wa elimu;

(ii) kuwezesha uchapaji na usambazaji wa Vitabu (Nakala Milioni 6) vya masomo ya Sayansi, Hisabati na

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Lugha pamoja na Mwongozo wa Mwalimu ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji;

(iii) kuandaa moduli za Elimu Jumuishi pamoja na Mwongozo wa Mafunzo ili kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu kwa makundi yote;

(iv) kuandaa kiunzi cha utoaji wa tuzo kwa walimu mahiri pamoja na uchapaji wa vyeti;

(v) kuboresha na kununua vifaa vya kujifundishia na kujifunzia katika shule za Sekondari 500 kwa ajili ya kuzifanya shule hizo kuwa vituo vya mafunzo kazini kwa walimu wa masomo ya Sayansi, Hisabati na Lugha;

(vi) kutoa mafunzo ya Elimu Jumuishi kwa angalau Walimu wawili katika Sekondari za Umma Nchini na kununua vifaa vya walimu wenye mahitaji maalumu ili kuwawezesha katika utekelezaji wa kazi zao;

(vii) kuandaa mkakati wa upatikanaji wa walimu wa masomo ya Sayansi na Hisabati;

(viii) kutoa mafunzo kazini kwa walimu 10,000 wa Sayansi, Hisabati na Lugha ili kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa masomo hayo;

(ix) kununua kompyuta, printa na projecta kwa shule za Sekondari 700 na kutoa mafunzo ya TEHAMA kwa walimu 1,000;

(x) kununua vifaa vya upimaji vya wanafunzi wa Sekondari wenye mahitaji maalumu kwa ajili ya kuboresha maendeleo ya wanafunzi hao kitaaluma; na

(xi) kufanya tathmini na ufuatiliaji wa utekelezaji wa programu katika Halmashauri na Mikoa yote ya Tanzania Bara pamoja na ukaguzi wa mradi.

## TUME YA TAIFA YA UNESCO (FUNGU 18)

**144. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20 Tume ya Taifa ya UNESCO imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:

- (i) kuendeleza na kukuza sayansi kwa ajili ya ustawi wa binadamu ili kuimarisha amani, maendeleo endelevu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali;
- (ii) kukuza na kuendeleza upatikanaji wa habari nchini kwa maendeleo endelevu;
- (iii) kuchangia upatikanaji wa Elimu Bora kwa wote na kujenga utamaduni endelevu wa kujifunza;
- (iv) kulinda, kukuza na kuimarisha urithi wa kitamaduni na asili kwa masilahi ya nchi;
- (v) kuchangia juhudi za kuwa na jamii zenye usawa wa kijinsia na ushirikishwaji wa vijana nchini katika kuchochea maendeleo endelevu;
- (vi) kuimarisha mahusiano ya ndani na wadau mbalimbali nchini pamoja na yale ya kikanda na kimataifa katika masuala yanayohusu UNESCO;
- (vii) kukuza uwezo wa Tasisi na Watumishi katika utendaji wake; na
- (viii) kununua magari tatu kwa ajili ya matumizi ya ofisi kwa lengo la kuboresha utendaji.

## D. SHUKRANI

**145. Mheshimiwa Spika**, napenda kutambua mchango mkubwa wa Viongozi wenzangu katika kutekeleza na kufanikisha majukumu ya Wizara yangu. Kipekee kabisa namshukuru Mheshimiwa William Tate Olenasha (Mb), Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa ushirikiano

mkubwa anaonipa katika kusimamia Wizara hii. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu, Dkt. Leonard Douglas Akwilapo, Manaibu Makatibu Wakuu; Profesa James Epiphan Mdoe na Dkt. Ave Maria Semakafu, Kamishna wa Elimu, Wakurugenzi, Wakuu wa Idara na Vitengo, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara yangu kwa ushirikiano wao wa karibu katika kusimamia na kutekeleza majukumu ya kila siku ya Wizara.

**146. Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru Viongozi wa vyama vya wafanyakazi, Watumishi wa Wizara na Taasisi zake, Wanafunzi na wadau wote wa Elimu, kwa ushirikiano wao katika kuendeleza Elimu, Sayansi na Teknolojia. Nawashukuru sana na natambua na kuthamini mchango wenu katika kuhakikisha kuwa sekta za Elimu, Sayansi na Teknolojia zinasonga mbele. Aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wamiliki wa Shule, Vyuo na Taasisi Binafsi ambao wamekuwa wakishirikiana na Serikali katika kuhakikisha Sekta ya Elimu inafikia malengo yake.

**147. Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru Washirika mbalimbali wa Maendeleo na Wadau wa Elimu ambao wamechangia kufanikisha Mipango ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kwa kuwa si rahisi kuwataja wote napenda kuwashukuru na kuwatambua baadhi ya kama ifuatavyo: Serikali za Algeria, Brazil, Canada, China, Cuba, Denmark, Uswisi, Finland, Hungary, India, Italia, Japan, Korea ya Kusini, Marekani, Mauritius, Misri, Ethiopia, Morocco, Msumbiji, Norway, Pakistan, Sweden, Thailand, Ubelgiji, Ufaransa, Uingereza, Ujerumani, Urusi na Uturuki. Aidha, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika.

**148. Mheshimiwa Spika**, napenda pia kuyashukuru baadhi ya mashirika yaliyochangia kufanikisha programu za Elimu, Sayansi na Teknolojia ambayo ni pamoja na; Benki ya Dunia, DfID, *Swedish International Development Agency* (SIDA), Umoja wa Nchi za Ulaya, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Jumuiya ya Madola, *Global Partnership in Education*, *United Nations International Children's Emergency Fund* (UNICEF),

*United Nations Development Programme (UNDP), United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization (UNESCO), USAID, Inter University Council for East Africa (IUCEA), Human Development Innovation Fund (HDIF), Deutscher Akademischer Austauschdienst (DAAD), National Bank of Commerce (NBC), Benki ya Barclays, British Council, Campaign for Female Education (CAMFED), Commonwealth Secretariat, AgaKhan Education Services, Japan International Cooperation Agency (JICA), Karibu Tanzania Organization (KTO), Korea International Cooperation Agency (KOICA), WaterAid, Plan International, Tanzania Education Network/Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET), Christian Social Services Commission (CSSC), Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA) na FEMINA.*

#### **E. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2019/20**

**149. Mheshimiwa Spika**, ili kuwezesha utekelezaji wa malengo ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2019/20, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu 46) inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 1,386,508,723,272.00**.

**150. Mheshimiwa Spika**, katika maombi haya:

(i) **Shilingi 523,788,923,012.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara ambapo **Shilingi 450,356,645,012.00** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 73,432,278,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo;

(ii) **Shilingi 87,358,577,499.00** zinaombwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya idara na vitengo vilivyoko Makao Makuu ya Wizara. Kati ya fedha hizo **Shilingi 62,010,347,000.00** ni mishahara na **Shilingi 25,348,230,499.00** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo;

(iii) **Shilingi 436,430,345,513.00** zinaombwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Wakala na Taasisi zilizo chini ya Wizara. Kati ya fedha hizo **Shilingi 388,346,298,012.00** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 48,084,047,501.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo; na



(iv) **Shilingi 862,719,800,260.00** zinaombwa k w a ajili ya Miradi ya Maendeleo a m b a p o **Shilingi 583,415,000,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 279,304,800,260.00** fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

**151. Mheshimiwa Spika**, kupitia Tume ya Taifa ya UNESCO (Fungu 18) inaomba jumla ya **Shilingi 2,156,017,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida (Mishahara ni **Shilingi 623,724,000.00** na Matumizi mengineyo ni **Shilingi 1,532,293,000.00**).

**152. Mheshimiwa Spika**, kwa heshima kubwa naomba sasa Bunge lako tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Bajeti ya Mafungu yote mawili (Fungu 46 na Fungu 18) yenye jumla ya **Shilingi 1,388,664,740,272.00**.

**153. Mheshimiwa Spika**, napenda kuhitimisha kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe pamoja na kwa waheshimiwa wabunge wote kwa kunisikiliza.

## **KUTOA HOJA**

**154. Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa wasilisho lako zuri. Tunaendelea kupokee taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii. Namwona Makamu wa Mwenyekiti, Mheshimiwa Nkamia, una muda usiozidi nusu saa.

**MHE. JUMA S. NKAMIA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kanuni ya

99(9) ya kanuni za Kudumu za Bunge toleo la Januari mwaka 2016, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pamoja na maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane 7 (1) (a) iliyo chini ya Kanuni ya 118 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, moja ya majukumu ya Kamati hii ni kushughulikia bajeti ya Wizara inayosimamia ikiwemo Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; Nyongeza ya Nane, Kanuni ya 6 Sehemu ya Tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara kupitia Fungu 46 ilikadiria kukusanya shilingi 460. Kamati imeeleza kuwa kufikia mwezi Machi, 2019, Makusanyo yalikuwa ni shilingi 289 sawa na asilimia 62.8 ya lengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa makusanyo ya Idara na Vitengo vya Wizara ni asilimia 37.7 ya lengo. Aidha, kwa upande wa Taasisi zilizo chini ya Wizara, makusanyo ni asilimia 62 ya lengo kama inavyooneshwa kwenye Kielezo Na.1

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Fungu 18 - Tume ya *UNESCO*, makadirio ya makusanyo yalikuwa ni shilingi milioni 70 ambayo yalikalidiriwa kukusanywa kutokana na mrabaha wa uchapishaji wa Jarida la Tume (*Tanzania and UNESCO*) ambao hadi Kamati inaandaa Taarifa hii, maduhuli haya yalikuwa bado hayajakusanywa. Kamati inatoa rai kwa Wizara kuhakikisha maduhuli haya yanakusanywa kabla ya mwaka wa fedha haujamalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Fungu 46 iliidhinishiwa shilingi trilioni 1.406 kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake na kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 476.5 sawa

na asilimia 34 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 929.9 ambayo ni sawa na asilimia 66 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeelezwa kuwa, kufikia mwezi Machi, 2019, Wizara ilikuwa imepokea shilingi bilioni 842.9 ambayo ni sawa na asilimia 60 ya bajeti yote iliyoidhinishwa kwa Fungu 46. Kati ya fedha hizo zilizopokelewa, shilingi bilioni 313.1 ambayo ni sawa na asilimia 37.1 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 529.8 sawa na asilimia 62.8 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kama inavyooneshwa kwenye kielelezo Na. 2

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imefanya uchambuzi wake na kubaini kuwa kati ya fedha za miradi ya maendeleo zilizopokelewa, asilimia 62.2 ni fedha za Bodi ya Mikopo kwa kuwa hata kwenye Bajeti ya Miradi ya Maendeleo iliyotengwa ya shilingi bilioni 929.9 asilimia 45.9 ni fedha za Bodi ya Mikopo kama inavyoonekana kwenye kielelezo Na.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Fungu 18 ambayo ni Tume ya *UNESCO*, imepokea shilingi milioni 200 sawa na asilimia 30 tu ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Tume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani ya Kamati kuwa kiasi cha fedha ambacho bado hakijatolewa kwa mafungu yote mawili kitatolewa kabla ya mwaka huu wa fedha kumalizika ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imefanya ziara ya kutembelea, kukagua na kujadili Taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka 2018/2019. Ziara hiyo ilifanyika mwezi Machi mwaka huu wa 2019 katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani. Kamati imekagua miradi saba ikiwemo miradi mitatu iliyo chini ya Wizara ambayo ni kama ifuatavyo: -

(a) Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (*DUCE*). Namba ya mradi ni 4385 – Fungu 46, ambapo katika mwaka wa fedha 2018/2019 ulitengewa shilingi bilioni mbili kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa jengo la utawala na vyumba vya utafiti ili kutatua changamoto ya uhaba wa vyumba vya utafiti na ofisi za wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi Kamati inatembelea mradi huo, shilingi milioni 582 sawa na asilimia 29.1 zilikuwa zimepokelewa.

(b) Mradi wa Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Ardhi, Fungu 46, ulitengewa shilingi bilioni 2.5 kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la Ardhi (*Lands Building*) na kuiunganisha na mfumo wa maji, ujenzi wa maabara (*Multipurpose Laboratory*) pamoja na kukarabati nyumba za watumishi na madarasa. Hadi Kamati inatembelea mradi huu fedha zote shilingi bilioni 2.5 sawa na asilimia 100 zilikuwa zimetolewa na Serikali. Kamati imeshuhudia utekelezaji wa mradi huo ukiendelea.

(c) Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (Mwalimu Nyerere *Memorial Academy*) unahusisha Ujenzi wa Jengo la Maktaba katika Kampasi ya Kivukoni na Hosteli za Wanafunzi katika Kampasi ya Zanzibar ambapo kiasi cha shilingi bilioni moja kiliidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Hadi Kamati inafanya ziara hakuna fedha yoyote iliyokuwa imepokelewa katika kampasi zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya jumla kuhusu miradi ya maendeleo ni kama ilivyoandikwa kwenye taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2018/2019, Kamati imetoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali kwa ajili ya kufanyiwa kazi. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa baadhi ya maoni yametokelezwa mengine yanaendelea kutekelezwa na baadhi bado hayajatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya masuala ambayo Kamati imeona imeona yana umuhimu lakini bado hayajatekelezwa ni kama ifuatavyo:-

- (a) Kuanzishwa kwa tuzo ya udhamini (*Scholarship Award*) hasa kwa wanafunzi wanaofanya vizuri katika mitihani ya Kidato cha Sita suala ambalo Kamati imeshauri kwa miaka zaidi ya mitatu mfululizo.
- (b) Umuhimu wa kuvigawa Vyuo Vikuu (*University Classifications*) kama ambavyo nchi za wenzetu kwa mfano Marekani wamefanya, suala hili pia bado halijatekelezwa licha ya Kamati kushauri kwa zaidi ya miaka mitatu.
- (c) Kuangalia upya mfumo wa elimu yetu nchini ni jambo ambalo Kamati inaona halijafanyiwa kazi kwa zaidi ya miaka mitatu hadi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaendelea kusesitiza ushauri huu kufanyiwa kazi na Wizara. Wizara kupitia Fungu 46 katika mwaka wa fedha 2019/2020 inakadiria kukusanya shilingi bilioni 553.7. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka huu wa fedha 2019/2020 ni ongezeko la asilimia 20.3 ya makadirio ya makusanyo kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ambayo hata hivyo ukusanyaji wake kufikia mwezi Machi ulikuwa ni asilimia 62.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatoa rai kwa Wizara kuhakikisha inafikia lengo la ukusanyaji wa maduhuli hayo kabla ya mwaka wa fedha kwisha. Aidha, Kamati inatoa angalizo kuwa ni vyema upangaji wa makadirio ya makusanyo ya maduhuli ukazingatia uwezo wa ukusanyaji wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Fungu 18 Tume *UNESCO* makadirio ya maduhuli ni shilingi milioni 27.1. Kamati imebaini kuwa makadirio hayo ni pungufu kwa asilimia 61.4 ya makadirio ya shilingi milioni 70 ya mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara kupitia Fungu 46 inakidiria kutumia shilingi trilioni 1.35, kati ya fedha hizo shilingi bilioni 494.3 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Idara na Taasisi na shilingi bilioni 862 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwa makadirio ya mwaka huu 2019/2020 ni pungufu kwa shilingi bilioni 59.4 ambayo ni sawa na asilimia 3.6 ya makadirio yaliyoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2018/2019. Aidha, Kamati imebaini pia kuwa upungufu huu unaonekana zaidi kwenye bajeti ya miradi ya maendeleo ambayo imepungua kwa shilingi bilioni 67.2 sawa na asilimia 7.2 kama inavyooneshwa kwenye kielelezo Na. 5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imegundua kuwa kwenye bajeti ya kutekeleza miradi ya maendeleo kwa mwaka wa 2018/2019 ambayo upatikanaji wake kufikia mwezi Machi ulikuwa asilimia 57, miradi hiyo ambayo haikupata fedha asilimia 43 baadhi yake pia kwa mwaka huu 2019/2020 haijatengewa fedha. Kamati imehoji Wizara na kuelezwa kuwa kuna matumaini ya fedha hizo kutoka, kabla ya mwaka wa fedha 2018 na 2020 kumalizika. Kamati inasisitiza fedha hizo zitoke ili miradi hii iweze kutekelezwa kwani kinyume na hapo ni wajibu wa Serikali kuitengea fedha miradi hii katika mwaka wa fedha 2019/2020. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Fungu 18 Tume *UNESCO* makadiro ya matumizi ni shilingi bilioni 2.15 ambayo yanajumuisha mishahara na matumizi mengine. Kamati imebaini kuwa makadirio hayo ya matumizi ya kawaida yameongezeka kwa shilingi bilioni moja sawa na asilimia 67.7 ya kiasi kilichoidhinishwa katika mwaka wa fedha uliopita. Kamati imeelezwa kuwa ongezeko hilo linatokana na kuongezeka kwa watumishi, kupandishwa kwa mishahara ya watumishi ambayo ilikuwa midogo pamoja na manunuzi ya magari 11.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uchambuzi huo na yale yaliyobainika, Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine tena Kamati inatoa rai kuhusu hali ya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kamati imebainisha kwamba uchambuzi wa Kamati fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo imekuwa inatolewa kwa asilimia ndogo mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali hii, Kamati inashauri fedha zilizotengwa katika bajeti ya mwaka 2018/2019 zitolewe zote kabla ya mwaka huu wa fedha kumalizika ili Wizara iweze kutekeleza miradi hiyo. Aidha, Kamati inaona ni wakati sasa kwa Serikali kuamua kuchagua miradi michache ya kipaumbele na kuipatia fedha zote kuliko kutenga fedha ilhali tunajua kuwa fedha hizo haziwezi kutolewa. Ushauri huu umekuwa ukitolewa mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa maamuzi yake ya kutoa elimu bila malipo. Tunafahamu lengo hili la Mheshimiwa Rais ni kupanua wigo na kuondoa vikwazo vyote vya uandikishaji wanafunzi. Kamati imeshuhudia ongezeko kubwa la wanafunzi wanaoandikishwa katika elimu ya msingi. Hata hivyo, ongezeko hilo limekuwa na changamoto kutokana na miundombinu finyu na uhaba wa walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuendelea kuboresha miundombinu ili wanafunzi waweze kusoma vizuri. Aidha, Kamati inashauri Serikali iendelee kuajiri na kuboresha maslahi ya walimu ili kuwapa morali ya kufundisha ongezeko hili la wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya uhaba wa walimu ni kubwa mno. Kamati inapongeza juhudi za Serikali kuendesha kuendelea kuajiri walimu kutoka walimu 164,418 mwaka 2018 hadi kufikia walimu 179,249 mwaka huu. Pamoja na ongezeko hili la walimu, Serikali inaendelea kutekeleza mpango wa utaratibu wa elimu bila malipo ambao nao unaendelea kuongezeka na kuongeza idadi ya wanafunzi wanaoandikishwa kwenye elimu ya msingi na sekondari na hivyo kuhitaji uwepo wa walimu wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba huu wa walimu unaonekana zaidi katika maeneo ya vijijini kutokana na changamoto zilizopo katika maeneo hayo. Kutokana na changamoto hii, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuajiri walimu wengi zaidi ili kutatua changamoto hii. Aidha, ili kuwavutia walimu kwenda kufundisha maeneo ya vijijini, Kamati inashauri motisha zaidi itolewe kwa walimu hao ikiwemo kuwapatia nyumba za kuishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeelezwa kuwa kuna utaratibu umewekwa na Wizara ya Elimu wa kuongeza muda zaidi wa kufanya mitihani kwa wanafunzi wenye ulemavu. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa utaratibu huu haufahamiki kwenye shule nyingi hali inayowafanya wanafunzi hawa wenye ulemavu wafanye mitihani kwa muda ule ule sawa na wanafunzi wasio na ulemavu. Kamati inashauri Wizara ihakikishe utaratibu huu unafahamika kwa shule zote na kwa wanafunzi wenye ulemavu kwa kutoa elimu ili wanafunzi hawa wenye ulemavu wasikose haki yao ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi bora wa Taifa lolote duniani unatokana na elimu bora. Kuanzia mwaka 2016 kamati imekuwa ikishauri kuhusu kuangaliwa kwa mfumo elimu nchini. Hata hivyo, ushauri huu bado haujatekelezwa kama ilivyoelezwa katika sehemu ya utekelezaji wa maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaendelea kushauri kuangaliwa upya kwa mfumo wa elimu kwani naamini mfumo wa elimu ni chachu katika maendeleo ya Taifa lolote. Mwanazuoni mmoja James Baldwin amewahi kusema *" Education has assumed great importance in the new world. It makes a man a thinker, completes him as a person. And if this foundation is faulty, the system and society collapse in all entirety. It is high time that we understand the gravity of the situation to an education system."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wa Elimu kwenye jamii na nchi kwa ujumla wake, Kamati inashauri



Wizara isome Ripoti ya Tume iliyoundwa na aliyekuwa Rais wa zamani wa Marekani Ronald Regan ya Mwaka 1983 inayoitwa *"A Nation of Risk, The Imperative Educational Reform"* ambayo ndiyo ilikuwa historia ya mafanikio ya mfumo wa elimu Marekani na kuiga yote mazuri yaliyomo kwenye Taarifa hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wa elimu kwenye jamii na nchi kwa ujumla, Kamati inaishauri Wizara isome Ripoti ya Tume iliyoundwa na aliyekuwa Rais wa zamani wa Marekani, Ronald Wilson Reagan ya mwaka 1983 inayoitwa *"A Nation of Risk, The Imperative Education Reform"* ambayo ndio ilikuwa historia ya mafanikio ya mfumo wa elimu Marekani na kuiga yote mazuri yaliyomo kwenye Taarifa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mitaala Kuendana na Mapinduzi ya Nne ya Viwanda. Dunia yetu kwa sasa inaelekea kwenye mapinduzi ya nne ya viwanda (*The Fourth Industrial Revolution*). Kwa mujibu wa Profesa Klaus Martin Schwab, ambaye ni mwanzilishi na Mwenyekiti wa Jukwaa la Dunia la Uchumi (*World Economic Forum*) amesema:

*"Dunia inaenda kuendeshwa kwa teknolojia ya hali ya juu ambapo robot na mitambo ya kisasa itakuwa inafanya kazi zaidi kuliko nguvu ya binadamu. Si hivyo tu, lakini hata magari yatakuwa yanajiendesha yenyewe na kwa ujumla mfumo wa maisha ya mwanadamu utabadilika mno."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko haya pamoja na changamoto zake inaelezwa kuwa ni fursa kwetu kama nchi, kwani dunia ina uwezo wa kuunganisha mabilionni ya watu zaidi kwenye mitandao, endapo tu tutakuwa na uwezo wa kufanya hivyo. Kwa mujibu wa *World Economic Forum*, mapinduzi ya nne ya viwanda yanahimizwa kufikia ubunifu katika uzalishaji mnyororo wa thamani, usambazaji wa huduma kwa wateja na mambo mengine ya namna hiyo. Hivyo, basi, elimu yetu inapaswa kuangalia zaidi maeneo haya na kimkakati kama inavyooneshwa kwenye kielelezo namba 6(a) hadi (b).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa msingi huo basi, Kamati inaishauri Serikali ione kwamba, haina budi sasa kuanza kujiandaa na kuhakikisha mitaala yetu ya elimu inazingatia mapinduzi hayo kwa kutoa elimu ambayo itaongeza ujuzi na maarifa kwa wanafunzi ili kuendana na mapinduzi haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Udhhibiti Ubora wa Shule; nchi yetu ikiwa ni moja kati ya nchi 193 Wanachama wa Umoja wa Mataifa inapaswa kutekeleza Lengo Na.4 la Maendeleo Endelevu la Milenia (*SDGS*) la elimu bora (*Quality Education*) kupitia mipango yake. Kamati inaamini kuwa utekelezaji wa lengo hili ambalo linasisitiza kuhusu elimu bora unategemea mambo mengi ikiwemo udhibiti ubora wa shule. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa, upatikanaji wa fedha kutokana na bajeti iliyotengwa kwa ajili ya idara hii kwa mwaka wa fedha uliopita haukufikia hata asilimia 30 ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri fedha za udhibiti ubora wa shule zitolewe zote kabla ya mwaka huu wa fedha kumalizika. Pia kuanzia sasa Serikali ihakikishe fedha zote zinazotengwa kwa ajili ya udhibiti ubora wa shule zinatolewa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Stahiki za Wahadhiri wa Vyuo Vikuu. Kamati inatambua umuhimu wa elimu ya juu ambapo wahadhiri na watumishi wengine ni nyenzo muhimu katika utoaji wa elimu. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa, kuna changamoto ya Wahadhiri na watumishi hawa wa vyuo vikuu kutolipwa stahiki zao ikiwemo posho za nyumba. Changamoto hii imesababisha baadhi ya Wahadhiri kuzuia matokeo ya mitihani, lakini Kamati inaona kuna athari zaidi baadaye. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha maslahi ya wahadhiri na watumishi wa vyuo vikuu, hususan posho ya nyumba, inatolewa mapema ili kuepuka hali ya sintofahamu baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu; Kamati inapongeza jitihada zinazofanywa na Serikali za kuongeza idadi ya wanafunzi

wanaopata mikopo ya elimu ya juu. Tumeshuhudia bajeti ya Bodi ya Mikopo imekuwa ikiongezeka mwaka hata mwaka kutoka shilingi bilioni 427.5 mwaka juzi hadi kufikia bilioni 450 mwaka jana, kiasi ambacho kitasaidia kuongeza idadi ya wanafunzi na kufikia 6,000. Hata hivyo, Kamati inafahamu changamoto zinazoikumba Bodi ya Mikopo pamoja na wanafunzi na hivyo inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa baadhi ya wanafunzi wamekuwa wakikosa mikopo kwa sababu mbalimbali ikiwemo kukosa vielelezo, Kamati inashauri bodi ishirikiane na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (*NIDA*) ili kubaini wanafunzi wanaostahili kupewa mikopo, lakini pia kurejesha baada ya kupata mikopo hiyo.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, wanafunzi wengi wamekuwa wakichelewa kupata fedha za mikopo hasa za kujikimu kutokana na baadhi ya vyuo kuwa na changamoto zake, ikiwemo za madeni katika mabenki, hali inayosababisha kuzuiliwa kwa fgedha hizo kwenye benki hizi, kamati inaona jambo hili si jema na hivyo inashauri fedha kujikimu wanafunzi kutoka Bodi ya Mikopo zipelekwe moja kwa moja kwenye akaunti za wanafunzi, ili kuepuka changamoto hii.

(c) Kama ambavyo imeonekana kwenye uchambuzi wa Kamati kati ya bajeti yake inayotengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ipatayo 40 ya Wizara, asilimia 62 ni fedha za Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Kamati inaona fedha za bodi zinaifanya Wizara ionekane inapewa fedha nyingi mno za miradi ya maendeleo wakati kiuhalisia sio kweli kwani asilimia 40 ndio inabaki kutekeleza miradi zaidi ya 40. Kamati inashauri kwa mara nyingine tena Serikali kuipa Bodi ya Mikopo Fungu lake (*Separate Vote*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Vyuo Vikuu (*TCU*); Kamati inatambua kazi za Tume ya Vyuo Vikuu (*TCU*) ni pamoja na kusimamia na kudhibiti ubora wa elimu ya juu na kufanya maboresho; kufanya udahili wa wanafunzi na kuratibu uhamisho wa idara wa wanafunzi pamoja na kufanya ukaguzi wa vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni *TCU* imefanya ukaguzi wa kushtukiza katika vyuo nane na kuvifungia kufanya udahili kutokana na upungufu waliobaini katika utoaji wa Elimu. Kamati imeeleza kuwa, baadhi ya vyuo vimeshindwa kulipa mishahara ya Walimu (Wahadhiri) hali iliyosababisha walimu hao kuzuia kutoa matokeo ya mitihani ya wanafunzi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapongeza juhudi hizi zilizofanywa na *TCU*, lakini inaona hatua zimechelewa kuchukuliwa hali ambayo imeathiri wanafunzi wengi wasio na hatia kutokana na vyuo hivyo kufungwa. Kamati inashauri ili kuepuka kufungia vyuo ni vyema *TCU* ikawa inavifuatilia kwa ukaribu na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika vyuo vyote nchini ili kubaini mapungufu mapema na kushirikiana nao kufanya marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (*COSTECH*); nchi yetu ikiwa inaelekea kwenye uchumi wa kati na uchumi wa viwanda kama nilivyosema awali, hivyo kuna kila sababu ya kuiwezesha *COSTECH* ili iweze kusaidia katika ubunifu wa masuala mbalimbali.

Pia tumeona hapo awali kwenye Taarifa hii kuwa dunia inaelekea kwenye Mapinduzi ya Nne ya Viwanda ambapo teknolojia ya hali ya juu inaanza kutumika. Kutokana na umuhimu wa *COSTECH* kuelekea kwenye mapinduzi hayo, Kamati inashauri Bajeti ya Taasisi hii iongezwe ili iweze kutekeleza majukumu yake ya sayansi, teknolojia na ubunifu kwa maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imekuwa inaelekea kwenye uchumi wa kati wa viwanda uzalishaji wa Mafundi Mchundo ni muhimu mno. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuendelea kujenga na kukarabati vyuo mbalimbali vya ufundi ili kuongeza idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa. Ni rai ya Kamati kuwa, vyuo hivi vya Ufundi Stadi pamoja na majukumu yake mengine, ni wakati sasa vijielekeze katika kuzalisha mafundi mchundo ambao ni nyenzo muhimu katika uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; kwa mara nyingine napenda kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa hii ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu. Kipekee nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano walioutoa ikiwa ni pamoja na kuonesha weledi wakati wa kuchambua Bajeti ya Wizara. Naomba kuwatambua Wajumbe kama ifuatavyo, kwa kuwa muda ninao:

Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mwenyekiti; Mheshimiwa Juma Nkamia, Makamu; Mheshimiwa Salma Rashid Jakaya Mrisho Kikwete, Mjumbe; Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, Mjumbe, Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve, Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mheshimiwa Peter Ambrose Lijualikali, Mheshimiwa Bernadetha Mushashu, Mheshimiwa Vicky Kamata, Mheshimiwa Deogratius Francis Ngalawa, Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa, Mheshimiwa Susan Anselm Lyimo, Mheshimiwa John Peter Kadutu, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Joseph Osmund Mbilinyi, Mheshimiwa Khamis Yahya Machano, Mheshimiwa Mchungaji Dokta Getrude Rwakatare, Mheshimiwa Seleman Said Bungara (Bwege), Mheshimiwa Kabwe Zuberi Ruyagwa, Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, Mheshimiwa Joseph Leonard Haule, Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa, Mheshimiwa Maulid Ally Mtulia na Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na kukupongeza uongozi thabiti ulionao wewe katika kuendesha Bunge letu Tukufu. Nawashukuru na kuwapongeza pia Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Profesa Joyce Ndalichako, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia; Mheshimiwa Ole Tata Nasha, Naibu Waziri; Dkt. Leonard Akwilapo, Katibu Mkuu; Profesa James Mdoe, Naibu Katibu Mkuu; na Dokta Ave Maria Semakafu, Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa utendaji kazi wao na mashirikiano waliyoipatia Kamati yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee namshukuru Katibu wa Bunge letu Ndugu Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vizuri. Napenda pia kumshukuru Ndugu Athumani Husseni, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge na Ndugu Dickson Bisile Mkurugenzi Msaidizi anayesimamia Kamati yetu kwa ushirikiano na ushauri wanaoipatia Kamati.

Aidha, nawashukuru sana Makatibu wetu wa Kamati Ndugu Pamela Pallangyo na Ndugu Agnes Nkwera kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kutoa msaada wakati wote unapohitajika. Pamoja nao nawashukuru Watumishi wote wa Bunge kwa utendaji kazi wake mzuri unaosaidia Kamati kutekeleza majukumu yake vizuri ikiwemo kukamilika kwa Taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, lakini siyo kwa umuhimu, napenda kuwashukuru wadau wote wa elimu ikiwemo *UNDP* kupitia Mradi wa *LSP* unaoendeshwa na Ofisi ya Bunge kwa elimu ambayo imekuwa ikiwezesha Kamati kupata uelewa wa masuala mbalimbali kutokana na mafunzo ambayo yamekuwa yakitolewa. Mafunzo hayo yamewezesha Kamati kutekeleza majukumu yetu ya Kibunge kwa ufanisi. Aidha, Kamati inawashukuru wadau wote wa elimu ambao wamekuwa wakifanya kazi na Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali, liridhie na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu 46) kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 shilingi trilioni moja mia tatu hamsini na saba na Tume ya *UNESCO* (Fungu 18) shilingi bilioni 2.156 kama yalivyowasilishwa na Mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono Hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA  
ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA KWA MWAKA WA FEDHA  
2018/2019 PAMOJA NA MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO  
YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI  
YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 - KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

***SEHEMU YA KWANZA***

---

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane (7) (1) (a) iliyo chini ya Kanuni ya 118 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016) moja ya majukumu ya Kamati hii ni kushughulikia bajeti ya Wizara inazozisimamia ikiwemo Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia [Nyongeza hiyo ya Nane, Kanuni ya 6 (5)].

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, kabla ya kupokea, kujadili na kuchambua Taarifa ya Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, Kamati ilifanya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2018/2019. Lengo la ziara hiyo ni kuona hatua ya utekelezaji wa Miradi hiyo ambayo iliidhinishiwa fedha na Bunge lako Tukufu ili kuweza kufanya ulinganisho.


**SEHEMU YA PILI**

- 2.0 UCHAMBUZI WA MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019
- 2.1 UKUSANYAJI WA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara kupitia **Fungu 46** ilikadiriwa kukusanya shilingi **460,011,442,840.89** kwa mchanganuo ufuatao:- Kutoka kwenye Idara na Vitengo zilikadiriwa kukusanywa shilingi **16,916,628,402.59** na kwa upande wa Taasisi zilizo chini ya Wizara zilikadiriwa kukusanywa shilingi **443,094,814,438.30**. Kamati imeelezwa kuwa, kufikia mwezi Machi 2019, Makusanyo yalikuwa ni shilingi **289,095,133,020.35** sawa na **asilimia 62.8** ya lengo.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa makusanyo ya Idara na Vitengo vya Wizara ni shilingi **6,381,964,577.31** sawa na **asilimia 37.7** ya lengo. Aidha, kwa upande wa Taasisi zilizo chini ya Wizara zimekusanywa shilingi **282,503,961,217.21** sawa na **asilimia 62** ya lengo kama inavyooneshwa kwenye Kielezo Na.1

**Kielelezo na. 1: Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka 2018/2019**



*Chanzo: Randama ya Wizara (2019) na usanifu wa Kamati*



**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa **Fungu 18** - Tume ya UNESCO, makadirio ya makusanyo yalikuwa ni shilingi **70,000,000/=** ambayo yalikadiriwa kukusanywa kutokana na mrabaha wa uchapishaji wa Jarida la Tume (Tanzania and UNESCO) ambao mpaka Kamati inaandaa Taarifa hii, maduhuli haya yalikuwa bado hayajakusanywa. ***Kamati inatoa rai kwa Wizara kuhakikisha Maduhuli haya yanakusanywa kabla ya mwaka wa fedha kuisha.***


## **2.2 UCHAMBUZI WA UPATIKANAJI WA FEDHA KUTOKA HAZINA KWA MWAKA 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (**Fungu 46**) iliidhinishiwa shilingi **1,406,469,626,000.00** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, shilingi **476,500,224,000.00** sawa na **asilimia 34** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi **929,969,402,000.00** sawa na **asilimia 66** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa, kufikia mwezi Machi 2019, Wizara ilikuwa imepokea shilingi **842,967,005,094.00** sawa na **asilimia 60** ya Bajeti yote iliyoidhinishwa kwa **Fungu 46**. Kati ya Fedha hizo zilizopokelewa, shilingi **313,116,309,921.38** sawa na **asilimia 37.1** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi **529,850,695,174.72** sawa na **asilimia 62.8** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya ulinganisho wa bajeti iliyoidhinishwa na kiasi kilichopokelewa na ilibaini kuwa, kati ya fedha za matumizi ya kawaida zilizoidhinishwa shilingi **476,500,224,000.00**, kiasi kilichopokelewa ni **shilingi 313,116,309,921.38** sawa na **asilimia 66**. Aidha, kwa upande wa fedha za kutekeleza Miradi ya Maendeleo shilingi **929,969,402,000.00**, ziliidhinishwa na Wizara tayari imepokea shilingi **529,850,695,174.72** sawa na **asilimia 57** kama inavyooneshwa kwenye Kielelezo Na. 2.


**Kielelezo Na.2: Hali ya Upatikanaji wa Fedha (Fungu 46) kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**



**Chanzo: usanifu wa Kamati na Randama ya Wizara 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya uchambuzi wake na kubaini kuwa, kati ya fedha za Miradi ya Maendeleo zilizopokelewa, **asilimia 62.2 ni fedha za Bodi ya Mikopo (329,448,673,494.20) kwa kuwa hata kwenye Bajeti ya Miradi ya Maendeleo iliyotengwa ya shilingi 929,969,402,000.00, takribani shilingi 427,554,000,000/= sawa na asilimia 45.9 ni fedha za Bodi ya Mikopo kama inavyoonekana kwenye kielelezo Na.3**

**Kielelezo Na. 3 Mchanganuo wa Bajeti ya Miradi wa Maendeleo**



**Chanzo: Randama ya Wizara (2019) na Usanifu wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa **Fungu 18** ambayo ni Tume ya UNESCO, imepokea **shilingi 200,000,000.00** sawa na **asilimia 30** tu ya **shilingi 666,855,000.00** zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Tume.

**Mheshimiwa Spika**, *Ni imani ya Kamati kuwa kiasi cha fedha ambacho bado hakijatolewa kwa mafungu yote mawili kitatolewa kabla ya mwaka huu wa fedha kuisha ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake.*

**2.3 MAELEZO NA MATOKEO YA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTEMBELEWA NA KUKAGULIWA NA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya ziara ya kutembelea, kukagua na kujadili Taarifa za utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka 2018/2019. Ziara hiyo ilifanyika kuanzia tarehe 14 hadi 23 Machi katika Mkoa wa Dar es salaam na Pwani. Kamati ilikagua jumla ya Miradi 7 ikiwemo miradi mitatu iliyo chini ya Wizara hii kama ifuatavyo: -

**a) Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE) Namba ya Mradi 4385 – Fungu 46)**

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu ambao gharama zake halisi ni shilingi **Bilioni 3.2**, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 ulitengewa shilingi **Bilioni 2** kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa Jengo la Utawala na vyumba vya Utafiti ili kutatua changamoto ya uhaba wa vyumba vya utafiti na Ofisi za wafanyakazi.

**Mheshimiwa Spika**, wakati Kamati inatembelea Mradi, shilingi **Milioni 582** sawa na **asilimia 29.1** zilikuwa zimepokelewa. Aidha, Kamati ilielezwa kuwa kutokana na kusuasua kwa utolewaji wa fedha kutoka Serikalini, Chuo kiliomba fedha kupitia Mradi wa P4R ulio chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na kupewa shilingi **Bilioni 1.150**. Sambamba na fedha hizo, Chuo kilikopa shilingi **Milioni 500** kutoka Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) zilizoweza Chuo kuendelea na upanuzi wa chuo katika Awamu ya Pili (Hatua ya Kwanza) ambao unahusisha ukarabati wa ghorofa ya chini iliyokuwepo awali pamoja na ujenzi wa ghorofa ya kwanza na ya pili ambazo hazikuwepo kabla. Kamati ilishuhudia ujenzi ukiwa unaendelea chini ya Mkandarasi SUMA JKT na ulikuwa umefikia **asilimia 75**. Kwa mujibu wa taarifa ya Mkuu wa Chuo, mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2019 endapo kiasi cha fedha kilichobaki cha shilingi **Bilioni 1.42** sawa na **asilimia 60.9** kitakapotolewa na Serikali.

**b) Mradi wa Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Ardhi (Namba ya Mradi 6354 – Fungu 46)**

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu ulitengewa kiasi cha shilingi **Bilioni 2.5** kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Ardhi (Lands Building) na kuliunganisha na mfumo wa maji, ujenzi wa Maabara (Multipurpose Laboratory) pamoja na kukarabati karakana, nyumba za watumishi na madarasa.

**Mheshimiwa Spika**, hadi Kamati inatembelea Mradi huo fedha zote kiasi cha shilingi **Bilioni 2.5 sawa na asilimia 100**

zilikuwa zimetolewa na Serikali. Kamati ilishuhudia utekelezaji wa mradi ukiwa unaendelea ikiwa ni pamoja na madarasa na nyumba za Walimu. Aidha, kwa upande wa ujenzi wa Jengo la Ardhi (Land Building) Kamati ilielezwa kuwa ujenzi ulitarajiwa kuanza mwezi Machi, 2019 na Chuo kilikuwa katika kufanya mawasiliano na DAWASA ili waweze kuruhusu Chuo kupitisha magari yao katika eneo la DAWASA ambalo wanapakana nalo. Kwa upande wa Ujenzi wa Maabara (Multipurpose Laboratory) Kamati ilielezwa kuwa zabuni zilitarajiwa kufunguliwa tarehe 27 Machi, 2019 kutokana na kubadilika kwa michoro.

**Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza Serikali kwa kutoa fedha hizi kwa wakati, utaratibu huu uendeleo kwa Miradi mingine ya Maendeleo. Aidha, Kamati inashauri Mradi utekelezwe kama ulivyopangwa kwani ilielezwa ndani ya miezi 4 mradi huu utakuwa umekamilika.**

**c) Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (*Mwalimu Nyerere Memorial Academy*) (Namba ya Mradi 4381- Fungu 46)**

**Mheshimiwa Spika, Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo hiki unahusisha Ujenzi wa Jengo la Maktaba katika Kampasi ya Kivukoni na Hosteli za Wanafunzi katika Kampasi ya Zanzibar ambapo kiasi cha shilingi **Bilioni 1** kiliidhinishwa na Bunge lako Tukufu.**

**Mheshimiwa Spika, mpaka Kamati inafanya ziara hakuna fedha yoyote iliyopokelewa kwa Kampasi zote mbili. Hata hivyo, Kamati ilipata fursa ya kuangalia Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Mihadhara katika Kampasi ya Kivukoni lililojengwa kwa kutumia fedha za ndani kwa **asilimia 100**. Jengo hilo lenye thamani ya shilingi **Bilioni 1.15**, utekelezaji umefikia **asilimia 95**. *Kamati inakipongeza Chuo kwa kuamua kutumia mapato yake ya ndani kutekeleza Mradi huu mkubwa na mzuri.***

**Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa rai kwa Serikali kuhakikisha inakipatia Chuo hiki fedha zote zilizo idhinishwa na Bunge hasa ikizingatiwa kuwa Chuo huku kina beba jina kubwa la Baba**

*wa Taifa lakini miundombinu yake hairidhishi wala haiendani na hadhi hiyo ikiwemo ukosefu wa Maktaba yenye kutosheleza wanafunzi pamoja na hosteli za wanafunzi hasa Kampasi ya Zanzibar.*

#### 2.4 MAONI YA JUMLA KUHUSU MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTEMBELEWA NA KUKAGULIWA NA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, kufuatia ziara ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo, na hali ambayo Kamati imeiona. Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

##### a) Upatikanaji wa Fedha

Hali ya upatikanaji wa fedha siyo ya kuridhisha kama ambavyo imeshuhudia katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere na Chuo kishiriki cha Elimu Dar es Salaam(DUCE). Si hivyo tu, lakini pia katika Miradi yote ya Maendeleo iliyotengewa fedha upatikanaji wa fedha hizo siyo wa kuridhisha. ***Kamati inaona kuna umuhimu na ulazima kwa Serikali kuhakikisha inapeleka kwa ukamilifu na kwa wakati fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu ili kufikia malengo yaliyopangwa.***

##### b) Kutumia Mapato ya Ndani

Baadhi ya Taasisi, pamoja na kukosa fedha za Serikali zimekuwa zikitekeleza miradi yake kwa fedha zake za ndani kama vile Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere na Taasisi ya Ustawi wa Jamii. ***Kamati inapongeza sana jitihada hizi na inashauri Taasisi kuiga mfano huu mzuri.***

##### c) Uhaba wa Watumishi

Kamati imebaini uwepo wa uhaba wa Watumishi katika Taasisi za Elimu kama vile Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere hali ambayo inadhorotesha utendaji kazi. Mwanasiasa Solomon Ortiz ambaye alikuwa ni alikuwa mwakilishi wa Jimbo la Texas huko Marekani amewahi kusema ***“ Education is the key to success in life, and teachers make a lasting impact in the lives of their students” Hivyo basi, Kamati inaona kuna umuhimu wa Serikali kuziangalia Taasisi hizi na***

***kuzipa umuhimu wa kipekee wa kuzipatia watumishi wa kutosha na hususan Walimu.***

**d) Vyuo kujielekeza kwenye Misingi ya kuanzishwa**

Kamati imebaini kuwa baadhi ya Vyuo kama vile Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere na Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE) Vimeanza kujielekeza katika kufundisha masomo mbalimbali na kusahau msingi wa kuundwa kwake (*The Niche*). ***Kamati inaona kuna haja ya Taasisi hizi za Elimu kurudi kwenye misingi ya kuanzishwa kwake ili ziweze kutoa elimu hizo ambazo ni muhimu sana kwa jamii.***

**e) Motisha kwa Watumishi**

Kamati imebaini kuwa changamoto ya malipo mbalimbali zikiwemo motisha ya posho ya nyumba kwa watumishi wa Vyuo vikuu ni kubwa na inaweza athiri utendaji kazi wao. **Kamati inashauri Serikali kulibeba suala hili kipekee na kulitafutia ufumbuzi wa haraka.**

**2.5 UCHAMBUZI WA MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA USHAURI WA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali kwa ajili yakufanyiwa kazi. Katika Taarifa ya utekelezaji wa maoni hayo ambayo iliwasilishwa na Wizara mbele ya Kamati imeonesha kuwa, baadhi ya maoni yametokelezwa vizuri ikiwemo suala la Kuundwa kwa Bodi ya Kitaalamu ya Walimu; Kuimarishwa kwa Tume ya Utumishi wa Walimu ili kuondoa changamoto za walimu kusimamiwa na chombo zaidi ya kimoja pamoja na Kutoa mwongozo wa ujenzi wa miundombinu inayozingatia watoto wenye ulemavu.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, baadhi maoni yanaendelea kutekelezwa na baadhi bado hayajatekelezwa kabisa. Baadhi ya masuala ambayo Kamati inaona yana umuhimu lakini bado hayajatekelezwa ni pamoja na:-

- a) Kuanzishwa kwa Tuzo ya Udhamini (*Scholarship Award*) hasa kwa wanafunzi wanaofanya vizuri katika mitihani ya kidato cha sita, suala ambalo Kamati imelishauri kwa miaka zaidi ya miaka mitatu mfululizo.
- b) Umuhimu wa kuvigawa Vyuo Vikuu (University Classification) kama ambavyo nchi za wenzetu kwa mfano Marekani wamefanya, suala hili pia bado halijatekelezwa licha ya Kamati kushauri kwa zaidi ya miaka 3 sasa.
- c) Kuangalia upya Mfumo wa Elimu yetu nchini ni jambo ambalo Kamati inaona halijafanyiwa kazi kwa zaidi ya miaka mitatu sasa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kusisitiza ushauri huu wa Kamati kufanyiwa kazi na Wizara. (**Rejea Taarifa za Kamati kwa Mwaka 2016/2017, 2017/2018 na 2018/2019**)

### **3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Randama ya Wizara, Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka huu wa fedha 2019/2020 yameandaliwa kwa kuzingatia Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/2017 -2020/2021) pamoja na Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Elimu (2016/2017-2020/20).

#### **3.1 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020**


**Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia **Fungu 46**, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 inakadiria kukusanya shilingi **553,739,899,119.13** kutoka katika vyanzo mbalimbali kama vile ada, ushauri elekezi na ukaguzi wa shule. Kati ya makadirio hayo, shilingi **13,942,894,000 (asilimia 2.5)** zinakadiriwa kukusanywa kutoka katika Idara na Vitengo vya Wizara na shilingi **539,797,005,119.13 (asilimia 97.5)** zinakadiriwa kukusanywa kutoka katika Taasisi zilizo chini ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka huu wa



fedha 2019/2020 ni ongezeko la **asilimia 20.3** ya Makadirio ya makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 (**Kielelezo Na. 4 (a na b)**) ambayo hata hivyo ukusanyaji wake kufikia mwezi Machi ulikuwa ni **asilimia 62**. Kamati inatoa rai kwa Wizara kuhakikisha inafikia lengo la ukusanyaji wa maduhuli hayo kabla ya mwaka wa fedha kuisha. Aidha, Kamati inatoa angalizo kuwa ni vyema upangaji wa makadirio ya makusanyo ya maduhuli ukazingatia uwezo wa kukusanya. Kielelezo Na. 4 (a)

ULINGANISHO WA UKUSANYAJI WA MADUHILI (FUNGU 46) KWAMWAKA 2018/2019 NA 2019/2020				
CHANZO	2018/2019	2019/2020	ONGEZIKO/PUNGUFU	ASILIMA
IDARANA VITENGO	16,916,628,402	13,942,894,000	(2,973,734,402)	-17.6
TAASISI	443,094,814,438	539,797,005,119	96,702,190,681	21.8
JUMA	460,011,442,840	553,739,899,119	93,728,456,279	20.4



Chanzo: Randama ya Wizara (2019) na Usanifu wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa **Fungu 18 (Tume ya UNESCO)**, makadirio ya maduhuli ni shilingi **27,101,880.00**. **Kamati** imebaini kuwa makadirio haya ni pungufu kwa **asilimia 61.4** ya makadirio ya shilingi **70,000,000.00** katika Mwaka wa Fedha 2018/2019.

### **3.2 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Wizara kupitia **Fungu 46** inakadiria kutumia shilingi **1,357,106,983,260/=**. Kati ya fedha hizo, shilingi **494,387,183,000/=** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Idara na Taasisi na shilingi **Bilioni 862,719,800,260/=** ni kwa ajili ya kutekeza Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, kati ya shilingi **494,387,183,000/=** za Matumizi ya Kawaida ya Wizara (**Fungu 46**), Mishahara (PE) inaombewa shilingi **420,954,905,000/=** sawa na **asilimia 85.1**, na Matumizi Mengineyo (OC) yanaombewa shilingi **73,432,278,260/=** sawa na **asilimia 14.9**. Aidha, kwa upande wa fedha za kutekeleza Miradi ya Maendeleo, zinaombwa shilingi **862,719,800,260/=**. Kati ya Fedha hizo shilingi **583,415,000,000/=** sawa na **asilimia 67.6** ni fedha za ndani na shilingi **279,304,800,260/=** sawa na **asilimia 32.4** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa makadirio ya Mwaka huu 2019/2020 ni pungufu kwa shilingi **59,453,642.740 (asilimia 3.5)** ya Makadirio yaliyoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2018/2019. Aidha, Kamati imebaini pia kuwa upungufu huu unaonekana zaidi kwenye bajeti ya Miradi ya Maendeleo ambayo imepungua kwa shilingi **67,249,601,740/=** sawa na **asilimia 7.2**. (Kielelezo Na. 5).


**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeenda mbali zaidi na kugundua kuwa kwenye bajeti ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 ambayo upatikanaji wake kufikia mwezi Machi 2019 ulikuwa ni **asilimia 57**, miradi hiyo

ambayo haikupata fedha (**asilimia 43**) baadhi yake pia kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 haijatengewa fedha. Kamati ilihoji Wizara na kuelezwa kuwa kuna matumaini ya fedha hizo kutoka kabla ya Mwaka wa Fedha 201/2019 kuisha.

***Mheshimiwa Spika, Kamati inasisitiza fedha hizo zitoke ili miradi hii iweze kutekelezwa kwani kinyume na hapo ni wajibu wa Serikali kuitengea fedha Miradi hii katika Mwaka wa Fedha 2019/2020.***

**Mheshimiwa Spika**, kupitia **Fungu 18** (Tume ya UNESCO), makadirio ya matumizi ni shilingi **2,156,017,000/=** ambayo yanajumuisha mishahara (PE) **623,724,000/=** na Matumizi Mengineyo (OC) shilingi **1,532,293,000/=**. Kamati imebaini kuwa makadirio haya ya Matumizi ya Kawaida yameongezeka kwa shilingi **1,489,162,000/=** sawa na **asilimia 69.7** ya shilingi **666,855,000/=** zilizoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2018/2019. ***Kamati ilielezwa kuwa ongezeko hilo linatokana na kuongezeka kwa Watumishi (ajira), kupandishwa kwa mishahara ya Watumishi ambayo ilikuwa midogo pamoja na manunuzi ya magari 11.***

**Kielelezo Na. 5: Ulinganisho wa Bajeti (Fungu 46) kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na 2019/2020**



**Chanzo: Randama ya Wizara (2019) na Usanifu wa Kamati**

## SEHEMU YA TATU

---

### 4.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na uchambuzi huo na yale yaliyobainika, Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo yafuatayo:-

#### 4.1 Upatikanaji wa Fedha za Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mara nyingine tena Kamati inatoa Rai kuhusu hali ya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kama ilivyobainishwa kwenye uchambuzi wa Kamati, fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo zimekuwa zinatolewa kwa asilimia ndogo. **Kutokana na hali hii, Kamati inashauri fedha zilizotengwa katika bajeti ya mwaka 2018/2019 zitolewe zote kabla ya mwaka huu wa fedha 2018/2019 kuisha ili Wizara iweze kutekeleza Miradi hiyo. Aidha, Kamati inaona ni wakati sasa kwa Serikali kuamua kuchagua miradi michache ya kipaumbele na kuipatia fedha zote kuliko kutenga fedha ili hali tunajua kuwa fedha hizo haziwezi kutolewa. Ushauri huu umekuwa ukitolewa mara kadhaa.**

#### 4.2 Elimu Bila Malipo

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli kwa maamuzi yake ya kutoa Elimu bila malipo. Tunafahamu lengo hili la Rais ni kupanua wigo na kuondoa vikwazo vyote vya uandikishaji wanafunzi. Kamati imeshuhudia ongezeko kubwa la wanafunzi wanaoandikishwa katika Elimumsingi. Hata hivyo, ongezeko hili limekuwa na changamoto kutokana na Miundombinu finyu na uhaba wa Walimu. **Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuendelea kuboresha miundombinu ili wanafunzi waweze kusoma vizuri. Aidha, Kamati inashauri Serikali iendeleo kuajiri na kuboresha maslahi ya Walimu ili kuwapa morali ya kufundisha ongezeko hili la wanafunzi.**

#### 4.3 Uhaba wa Walimu Nchini

**Mheshimiwa Spika**, Changamoto ya uhaba wa Walimu ni kubwa. Kamati inapongeza jitihada za Serikali kuendelea kuajiri walimu kutoka Walimu **164,618** mwaka 2018 hadi kufikia Walimu **179,249** mwaka 2019. Pamoja na ongezeko hili la Walimu, Serikali inaendelea kutekeleza Mpango utaratibu wa Elimu Bila Malipo ambao nao unaendelea kuongeza idadi ya wanafunzi wanaoandikishwa kwenye Elimumsingi na Sekondari na hivyo kuhitaji uwepo wa Walimu wa kutosha.

**Mheshimiwa Spika**, Uhaba huu wa Walimu unaonekana zaidi katika maeneo ya vijijini kutokana na changamoto zilizopo katika maeneo hayo. **Kutokana na changamoto hii, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuajiri walimu wengi zaidi ili kutatua changamoto hii. Aidha, ili kuweza kuwavutia walimu kwenda kufundisha maeneo ya vijijini, Kamati inashauri motisha zaidi zitolewe kwa walimu hao ikiwemo kuwapatia nyumba za kuishi.**

#### 4.4 Muda wa kufanya Mitihani kwa wanafunzi wenye Ulemavu

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeelezwa kuwa kuna utaratibu umewekwa na Wizara wa kuwaongezea muda wa ziada wa kufanya mitihani kwa watoto wenye ulemavu. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa utaratibu huu haufahamiki kwenye shule nyingi hali inayowafanya wanafunzi hawa wenye ulemavu wafanye mitihani kwa muda ule ule sawa na wanafunzi wasio na ulemavu. **Kamati inashauri, Wizara ihakikishe utaratibu huu unafahamika kwa shule zote na kwa wanafunzi wenye ulemavu kwa kutoa elimu ili wanafunzi hawa wenye ulemavu wasikose haki yao ya Elimu.**

#### 4.5 Mfumo wa Elimu

**Mheshimiwa Spika**, Msingi bora wa Taifa lolote unatokana na Elimu bora. Kuanzia Mwaka 2016 Kamati imekuwa ikishauri kuhusu kuangaliwa kwa Mfumo wa Elimu nchini. Hata hivyo, ushauri huu bado haujatekelezwa kama ilivyoelezwa katika sehemu ya utekelezaji wa Maoni ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kushauri kuangaliwa upya kwa Mfumo wa Elimu kwani ina amini Mfumo wa Elimu ni chachu katika Maendeleo ya Taifa lolote. Mwanazuoni James Baldwin amewahi kusema “ *Education has assumed great importance in the new world. It makes a man a thinker, completes him as a person. And if this foundation is faulty, the system and society collapse in all entirety. It is high time that we understand the gravity of the situation to an education system*” .

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na umuhimu wa Elimu kwenye jamii na nchi kwa ujumla wake **Kamati inashauri Wizara (Serikali) isome Ripoti ya Tume iliyoundwa na aliyekuwa Rais wa Marekani Ronald Kegan ya Mwaka 1983 inayoitwa “A Nation at Risk” The Imperative for Educational Reform**” ambayo ilikuwa ndiyo historia ya mafanikio ya mfumo wa Elimu Marekani na kuiga yale mazuri yaliyomo kwenye Taarifa hiyo.

#### 4.6 Mitaala kuendana na Mapinduzi ya Nne ya Viwanda


**Mheshimiwa Spika**, Dunia yetu kwa sasa inaelekea kwenye Mapinduzi ya Nne ya Viwanda (**The Fourth Industrial Revolution – 4IR**). Kwa mujibu wa Profesa Klaus Schwab ambaye ni Mwanzilishi na Mwenyekiti wa Jukwaa la Dunia la Uchumi (**World Economic Forum - WEF**), dunia inaenda kuendeshwa kwa teknolojia ya hali ya juu ambapo roboti na mitambo ya kisasa itakuwa inafanya kazi zaidi kuliko nguvu ya binadamu. Si hivyo tu, lakini hata magari yatakuwa yanajiendesha yenyewe na kwa ujumla mfumo wa maisha ya mwanadamu utabadilika.

**Mheshimiwa Spika**, Mabadiliko haya pamoja na changamoto zake, inaelezwa kuwa ni fursa kwetu kama nchi kwani Dunia ina uwezo wa kuunganisha mabilioni ya watu zaidi kwenye mitandao endapo tu tutakuwa na uwezo wa kufanya hivyo.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu WEF, Mapinduzi ya Nne ya viwanda yanahimiza kufikiria ubunifu kuhusu uzalishaji, mnyororo wa thamani, usambazaji wa huduma kwa wateja


na mambo mengine ya namna hiyo. Hivyo basi, elimu yetu inapaswa kuangalia zaidi maeneo haya na kimkakati kama inavyooneshwa kwenye kielelezo Na. 6 (a-b)

**Kielelezo Na. 6a: Ujuzi unaotakiwa kuelekea 4IR**



*Chanzo: Word Economic Forum*

**Kielelezo Na.6b**



*Chanzo: Word Economic Forum*

**Mheshimiwa Spika**, ni kwa msingi huo, Kamati inashauri, Serikali kuanza kujiandaa na kuhakikisha Mitaala yetu ya elimu inazingatia mapinduzi haya kwa kutoa elimu ambayo itaongeza ujuzi na maarifa kwa wanafunzi ili kuweza kuendana na mapinduzi haya.

#### **4.7 Uthibiti Ubora wa Shule**

**Mheshimiwa Spika**, Nchi yetu ikiwa ni moja kati ya nchi 193 wanachama wa Umoja wa Mataifa inapaswa kutekeleza lengo Namba 4 la Maendeleo Endelevu ya Milenia (SDGs) la Elimu Bora (Quality Education) kupitia mipango yake . Kamati ina amini kuwa utekelezaji wa lengo hili ambalo linaisitiza kuhusu Elimu Bora unategemea mambo mengi ikiwemo uthibiti Ubora wa Shule. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa upatikanaji wa fedha kutokana na bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Idara hii kwa Mwaka 2018/2019 haukufika hata **asilimia 30** ya bajeti.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri fedha za Uthibiti Ubora wa Shule zitolewe zote kabla ya mwaka huu wa fedha kuisha na pia kuanzia sasa Serikali ihakikishe fedha zote zinazotengwa kwa ajili ya uthibiti Ubora wa Shule zinatolewa zote na kwa wakati.

#### **4.8 Stahiki za Wahadhiri wa Vyuo Vikuu**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua umuhimu Elimu ya Juu ambapo Wahadhiri na Watumishi wengine ni nyezo muhimu katika utoaji wa Elimu. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa kuna changamoto ya Wahadhiri na Watumishi hawa wa Vyuo Vikuu kutolipwa stahiki zao zikiwemo posho za nyumba. Changamoto hii imepelekea baadhi ya Wahadhiri kuzuia matokeo ya mitihani lakini Kamati inaona kuna hatari ya kutokea mgomo baridi.

***Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha maslahi ya Wahadhiri hawa na Watumishi wa Vyuo Vikuu, hususan posho ya nyumba, inatolewa mapema ili kuepuka madhara yoyote ambayo yanaweza kutokea.***



**4.9 Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza jitihada zinazofanywa na Serikali za kuongeza idadi ya wanafunzi wanaopata Mikopo ya Elimu ya Juu. Tumeshuhudia Bajeti ya Bodi ya Mikopo imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka kutoka shilingi **Bilioni 427.5** mwaka 2017/2018 hadi kufikia **Bilioni 450** mwaka 2019/2020 kiasi ambacho kitasaidia kuongeza idadi ya wanafunzi wapatao 6000. Hata hivyo, Kamati inafahamu changamoto zinazoikumba Bodi ya Mikopo pamoja na wanafunzi na hivyo inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

a) Kwa kuwa baadhi ya wanafunzi wamekuwa wakikosa mikopo kwasababu mbalimbali ikiwemo kukosa vielelezo, ***Kamati inashauri Bodi ishirikiane na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) ili kubaini wanafunzi wanaostahili kupewa mikopo lakini pia kurejesha baada ya kunufaika;***

b) Kwa kuwa Wanafunzi wengi wamekuwa wakichelewa kupata fedha za mikopo hasa za kujikimu kutokana na baadhi ya Vyuho kuwa na changamoto zake zikiwemo za madeni katika Mabenki, hali inayopelekea kuzuiliwa kutoa fedha kwenye Benki hizo. ***Kamati inaona jambo hili si jema na hivyo inashauri fedha za kujikimu wanafunzi kutoka Bodi ya Mikopo ziwekwe moja kwa moja kwenye akaunti za wanafunzi ili kuepuka changamoto hii;*** na

c) Kama ambavyo imeonekana kwenye uchambuzi wa Kamati, kati ya bajeti yote inayotengwa kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo ya Wizara ipatayo 41, **asilimia 62** ni fedha za Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Kamati inaona fedha za Bodi zinaifanya Wizara ionekane inapewa fedha nyingi za Miradi ya Maendeleo wakati kiuhalisi siyo kweli kwani **asilimia 40** ndo inabaki kutekeleza Miradi zaidi ya 40. **Kamati inashauri kwa mara nyingine tena Serikali kuipa Bodi ya Mikopo Fungu lake (Separate vote).**

#### **4.10 Tume ya Vyuho Vikuu (TCU)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kazi za Tume ya Vyuho Vikuu (TCU) ni pamoja na kusimamia na kuthibiti ubora wa

Elimu ya Juu na kufanya maboresho, kufanya udahili wa wanafunzi na kuratibu uhamisho wa ndani wa wanafunzi pamoja na kufanya ukaguzi wa vyuo Vikuu. Hivi karibuni TCU ilifanya ukaguzi wa kushtukiza katika vyuo nane na kuvifungia kufanya udahili kutokana na mapungufu waliyoyabaini katika utoaji wa Elimu. Kamati ilielezwa kuwa baadhi ya vyuo vimeshindwa kulipa mishahara ya walimu (Wahadhiri) hali iliyopelekea walimu hao kuzuia kutoa matokeo ya mitihani.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza juhudi hizi zilizofanywa na TCU lakini inaona hatua zimechelewa kuchukuliwa hali ambayo imeathiri wanafunzi wengi wasio na hatia kutokana na vyuo hivyo kufungwa. **Kamati inashauri ili kuepuka kufungia vyuo ni vyema TCU ikawa inavifuatilia kwa ukaribu na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika Vyuo vyote nchini ili kubaini mapungufu mapema na kushirikiana nao kufanya maboresho.**

#### 4.11 Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH)

**Mheshimiwa Spika**, nchi yetu ikiwa inaelekea kwenye Uchumi wa Kati na Uchumi wa Viwanda. Hivyo, kuna kila sababu ya kuiwezesha COSTECH ili iweze kusaidia katika ubunifu wa masuala mbalimbali. Pia tumeona hapo awali kwenye Taarifa hii kuwa Dunia inaelekea kwenye Mapinduzi ya Nne ya Viwanda (4IR) ambapo teknolojia ya hali ya juu inaanza kutumika. Kutokana na umuhimu wa COSTECH kuelekea kwenye Mapinduzi hayo, **Kamati inashauri Bajeti ya Taasisi hii iongezwe ili iweze kutekeleza majukumu yake ya sayansi, teknolojia na ubunifu kwa Maendeleo ya Taifa.**

#### 4.12 Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA)

**Mheshimiwa Spika**, Nchi yetu ikiwa inaelekea kwenye Uchumi wa Kati wa Viwanda uzalishaji wa Mafundi Mchundo ni muhimu sana. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuendelea kujenga na kukarabati vyuo mbalimbali vya ufundi ili kuongeza idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa. **Ni rai ya Kamati kuwa, vyuo hivi vya Ufundi**

**Stadi pamoja na majukumu yake mengine, ni wakati sasa vijielekeze katika kuzalisha mafundi mchundo ambao ni nyenzo muhimu katika uchumi wa Viwanda.**

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, kwa mara nyingine napenda kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa hii ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu. Kipekee nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano wanaoutoa ikiwa ni pamoja na kuonesha weledi wakati wa kuchambua Bajeti ya Wizara. Naomba kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Peter Joseph Serukamba, Mb	Mjumbe
2. Mhe. Juma Selemani Nkamia, Mb	Mjumbe
3. Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb	Mjumbe
4. Mhe. Hussein Mohamed Bashe, Mb	Mjumbe
5. Mhe. Rose Cyprian Tweve, Mb	Mjumbe
6. Mhe. Grace Victor Tendega, Mb	Mjumbe
7. Mhe. Peter Ambroce Lijualikali, Mb	Mjumbe
8. Mhe. Bernadetha K. Mushashu, Mb	Mjumbe
9. Mhe. Vicky Paschal Kamata, Mb	Mjumbe
10. Mhe. Deogratius Francis Ngalawa, Mb	Mjumbe
11. Mhe. Amina Nassoro Makilagi, Mb	Mjumbe
12. Mhe. Khalifa Mohamed Issa, Mb	Mjumbe
13. Mhe. Susan Anselm Lyimo, Mb	Mjumbe
14. Mhe. John Peter Kadutu, Mb	Mjumbe
15. Mhe. Mgeni Jadi Kadika, Mb	Mjumbe
16. Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi, Mb	Mjumbe
17. Mhe. Khamis Yahya Machano, Mb	Mjumbe
18. Mhe. Mch. Dkt. Getrude Rwakatatare, Mb	Mjumbe
19. Mhe. Seleman Said Bungara, Mb	Mjumbe
20. Mhe. Kabwe Zuberi Ruyagwa Zitto, Mb	Mjumbe
21. Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mb	Mjumbe
22. Mhe. Joseph Leonard Haule, Mb	Mjumbe
23. Mhe. Oscar Rwegasira Mukasa, Mb	Mjumbe
24. Mhe. Maulid Ally Mtulia, Mb	Mjumbe
25. Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia, Mb	Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, nakushukuru na kukupongeza uongozi thabiti ulionao katika kuendesha Bunge letu. Nawashukuru na kuwapongeza pia Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yenu.

**Mheshimiwa Spika**, namshukuru sana Prof. Joyce Ndalichako (Mb)-Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. Ole Tata Nasha (Mb) - Naibu Waziri, Dkt. Leonard Akwilapo - Katibu Mkuu, Prof. James Mdoe- Naibu Katibu Mkuu na Dkt. Ave Maria Semakafu Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa utendaji kazi wao na mashirikiano yaliyopo na Kamati yetu.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee namshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vizuri. Napenda pia kumshukuru Ndg. Athumani B. Husseni, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, na Ndg. Dickson Bisile Mkurugenzi Msaidizi anayesimamia Kamati yetu kwa ushirikiano na ushauri wanaoipa Kamati. Aidha, nawashukuru sana Makatibu wetu wa Kamati Ndg. Pamela Pallangyo na Ndg. Agnes Nkwera kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kutoa msaada wakati wote unapohitajika. Pamoja nao wanawashukuru Watumishi wote wa Bunge kwa utendaji kazi wake mzuri unaosaidia Kamati kutekeleza majukumu yake vizuri ikiwemo kukamilika kwa Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, napenda kuwashukuru wadau wote wa elimu ikiwemo UNDP kupitia Mradi wa LSP unaoendeshwa na Ofisi ya Bunge kwa Elimu ambayo imekuwa ikiwezesha Kamati kupata uelewa wa masuala mbalimbali kutokana na mafunzo ambayo yamekuwa yakitolewa. Mafunzo hayo yamewezesha Kamati kutekeleza majukumu yetu ya Kibunge kwa ufanisi. Aidha, Kamati inawashukuru wadau wote wa Elimu ambao wamekuwa wakifanya kazi na Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Kamati, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali, liridhie na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na

Teknolojia (Fungu 46) kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 shilingi 1,357,106,983,260/= na Tume ya UNESCO (Fungu 18) shilingi 2,156,017,000/= kama yalivyowasilishwa na Mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha, ninaunga mkono Hoja.

Juma S. Nkamia, Mb  
**MAKAMU MWENYEKITI**  
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA**  
**MAENDELEO YA JAMII**  
29 APRILI, 2019

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Juma Nkamia kwa Taarifa ya Kamati na kwa jinsi ulivyoiwasilisha vizuri. *(Makoff)*

Tusikie sasa taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa Wizara hii ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Mheshimiwa Susan Anselm Jerome Lyimo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Napenda kuanza hotuba yangu kwa kunukuu sehemu ya mahubiri ya Askofu Almachius Vincent Rweyongeza wa Jimbo Katoliki la Kayanga Mkoani Kagera wakati wa ibada ya Ijumaa Kuu tarehe 19 Aprili, 2019 kwa ajili ya kujenga msingi wa hoja nitakazozitoa kuhusu mfumo wa elimu hapa nchini. Akinukuu maneno aliyoyasoma katika Geti la Chuo Kikuu fulani ambacho hakukitaja jina alisema:

*“Ukitaka kuangamiza Taifa lolote, huhitaji kutumia silaha za nuclear au atomic. Njia nzuri ya kuangamiza Taifa ni kuharibu Mfumo wa Elimu. Ruhusu mbumbumbu waonekane kuwa wamefaulu na wasonge mbele hadi vyuo vikuu; matokeo yake yatajidhihirisha baada ya muda. Mbumbumbu hao wakishahitimu, kwa kupata vyeti hewa,*

*vyeti feki, wagonjwa watafia mikononi mwa Madaktari na Manesi, majengo yataporomoka mikononi mwa Wahandisi, pesa zitapotelea mikononi mwa Wachumi na mafisadi, utu utapotea mikononi mwa Viongozi wa Dini na Serikali na haki itapotea mikononi mwa Mahakimu na Wanasheria.*” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Askofu Rweyongeza alihoji, kama mfumo wetu wa elimu ni kama biashara au ni haki ya elimu bila wajibu. Msingi wa swali hili ulitokana ukweli kwamba, mfumo wetu wa elimu umeyumba sana kutokana na kubadilishwa badilishwa kwa sera na miongozo ya elimu jambo ambalo linaashiria kwamba; Watanzania kama Taifa bado hatujui tunachokitaka hatujui rasilimali watu wetu wawe na sifa gani na hatujui tunataka Taifa letu la leo na kesho liweje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baba Askofu alisisitiza kwamba, tunahitaji elimu bora kama taifa itakayomwezesha mwanafunzi kukabiliana na changamoto za maisha ya kila siku nje ya darasa. *(Not for school we learn but for life).*

Nimeona ninukuu sehemu ya homilia hiyo ya Baba Askofu pengine Serikali itasikia na kufanyia kazi kwa kuwa, kwa zaidi ya miaka kumi iliyopita Kambi Rasmi ya Upinzani imekuwa ikiishauri Serikali hii juu ya hatari ya kupuuza ushauri wa wataalam kuhusu mfumo wa elimu, lakini badala yake imekuwa ikifanya maamuzi ya kisiasa kuhusu elimu kwa malengo ya kupata kura katika chaguzi. Maamuzi kama vile kushusha viwango vya ufaulu, kutoa elimu bila ada, ni maamuzi ya kisiasa, ambayo hayakufanyiwa tafiti kujua athari zake kwa mfumo mzima wa elimu baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ongezeko la Idadi ya Watu na Athari zake katika Ubora wa Elimu Nchini; kutokana na ongezeko kubwa la idadi ya watu Afrika hasa kusini mwa Jangwa la Sahara, kazi kubwa ya kuhakikisha ubora wa elimu kwa wote limekuwa ni hitaji kubwa kuliko wakati mwingine wowote. Hali hiyo imekuwa janga kwa kuwa zaidi ya nusu ya

watoto ambao hawajaandikishwa shule wanaishi katika nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Mheshishimiwa Mwenyekiti, ongezeko hili la watu linaonekana pia Tanzania kwa ukuaji wa asilimia 2.7 kwa mwaka ambapo inakadiriwa kwamba, ifikapo mwaka 2036 Watanzania tutakuwa takribani milioni 90. Hivyo basi, kwa ukuaji huu usioendana na kasi ya uboreshaji na upanuzi wa miundombinu ya elimu, Tanzania itaendelea kukumbwa na ugumu wa kutoa elimu bora kwa wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya juhudi zilizofanywa, utoaji wa elimu bila malipo au bila ada hautoshi. Ubora wa elimu hapa nchini umelalamikiwa mara nyingi kuwa unaporomoka na hauridhishi kabisa. Aidha, watoto wanaohitimu katika ngazi za elimu ya msingi na sekondari wamekuwa na uwezo mdogo katika ujuzi na maarifa kutokana na kile kinachoitwa kupikwa nusu nusu na hivyo kushindwa kuingia katika soko la ajira au kuendelea na elimu ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na matatizo ya mitaala, utafiti wa uwezo wa mwaka 2017 unaonesha kwamba, uwezo wa kusoma na kuhesabu miongoni mwa wanafunzi wa shule za msingi bado uko chini ya kiwango kinachohitajika na mitaala. Hali hii imesababishwa na uwezo mdogo pia wa walimu kufundisha. Kwa mujibu wa Ripoti ya Benki ya Dunia ya mwaka 2014, walimu wengi wanakosa ujuzi na mbinu za kielimu za kufundisha. Ripoti hiyo inaonesha kuwa ni moja ya tano tu, yaani asilimia 20 tu ya Walimu wanaweza kumudu mitaala wanayofundisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto hizo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haitachoka kuishauri Serikali kuwa na mikakati mahsusi ya kuboresha mitaala kwa kuwashirikisha walimu ambao ndio wafundishaji, pamoja na kuwapatia mafunzo ili waweze kufundisha mitaala hiyo kwa weledi na hivyo kupandisha viwango vya ubora wa elimu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Upungufu wa Kutisha wa Walimu Katika Shule za Msingi na Sekondari. Kambi Rasmi ya Upinzani kwa zaidi ya miaka kumi iliyopita, imekuwa ikiikumbusha Serikali hii ya CCM kwamba, hakuna elimu bila walimu. Sarakasi na mbwembwe zote za kisiasa za elimu bure, elimu bila malipo na sasa elimu bila ada hazitasaidia chochote kama hakuna idadi ya kutosha ya Walimu wenye weledi na motisha wa kufanya kazi ya kufundisha; upungufu umeoneshwa kuanzia Aya ya 16 hadi ya 23.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa takwimu za *BEST* ambacho ni kitabu cha Serikali, idadi ya Walimu kwa shule za msingi imeshuka kutoka Walimu 191 mwaka 2016 hadi kufikia laki moja na sabini na tisa mwaka 2017 ikiwa ni anguko la asilimia takribani asilimia 6.5.

Aidha, katika shule za awali idadi imepungua ya walimu kutoka 1948 na kufanya uwiano wa mwalimu na wanafunzi kuongezeka kutoka Mwalimu mmoja kwa wanafunzi 135 mwaka 2016 hadi Mwalimu mmoja kwa walimu 159 mwaka 2017, badala ya ile ya Mwalimu mmoja kwa wanafunzi 25. Kwa uwiano huu hatutegemei kuona kwamba, kuna ubora wa elimu na watoto wetu wataendelea kufeli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni rai ya Kambi ya Upinzani Bungeni kwamba Serikali iongeze kasi ya kuajiri Walimu maradufu ili waendane na wimbi kubwa la wanafunzi wanaojunga na elimu ya awali na msingi. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kupitia Wizara zinazohusika na elimu kutengeneza mpango wa bajeti wa miaka mitano kwa ajili ya ajira ya Walimu ili kutatua kabisa tatizo la upungufu wa Walimu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa Walimu umevikumba pia vyuo vya ufundi stadi hasa ikizingatiwa pia, kuna mpango maalum wa Serikali kujenga Vyuo vya *VETA* kila wilaya na kila mkoa huku tukitegemea chuo kimoja tu cha Walimu. Kwa hiyo, tunashauri Serikali pia, izingatie ushauri huo wa kujenga vyuo vya ualimu wa *VETA*.



Mheshimiwa Mwenyekiti, Uhaba mkubwa wa Miundombinu katika Shule za Msingi na Sekondari; mazingira bora ya kufundisha na kujifunza yanategemea sana uwepo wa miundombinu rafiki na wezeshi. Ni jambo ambalo haliwezekani kutegemea kupanda kwa ubora wa elimu ikiwa hakuna jitihada zozote za kuboresha miundombinu itakayosaidia zoezi la kufundisha na kujifunza kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba wa miundombinu una uhusiano mkubwa sana na kushuka kwa viwango vya ubora wa elimu. Kwa mujibu wa takwimu za *BEST*, mwaka 2016 na 2017 ni kwamba, uhaba wa maktaba katika shule za msingi umeongezeka kutoka asilimia 88 hadi kufikia asilimia 91 mwaka 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu hizo zinaonesha pia kwamba; upungufu wa maabara katika shule za sekondari kwa mfano kwa bailojia ni asilimia 51.5, fizikia asilimia 54 na kemia asilimia 43. Takwimu hizo pia zinaonesha kwamba, kuna upungufu wa nyumba za Walimu 186,000 sawa na asilimia 83, upungufu wa majengo ya utawala 10,943 sawa na asilimia 83. Vilevile Ripoti ya Benki ya Dunia mwaka 2016 inaonesha kwamba ni asilimia 41 tu ya shule za msingi na sekondari nchini Tanzania zenye miundombinu inayokidhi viwango vinavyotakiwa; hii ina maana kwamba, asilimia 59 hakuna kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu nilizozitaja hapo juu pia, zinatiliwa nguvu na Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka wa fedha 2016/2017 inayoonyesha kwamba shule za msingi zina upungufu wa madarasa asilimia 85, upungufu wa vyoo asilimia 66 na upungufu wa nyumba za Walimu asilimia 14. Kwa upande wa sekondari kuna upungufu wa vyumba vya madarasa asilimia 52, upungufu wa maabara asilimia 84 na upungufu wa madawati asilimia 86. Nataka tu nichomekee kwamba kwa hii nyongeza ya elimu bure maana yake tunaendelea kuwa na upungufu mkubwa wa madarasa, Walimu pamoja na nyumba zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nchi washirika wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wako kwenye mpango wa kuwapatia wanafunzi wote wa shule za msingi kompyuta mpakato (*laptops*) sisi Tanzania bado tunazungumzia uhaba wa matundu ya vyoo. Ni aibu sana kwa Serikali hii inayojitapa kwamba inatoa elimu bure wakati mazingira ya kutolea elimu hiyo ni mabaya na yanachangia kwa kiwango kikubwa kushuka kwa ubora wa elimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inafahamu upungufu huu kwa kuwa takwimu zilizotumika ni za Serikali. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inafahamu kwamba ni vigumu kutatua changamoto zote zilizoainishwa katika taarifa ya CAG kwa wakati mmoja. Hata hivyo, tunashauri na kupendekeza kwamba Serikali iwe na mpango wa kutenga bajeti kila mwaka wa fedha kwa ajili ya kupunguza upungufu wa miundombinu ulioonekana hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanzia, Kambi Rasmi ya Upinzani ingependa Serikali itoe taarifa mbele ya Bunge lako Tukufu kuhusu shilingi bilioni 29 zilizotolewa ahadi na Mheshimiwa Jafo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI kwamba fedha hizo zingejenga madarasa 478 na mabweni 269 kwa ajili ya wanafunzi 21,000 wa elimu ya sekondari ya juu yaani kidato cha tano na cha sita ambao walifaulu lakini wakakosa maeneo ya kwenda. Kwa hiyo, tulitaka kwanza tuanzie hapo, tujue tamko hilo kama limetekelezwa na limetekelezwa kwa kiasi gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupungua kwa bajeti ya sekta ya elimu. Tofauti na wakati wa utawala wa Serikali ya Awamu ya Nne ambapo bajeti ya sekta nzima ya elimu ilikuwa ikiongezeka kila mwaka, bajeti hiyo sasa imekuwa na mserereko wa kushuka kwa miaka mitatu mfululizo tangu Serikali ya Awamu ya Tano iingie madarakani. Mathalan, bajeti hiyo ilipungua kutoka shilingi trilioni 4.77 mwaka 2016/2017 hadi kufikia shilingi trilioni 4.7 mwaka 2017/2018 na ikazidi kupungua hadi kufikia shilingi trilioni 4.6 mwaka 2018/2019. Aidha, uwiano wa bajeti ya sekta ya elimu ukilinganisha na

bajeti kuu ya Serikali umekuwa ukipungua licha ya bajeti ya kuu ya Serikali kuongezeka kwa miaka yote mitatu mfululizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi uliofanywa na Shirika la Haki Elimu kuhusu mwenendo wa bajeti ya sekta ya elimu unaonyesha kwamba uwiano wa bajeti ya sekta ya elimu na bajeti kuu ya Serikali ulishuka kutoka asilimia 16 mwaka 2016/2017 hadi asilimia 15 mwaka 2017/2018 na baadaye tena hadi asilimia 14 mwaka 2018/2019. Mwenendo huo wa kupungua unazidi kutupeleka mbali na Azimio la Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara – Tanzania ikiwemo, la kutenga asilimia 20 ya bajeti kuu ya Serikali na kuipeleka kwenye sekta ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuinyima sekta ya elimu takriban shilingi trilioni 4 ndani ya miaka mitatu bila shaka changamoto zinazoikabili sekta ya elimu hususan za upungufu wa miundombinu wa walimu na vifaa vya kufundishia zingepungua sana kama siyo kumalizika kabisa. Upangaji huu wa bajeti ya sekta ya elimu chini ya asilimia 20 unakwenda kinyume na makubaliano ya Kikanda na Kimataifa ambayo nchi imeridhia ikiwemo *Dakar Framework for Action on Education for All, 2000* na *Incheon Declaration and Framework for Action, 2015*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa bajeti ya Wizara ya Elimu pekee, bajeti hiyo pia imepungua kutoka shilingi trilioni 1.4 kwa mwaka 2018/2019 hadi shilingi trilioni 1.357 kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Upungufu huu ni wa shilingi bilioni 51. Uchambuzi wa randama ya Wizara ya Elimu kwa mwaka 2018/2019 na 2019/2020 unaonyesha kwamba pamoja na kupungua kwa bajeti nzima ya Wizara, bajeti ya matumizi ya kawaida imekuwa ikiongezeka wakati ile ya miradi ya maendeleo imekuwa ikipungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, bajeti ya matumizi ya kawaida imeongezeka kutoka shilingi bilioni 478 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 hadi shilingi bilioni 494 kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Kwa upande wa bajeti ya maendeleo ya Wizara, bajeti hiyo imepungua kutoka shilingi

bilioni 929 mwaka jana hadi kufikia shilingi bilioni 863 kwa mwaka huu, sawa na punguzo la shilingi bilioni 67. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa maelezo ni kwa namna gani itaweza kutekeleza miradi halisi ya maendeleo ikiwa bajeti ya maendeleo imekuwa na mserereko wa kupungua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji duni wenye mashaka makubwa katika miradi ya maendeleo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imefanya uchambuzi wa utekelezaji wa miradi halisi ya maendeleo katika sekta kwa miaka miwili mfululizo ma kugundua kwamba, ipo miradi ambayo imekuwa ikitengewa fedha za maendeleo lakini fedha hizo zimekuwa hazipelekwi kabisa na kama zikipelekwa ni kwa kiasi kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa miradi ambayo haikupata fedha kabisa za utekelezaji licha ya kutengewa bajeti ni kama inavyoonekana katika aya ya 46 hadi 49. Jambo la kushangaza katika miradi ya maendeleo 41 yenye thamani ya takribani shilingi bilioni 929, miradi 24 yenye thamani ya takribani shilingi bilioni 100 haikupatiwa hata senti moja kwa ajili ya utekelezaji wa miradi yake. Ni ukweli usiopingika kwamba kutotekelezwa kwa miradi hii muhimu kutachangia sana kushuka kwa ubora wa elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani haina mgogoro na Serikali juu ya matumizi ya fedha za nje katika kutekeleza miradi ya maendeleo. Ila jambo la msingi ambalo Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa angalizo ni katika kupanga miradi ipi itekelezwe na fedha za nje na miradi ipi itekelezwe na fedha za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani imeshtushwa sana kuona miradi mingi ya maendeleo katika sekta ya elimu ambayo ndiyo moyo wa maendeleo ya sekta nyingine zote ikitengewa asilimia sifuri ya fedha za ndani na kubaki tegemezi kwa fedha za nje. Miradi tisa ya maendeleo iliyopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha imeelezwa

katika aya hii. Kitendo cha Serikali kupanga bajeti ya miradi ya maendeleo katika sekta ya elimu kwa kutumia fedha za nje ni kuiweka elimu yetu rehani na kwa maneno mengine ni kuliangamiza taifa kwa kuwa mafanikio ya sekta nyingine zote yanategemea sana ukuaji na ubora wa sekta ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hayati Baba wa Taifa, alisema “Kupanga ni Kuchagua”. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haioni mantiki yoyote ya Serikali hii ya CCM kuchagua miradi muhimu kama vile Mafunzo ya KKK – ambayo ndio moyo wa Elimu Msingi itekelezwe kwa fedha za nje. Aidha, hakuna mantiki yoyote miradi ya utafiti katika elimu na kuendeleza elimu ya ualimu na ule wa huduma ya maji ikiwa ni pamoja na ujenzi wa vyoo kutegemea fedha za nje. Haiwezekani vyoo kwa ajili ya watoto wetu vitegemee nje na ndiyo sababu kumekuwa na matatizo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vitu ambavyo Serikali hii haitakiwi kuvifanyia majaribio ni sekta ya elimu. Madhara si ya muda mfupi ni ya muda mrefu kama ambavyo nimesema. Ndiyo sababu tunaweza tukaona kwamba madaktari na leo pia nimesikia asubuhi kwamba kuna daktari mmoja nadhani ni feki ambaye amesababisha kifo cha mtu kule Tabora. Kwa hiyo, haya ni mambo ambayo tunaweza tukaona kwamba ni kwa sababu gani tunatetea ubora wa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, nichomekee pia kwamba hata hivi majuzi Mheshimiwa Waziri nadhani anajua, Mkuu wa Mkoa wa Mara amefunga shule kule Butiama eti kwa kuwa mtoto amebakwa, kwa hiyo, shule imefungwa kwa mwezi mzima na hivi wazazi wanataka kuandamana. Kwa hiyo, nadhani hilo nalo linachangia sana kushusha ubora wa elimu kwa wanasiasa kufanya kazi ambazo siyo zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkopo wa elimu ya juu na ruzuku kwa shule. kutokana na mabadiliko ya kiuchumi yaliyopelekea kupanda kwa gharama za maisha, kiasi cha ruzuku ya Sh.10,000 na Sh.25,000 haziwezi tena kukidhi

mahitaji kwa kuwa fedha hizi zilikuwa zimetengwa mwaka 2001. Hivyo, ni rai ya Kambi ya Upinzani kuona kwamba fedha hizo zinaongezwa au kama ni dola iwe dola kwa *rate* ya sasa hivi ambayo ni Sh.2,300. Kwa hiyo, tunashauri kwamba *capitation fee* iwe Sh.25,000 na Sh.50,000 kwa sekondari. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa elimu ya juu, Kambi Rasmi ya Upinzani kwa miaka mingi, imekuwa ikitaka Serikali kutochanganya fedha za mikopo ya elimu ya juu katika fedha za maendeleo. Hii ni kwa sababu fedha hizo huonekana kuwa ni nyingi lakini kumbe zote zinakwenda kutoa mikopo ya elimu ya juu na ile miradi halisi ya maendeleo inakosa fedha. Kwa mfano, tumeona kwamba kwa mwaka huu tu shilingi bilioni 427 sawa na asilimia takribani 45.6 ambayo ni 46 zimekwenda Bodi ya Mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo linazidi kuwa kubwa kwa kuwa fedha za mikopo ya elimu ya juu zinazidi kuongezeka na kuiacha miradi halisi ya maendeleo. Kwa mfano, fedha za mwaka huu, bajeti nzima ya maendeleo ni shilingi bilioni 863 na kati ya hizo shilingi bilioni 450 ni fedha za mikopo ya elimu ya juu sawa na asilimia 52 ya bajeti ya maendeleo huku kiasi cha shilingi bilioni 413 sawa na asilimia 48 kikibaki kwa ajili ya utekelezaji wa miradi halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuondoa mkanganyiko huo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kama ambavyo Kamati imeshauri lianzishwe Fungu maalum kama Tume ya *UNESCO* kwa sababu ukiangalia Tume ya *UNESCO* ina shilingi bilioni 2 tu lakini ina fungu lake wakati hii ina takribani shilingi bilioni 500 lakini haina fungu. Kikubwa zaidi tunachozungumzia ni kwa sababu gani fedha hizi ziwekwe kwenye maendeleo wakati ni sawa tu na mishahara sababu zile hela ni za chakula, malazi na *tuition*. Kwa hiyo, tunafikiri kwamba ni lazima kuwe na fungu lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba fedha hizo zinaenda, tumepata pia taarifa kwamba baadhi ya vyojo wanachelewa kuwapa wanafunzi fedha hizo pamoja na

kwamba Bodi inapeleka na matatizo haya yanapelekea wanafunzi kupata kadhia mbalimbali. Vilevile vyuo vingine vimekuwa na masharti mbalimbali ya kuwalipa wanafunzi fedha zao. Kwa hiyo, tunashauri Serikali kupitia hasa vyuo binafsi waangalie tatizo lipo wapi ili waweze kutatua tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu kwa mtoto wa kike. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikipigia kelele suala la kupanga bajeti kwa kuzingatia masuala ya jinsia (*gender budgeting*). Jitihada hizo ni pamoja na taulo za kike ambapo Kambi ya Upinzani ilipeleka hoja binafsi kuhusiana na suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na dhamira hiyo njema ya Serikali kutoa VAT kwenye *pads* kumekuwa na mwitiko mdogo sana wa utekelezaji wa maagizo hayo ya Serikali. Bado bei ya taulo za kike imebaki kuwa ya wastani wa Sh.2,000; gharama ambayo imekuwa ni vigumu kwa familia maskini kumudu. Hivyo, inapelekea baadhi ya watoto wa kike hasa wanaotoka familia maskini kushindwa kwenda shuleni kwa takribani mwezi mmoja katika miezi kumi ambayo wanakuwa darasani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Kambi Rasmi ya Upinzani kutambua kusudio la Serikali kuwapatia wanafunzi wa kike taulo hizo za kujisitiri, tunashauri na kupendekeza kwamba Serikali iwe inatenga bajeti maalum kwa ajili ya kununua taulo hizo na kuzipeleka shuleni moja kwa moja. Bajeti hiyo inaweza kuongezwa kwenye ruzuku inayokwenda shuleni (*Capitation Grants*) kwa sababu tunatambua kwamba watoto ambao ni *adolescent girls* sio wengi kiasi hicho hasa ukizingatia wanaanza shule wakiwa wadogo, tulidhani ikienda kule itakuwa na maana zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, motisha kwa Wakaguzi wa Elimu unaotolewa kwa ubaguzi. Mwaka 2014, Serikali ilitoa Waraka wa Watumishi wa Serikali Na.3 wa mwaka 2014 kuhusu mishahara na posho ya madaraka kwa viongozi wa elimu nchini. Waraka huo ulikuwa ni juu ya uamuzi wa Serikali

wa kuwaingiza Wakaguzi Wakuu wa Shule wa Wilaya na Kanda katika Muundo wa Mshahara wa Viongozi wa Serikali (LSS – E) na kulipa posho ya madaraka kwa Wakuu wa Shule za Msingi na Sekondari, Wakaguzi wa Elimu Kata na Wakuu wa Vyuo vya Ualimu nchini na kuwaweka pembeni Wakaguzi Wakuu wa Shule wa Wilaya na Kanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutumia uzoefu mdogo tu, hivi kati ya Mratibu wa Elimu wa Kata na Mkaguzi wa Shule wa Wilaya na Kanda ni nani mwenye majukumu makubwa ambaye angestahili kulipwa posho hiyo ya madaraka? Ikiwa hawa wametengwa katika kupewa motisha, kuna hatari kubwa ya kuporomoka kwa ubora wa elimu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili ni lini itawaingiza Wakaguzi Wakuu wa Shule wa Wilaya na Kanda katika utaratibu wa kulipwa posho ya madaraka. Kwa sababu tunaamini kabisa kwamba wakiwapa posho hii ya madaraka itaongeza ubora katika elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa ugunduzi na ubunifu katika elimu. Maendeleo yoyote ya kisayansi na kiteknolojia ambayo ndiyo msingi wa maendeleo ya kiuchumi katika taifa lolote unategemea sana kiwango cha ugunduzi na ubunifu unaotokana na elimu bora. Ugunduzi na ubunifu ni zao la tafiti za kisayansi, tafiti ambazo huleta majibu ya changamoto mbalimbali zinazoikabili jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tafiti hizo zifanyike rasilimali fedha inahitajika. Mataifa yaliyoendelea katika nyanja za sayansi na teknolojia yamewekeza sana katika tafiti. Kwa maneno mengine, ili Tanzania iweze kuwa na wagunduzi na wabunifu wazuri tunahitaji kama taifa kuwekeza sana katika tafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ukweli huo, Serikali hii ya CCM imekuwa haitengi fedha kwa ajili ya tafiti jambo ambalo linazidi kudumaza viwango vya ubunifu na ugunduzi na yamkini uchumi wetu umeendelea kushuka.



Nathubutu kusema hivyo kwa sababu katika bajeti ya mwaka 2018/2019 Mradi Na.6345 ambao ni Mfuko wa Utafiti na Maendeleo wa *COSTECH* ulitengewa shilingi bilioni 9.8 lakini mpaka naandika hotuba hii fedha hizo hazijatolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/2017 – 2020/2021, Serikali ilijiwekea kiwango cha kutenga asilimia moja (1%) ya Pato Ghafi la Taifa (*GDP*) kwa ajili ya shughuli sayansi, teknolojia na ugunduzi. Hata hivyo, Serikali haijawahi kutenga kiasi hicho tangu imejiwekea utaratibu huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pato Ghafi la Taifa kwa sasa ni Dola za Kimarekani bilioni 52.09 ambazo ni sawa na Sh. 119,807,000,000,000. Hii ina maana kwamba ikiwa Serikali ingefuata utaratibu iliyojiwekea wa kutenga asilimia moja ina maana kwamba *COSTECH* leo inhekuwa inapata trilioni 1.198 na hii ni kwa sababu *COSTECH* ndio inasimamia tafiti katika vyuo vyote nchini na kwa hiyo ilipewa jukumu hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha iliyotengwa kwa Tume ya Sayansi na Teknolojia (*COSTECH*) kwa ajili ya tafiti kwa mwaka huu wa fedha ni shilingi bilioni 7.574 sawa na asilimia 0.00632. Hiki ni kiwango kidogo kuliko vyote tangu Serikali hii ya Awamu ya Tano iingie madarakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa tafiti katika kukuza na kuendeleza sayansi na teknolojia, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kupitia CHADEMA imeeleza bayana katika Sera yake ya Elimu, sura ya 6.1 inayosema kwamba: "CHADEMA inaamini kwamba msingi wa ugunduzi na ubunifu katika elimu unajengwa katika tafiti za kisayansi. Kwa hiyo, kwa kushirikiana na sekta binafsi, CHADEMA itawekeza kikamilifu katika elimu ya utafiti kuanzia elimu ya awali ili kumjengea mtoto uwezo wa ubunifu". *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya siasa katika vyuo vikuu na katazo la Serikali kwa wanafunzi wa vyuo vikuu kujihusisha na siasa. Serikali kupitia menejimenti za vyuo vikuu kwa muda mrefu sasa imekuwa ikiwakataza wanafunzi wa

vyuo vikuu kujihusisha na siasa vyuoni. Wanafunzi wengi wamekuwa wahanga wa kufukuzwa vyuoni au kusimamishwa masomo kwa muda (*suspension*) kutokana na kuonekana kuwa wafuasi wa vyama vya siasa na wengine kufukuzwa moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani isingekuwa na tatizo kama katazo hilo la kufanya siasa vyuoni lingekuwa ni kwa wanafunzi wote. Hata hivyo, imebainika bila kificho kwamba kuna ubaguzi wa kiitikadi kati ya wafuasi wa CCM na wa vyama vya upinzani katika vyuo vya elimu ya juu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haioni mantiki ya Serikali kuwakataza wanafunzi wa vyuo vikuu kujihusisha na siasa vyuoni ilhali vyuo hivyo vinafundisha Masomo ya Sayansi ya Siasa (*Political Science*). Kambi Rasmi ya Upinzani ilidhani kwamba kufanya shughuli za kisiasa ingekuwa kama mafunzo kwa vitendo hasa kwa wanafunzi wale wanaosoma Masomo ya Sayansi ya Siasa na Utawala ili kuonyesha umahiri na ubobezi wao katika masomo hayo badala ya kuwakataza. Kuwakataza wanafunzi hao kufanya siasa ni sawa na kuwapa ujumbe kwamba hata masomo hayo ya siasa wanayosoma hayana maana yoyote na kwa hiyo ni bora yaondolewe kwenye mtaala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna baadhi ya Wabunge hapa ambao wamepitia vyuo vikuu wamekuwa viongozi vyuoni na wamekuwa Wabunge. Mfano, Mheshimiwa Waitara na Mheshimiwa Zitto. Kwa hiyo, tulidhani hili ni jambo jema.

**MBUNGE FULANI:** Na Nsanzugwanko.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Naambiwa na Mheshimiwa Nsanzugwanko, nadhani na Mheshimiwa Chenge, ahsante. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utunzi wa vitabu. Kwenye suala la vitabu pamoja na kwamba tunawapongeza wamejitahidi kurekebisha vitabu lakini bado tuna tatizo kidogo na nitaomba Waziri wafuatilie. Sisi hoja yetu ya msingi tunataka tujue baada ya ile *EMAC* kutoka ni watu gani ambao wanapitia hivi vitabu pamoja ni mara ya kwanza lakini wamerekebisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunadhani kuna kila sababu ya kuona ni jinsi gani mnaweza sasa kutumia wale watunzi wa zamani ambao wamekaa. Kwa sababu utunzi wa vitabu *is an art*, huwezi tu ukasema kwa sababu mimi ni Profesa naweza, haiwezekani.

Kwa hiyo, Kambi inasema kwamba waangalie jinsi gani wale watunzi wa zamani wanaweza kusaidiana na waliopo pale ili iweze kuboresha tusiendeleo kupata hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Hotuba hii imeainisha maeneo mengi yenye kasoro na mapungufu katika sekta nzima ya elimu. Masuala yanayotakiwa kushughulikiwa mapema ili kukabiliana na mapungufu hayo ni pamoja na upungufu wa walimu; maslahi ya walimu; upungufu wa miundombinu; ubora wa vitabu; kuongeza bajeti ya maendeleo ya elimu; kutenganisha fedha za mikopo ya elimu ya juu na fedha za miradi halisi ya maendeleo na masuala mengine ambayo yameainishwa katika hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii pia imeeleza umuhimu wa sekta ya elimu katika ukuaji wa sekta nyingine za kiuchumi na hivyo kupendekeza kuwekeza zaidi katika elimu ili kuweza kufikia malengo ya kitaifa katika sekta nyingine hususani eneo la uchumi wa viwanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetoa pia angalizo la kutofanya majaribio katika sekta ya elimu, kwa kuwa madhara ya kufanya hivyo ni makubwa na endelevu kuliko yangefanywa katika sekta nyingine. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaendelea kusisitiza kwamba Serikali isifanye siasa katika suala la elimu. Aidha, Kambi Rasmi

ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kupitia kwa makini maeneo yote yenye mapungufu yaliyoainishwa ndani ya hotuba hii ikiwa ni pamoja na ile ya Kamati na kuelezea mikakati ya kuondoa mapungufu hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana kuwashukuru Sekretarieti ya Kambi ya Upinzani Bungeni, Waheshimiwa Wabunge wote wa Upinzani, taasisi mbalimbali zilizosaidia kutupa data mbalimbali ili kuboresha hotuba yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa heshima kabisa, naomba kuwasilisha na nashukuru sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI, MHESHIMIWA SUSAN ANSELM JEROME LYIMO (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KATIKA WIZARA HIYO, KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**A. UTANGULIZI**

1. **Mheshimiwa Spika**, napenda kuanza hotuba yangu kwa kunukuu sehemu ya mahubiri ya Askofu Almachius Vincent Rweyongeza wa Jimbo Katoliki la Kayanga Mkoani Kagera wakati wa ibada ya Ijumaa Kuu tarehe 19 Aprili, 2019 kwa ajili ya kujenga msingi wa hoja nitakazozitoa kuhusu mfumo wa elimu hapa nchini. Akinukuu maneno aliyoyasoma katika Geti la Chuo Kikuu fulani ambacho hakukitaja jina alisema kwamba:- *"Ukitaka kuangamiza Taifa lolote, huhitaji kutumia silaha za nuclear au atomic. Njia nzuri ya kuangamiza Taifa ni kuharibu Mfumo wa Elimu. Ruhusu mbumbumbu waonekane kuwa wamefaulu, na wasonge mbele hadi vyuo vikuu; matokeo yake yatajidhihirisha baada ya muda. Mbumbumbu hao wakashahitimu, kwa kupata vyeti hewa, vyeti feki, wagonjwa watafia mikononi mwa madaktari na manesi, majengo yataporomoka mikononi mwa wahandisi, pesa zitapotelea mikononi mwa wachumi na mafisadi, utu utapotea mikononi mwa viongozi wa dini na*

***Serikali; na haki itapotea mikononi mwa mahakimu na wanasheria”***

2. **Mheshimiwa Spika**, Askofu Rweyongeza alihoji, kama mfumo wetu wa elimu ni kama biashara au ni haki elimu bila wajibu. Msingi wa swali hili ulitokana ukweli kwamba mfumo wetu wa elimu umeyumba sana kutokana na kubadilishwa badilishwa kwa sera na miongozo ya elimu jambo ambalo linaashiria kwamba; watanzania kama taifa bado hatujui tunachokitaka hatujui rasilimali watu wetu wawe na sifa gani na hatujui tunataka Taifa letu la leo na kesho liweje. Kila mara mitaala ya elimu inabadilishwa badilishwa bila kufanyiwa utafiti wa kina na kujiridhisha kwa maslahi mapana na kwa mustakabali wa taifa.

3. **Mheshimiwa Spika**, Baba Askofu Rweyongeza alisisitiza kwamba tunahitaji elimu bora kama taifa itakayomwezesha mwanafunzi kukabiliana na changamoto za maisha ya kila siku nje ya darasa. (Not for school we learn but for life). Na mfumo utakaowezesha elimu ya namna hiyo lazima uwe imara la sivyo baada ya miaka michache ijayo Tanzania itakuwa Taifa la ajabu sana ambapo vijana walioandaliwa kwa gharama kubwa kuwa rasilimali watu wajenzi wa taifa; kuhudumu katika viwanda na sekta nyinginezo watajikuta ni vibarua na watumwa katika nchi yao wenyewe au wataunguza viwanda na kuzika sekta hizo. Hayo yalishatokea kwani hata viwanda na mashamba ambavyo baba wa taifa alikuwa amevipa kipaumbele – vyote vimesharibika Hata hivyo jitihada za sasa za kufufua viwanda haziwezi kuwa na matokeo makubwa ikiwa hazitakwenda sambamba na maboresho makubwa ya mfumo wetu wa elimu utakaozalisha rasilimali watu wenye ujuzi na weledi wa kuviendesha.

4. **Mheshimiwa Spika**, jambo la pila na la hatari aliloliubua Askofu Rweyongeza ni kulegeza vigezo au viwango vya ufaulu kuhusu elimu. Alisema badala ya kumwezesha mwanafunzi kuwa mahiri katika Nyanja mbalimbali za ujenzi wa taifa, na zaidi kujajiri mwenyewe, sera miongozi mingi ya elimu inaonekana kulenga kurahisishia wanafunzi kufaulu kwa kushusha wastani wa mitihani kinyume na viwango vya

kimataifa. Ubora wa elimu hauwezi kupimwa kwa kulegeza vigezo vya ufauli ili kuongeza idadi ya washindi, bali kinyume chake ni kuongeza vipele na majipu katika taifa.

**5. Mheshimiwa Spika**, nimeona ninukuu sehemu ya homilia hiyo ya Baba Askofu Rweyongeza pengine Serikali itasikia na kufanyia kazi kwa kuwa; kwa zaidi ya miaka kumi iliyopita Kambi Rasmi ya Upinzani imekuwa ikiishauri Serikali hii juu ya hatari ya kupuuza ushauri wa wataalam kuhusu mfumo wa elimu lakini badala yake imekuwa ikifanya maamuzi ya kisiasa kuhusu elimu kwa malengo ya kupata kura katika chaguzi.

**6. Mheshimiwa Spika**, Maamuzi kama vile kushusha viwango vya ufaulu; kutoa elimu bila ada; ni maamuzi ya kisiasa, ambayo hayakufanyiwa tafiti kujua athari zake kwa mfumo mzima wa elimu baadaye. Aidha, tumesisitiza sana kuhusu kujenga taasisi imara zinazoweza kujisimamia na kujiendesha ili kuwa na uendelevu (sustainability) wa sera na miongozo ya kitaasisi; lakini badala yake kila siku tunamjenga na kumtukiza mtu mmoja ambaye muda wake ukimalizika kunakuwa na ombwe katika masuala muhimu ya kitaifa.

## **B. ONGEZEKO LA IDADI YA WATU NA ATHARI ZAKE KATIKA UBORA WA ELIMU NCHINI**

**7. Mheshimiwa Spika**, kutokana na ongezeko kubwa la idadi ya watu Afrika hasa kusini mwa Jangwa la Sahara, kazi kubwa ya kuhakikisha ubora wa elimu kwa wote limekuwa ni hitaji kubwakuliko wakati mwingine wowote. Hali hii imekuwa janga kwa kuwa zaidi ya nusu ya watoto ambao hawajaandikishwa shule wanaishi katika nchi zilizo kusini mwa jangwa la Sahara<sup>1</sup>

**8. Mheshimiwa Spika**, Ongezeko hili la watu linaonekana pia Tanzania kwa ukuaji wa asilimia 2.7 kwa

---

<sup>1</sup>UN (n.d. a). Quality education: Why it matters, available at: <https://www.un.org/sustainabledevelopment/wpcontent/uploads/2018/09/Goa-I-4.pdf>

[accessed on 03 October 2018]

mwaka. Kiasi hicho cha ongezeko kitaifanya idadi ya watu Tanzania kuongezeka mara mbili kutoka watu takriban milioni 50 kwa sasa, hadi kufikia watu milioni 90 ifikapo mwaka 2036. Hali hii itaacha idadi kubwa ya vijana bila huduma za kijamii za kutosha ikiwa ni pamoja na ajira. Vile vile kwa ukuaji huu usioendana na kasi ya uboreshaji na upanuzi wa miundombinu ya elimu, Tanzania itandelea kukumbwa na ugumu wa kutoa elimu bora kwa wote.

**9. Mheshimiwa Spika**, kupitia maboresho ya elimu ya mwaka 2011 na 2016, kila mwanafunzi nchini sasa anaweza kupata elimu msingi bila ada<sup>2</sup>. Maboresho haya yanatokana na Tanzania kusaini mikataba mbalimbai ya kimataifa kama vile *United Nation's Convention on the Rights of the Child of 1989; Universal Right to Education*<sup>3</sup>, pamoja na *African Charter on the Rights and Welfare of the Child* ambapo Tanzania iliridhia mwaka 2003. Haki hii ya Elimu inamwezesha mtoto kupata fursa ya kushiriki kikamilifu kwenye jamii katika nyanja za kiuchumi, kisiasa na kijamii.

**10. Mheshimiwa Spika**, Licha ya juhudi zinazofanywa; utoaji wa elimu bila ada peke yake hautoshi. Ubora wa Elimu hapa nchini umelalamikiwa mara nyingi kuwa unaporomoka; na hauridhishi kabisa<sup>4</sup> Aidha, watoto wanaohitimu katika ngazi za elimu ya msingi na sekondari wamekuwa na uwezo mdogo katika ujuzi na maarifa kutokana na kile kinachoitwa "kupikwa nusu nusu" na hivyo kushindwa kuingia katika soko la ajira au kuendelea na elimu ya juu<sup>5</sup>.

---

<sup>2</sup>El-Noshokaty, D./Gebert, M. (2017). Country Report: False Promises in the Tanzanian Education Sector, Dar es Salaam.

<sup>3</sup>United Nation's Convention on the Rights of the Child, Article 28.(UNCRC, Art. 28)

<sup>4</sup>USAID (2017). Education Tanzania: Factsheet, available at: [https://www.usaid.gov/sites/default/files/documents/1860/Education\\_Fact\\_Sheet\\_2017\\_FINAL.pdf](https://www.usaid.gov/sites/default/files/documents/1860/Education_Fact_Sheet_2017_FINAL.pdf) [accessed on 03 October 2018].

<sup>5</sup>Brinkel, S. et al. (2018). Social Market Economy Model for Tanzania: Towards inclusive and sustainable economic development, Dar es Salaam.

11. **Mheshimiwa Spika**, mitaala yetu imekuwa ikilalamikiwa sana; na tunapoongelea mitaala ni pamoja na vitabu – ndiyo maana Taasisi ya Elimu Tanzania; jukumu lake ni kutayarisha vitabu vya kiada na mitaala. Mitaala yetu imekuwa ikibadilishwa mara kwa mara bila kuwashirikisha walimu ambao ndio wadau wakubwa. Mitaala yetu haiangalii maarifa (competency)na pia haitoi ujuzi ili mwanafunzi aweze kuendeleza vipaji vyake . Mitaala umekuwa zaidi wa kuwakaririsha wanafunzi.

12. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na matatizo ya mitaala, bado kumekuwa na tatizo kubwa la wataalamu washauri katika kuwashauri wanafunzi kwenye kuchagua vyo na kozi mbalimbali watakazosoma katika elimu ya juu. Haya yote yanachangia kwa kiwango kikubwa kuporomoka kwa ubora wa elimu na athari zake zinawagusa hata walimu ambao wametokana na mfumo mbovu wa elimu nchini. Kwa mfano; utafiti wa UWEZO wa mwaka 2017; unaonyesha kwamba; uwezo wa kusoma na kuhesabu miongoni mwa wanafunzi wa shule za msingi bado uko chini ya kiwango kinachohitajika na mtaala. Hali hii imesababishwa na uwezomdogo wa walimu kufundisha. Kwa mujibu wa Ripoti ya Benki ya Dunia ya mwaka 2014, walimu wengi wanakosa ujuzi na mbinu za kielimu za kufundisha. Ripoti hiyo inaonyesha kuwa ni moja ya tano (<sup>1/5</sup>) tu ya walimu wanaoweza kumudu mtaala wanaofundisha.

13. **Mheshimiwa Spika**, sambamba na kukosa ujuzi na mbinu za kufundisha, bado walimu wengi hawavutiwi na kazi ya kufundisha jambo ambalo linawafanya kutofundisha kwa bidii na hivyo kupelekea kushuka kwa ubora wa elimu. Utafiti ulifanywa na Haki Elimu 2016 ulibaini kwamba ni asilimia 37.8 tu ya walimu ndio waliokuwa wanaipenda kazi yao ya ualimu. Hii ina maana kwamba, zaidi ya asilimia 60 ya walimu hawaipendi kazi hiyo; na kwa maana hiyo hawafanyi kwa ufanisi. Changamoto zote hizi zimepelekea kushuka kwa ufaulu wa wanafunzi katika mitihani yao ya kuhitimu.

14. **Mheshimiwa Spika**,kutokana na changamoto hizo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haitachoka kuishauri Serikali



kuwa na mikakati mahsusi ya kuboresha mitaala na kuwashirikisha walimu ambao ndio wafundishaji, pamoja na kuwapatia mafunzo ili waweze kufundisha mitaala hiyo kwa weledi na hivyo kupandisha viwango vya ubora wa elimu nchini.

**C. UPUNGUFU WA KUTISHA WA WALIMU KATIKA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI**

**15. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani kwa zaidi ya miaka kumi iliyopita, imekuwa ikiikumbusha Serikali hii ya CCM kwamba; hakuna elimu bila walimu. Sarakasi na mbwembwe zote za kisiasa za elimu bure; elimu bila malipo na sasa elimu bila ada hazitasaidia chochote kama hakuna idadi ya kutosha ya walimu wenye weledi na motisha wa kufanya kazi ya kufundisha.

**16. Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa takwimu za BEST za mwaka 2016 na 2017; idadi ya walimu kwa shule za msingi imeshuka kutoka walimu 191,772 mwaka 2016 hadi kufikia 179,291 mwaka 2017 ikiwa ni anguko la asilimia 6.5 na kufanya uwiano wa mwalimu na wanafunzi kuwa 1:50. Aidha, katika shule za awali, idadi iliyopungua ni walimu 1948 na kufanya uwiano wa mwalimu na wanafunzi kuongezeka kutoka 1:135 mwaka 2016 hadi kufikia 1:159 mwaka 2017 badala ya 1:25 ambao ni uwiano unaokubalika.

**17. Mheshimiwa Spika**,kwa mujibu wa takwimu za Elimu Msingi za Mikoa (BEST Regional Data, 2017); walimu 7, 743 wanatarajiwa kustaafu kati ya mwaka 2018 na 2019. Aidha, takriban walimu zaidi ya 30,000 wana umri wa zaidi ya miaka 51ya kuzaliwa; hivyo na wao wanatarajiwa kustaafu muda mfupi ujao.

**18. Mheshimiwa Spika**, pamoja na takwimu hizo; Waziri wa Elimu katika hotuba yake ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/19 alisema kwamba shule za msingi zilikuwa na upungufu wa walimu 85,916 hadi kufikia Aprili, 2018. Tarehe 2 Mei, 2018 Naibu Waziri – Ofisi ya Rais TAMISEMI Mheshimiwa Joseph Kakunda akatangaza Bungeni kwamba kufikia Juni, 2018

Serikali itakuwa imeajiri jumla ya walimu wa shule za msingi wapatao 10,140 ili kupunguza uhaba wa walimu katika shule za msingi. Mwezi Julai, 2018 jumla ya walimu 4,840 walijajiriwa katika shule za msingi na sekondari; na mwezi Februari, 2019 Serikali ilitangaza ajira mpya za walimu zipatazo 4,549 katika ngazi mbalimbali na hivyo kushindwa kufikia lengo la kuajiri walimu 10,140 kama ilivyoahidi.

**19. Mheshimiwa Spika**, hata kama lengo la kuajiri walimu 10,140 lingefikiwa; na kuendelea kufanyika kila mwaka, bado ingetuchukua takriban miaka nane (8) kumaliza tatizo la upungufu wa walimu katika shule za msingi (kwa kuzingatia takwimu za Wizara ya Elimu zinazoonyesha kuwa upungufu ni walimu 85,916).

**20. Mheshimiwa Spika**, ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwamba Serikali iongeze kasi ya kuajiri walimu maradufu ili waendane na wimbi kubwa la wanafunzi wanaojiunga na elimu ya awali na msingi. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kupitia Wizara zinazohusika na Elimu kutengeneza mpango wa bajeti wa miaka mitano kwa ajili ya ajira za walimu ili kutatua kabisa tatizo la upungufu wa walimu. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ingependa kujua hatma ya wanafunzi wa sayansi waliokuwa wanasomea ualimu walioondolewa katika Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) kwa madai kwamba walikuwa "vilaza". Swali hili ni muhimu kujibiwa kwani kuna upungufu mkubwa sana wa walimu wa sayansi na kwamba kama wanafunzi hao wangeendelezwa na kuhitimu masomo yao pengo la upungufu lingepungua sana.

**21. Mheshimiwa Spika**, sambamba na juhudi za kupunguza changamoto ya uhaba wa walimu na hususan katika masomo ya sayansi; Kambi Rasmi ya Upinzani ingependa pia kujua Serikali ina mkakati gani wakuongeza idadi ya wanafunzi wa kike kwenye vyyo vikuu kwa masomo ya sayansi. Hii ni kwa sababu, licha ya kuwa na upungufu wa walimu katika masomo hayo; lakini kwa upande wa walimu wa kike wa sayansi upungufu ni mkubwa zaidi. Kwa hiyo, kuna haja ya kuweka mkakati maalumu wa kuongeza udahili wa

wanafunzi wa kike katika vyuo vikuu kwa masomo ya sayansi ili:- mosi, kuwa na uwiano au usawa wa kijinsia katika fursa za ualimu wa masomo ya sayansi; lakini pili kuziba pengo la upungufu mkubwa wa walimu wa sayansi nchini.

**22. Mheshimiwa Spika,** Upungufu wa walimu umevikumba pia vyuo vya ufundi stadi hasa ikizingatiwa kuna chuo kimoja tu cha ualimu wa ufundi stadi ukilinganisha na ujangaji na upanuzi wa vyuo vya VETA nchi nzima kwa kila Wilaya na mikoa na vile vya FDCs. Kwa hiyo, wakati Serikali inapanga mipango ya kuajiri walimu kwa ajili ya shule za msingi na sekondari ili kupunguza changamoto ya upungufu wa walimu, ifikirie pia kujenga vyuo vya ualimu wa ufundi stadi ili kukabiliana na upungufu wa walimu katika vyuo hivyo na hivyo kuweza kuzalisha wahitimu wengi wa ufundi stadi wenye ujuzi ambao watahitajika sana kuendesha uchumi wa viwanda.

**23. Mheshimiwa Spika,** kwa kutambua umuhimu wa walimu katika kukuza na kuboresha elimu kwa ajili ya kizazi cha sasa na cha baadaye katika nchi yetu; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kupitia CHADEMA; imeweka bayana msimamo wake wa kiseru kuhusu masuala ya walimu ikiwa itapewa ridhaa ya kushika madaraka ya Dola. Katika Sera ya Elimu ya CHADEMA, Sura ya 6.3 inasema kwamba; *“Chadema inatambua kwamba hakuna elimu bila mwalimu. Kwa hiyo, itaajiri walimu wa kutosha wenye sifa stahiki katika ngazi zote za elimu na kuwaendeleza kitaaluma ili wafundishe kwa ufanisi mkubwa. Chadema itaboresha maslahi ya walimu ikiwa ni pamoja na mishahara kuwapandisha madaraka kwa wakati, kuwapatia nyumba na bima ya afya kama stahili zao”*

**D. UHABA MKUBWA WA MIUNDOMBINU KATIKA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI NCHINI**

**24. Mheshimiwa Spika;** mazingira bora ya kufundisha na kujifunza yanategemea sana uwepo wa miundombinu rafiki na wezeshi. Ni jambo ambalo haliwezekani kutegemea kupanda kwa ubora wa elimu ikiwa hakuna jitihada zozote za kuboresha miundombinu itakayosaidia zoezi la kufundisha na kujifunza kufanikiwa.

25. **Mheshimiwa Spika**, kuna uhaba mkubwa sana wa miundombinu katika shule za msingi na sekondari za umma, jambo linalopelekea mazingira magumu ya kufundisha na kujifunza na hivyo kushusha viwango vya ubora wa Elimu. Kwa mujibu wa takwimu za BEST, 2016 na 2017; ni kwamba, uhaba wa maktaba katika shule za msingi umeongezeka kutoka asilimia 88 mwaka 2016 hadi kufikia asilimia 91.1 mwaka 2017.

26. **Mheshimiwa Spika**, takwimu hizo zinaonyesha pia kwamba; upungufu wa maabara katika shule za sekondari unatofautiana kulingana na masomo husika. Kwa mfano upungufu wa maabara za somo la Baiolojia ni asilimia 51.5, Fizikia ni asilimia 54.3 na Kemia ni asilimia 43.3

27. **Mheshimiwa Spika**, takwimu hizo pia zinaonyesha kwamba, kuna upungufu wa nyumba za walimu 186,008 sawa na asilimia 83.1 na upungufu wa majengo ya utawala 10,943 sawa na asilimia 83.4. Ripoti ya Benki ya Dunia ya mwaka 2016 inaonyesha kwamba; ni asilimia 41 tu ya shule za msingi na sekondari nchini Tanzania zenye miundombinu inayokidhi viwango vinavyotakiwa.

28. **Mheshimiwa Spika**, takwimu nilizozitaja hapo juu zinatiliwa nguvu na Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka wa fedha 2016/17 inayoonyesha kwamba shule za msingi zina upungufu wa madarasa kwa asilimia 85; upungufu wa vyoo asilimia 66; na upungufu wa nyumba za walimu asilimia 14. Kwa upande wa sekondari kuna upungufu wa vyumba vya madarasa asilimia 52, upungufu wa maabara asilimia 84; upungufu wa madawati asilimia 86; upungufu wa nyumba za walimu asilimia 85; upungufu wa mabweni asilimia 88 na upungufu wa matundu ya vyoo asilimia 53

29. **Mheshimiwa Spika**, wakati nchi washirika wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wako kwenye mpango wa kuwapatia wanafunzi wote wa shule za msingi Kompyuta Mpakato (Laptops) sisi Tanzania bado tunazungumzia uhaba wa matundu ya vyoo. Ni aibu sana kwa Serikali hii inayojitapa kwamba inatoa elimu bure wakati mazingira ya kutolea elimu

hiyo ni mabaya na yanachangia kwa kiwango kikubwa kushuka kwa ubora wa elimu.

**30. Mheshimiwa Spika**, Serikali inafahamu upungufu huu kwa kuwa takwimu zilizotumika ni za Serikali. Swali ni je; kwanini upungufu huu umekuwa ukiongezeka? Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge; imepunguza tatizo la uhaba wa miundombinu mashuleni kwa kiwango gani hadi sasa? Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kueleza imetenga bajeti kiasi gani katika mwaka wa fedha 2019/20 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu mashuleni ili kukabiliana na uhaba ulipo sasa?

**31. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inafahamu kwamba ni vigumu kutatua changamoto zote zilizoainishwa katika taarifa ya CAG kwa wakati mmoja. Hata hivyo, tuna mtazamo kwamba, Serikali iandae mpango wa kutatua changamoto hizo kidogo kidogo hadi hapo zitakapomalizika. Kwa mfano; tunashauri na kupendekeza kwamba; Serikali iwe na mpango wa kutenga bajeti kila mwaka wa fedha, kwa ajili ya kupunguza upungufu miundombinu iliyotajwa na CAG angalau kwa asilimia 25. Jambo hili likifanyika kwa uaminifu, itatuchukua miaka minne tu kumaliza tatizo la upungufu wa miundombinu katika shule za msingi.

**32. Mheshimidwa Spika**, kwa kuanzia, Kambi Rasmi ya Upinzani ingependa Serikali itoe taarifa mbele ya Bunge lako tukufu juu ya ahadi iliyoitoa kupitia Waziri wa Nchi – Ofisi ya Rais TAMISEMI Mheshimiwa Selemani Jafo tarehe 10 Juni, 2018 kwamba ingetoa shilingi billioni 29 kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu kwa Shule za Sekondari za Juu (A' Level Schools). Fedha hizo zilikusudiwa kujenga vyumba vya madarasa 478 na mabweni 269 kwa ajili ya wanafunzi 21,808 ambao walifaulu kujiunga na kidato cha tano lakini wangeachwa kutokana na upungufu wa vyumba vya madarasa na mabweni. Mamlaka za Serikali za Mitaa zilipewa muda wa miezi miwili kukamilisha ujenzi wa miundombinu hiyo.

33. **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ingependa kujua kama fedha hizo zilitolewa, kama madarasa na mabweni hayo yalijengwa; na kama wanafunzi walipokelewa shuleni kwa muda uliotakiwa. Majibu kwa maswali haya yatatoa picha ya mwelekeo wa kutatua changamoto za upungufu wa miundombinu mashuleni.

34. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na ukweli kwamba masuala ya miundombinu mashuleni yanasimamiwa na TAMISEMI; kwa kuwa mimi ni Waziri Kivuli ninayesimamia masuala yote ya Elimu bila kujali ni elimu msingi au elimu ya juu; na kwa kuwa Serikali ni moja; ningependa kupatiwa majibu hayo ili Bunge na taifa kwa jumla liweze kujua hali halisi ya mazingira ya kujifunza ya vijana wetu katika shule zetu za msingi na sekondari.

35. **Mheshimiwa Spika**, kwa kutambua umuhimu wa miundombinu mashuleni katika kuboresha mazingira ya kujifunzia; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kupitia CHADEMA, imeweka bayana msimamo wake wa kisera kuhusu uboreshaji wa mazingira ya kujifunzia. Sura ya 6.5 ya Sera ya Elimu ya CHADEMA inasema kwamba: ***“Chadema inatambua kwamba, mazingira ya kujifunzia yanaweza kuwa na athari chanya au hasi, katika ubora wa elimu kulingana na jinsi yalivyo. Kwa hiyo, itaboresha mazingira ya kujifunza, kwa kuanzisha miundombinu mipya na kukarabati iliyopo katika shule na taasisi zote za elimu nchini”.***

#### E. KUPUNGUA KWA BAJETI YA SEKTA YA ELIMU

36. **Mheshimiwa Spika**, tofauti na wakati wa utawala wa Serikali ya awamu ya nne ambapo bajeti ya sekta nzima ya elimu ilikuwa ikiongezeka kila mwaka; bajeti hiyo imekuwa na mserereko wa kushuka kwa miaka mitatu mfululizo tangu Serikali ya awamu ya tano iingie madarakani. Mathalan, bajeti hiyo ilipungua kutoka shilingi trilioni 4.770 mwaka 2016/17 hadi kufikia shilingi trilioni 4.706 mwaka 2017/18 na ikazidi kupungua hadi kufikia shilingi trilioni 4.628 mwaka 2018/2019. Aidha, uwiano wa bajeti ya sekta ya elimu ukilinganisha na

Bajeti Kuu ya Serikali umekuwa ukipungua kwa miaka yote mitatu ya utawala wa Serikali ya awamu ya tano, licha ya bajeti ya Kuu ya Serikali kuongezeka kwa miaka yote mitatu

**37. Mheshimiwa Spika**, uchambuzi uliofanywa na Shirika la Haki Elimu kuhusu mwenendo wa bajeti ya sekta ya elimu unaonyesha kwamba, uwiano wa bajeti ya sekta ya elimu na bajeti kuu ya Serikali ulishuka kutoka asilimia 16.1 mwaka 2016/17 hadi asilimia 15 mwaka 2017/18 na baadaye kushuka tena hadi asilimia 14 mwaka 2018/19. Mwenendo huo (wa kupungua) unazidi kutupeleka mbali na azimio la nchi za kusini mwa jangwa la sahara – Tanzania ikiwemo, la kutenga asilimia 20 ya bajeti kuu ya serikali na kuipeleka kwenye sekta ya elimu.

**38. Mheshimiwa Spika**, kitendo cha kutokutenga asilimia 20 ya bajeti kuu kumeikosha sekta ya elimu kiasi cha takriban shilingi trilioni 4.666 kwa miaka mitatu mfululizo tangu Serikali hii ya awamu ya tano iingie madarakani. Sekta ya elimu ilikoseshwa shilingi trilioni 1.138 wakati asilimia 16 ya bajeti kuu ilipotengwa kwa ajili ya sekta ya elimu; ilikoseshwa pia shilingi trilioni 1.634 wakati asilimia 15 ilipotengwa na ikakoseshwa tena shilingi trilioni 1.894 wakati ilipotengwa asilimia 14.

**39. Mheshimiwa Spika**, kuinyima sekta ya elimu takriban shilingi trilioni 4.7 ndani ya miaka mitatu ni jambo kubwa, hasa ukizingatia kwamba changamoto katika sekta ya elimu kuhusu mazingira magumu ya kujifunzia, miundombinu duni, upungugufu wa vifaa vya kufundishia na uhaba wa rasilimali watu zinazidi kuongezeka. Kama fedha hizo zingetengwa na kutolewa, bila shaka changamoto zinazoikabili sekta ya elimu hususan za upungufu wa miundombinu, walimu, vifaa vya kufundishia n.k. zingepungua sana, kama sio kumalizika kabisa.

**40. Mheshimiwa Spika**, upangaji huu wa bajeti ya sekta ya elimu chini ya asilimia 20 ya bajeti kuu, unakwenda kinyume na makubaliano ya kikanda na kimataifa ambayo nchi imeridhia ikiwemo Dakar Framework for Action on

Education for All, 2000 na Incheon Declaration and Framework for Action, 2015; ambapo ilikubaliwa kwamba nchi wanachama watenge angalau asilimia 20 ya bajeti zao za taifa kwa ajili ya elimu.

**41. Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa imeonekana dhahiri kwamba nchi yetu badala ya kutenga bajeti inayokaribia asilimia 20; sasa kumekuwa na mwenendo wa kushusha bajeti hiyo mwaka hadi mwaka; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali si tu kuheshimu makubaliano ya kimataifa ya kutenga asilimia 20 ya bajeti yake kwenda kwenye elimu; bali ijali mustakabali wa nchi yetu na malengo makubwa ya maendeleo ya nchi kwa kuwekeza vya kutosha katika sekta ya elimu.

**42. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa bajeti ya Wizara ya ELimu pekee, bajeti hiyo pia imepungua kutoka shilingi trilioni 1.408 kwa mwaka 2018/19 hadi shilingi trilioni 1.357 kwa mwaka wa fedha 2019/20. Upungufu huu ni wa shilingi bilioni 51. Uchambuzi wa randama za wizara ya elimu kwa mwaka wa fedha 2018/19 na 2019/2020 unaonyesha kwamba pamoja na kupungua kwa bajeti nzima ya wizara, bajeti ya matumizi ya kawaida imekuwa ikiongezeka wakati ile ya miradi ya maendeleo imekuwa ikipungua. Kwa mfano, bajeti ya matumizi ya kawaida imeongezeka kutoka shilingi bilioni 478 kwa mwaka wa fedha 2018/19 hadi shilingi bilioni 494 kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**43. Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa bajeti ya maendeleo ya wizara, bajeti hiyo imepungua kutoka shilingi bilioni 929 mwaka 2018/19 hadi kufikia shilingi bilioni 863 kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Hili ni anguko la asilimia 7.2 ambayo ni sawa na shilingi bilioni 67.

**44. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatiaka Serikali kutoa maelezo ni kwa namna gani itaweza kutekeleza miradi halisi ya maendeleo ikiwa bajeti ya maendeleo imekuwa na msereko wa kupungua?



**F. UTEKELEZAJI DUNI NA WENYE MASHAKA MAKUBWA WA MIRADI HALISI YA MAENDELEO KATIKA SEKTA YA ELIMU**

**45. Mheshimiwa Spika**,Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imefanya uchambuzi wa utekelezaji wa miradi halisi ya maendeleo katika sekta ya Elimu kwa miaka miwili mfululizo – yaani mwaka wa fedha 2017/18 na 2018/19 na kugundua kwamba kuna utekelezaji duni na wenye mashaka makubwa wa miradi halisi ya maendeleo katika sekta hiyo. Uchambuzi wetu umebaini kwamba, ipo miradi ambayo imekuwa ikitengewa fedha za maendeleo lakini fedha hizo zimekuwa hazipelekwi kabisa na kama zikipelekwa ni kwa kiasi kidogo sana.

**46. Mheshimiwa Spika**, miongoni mwa miradi ambayo haikupata fedha kabisa za utekelezaji licha ya kutengewa bajeti ni pamoja na miradi ifuatayo:

i. Mradi namba 6324 (Ukarabati wa Maktaba za Mkoa) mwaka 2017/18 mradi huu ulitengewa shilingi milioni 500; na mwaka 2018/19 ulitengewa shilingi bilioni 2.5. Kwa miaka yote miwili hakuna hata senti moja iliyopelekwa.

ii. Mradi namba 4305 (Kutegemeza Elimu ya Msingi) mwaka 2017/18 mradi huu ulitengewa shilingi bilioni 1.762;na mwaka 2018/19 ulitengewa kiasi hicho hicho cha shilingi bilioni 1.762 na kwa miaka yote miwili hakuna kilichopelekwa.

iii. Mradi namba 4320 (Kuimarisha Taasisi ya Elimu Tanzania) mradi huu ulikuwa umetengewa shilingi bilioni 40 mwaka 2017/18; na hakuna kilichopelekwa. Mwaka 2018/19 ulitengewa kiasi hicho hicho cha bilioni 40 lakini kiasi kilichotolewa hadi kufikia Februari, 2019 ni shilingi bilioni 4 sawa na asilimia 10 tu ya fedha zilizoidhinishwa.

iv. Mradi namba 6235 (Kuimarisha Uthibiti wa Ubora wa Shule). Mradi huu ulitengewa shilingi bilioni 1 mwaka 2017/18 na mwaka 2018/19 ukatengewa shilingi bilioni 1.5; na kwa miaka yote miwili hakuna fedha yoyote iliyotolewa kwa ajili ya kutekeleza mradi huo.

v. Mradi namba 2228 (Kuboresha Utafiti na Maendeleo katika Elimu Sayansi na Teknolojia) ambao ulitengewa shilingi bilioni 16.338 mwaka 2017/18. Bajeti hiyo ilishushwa hadi kufikia shilingi bilioni 5.240 mwaka 2018/19 na haikutekelezwa kwa miaka yote miwili.

**47. Mheshimiwa Spika**, miradi mingine ambayo haikupatiwa fedha kabisa ni pamoja na mradi wa upanuzi na ukarabati wa Chuo Kikuu cha Dodoma uliokuwa umetengewa shilingi bilioni 1.7 mwaka 2017/18 lakini mwaka 2018/19 haukutengewa fedha yoyote; Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa ambao ulitengewa shilingi bilioni 1 mwaka 2017/18 na shilingi bilioni 2 mwaka 2018/19 lakini fedha hizo hazikutolewa kabisa kwa miaka yote miwili; Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mwalimu J.K.Nyerere kilitengewa shilingi bilioni 3 mwaka 2017/18 lakini bajeti hiyo ikashushwa hadi kufikia shilingi bilioni 1 mwaka 2018/19 na bado hakuna fedha yoyote iliyopelekwa kwa miaka yote miwili; Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE) kilitengewa shilingi bilioni 1 mwaka 2017/18 na hakuna kilichopelekwa, isipokuwa mwaka 2018/19 kilitengewa shilingi bilioni 2 ambapo hadi kufikia Februari, 2019 ni shilingi milioni 582.281 sawa na asilimia 29.1 tu ndizo zilikuwa zimetolewa;

**48. Mheshimiwa Spika**, mradi mwingine ni mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Mradi huo ulitengewa shilingi bilioni 5.5 mwaka 2017/18 na bajeti hiyo ikashushwa hadi kufikia shilingi bilioni 2 mwaka 2018/19 lakini kwa miaka yote miwili fedha hiyo haikupelekwa; Mradi wa Upanuzi na Ukarabati Chuo Kikuu Mzumbe mwaka 2017/18 ulitengewa shilingi bilioni 1 na hakuna kilichopelekwa. Mwaka 2018/19 mradi huo ukatengewa tena shilingi bilioni 2.5 lakini mpaka kufikia Februari, 2019 hakuna fedha yoyote iliyokuwa imetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo. Mradi wa Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili mwaka 2017/18 ulitengewa shilingi bilioni 1 hakuna kilichopelekwa na mwaka 2018/19 mradi huo ukatengewa tena shilingi bilioni 1.8 na hakuna fedha iliyotolewa mpaka sasa; Chuo Kikuu cha

Biashara na Ushirika- Moshikilitengewa shilingi bilioni 1.3 mwaka 2017/18 kwa ajili ya ukarabati na mwaka 2018/19 kikatengewa shilingi bilioni 2 lakini kwa miaka yote miwili hakuna hata senti moja iliyopelekwa kwa ajili hiyo. Aidha, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya, mwaka 2017/18 kilitengewa shilingi bilioni 3 hakuna kilichopelekwa na mwaka 2018/19 kililitengewa shilingi bilioni 2 na mpaka sasa hakuna kilichopelekwa.

**49. Mheshimiwa Spika**, ipo miradi mingine ya maendeleo katika sekta ya elimu ambayo haikutengewa bajeti katika mwaka 2017/18 lakini kwa mwaka wa fedha 2018/19 miradi hiyo imetengewa fedha lakini hadi kufikia Februari 2019 hakuna fedha yoyote iliyotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo. Miradi hiyo ni pamoja na mradi namba 6229 (Ukarabati na Upanuzi wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi –FDCs) uliotengewa shilingi bilioni 2; Mradi namba 6363 (Upanuzi na Ukarabati wa Chuo cha Ufundi – Arusha) uliotengewa shilingi bilioni 2.295; Mradi namba 4358 (Upanuzi wa NM-AIST) uliotengewa shilingi bilioni 1; Mradi namba 4384 (Ujenzi wa “DIT” Teaching Tower) uliotengewa shilingi bilioni 1; Mradi namba 6345 (Mfuko wa Utafiti na Maendeleo wa COSTECH) ambao ulitengewa shilingi bilioni 9.680 na Mradi namba 4390 (Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Sekondari) uliotengewa shilingi bilioni 25.

**50. Mheshimiwa Spika**, kati ya miradi ya maendeleo 41 yenye thamani ya **shilingi 929,969,402,000/=** miradi 24 yenye thamani ya shilingi **100,894,000,000/-** haikupatiwa hata senti moja kwa ajili ya utekelezaji wa miradi.

**51. Mheshimiwa Spika**, ni ukweli usiopingika kwamba kutotekelezwa kwa miradi hiyo; hakupandishi viwango vya ubora wa elimu hapa nchini; bali kunazidi kushusha viwango vya ubora na hatimaye kudumaza sekta nzima ya elimu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kueleza ni kwa nini haikutekeleza bajeti ya maendeleo katika miradi iliyotajwa licha ya bajeti kwa ajili ya miradi hiyo kutengwa na kupitishwa na Bunge.

**G. BAJETI YA MAENDELEO KATIKA SEKTA YA ELIMU NI TEGEMEZI KWA FEDHA ZA NJE**

**52. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani haina mgogoro na Serikali juu ya matumizi ya fedha za nje katika kutekeleza miradi ya maendeleo. Ila jambo la msingi ambalo Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa angalizo ni katika kupanga miradi ipi itekelezwe na fedha za nje na miradi ipi itekelezwe na fedha za ndani.

**53. Mheshimiwa Spika**, ipo miradi ambayo kutokana na umuhimu wake kwa ustawi wa taifa, inapaswa kutekelezwa na fedha za ndani. Kwa mfano miradi ya maendeleo katika sekta ya afya, elimu na huduma nyingine za jamii inapaswa kutekelezwa kwa kutumia fedha za ndani. Miradi ya maendeleo katika sekta nyingine ambazo hazina athari za moja kwa moja na za haraka kwa maisha na ustawi wa jamii kama vile miradi ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali inaweza kutekelezwa na fedha za nje.

**54. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani imeshtushwa sana kuona miradi mingi ya maendeleo katika sekta ya elimu – sekta ambayo ndio moyo wa maendeleo ya sekta nyingine zote; ikitengewa asilimia sifuri ya fedha za ndani na kubaki tegemezi kwa fedha za nje pekee kwa ajili ya utekelezaji.

**55. Mheshimiwa Spika**, miradi tisa (9) ya maendeleo iliyopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2019/2020; haijatengewa hata senti moja ya fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji<sup>6</sup>. Miradi hiyo ni pamoja na:-

i. Mradi namba 4312(Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo kwa ajili ya motisha – Education Programme for Results) uliotengewa shilingi milioni 94.6;

ii. Mradi namba 3280 (Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira ya Shule) uliotengewa shilingi bilioni 6.948;

---

<sup>6</sup> Tazama Randama ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu 46) ya mwaka 2019/2020 uk. 103 -105

- iii. Mradi namba 4305 (Kutegemeza Elimu ya Msingi uliotengewa shilingi bilioni 1. 065);
- iv. Mradi namba 4321 (Programu ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi – Primary Education Development Programme – Kuimarisha mafunzo ya KKK) uliotengewa shilingi bilioni 20.445;
- v. Mradi namba 4390 (Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Sekondari – Secondary Education Quality Improvement Programme – SEQIP) uliotengewa shilingi bilioni 30.818;
- vi. Mradi namba 4323 (Kuendeleza Elimu ya Ualimu – Teacher Education Support Programme – TESP) uliotengewaa shilingi bilioni 20.3;
- vii. Mradi namba 2228 (Kuboresha Utafiti na Maendeleo katika Elimu na Mafunzo - Support on Research and Development) uliotengewa shilingi bilioni 10.475;
- viii. Mradi namba 4392 (Kukuza Stadi za Kazi kwa ajili ya Shughuli za Kuzalisha na Kukuza Uchumi – Education and Skills for Productive Job – ESPJ) uliotengewa shilingi bilioni 56.556
- ix. mradi namba mradi namba 6574 (Mradi wa Kituo cha Taifa cha Udhibiti wa Hewa Ukaa - National Carbon Monitoring Center) uliotengewa shilling milioni 817.367

**56. Mheshimiwa Spika**, miradi iliyotajwa hapo juu imepangwa kutekelezwa kwa kutumia fedha za nje tu. Tafsiri ya Mpango huo wa bajeti ni kwamba miradi hiyo siyo ya kipaumbele kwa kuwa fedha za nje sio za kutegemea kwa asilimia mia moja. Hii ni kwa sababu uzoefu unaonyesha kwamba, fedha za nje huchelewa sana kutolewa na wakati mwingine hazitolewi kabisa.

**57. Mheshimiwa Spika**, kitendo cha Serikali kupanga bajeti ya miradi ya maendeleo katika sekta ya elimu kwa kutumia fedha za nje; ni kuiweka elimu yetu rehani na kwa maneno mengine ni kuliangamiza taifa kwa kuwa mafanikio

ya sekta nyingine zote yanategemea sana ukuaji na ubora wa sekta ya elimu.

**58. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani imeshangazwa sana kwamba hata fedha za mradi wa mafunzo ya KKK (Kusoma, Kuandika, na Kuhesabu) na mradi wa kuimarisha ubora wa elimu ya Sekondari au mradi wa kuendeleza elimu ya ualimu tunategemea wafadhili watusaidie kwa asilimia mia moja!!!. Ndio maana hatushangai kuona ripoti za utafiti kama za TWaweza na Benki ya Dunia zikionyesha kwamba; uwezo wa kusoma, kuandika na kuhesabu miongoni mwa wanafunzi wa shule za msingi bado uko chini ya kiwango kinachohitajika na mtaala.

**59. Mheshimiwa Spika**, Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere aliwahi kusema “Kupanga ni kuchagua” Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haioni mantiki yoyote ya Serikali hii ya CCM kuchagua miradi muhimu kama vile Mafunzo ya KKK – ambayo ndio moyo wa Elimu Msingi itekelezwe kwa fedha za nje. Aidha, hakuna mantiki yoyote miradi ya utafiti katika elimu na kuendeleza elimu ya ualimu kutegemea fedha za nje.

**60. Mheshimiwa Spika**, katika vitu ambavyo Serikali hii haitakiwi kuvifanyia majaribio ni sekta ya elimu. Madhara yanayopatikana kwa kufanya makosa katika sekta ya elimu ni ya muda mrefu na pia madhara hayo hayaishii kwenye elimu tu bali huathiri pia sekta nyingine. Mtabibu aliyepewa mafunzo kengeufu katika elimu yake; athari zake zitakwenda kuathiri sekta ya afya pia na nyinginezo.

#### **H. MIKOPO YA ELIMU YA JUU NA RUZUKU KWA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI**

**61. Mheshimiwa Spika**, kutokana na mabadiliko ya kiuchumi yaliyopelekea kupanda kwa gharama za maisha; kiasi cha ruzuku ya shilingi 10, 000/= kwa mwanafunzi wa shule ya msingi na shilingi 25,000/= kwa mwanafunzi wa sekondari kilichopangwa tangu mwaka 2001 hakiwezi tena kukidhi mahitaji kwa sasa.

**62. Mheshimiwa Spika**, wakati kiwango hicho kinapangwa; thamani ya dola moja ya kimarekani ilikuwa ni shilingi 1,000/= na lengo lilikuwa ni angalau kutoa dola kumi kwa mwanafunzi wa shule ya msingi na dola 20 kwa mwanafunzi wa sekondari. Thamani ya dola moja kwa sasa imepanda; ambapo kwa sasa tunahitaji makadirio ya shilingi 2,300 kununua hiyo dola moja.

**63. Mheshimiwa Spika**; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inafahamu kwamba Serikali iko katika hatua za mwisho za kuanza utekelezaji wa utoaji wa ruzuku kwa mwanafunzi kwa kutumia kanuni mpya, hivyo tunashauri kuwa utekelezaji huo uwe na lengo la kuongeza kiwango cha ruzuku kwa mwanafunzi ili kulinda nguvu ya manunuzi ya ruzuku hii. Kwa sababu hiyo; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri na kupendekeza kwa Serikali kutenga angalau shilingi 20,000/= kama ruzuku kwa kila mwanafunzi mmoja wa shule ya msingi na shilingi 50,000/= kwa kila mwanafunzi wa sekondari wakati wa utekelezaji wa zoezi la utoaji wa ruzuku kwa shule za msingi na sekondari kwa kutumia kanuni mpya.

**64. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa elimu ya juu; Kambi Rasmi ya Upinzani kwa miaka mingi, imekuwa ikiitaka Serikali kutochanganya fedha za mikopo ya elimu ya juu katika fedha za maendeleo kwa kuwa fedha hizo huonekana kuwa ni nyingi lakini fedha zinazokwenda kutekeleza miradi halisi ya maendeleo ni kidogo sana. Kwa mfano fedha za maendeleo zilizotengwa kwa ajili ya Wizara ya Elimu kwa mwaka wa fedha 2018/19 zilikuwa ni shilingi 929,969,402,000/=. Kati ya fedha hizo shilingi 427,554,000,000/= zilikuwa ni fedha za mikopo ya elimu ya juu. Hii ni sawa na asilimia 45.9 ya fedha yote ya maendeleo iliyotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika Wizara ya Elimu.

**65. Mheshimiwa Spika**, hii maana yake ni kwamba; asilimia 45.9 ya fedha za mendeleo katika Wizara ya Elimu hazikwenda kwenye utekelezaji wa miradi halisi ya maendeleo jambo ambalo limesababisha miradi 24 kati ya 41 haijapatiwa hata senti moja kwa ajili ya utekelezaji wake kama nilivyoonesha hapo awali.

**66. Mheshimiwa Spika**, tatizo linazidi kuwa kubwa kwa kuwa fedha za mikopo ya elimu ya juu inazidi kuongezeka na kuiacha miradi halisi ya maendeleo ikitengewa fedha kidogo. Kwa mfano mwaka 2018/19 kati ya shilingi bilioni 502.4 ya miradi ya maendeleo, shilingi bilioni 427 sawa na asilimia 46 ya bajeti yote ya maendeleo ilikuwa ni fedha za mikopo ya elimu ya juu. Mwaka wa fedha 2019/2020 bajeti nzima ya maendeleo ni shilingi bilioni 863; kati ya hizo shilingi bilioni 450 ni fedha za mikopo ya elimu ya juu sawa na asilimia 52 ya bajeti ya maendeleo huku kiasi cha shilingi bilioni 413 sawa na asilimia 48 kikibaki kwa ajili ya utekelezaji wa miradi halisi ya maendeleo.

**67. Mheshimiwa Spika**, ili kuondoa mkanganyiko huo; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri na kupendekeza kwamba; lianzishwe fungu maalum(vote) kwa ajili ya kuweka fedha za mikopo ya elimu ya juu ili fedha za miradi halisi ya maendeleo ziweze kuonekana na kufuatiliwa utekelezaji wake; kuliko ilivyo sasa ambapo taswira chanya inajengwa kwamba kuna bajeti kubwa ya maendeleo katika Wizara ya Elimu ilihali uhalisia ni kwamba zaidi ya asilimia 50 ya fedha hizo ni mikopo na miradi halisi ya maendeleo haitaitekelezwi.

#### **I. BAJETI YA ELIMU IZINGATIE MAHITAJI MAALUM YA MTOTO WA KIKE SHULENI**

**68. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikipigia kelele suala la kupanga bajeti kwa kuzingatia masuala ya jinsia (gender budgeting) na mara kadhaa tumeitaka Serikali kutenga fedha kwa ajili ya kuwapatia wanafunzi wa kike wenye umri wa hedhi taalo za kujihifadhi wakati wa hedhi ili kuhakikisha kwamba hedhi haiwi kikwazo kwa wanafunzi hao kupata elimu sawa na wenzao wa kiume.

**69. Mheshimiwa Spika**, jitihada hizo za Kambi ya Upinzani zilikuwa ni pamoja na kupeleka hoja binafsi Bungeni kuitaka Serikali kutenga fedha kwa ajili ya kununua taalo hizo. Hata hivyo, pamoja na hoja hiyo kukataliwa kujadiliwa ndani ya Bunge; Serikali baada ya kujitafakari, iliamua kuondoa Kodi



ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwenye bidhaa za taulo za kike katika bajeti ya 2018/19 ili kuwapa nafuu ya bei wanafunzi wa kike walio katika umri wa kupata hedhi.

**70. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua dhamira, busara na utashi wa Serikali wa kuondoa kodi hiyo ili kuondoa changamoto ya muda mrefu ya watoto wa kike kukosa masomo kwa siku mbili au tatu kwa kila mwezi kutokana na kushindwa kumudu gharama za kununua taulo za kujisitiri wakati wa hedhi. Lengo la kuondoa kodi hiyo kwenye taulo za kike lilikuwa ni kushusha bei ya bidhaa hizo ili kuziwezesha familia nyingi zaidi kumudu gharama hizo kwa ajili ya kuwanunulia watoto wao.

**71. Mheshimiwa Spika**, pamoja na dhamira hiyo njema ya Serikali, uchunguzi unaonyesha kuwa kumekuwa na mwitikio mdogo katika utekelezaji wa maagizo hayo ya Serikali. Maduka mengi yaliyotembelewa kwenye uchunguzi huo, bei ya taulo za kike imebaki kuwa ya wastani wa shilingi 2,000/=; - gharama ambayo imekuwa ni vigumu kwa familia maskini kuweza kumudu. Hii ni hali inayokatisha tamaa si tu kwa wanafunzi wa kike; bali kwa Serikali pia. Hii inadhahirishwa na tamko la Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu alilolitoa tarehe 15 Februari, 2019 wakati akihutubia mkutano wa wadau Dar es Salaam; ambapo alieleza kusikitishwa kwake baada ya kufahamu kwamba taulo za kike bado zilikuwa zikiuzwa kwa bei ya juu licha ya Serikali kufuta VAT katika bidhaa hizo, na kuongeza kwamba alishamwandikia Waziri wa Fedha na Waziri wa Viwanda na Biashara juu ya kutoridhishwa kwake na jambo hilo.

**72. Mheshimiwa Spika**, pamoja na Kambi Rasmi ya Upinzani kutambua kusudio la Serikali kuwapatia wanafunzi wa kike nafuu ya taulo za kujisitiri wakati wa hedhi; tunashauri na kupendekeza kwamba Serikali iwe inatenga bajeti maalum kwa ajili ya kununua taulo hizo na kuzipeleka shuleni moja kwa moja. Bajeti hiyo inaweza kuongezwa kwenye ruzuku inayokwenda shuleni (Capitation Grants) kwa kila mwanafunzi balehe wa kike (adolescent girl).

**73. Mheshimiwa Spika**, sambamba na hilo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa pia wito kwa serikali kutenga fedha za kujenga na kuimarisha miundombinu ya maji, elimu ya afya na usafi wa mazingira mashuleni (SWASH) ili kusaidia jitihada za kupunguza utoro na kuboresha ufaulu wa mtoto wa kike. Ni bahati mbaya sana kwamba; katika mwaka wa fedha 2017/2018 serikali ilitenga shilingi bilioni 1 kwa ajili ya mradi wa maji, elimu ya afya na usafi wa mazingira shuleni. Lakini hadi kufikia mwezi Machi 2018, ni kiasi cha shilingi milioni 170 tu sawa na asilimia 17, ndicho kilichokuwa kimetolewa kwa ajili ya mradi huu.

**74. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2018/19 mradi huu ulitengewa shilingi bilioni 17.033 lakini hadi kufikia Machi, 2019 ni shilingi milioni 170 sawa na asilimia 0.9 tu ya fedha zilizoidhinishwa. Hii ni sawa na kusema kwamba asilimia 99.1 ya bajeti ya mradi huo haikutekelezwa. Hii inaonyesha dhahiri jinsi ambavyo Serikali hii ya awamu ya tano isivyojali mazingira bora ya elimu hasa kwa mtoto wa kike. Na ushahidi kwamba Serikali hii haijali ni kwamba imepunguza fedha za mradi huu katika bajeti ya 2019/2020 hadi kufikia shilingi bilioni 6.948<sup>7</sup> kutoka shilingi bilioni 17.033 zilizotengwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2018/19. Hili ni sawa na anguko la asilimia 60.9 la bajeti ya mradi huo.

**75. Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa wasichana ndio waathirika wakuu wa mazingira na miundombinu duni ya kujifunzia katika shule za serikali, ni muhimu masuala yanayoboresha ustawi wao yakapewa kipaumbele katika bajeti ya mwaka wa fedha 2019/20.

**76. Mheshimiwa Spika**, kwa kutambua umuhimu wa elimu kwa mtoto wa kike; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kupitia CHADEMA imeenda mbali zaidi na kuingiza katika sera yake ya elimu namna ya kuboresha elimu ya mtoto wa kike. Sura ya 6.5 ya Sera za Chadema kuhusu mazingira ya kujifunzia

---

<sup>7</sup> Tazama Randama ya Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi (fungu 46) ya mwaka 2019/2020 uk.112.

inasema kwamba *“Chadema itahakikisha kwamba inaweka mazingira rafiki kwa mtoto wa kike kupata elimu bora; ikiwa ni pamoja na kuanzisha program maalum ya kuwaendeleza wanafunzi wa kike waliopata mimba wakiwa shuleni”*.

**J. MOTISHA KWA WAKAGUZI WA ELIMU UNATOLEWA KWA UBAGUZI**

**77. Mheshimiwa Spika;** mwaka 2014, Serikali ilitoa Waraka wa Watumishi wa Serikali Namba 3 wa mwaka 2014 kuhusu mishahara na posho ya madaraka kwa viongozi wa Elimu Nchini. Waraka huo ulikuwa ni juu ya uamuzi wa Serikali wa kuwaingiza Wakaguzi Wakuu wa Shule wa Wilaya na Kanda katika muundo wa mishahara wa viongozi wa Serikali (LSS – E); na kulipa posho ya madaraka kwa wakuu wa shule za msingi na sekondari, Wakaguzi wa Elimu Kata na Wakuu wa Vyuo vya Ualimu nchini.

**78. Mheshimiwa Spika;** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haipingi kuwapa motisha wakaguzi wa elimu; isipokuwa ina mgogoro na mfumo wa kibaguzi wa utoaji wa motisha huo. Ukisoma waraka huo, utaona kwamba Serikali imeamua kutoa posho ya madaraka kwa wakuu wa shule za msingi na sekondari, Wakaguzi wa Elimu Kata na Wakuu wa Vyuo vya Ualimu nchini na kuwaweka pembeni Wakaguzi Wakuu wa Shule wa Wilaya na Kanda.

**79. Mheshimiwa Spika,** kwa kutumia uzoefu mdogo tu, kati ya mratibu wa elimu wa Kata; na Mkaguzi wa Shule wa Wilaya na Kanda; ni nani mwenye majukumu makubwa ambaye angestahili kulipwa posho hiyo ya madaraka? Tukumbuke kwamba hawa wakaguzi wa shule wa Wilaya na Kanda ndio wadhibiti wakuu wa ubora wa elimu katika Wilaya zote na Kanda zote Tanzania Bara. Ikiwa hawa wametengwa katika kupewa motisha; kuna hatari kubwa ya kuporomoka kwa ubora wa elimu kwa nchi nzima kwa mara moja.

**80. Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili ni lini itawaingiza wakaguzi wakuu wa shule wa wilaya na kanda katika utaratibu wa

kulipwa posho ya madaraka kama wanavyolipwa wakuu wa shule za msingi na sekondari; wakaguzi wa elimu Kata na Wakuu wa Vyuo vya Ualimu? Ikiwa Serikali itaridhia kuwalipa posho hiyo; Je, itakuwa tayari kuwalipa malimbikizo ya posho hiyo tangu Julai, 2016 ilipoanza kuwalipa wakuu wa shule za msingi na sekondari, wakaguzi wa elimu Kata na Wakuu wa Vyuo vya Ualimu?

**K. UTUNZI MBOVU WA VITABU VYA ELIMU: SUMU KALI ITAKAYOUA ELIMU YA TANZANIA**

**81. Mheshimiwa Spika**, katika hotuba yangu ya mwaka jana nilieleza kuwa vitabu ni nyenzo muhimu sana katika utoaji wa elimu bora, hasa katika kipindi hiki chenye uhaba mkubwa wa walimu. Vitabu visipotungwa kwa ubora ni sumu mbaya sana kwa elimu hasa elimu ya shule ya msingi (awali hadi darasa la saba).

**82. Mheshimiwa Spika**, nilieleza kwamba; Taasisi ya Elimu Tanzania ilipewa mamlaka ya uchapishaji wa vitabu vya kiada nchini na imechapisha vitabu vipya kwa shule za msingi na Sekondari; Ni wazi kuwa vitabu hivyo vilikuwa na mapungufu makubwa ambayo yangesababisha madhara makubwa katika utoaji wa elimu, na hivyo kushusha ubora wa elimu yetu. Miongoni mwa mapungufu au matatizo ya vitabu hivyo yalikuwa ni pamoja na kutokuchapishwa Kiongozi cha Mwalimu; Kuchapisha mambo yaliyostahili kuingizwa kwenye kiongozi cha mwalimu. Aidha, kulikuwa na makosa ya Usanifu wa Vitabu hivyo kama vile picha zisizo na ubora pamoja na makosa ya lugha.

**83. Mheshimiwa Spika**, Serikali ilikiri kuwa vitabu hivyo vilikuwa na mapungufu; na kuchukua hatua ya kuwawajibisha waliohusika na makosa hayo pamoja na kuagiza vitabu hivyo vichapwe upya. Hata hivyo; vitabu vipya vilivyotolewa na Taasisi ya Elimu ambavyo vimesahihishwa bado baadhi vina makosa mengi.

**84. Mheshimiwa Spika**, hitilafu nyingine katika vitabu vipya ni udhaifu wa usanifu wa vitabu vyenyewe. Kwanza,

kuna matumizi mabaya ya kurasa za vitabu husika. Kurasa nyingi zimeachwa wazi bila kuandikwa chochote – jambo ambalo linasababisha gharama kubwa za uchapishaji bila sababu na pia uwazi huo unatoa nafasi kwa watoto kuchezea kurasa hizo kwa kuzichora chora na hivyo kupelekea kuchakaa kwa vitabu mapema kabla ya muda. Aidha, picha nyingi zilizo kwenye vitabu hivi zimefifia na haziendani na maelezo.

**85. Mheshimiwa Spika;** Ifahamike kwamba utunzi wa vitabu ni taaluma (its an art) hivyo watunzi wa vitabu wanatakiwa kusomea na kubobea katika taaluma hiyo vinginevyo tutaendelea kuwa na mapungufu makubwa katika utunzi wa vitabu jambo ambalo ni hatari katika ubora wa elimu nchini.

**86. Mheshimiwa Spika,** kitendo cha Taasisi ya Elimu kutoa vitabu vyenye makosa; na kushindwa kurekebisha makosa hayo hata pale ilipoamriwa kuchapisha upya vitabu vilivyokuwa na makosa; kunaiondolea taasisi hiyo sifa za kuendelea kuwa na mamlaka ya kuchapisha vitabu vya elimu katika nchi yetu. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuunda timu ya uchunguzi itakayofanya ukaguzi wa utendaji wa Taasisi hiyo, ili kubaini uwezo wa watunzi wa vitabu kwani imekuwa ni kawaida kuchapa vitabu vyenye makosa na hivyo kuliingiza taifa hasara na mbaya zaidi kuwapa watoto elimu potofu jambo ambalo ni hatari kwa mustakabali wa taifa.

**87. Mheshimiwa Spika,**kwa kuwa kuna watunzi wa vitabu wenye uzoefu wa miaka mingi; Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri na kupendekeza kwamba Serikali kupitia Taasisi ya Elimu iwape mikataba watunzi hao kwa kipindi cha mpito ili waweze kuwaelekeza kazi watendaji waliopo sasa.

**L. MFUMO WA UGUNDUZI NA UBUNIFU KATIKA ELIMU UMESINYAA**

**88. Mheshimiwa Spika,** maendeleo yoyote ya kisayansi na kiteknolojia ambayo ndio msingi wa maendeleo ya

kiuchumi katika taifa lolote yanategemea sana kiwango cha ugunduzi na ubunifu unaotokana na elimu bora.

**89. Mheshimiwa Spika**, ugunduzi na ubunifu ni zao la tafiti za kisayansi – tafiti ambazo huleta majibu ya changamoto mbalimbali zinazoikabili jamii. Ndiyo kusema kwamba, kadiri dunia inavyozidi kubadilika kutokana na maendeleo ya shughuli mbalimbali za binadamu; na kadiri changamoto mbalimbali zinavyozidi kuongezeka kutokana na mwingiliano wa shughuli za binadamu na mazingira ndivyo tafiti nyingi zinahitajika kufanywa ili kutoa majibu ya changamoto hizo na hivyo kumwezesha binadamu kuweza kuyamudu mazingira yake.

**90. Mheshimiwa Spika**, ili tafiti hizo zifanyike rasilimali fedha inahitajika. Mataifa yaliyoendelea katika nyanja za sayansi na teknolojia yamewekeza sana katika tafiti. Kwa maneno mengine, ili Tanzania iweze kuwa na wagunduzi na wabunifu wazuri tunahitaji kama taifa kuwekeza sana katia tafiti.

**91. Mheshimiwa Spika**, pamoja na ukweli huo, Serikali hii ya CCM imekuwa na ugumu sana wa kutenga fedha kwa ajili ya tafiti jambo ambalo linazidi kudumaza viwango vya ubunifu na ugunduzi na yamkini uchumi wetu umeendelea kushuka kutokana na ubahili huo wa Serikali. Nathubutu kusema hivyo kwa sababu katika bajeti ya mwaka 2018/19 Mradi namba 6345 ambao ni Mfuko wa Utafiti na Maendeleo wa COSTECH ulitengewa shilingi bilioni 9.680 lakini mpaka naandika hotuba hii fedha hizo hazijatolewa.

**92. Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21, Serikali ilijiweka kiwango cha kutenga asilimia moja (1%) ya pato ghafi la Taifa (GDP) kwa ajili ya shughuli Sayansi, Teknolojia na Ugunduzi<sup>8</sup>. Hata hivyo, Serikali haijawahi kutenga kiasi hicho tangu imejiweka utaratibu huo.

---

<sup>8</sup> Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2016/17 - 2020/21 (uk.17)

**93. Mheshimiwa Spika**, pato ghafi la taifa kwa sasa ni dola za Kimarekani bilioni 52.09 ambazo ni sawa na shilingi 119,807,000,000,000 (trilioni 119.807) Hii ina maana kwamba ikiwa Serikali ingefuata utaratibu iliyojiwekea wa kutenga asilimia moja ya Pato Ghafi la Taifa, ingetakiwa kutenga shilingi 1, 198,070,000,000 (trilioni 1.198).

**94. Mheshimiwa Spika**, fedha iliyotengwa kwa Tume ya Sayansi na Teknolojia - COSTECH kwa ajili ya tafiti kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ni shilingi bilioni 7.574 sawa na asilimia 0.00632. Hiki ni kiwango kidogo kuliko vyote tangu Serikali hii ya awamu ya tano iingie madarakani.

**95. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa angalizo kwa Serikali kuwa makini katika suala hili la tafiti za kisayansi kwa kuwa kuna hatari ya Tanzania kuendelea kuwa watumwa wa teknolojia ya nje jambo ambalo litazidi kuwaweka watazania mbali katika kushiriki kujenga uchumi wa nchi yao. Mwenendo huu wa kuendelea kutenga fedha kidogo kwa ajili ya tafiti hauna afya hata kidogo kwa mustakabali wa Sayansi, Teknolojia na Ugunduzi katika taifa. Hata ndoto za Serikali za kujenga uchumi wa viwanda haziwezi kufikiwa ikiwa hakuna uwekezaji wa kutosha katika tafiti.

**96. Mheshimiwa Spika**, kwa kutambua umuhimu wa tafiti katika kukuza na kuendeleza Sayansi na Teknolojia; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kupitia CHADEMA imeeleza bayana katika sera yake ya elimu sura ya 6.1 inayohusu Mfumo wa Ugunduzi na Ubunifu juu ya umuhimu wa tafiti. Sera hiyo inaeleza kama ifuatavyo: *“Chadema inaamini kwamba msingi wa ugunduzi na ubunifu katika elimu unajengwa katika tafiti za kisayansi. Kwa hiyo, kwa kushirikiana na sekta binafsi, Chadema itawekeza kikamilifu katika elimu ya utafiti kuanzia elimu ya awali ili kumjengea mtoto uwezo wa ubunifu”*.

**M. ELIMU YA SIASA KATIKA VYUO VIKUU NA KATAZO LA SERIKALI KWA WANAFUNZI WA VYUO VIKUU KUJIHUSISHA NA SIASA**

**97. Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia menejiment za vyuo vikuu kwa muda mrefu sasa imekuwa ikiwakataza wanafunzi wa vyuo vikuu kujihusisha na siasa vyuoni. Wanafunzi wengi wamekuwa wahanga wa kufukuzwa vyuoni au kusimamishwa masomo kwa muda (suspension) kutokana na kuonekana kuwa wafuasi wa vyama vya siasa.

**98. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani isingekuwa na tatizo kama katazo hilo la kufanya siasa vyuoni lingekuwa ni kwa wanafunzi wote. Lakini imebainika kwamba kuna ubaguzi wa kiitikadi kati ya wafuasi wa CCM na wa vyama vya upinzani katika vyuo vya elimu ya juu. Wakati wanafunzi wafuasi wa CCM wanapewa ushirikiano wote na menejimenti za vyuo kufanya shughuli za siasa wale wa vyama vya upinzani wananyimwa haki hiyo na wengi wamefukuzwa vyuo na wengine kuondolewa kwenye nafasi zao za uongozi wa Serikali za wanafunzi. Itakumbukwa kwamba katika muundo wa kitaasisi wa CCM Umoja wa Vijana wa CCM unaunda mkoa wa Vyuo Vikuu. Kwa hiyo wanafunzi wote wa UVCCM katika vyuo vikuu wanaruhusiwa kufanya mikutano yao na wakati mwingine kuwakaribisha viongozi wa ngazi za juu za chama chao lakini hilo halionekani kuwa kosa kwao. Isipokuwa wakifanya wa vyama vingine ni kosa linalostahili kufukuzwa chuo. Huu ni ubaguzi wa hali ya juu na unajenga chuki na uhasama baina ya wanafunzi na tatizo hili lisipokemewa sasa tunakwenda kuwa na taifa lenye mpasuko kutokana na itikadi za vyama.

**99. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haioni mantiki ya Serikali kuwakataza wanafunzi wa vyuo vikuu kujihusisha na siasa vyuoni ilhali vyuo hivyo vinafundisha masomo ya sayansi ya siasa (Political Science). Kambi Rasmi ya Upinzani ilidhani kwamba kufanya shughuli za kisiasa kungekuwa kama mafunzo kwa vitendo hasa kwa wanafunzi wale wanaosoma masomo ya sayansi ya siasa na utawala ili kuonyesha umahiri na ubobezi wao katika masomo hayo



badala ya kuwakataza. Kuwakataza wanafunzi hao kufanya siasa ni sawa na kuwapa ujumbe kwamba hata masomo hayo ya siasa wanayosoma hayana maana yoyote na kwa hiyo ni bora yaondolewe kwenye mtaala.

**100. Mheshimiwa Spika**, Katiba yetu inaruhusu raia yeyote wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 na kuendelea kupiga kura au kuchaguliwa katika nafasi ya uongozi kupitia chama cha siasa kitakachokuwa kimemdhamini. Ruhusa hii ya kikatiba inawahusu pia wanafunzi wa vyuo vikuu ambao wanakidhi kigezo hicho cha umri. Kuwakataza kushiriki siasa ni kuvunja katiba ya nchi. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwaruhusu wanafunzi wa elimu ya juu kutumia haki yao ya kikatiba ya kushiriki shughuli za siasa vyuoni kwani ndio kundi linalotegemewa kutoa viongozi wa taifa hili.

## **N. HITIMISHO**

**101. Mheshimiwa Spika**, hotuba hii imeainisha maeneo mengi yenye kasoro na mapungufu katika sekta nzima ya elimu. Masuala yanayotakiwa kushughulikiwa mapema ili kukabiliana na mapungufu hayo ni pamoja na upungufu wa walimu, miundombinu, ubora wa vitabu, kuongeza bajeti ya maendeleo ya elimu, kutenganisha fedha za mikopo ya elimu ya juu na fedha za miradi halisi ya maendeleo, na masuala mengine ambayo yameainishwa katika hotuba hii.

**102. Mheshimiwa Spika**, hotuba hii pia imeeleza umuhimu wa sekta ya elimu katika ukuaji wa sekta nyingine za kiuchumi na hivyo kupendekeza kuwekeza zaidi katika elimu ili kuweza kufikia malengo ya kitaifa katika sekta nyingine hususani eneo la uchumi wa viwanda.

**103. Mheshimiwa Spika**, nimetoa pia angalizo la kutofanya majaribio katika sekta ya elimu, kwa kuwa madhara ya kufanya hiyo ni makubwa na endelevu kuliko yangefanywa katika sekta nyingine. Kwa sababu hiyo; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaendelea kusesitiza kwamba; Serikali isifanye siasa katika suala la elimu. Aidha; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kupitia kwa makini maeneo

yote yenye mapungufu yaliyoainishwa ndani ya hotuba hii na kueleza mikakati ya kuondoa mapungufu hayo.

**104. Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

Susan Anselm Jerome Lyimo (Mb)

**WAZIRI KIVULI WA ELIMU NA MSEMAJI MKUU WA KAMBI  
RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA ELIMU,  
SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI**

29 Aprili, 2019

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Susan Lyimo kwa taarifa ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa upande wa Wizara hii, tunakushukuru sana. Tunaendelea Waheshimiwa; nina orodha ya wachangiaji hapa kwa taratibu zetu, naanza na Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi na Mheshimiwa Phillipa Mulugo ajiandae kutegemeana na muda, ahsante. *(Makofi)*

Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwa mchangiaji wa kwanza katika Wizara hii muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeskiliza vizuri hotuba zote tatu, lakini kipekee napenda sana niwapongeze Wizara hii ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na Makatibu wao Wakuu pamoja na watendaji wote wa Wizara hii, kwa kazi kubwa ambayo wameifanya. Ipo kazi kubwa ya kuboresha miundombinu ya shule zetu zile kongwe ambayo imefanyika, kila mwenye macho anaona, kazi kubwa imefanyika, tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia taasisi ambazo wanazisimamia zipo taasisi ambazo zinafanya kazi nzuri, tunawashukuru sana. Na miongoni mwa taasisi hizo ni Bodi ya Mikopo; bodi hii tunaona kabisa kwamba sasa hivi inafanya kazi nzuri sana, tumeona kabisa wanafunzi sasa wanajielekeza kwenye masomo peke yake, hakuna mambo yale ya kugomea au ya kutafuta fomu za mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunawaomba pamoja na pongezi hizo lakini wazidi kuboresha kama ambavyo tumeendelea kushauri miaka yote, kwamba kwa kuwa hii ni Bodi ya Mikopo na ni mikopo, kama hata Mheshimiwa Rais amezungumza mara nyingi, basi ni vizuri hii mikopo isiwe na ubaguzi kwa maana ya mwanafunzi yeyote aweze kuwa na stahiki ya kuweza kupata mikopo kwa vigezo vile tu vya kitaaluma lakini visiwepo kwamba huyu sijui baba yake ni nani, huyu baba yake ni nani. Hii itakuwa ni nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwapongeze TCU; wamekuwa wanasimamia eneo hili vizuri, tumeona maboresho ya vyuo mbalimbali vikielekezwa kuboresha maeneo yao mbalimbali. Lakini niwashauri kwamba wasiwe sana wanafanya kazi kama matarishi, kama migambo, ni vizuri kwa kuwa hapa wanasimamia elimu wakae na wale wadau, haswa vyuo hivi ambavyo viko chini ya taasisi za dini, wazungumze nao, wawaelekeze na wawaelekeze mwelekeo wa Serikali unakotaka twende, lakini kuvifungia tu ama kuvinyang'anya baadhi ya kozi na kadhalika sio jambo zuri. Kwa hiyo, ni vizuri sana wakae na wadau hawa vizuri, hawa ni wadau wa maendeleo ambao wanasaidia katika Sekta hii ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Sera ya Elimu; juzi hapa niliuliza swali katika eneo hili linalogusa Sera ya Elimu, lakini majibu ambayo nimeyapata bado kwa kuwa ilikuwa kwenye swali nahitaji nipate ufafanuzi zaidi. Sera ya Elimu ya Mwaka 2014 imeweka bayana kwamba elimu ya msingi itaishia Darasa la Sita na Naibu Waziri wakati analijibu akasema sera sio msahafu, lakini sasa japokuwa sio msahafu

lakini hata mitaala inayotengenezwa inaishia Darasa la Sita. Maana yake ni kwamba wanafunzi wa Darasa la Saba ni kama wanakwenda kuota jua tu kwa mwaka mzima, wanapoteza muda. Kwa hiyo tunapenda tupate majibu yanayoeleweka; ni lini hii sera itatekelezwa kwa mujibu wa sera yenyewe ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, kwenye Sera ya Elimu vitabu bado ni tatizo. Hivi ninavyozungumza hapa Darasa la Tano mpaka sasa hivi bado vitabu vya huu mtaala mpya havijakwenda. Kwa hiyo, Serikali itumbie, hawa wanafunzi wa Darasa la Tano watasoma kwa vitabu gani? Maana wanaendelea sasa hivi tuko kwenye mwezi wa nne sasa, wanasoma vitabu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema juzi, kwamba sera sio msahafu inawezekana tukafika mpaka Darasa la Saba; sera hii mpya imefafanua kabisa kwamba mitaala ya elimu itaishia Darasa la Sita, hao Darasa la Saba watakuwa wanasoma mtaala upi maana hakuna kitu ambacho kimeandaliwa kwa ajili ya Darasa la Saba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sambamba na hilo kwenye hiyo Sera ya Elimu pia tupate majibu ni mitaala ya shule za mchepuo wa Kiingereza. Mpaka sasa hivi kuanzia Darasa la kwanza mpaka la tatu bado hawana vitabu, inabidi wachukue vitabu hivihivi vya Kiswahili wafanye *direct translation* ambacho sio kitu kizuri. Kwa hiyo, tunapenda kuona kwamba kuna vitabu vya mchepuo wa Kiingereza ambavyo vimeandaliwa kwa ajili ya watoto hao wanaosoma mchepuo huo. Na Waheshimiwa Wabunge, kwa taarifa yenu hapa tunazungumza watoto wengi ambao ni watoto wetu sisi Wabunge na watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine katika suala la elimu nizungumzie suala zima la watoto hawa wanaosoma shule hizi za *private*, watoto wetu. Ukisoma Katiba, Ibara ya 13(4) – wewe ni mwanasheria mbobezi – *inasema ni marufuku kwa mtu yeyote kubaguliwa na mtu au mamlaka yoyote inayotekeleza madaraka yake chini ya sheria yoyote au*

*katika utekelezaji wa kazi au shughuli yoyote ya mamlaka ya nchi. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hapa kuna ubaguzi wa wazi tunawafanyia watoto wanaosoma katika shule za *private*. Kwa sababu sasa hivi tuna elimu bila malipo kwa watoto ambao wanasoma shule za Serikali, lakini huku kwenye *private* wazazi tumekubali tunalipa ada, lakini kwa kuwa kuna ruzuku ambayo Serikali inatoa kusaidia watoto hawa wa shule za Serikali kwenye mitihani, basi hii iende pia kwenye shule za *private* kwa sababu na hawa ni watoto wa Watanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa bahati mbaya sana – Mheshimiwa Waziri ulitazame hili kwa kina – katika utoaji wa elimu kuna wadau wakuu kama watatu; kuna Serikali yenyewe na wewe kama Wizara na TAMISEMI lakini na hawa *private secor*, hizi *private schools* nyingi ni shule za dini na kwenye shule za dini mara nyingi wanatoa elimu hii kwa watoto wale wegine ni yatima kabisa ambao hawana uwezo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa watoto hawa hawana uwezo, mashirika ya dini yanasaidia kuchukua gharama zile za ada, Serikali ichukue jukumu tu hizi gharama ndogo ya kwenye ada za mitihani tuwasaidie ili waweze kuwa na usawa. Lakini hii haitakuwa haki kabisa kwamba hawa wanapata haki hawa wengine hawapati. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu hii Taasisi ya Elimu Tanzania; nimesoma hapa katika hotuba ya Wizara, ukurasa wa 147 kipengele kidogo cha (4) anasema "*Kuendelea na uandishi wa vitabu vya kiada kwa Darasa la Sita, Saba, Kidato cha Kwanza mpaka cha Sita na moduli kwa ajili ya Elimu ya Ualimu pamoja na kuandaa maudhui ya kielektroniki*".

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa changamoto iliyoko hapa ni kwamba mpaka sasa hivi mamlaka hii pia sisi tunadhani kwamba imeshindwa kwenye hili eneo la

uchapishaji wa vitabu. Na hili eneo huko nyuma lilikuwa linafanywa na *private sector*, tumepitisha Sheria hapa ya *PPP*. Sasa nasikitika kuona kwamba mamlaka hii kwa maoni yangu bado haijafanya vizuri katika eneo hili, kwa nini msikae na hao wadau wa sekta binafsi ninyi mkawa tu kama mwongozo kama ilivyokuwa kwenye ile Bodi ya *EMAC* zamani ambapo wachapishaji binafsi walikuwa wanapewa miongozo wanaandaa, *EMAC* inafanya *approval* na mwisho wa siku kitabu kinakwenda sokoni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake sasa hii ndiyo imetutia hasara kubwa ile ya vitabu ambavyo vimeondolewa katika mfumo, kwamba mamlaka yenyewe imechapisha vitabu, imeharibu na vimeondolewa katika mfumo. Lakini mpaka leo hatuambiwi ni hasara kiasi gani tumepata na nani amewajibika kwa hasara ile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri hebu hili lione kwa sababu tumepitisha Sheria ya *PPP* tuboreshe hii idara vizuri, Taasisi hii ya Elimu Tanzania iwe na majukumu mahususi ili majukumu mengine tuwaachie sekta binafsi waweze kufanya ili kama kutatokea hata kama kuna makosa tunaondoka kwenye *risk*. Maana yake sasa hivi tatizo ni kwamba taasisi inapofanya yenyewe inachukua pia na *risks* zinapotokea. Kwa hiyo, nikuombe sana kama mwanzo kulikuwa na nia njema lakini kwa nia njema hiyo tukae na hao wadau tuwashirikishe tuone katika eneo hili tunatokaje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa mchango wako. Mheshimiwa Phillipo Mulugo.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, kwanza ni-*declare interest*, mimi ni mwalimu na mdau wa shule binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuipongeza Serikali kwa maamuzi ya kutoa elimu bure nchini, na sisi tunaona na kama walimu tunaona kabisa namna ambavyo hali ni nzuri sana kwenye shule za msingi vijijini huko, wilayani, mkoani, mambo ni mazuri sana. Na hii inasababisha hata kuongezeka kwa uandikishaji na namna ambavyo *Form One* wanakuwa wengi, *Form Five*, kwa kweli hali ni nzuri sasa tumebaki tu kwenye ule ubora wa elimu (*quality education*) ndilo tatizo ambalo kidogo naomba Serikali niweze kuingia kuwashauri katika upande huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, dada yangu na rafiki yangu, Mheshimiwa Prof. Ndalichako, kwa kweli ni mtu ambaye ukienda kwenye dawati lake ukimueleza jambo anashaurika, pamoja na Naibu Waziri, na inatusaidia sana kupunguza baadhi ya kero. Ukienda ukimwambia Mheshimiwa kuna hiki na hiki kwa kweli anafuatilia na mambo yanakwenda vizuri, na ndiyo maana mmeona hata kelele zimepungua sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani siku kama ya leo wamiliki wa shule binafsi wangekuwa Dodoma hapa zaidi ya mia wanalalamikia mambo yanayoendelea kutokea huko, lakini baada ya kuingia Waziri huyu na Naibu wake wameweka dawati maalum pale Wizarani, pamoja na Katibu Akwilapo, wameweka baadhi ya viongozi, kamishna wanakaa pamoja wanajadili mambo ya kero zinazoendelea kutokea kwenye shule binafsi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema mwaka jana kwamba elimu ni ya wote, Serikali ina shule, Wizara ya Elimu ina shule, shule za mazoezi za sekondari na za *primary*, lakini TAMISEMI ina shule nyingi sana kwenye halmashauri huko na wadau; *TAPIE*, *TAMONGSCO* nao wana shule. Kwa hiyo, kwa pamoja nikawa nimeshauri kwamba tupate chombo fulani hapa juu kitakachokuwa kinamulika hizi shule zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nadhani nilitoa hilo wazo mwaka juzi, mwaka jana nikarudia, na mwaka huu

naendelea kushauri. Tupate chombo kitakachokuwa kinaangalia mifumo ya elimu nchini, kwamba shule za TAMISEMI zikaguliwe na chombo hicho, shule za Serikali zikaguliwe na chombo hicho na shule za binafsi zikaguliwe na chombo hicho kuliko kuacha Serikali yenyewe inajikagua yenyewe inafanya kila kitu yenyewe halafu inakwenda na kuwakagua wenzao, wakiharibu ndiyo wanawafungia, hii sio sawa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba kuendelea kumshauri Waziri, pamoja na hizi changamoto ambazo zipo za kitaaluma, za ubora wa elimu nchini, hebu tupeni nafasi na sisi tuwe tunawashauri mambo yatakwenda vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali kwa kuimarisha Idara ya Udhubiti Ubora wa Elimu Nchini. Kwa kweli Idara ya Ukaguzi – sasa hivi wanaita Udhubiti. Sasa hivi kwa kweli nimeona kwenye bajeti ya Waziri mtajenga ofisi, mtaongeza na magari, nimefarijika sana kwa sababu hii idara naifahamu vizuri sana, bila ukaguzi shuleni huko hakuna kitakachokuwa kinaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamesema wenzetu hapa, hata Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, kuhusu walimu wa Sayansi. Ni kweli kabisa huko shuleni, kwa sababu wanaotakiwa wakaone walimu wa Sayansi hawapo, vipindi vinafundishwa, *lesson plans* zinaandaliwa, ni wakaguzi ambao ndio wadhubiti ubora, naomba muwawezeshe wafike katika shule, wafike vijijini muwape wagari wakakague shule halafu walete ripoti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ndicho nilichokuwa nasema, kwamba hiyo ripoti kwa sababu wewe ni Serikali unajikagua mwenyewe ripoti unapeleka wapi? Tupate chombo ambacho hicho sasa ndiyo mtakuwa mnapeleka hizo ripoti ili hiyo ripoti inakuja inawasema jamani hapa ni pabaya, hapa ni pazuri, ndiyo hasa hoja yangu ya kusema kwamba tutafute chombo ambacho kitakuwa kinaangalia hizi shule. *(Makofi)*



Mheshimiwa Mwenyekiti VETA; miaka minne iliyopita tulikuwa tuna mpango wa kujenga VETA kila wilaya, na wakati ule ikiwa Wilaya ya Chunya tulichagua mahali fulani tujenge VETA, panaitwa Mkwajuni ambapo sasa hivi ndiyo Jimbo la Songwe. Sasa hii hoja sijui imekimbilia wapi, naona wanatangaza vyyo vya VETA 16 hapa lakini ile Mkwajuni haipo, Wilaya ya Songwe sasa sijui imetupiliwa mbali, sijajua. Kwa hiyo, ninaomba tayari tulishatafuta uwanja, hatimiliki tayari ipo ekari 100, mtuletee VETA pale Songwe, wilaya mpya kwa sababu kitika vigezo ilikuwa inakubalika, kwamba kuna migodi, kuna Ziwa Rukwa, kuna kilimo, kuna misitu ambavyo ndiyo vitu hasa vinavyosababisha tuweze kupata VETA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Shangazi kidogo amejaribu kutafuna zile *points* ambazo nilikuwa nimeziandaa, lakini ntazirudia tu katika ubora wa kualimu kwa sababu yeye sio mwalimu, mimi ngoja nizirudie upya. Kuhusu TET, Taasisi ya Elimu Tanzania, wanaochapisha vitabu; kwa kweli naweza nikasema, nitumie neno kwamba majanga bado ni makubwa, Mheshimiwa Waziri naomba tupia jicho pale. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu nitoe mfano mdogo tu; mwaka juzi Bunge tuliama, na Mheshimiwa Waziri alitamka, vitabu vyote ambavyo vilikuwa vimeletwa shuleni vimesambaa vilikuwa vibovu vikatolewa, aidha kama mmechoma, hamkutuambia mmepeleka wapi, mlivitoa, na sisi shule za *private* na sisi tukavitoa tukawa tumekula hasara kwa sababu sisi tulinunua, shule za Serikali waligawiwa bure ila sisi tulinunua kwa fedha zetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikawa nimemwambia Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wakati ule alikuwa bwana nani yule, nikataka kuandika barua, wenzangu walisema kwamba tuandike barua tuiambie Serikali na sisi watugawie bure kwa sababu makosa waliyafanya wao na sisi tulinunua kwao. Kwa hiyo, naomba hoja hii niilete tena mwaka huu, na leo nitashika shilingi kwenye kipengele cha Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba vitabu vyote ambavyo shule za *private* tulinunua vikaonekana ni vibovu tukavitoa, shule za Serikali zimeshagawiwa tayari bure na sisi tupewe bure kwa sababu tuligharamia aidha, mturudishie fedha zetu kwa sababu tulinunua kwenu ninyi wenyewe na mkaviharibu ninyi wenyewe, kwa hiyo naomba baadaye nitashika shilingi, leo nina shilingi kama tatu hivi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyosema Darasa la Kwanza hadi la Tatu hakuna vitabu vya lugha ya kiingereza kwenye shule za *English Medium*, amesema Mheshimiwa Shangazi hapa. Na Waheshimiwa Wabunge mjue watoto wenu wengi, asilimia 80 ya Wabunge mnasomesha watoto huko, hata Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wengine pale Wizarani, mnasomesha watoto huko; hatuna vitabu. Wanachofanya walimu wa shule za *private* ni kuchukua kitabu kilichaondikwa Kiswahili *Histori* wanakwenda kufanya *translation*. Sasa mwalimu wa *History* hajui kiingereza ila anajua *History*, anajua *content* ya Somo la *History* kwa kiingereza lakini hajui Lugha ya kiingereza kwa hiyo tunawapotosha watoto kule shuleni. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba hii Taasisi ya Elimu kama imeshindwa kazi warudishe kama mfumo wa zamani kuwapa ma-*publishers private* ili mambo yaweze kwenda vizuri. Naongea kama mwalimu na kama nina shule ambaye naona kule tunahangaika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jamaa mmoja yuko pale lringa ni muuzaji wa vitabu vizuri sana, nimemsahau jina lake. Anasema tuna miaka miwili tunatafuta vitabu havipo, na Serikali ilitoa mwongozo na waraka tuwe na *text mode* moja tu, yaani tuwe na kitabu kimoja nchi nzima tukitumie kama *text book*. Sasa umetu-*limit* tusinunue kwa *publishers* wengine, tunununue *TIE*, *TIE* huna sasa tufanyeje? Kwa hiyo, ninaomba Mheshimiwa Waziri, fanya ziara pale *TIE* uhakikishe vitabu vinatolewa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka juzi Serikali ilifuta baadhi ya tozo kwenye shule za *private*, lifuta tozo ya kodi

ya zimamoto (*fire*) na ikafuata na *SDL* na kodi ya mabango, lakini bado watumishi wa Serikali wa halmashauri wanakuja kwenye shule kuwasumbua wamiliki na wengine mpaka wanawaweka na ndani, na Mheshimiwa Waziri ntakupa ushahidi, wanasumbuliwa sana. Hebu tupeni basi tamko leo, tupeni waraka – hili na lenyewe ntashika shilingi – mtupe waraka unao sema mwaka 2017 Waziri wa Fedha alifuta tozo hizi na hizi kwenye shule za *private*. Kwa nini halmashauri kule wanasumbua, ndiyo maana nimesema kuna *disorganization* kati ya halmashauri, wizara na wamiliki, tukae pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ungeweka dawati la *dialogue* au wewe mwenyewe na Katibu Mkuu. Kama tulivyokaa siku moja Serena pale; mimi, wewe, Mheshimiwa Rweikiza, Mheshimiwa Esther na wadau mbalimbali, tukakaa tukaongea mambo yakaenda vizuri. Tuwe tunakaa angalau mara mbili kwa mwaka mambo yatakwenda vizuri sana. Kwa hiyo, ninashauri Mheshimiwa Waziri tufanye hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kingine naomba niishauri Serikali, mpaka hivi ninavyoongea – na hii ntashika shilingi baadaye...

**WABUNGE FULANI:** Ziko kumi.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** ...kabisa, ntashika shilingi.  
(*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Unashika shilingi eeh!

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna chuo chochote cha Serikali kinachotoa mafunzo ya walimu au kuna mtaala wa shule binafsi kwa *English Medium*. Labda nirudie tena; Waheshimiwa Wabunge naomba mnielewe, nimetoka kwenye *field* najua; hakuna chuo chochote chenye mtaala wa *English Medium* hapa Tanzania na Serikali haijajenga chuo hata kimoja, ila vipo vyuo vinafundisha mtaala huo kwa Lugha ya Kiswahili lakini hakuna kwa *English Medium*, ndiyo tukiwachukua walimu Kenya

tunakuja tunakumbana na matatizo makubwa sana ya namna ya *immigration* hapa Tanzania.

Naomba Serikali, katika hivyo vyo Mheshimiwa Prof. Ndalichako unavyovikarabati tenga kimoja *TET* watengeneze mtaala wa kufundishia masomo ya *English Medium* kwenye shule za *private*, mtakuwa mmetuokoa. Nasema hayo kwa sababu najua shule zinahangaika namna ya kutafsiri... tunatasiri na mitihani. (*Makofi*)

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Unga mkono hoja basi. (*Makofi*)

Mheshimiwa, unga mkono hoja.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja lakini nitashika shilingi kesho. (*Makofi/ Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mulugo kwa ushauri wako mzuri tu na mchango wako mzuri sana. Kwa jioni tutakuwa na Mheshimiwa Almas Maige, Mheshimiwa Hassan Elias Masala, Mheshimiwa Leah Komanya na Mheshimiwa Ismael Joram Hongoli, tutakwenda kwa utaratibu huo. Hakuna huko leo kuchangia.

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha Shughuli za Bunge hadi saa 11.00 leo jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge Lilitishwa hadi saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Nilikuwa nimewataja wachangiaji wetu wanne wa kwanza. Nianze na Mheshimiwa Alhaj Maige Almas.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kuniruhusu nami nichangie hoja hii ya hotuba ya Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia. Nami nitachangia mambo mawili tu. La kwanza, nitatoa shukurani kwa ajili ya kazi nzuri inayofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano, lakini nitachangia sana kwenye sera ambayo itakuwa na vijipengele viwili; kipengele cha Elimu ya Fundi kama ilivyo kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri lakini pia kipengele cha lugha ya kufundishia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pongezi kubwa kwa Rais Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa fedha nyingi ambazo amezitenga kwa ajili ya Wizara hii. Fedha nyingi ambazo zimefika ni pamoja na elimu bure na ujenzi wa shule, ujenzi wa madarasa na kwangu katika Jimbo langu la Tabora Kaskazini Uyui, tumepata fedha za kutosha karibu shilingi bilioni 1.3 kwa ajili ya ujenzi wa shule za *high school* na shule za msingi na shule za sekondari. Kwa hilo nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na watendaji wote katika Wizara hii Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye sera. Nianze kwa ufafanuzi wa maneno ambayo yamekuwa hayaeleweki; na katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuna baadhi ya ufundi hakuutaja kabisa; na ndiyo ilivyo katika Wizara ya Sayansi na Teknolojia. Kwa hiyo, nianze na *Technical Colleges* (Vyuo vya Ufundi). Hivi vinazalisha mafundi wanaitwa *technicians* au kwa Kiswahili ni Fundi Sadifu; na hili Mheshimiwa Waziri hakulitaja kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna vituo vya ufundi vinaitwa *VETA* kwa Kiingereza. Hivi vinazalisha *Artsans* ambao ni Fundi Mchundo. Sasa taaluma nzima ya fundi inafanya kazi hivi: Juu tuna *engineer*, wanatafuata *technician* halafu *Artsans*. Ni kama vile madaktari, ukiwatoa ma-*nurse* pale hawafanyi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka wataalam wa elimu wamweleweshe vizuri Waziri wangu. Waziri ametoka kwenye ule mfumo wa kuanzia *form one, form five, form six, university*.

Na sisi tumetokea shule za ufundi miaka minne ya ufundi uliochagua kama ni umeme au *Civil Engineering* halafu unaenda *Technical College* miaka mitatu unachukuwa *FTC*, unatoka kwenda kufanya kazi, unarudi unachukua *Diploma in Engineering (DE)* miaka mitatu, unakuwa na miaka kumi katika ufundi ambao umeusomea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *field* hii ikifa tutafanya jambo ambalo haliwezekani. Wahandisi hawawezi kufanya kazi na *Artsans*. Kwa hiyo, kunakuwa na *engineer* huku kichwani, kiwiliwili hakuna, kuna miguu (*Artsan*) kule chini. Kwa hili lazima lisahihishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba nzima Mheshimiwa Waziri ameongelea mambo ya vyuo. Neno "vyuo" akiwa na maana ya vituo vya *VETA*. Tunajenga vyuo vingi; hatujengi vyuo vingi, tunajenga vituo vya *VETA*. Vyuo vya ufundi ni *Dar Tech*. ilivyokuwa nao wakapelekwa watu pale wakajaribu kuifanya iwe *University College* au *University*. Ikaacha mfumo mzima wa ufundi ikaenda kwenye mambo ya *academicians*. Halafu kimebakia chuo kimoja *Arusha Technical College*, maana yake hata Mbeya mmebadilisha, siyo *college* ya ufundi, imekuwa *University*. Matokeo yake tunakuwa na *white collars* hatuna *Blue collars* katika *engineering* na jambo hilo haliwezi kufanikiwa hata kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba, kwangu nina shule 22 za *secondary school* na nina shule za msingi 222, hatuna chuo cha *VETA*. Vyuo vya Ufundi nafikiri nisimseme sana Mheshimiwa Waziri wangu, amenielewa; ni kwamba hakuna vyuo vya ufundi vinavyozalisha *technicians* wanaoitwa Fundi Sadifu. Fundi Sadifu ni tofauti na Fundi Mchundo. Serikali inajenga Vyuo vya Ufundi Mchundo ambapo katika elimu tunakokwenda huko kwenye Sera ya Uchumi na Viwanda hawatatusaidia *Artsans*, tunahitaji Fundi Sadifu (*Technicians*) hili lisahihishwe mara moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnaotuna wengi hapa, humu tuna mafundi; mimi ni fundi tena mkongwe. Wamo

mafundi wengine kumi humu ndani tumetokea Ifunda au *Moshi Technical*, au *Tanga Technical* au *Mtwara Technical College*, tukasoma *FTC* halafu tena tukarudi, tukachukuwa Diploma...

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa. Nataka nimpe taarifa muongeeji.

**MWENYEKITI:** Unataka umpe taarifa eeh! Mheshimiwa Maige, mnakutana mafundi mchundo.

### T A A R I F A

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa mzungumzaji kwamba ameitaja *Arusha Technical*. Hiyo *Arusha Technical College* sasa hivi kuna kozi ya kusuka nywele. Kwa hiyo, tunakwenda kuharibu utamaduni ule wa ufundi. Kuna kozi za kusuka nywele, kuna shule upishi. Wakati mimi nipo pale *Arusha Techn*. Zile kozi hazikuwepo. Sasa hivi tunaanza kuwachanganya, hatuwezi kupata mafundi kwenye *style* hiyo. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Almasi.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni sawa kabisa, nakubali, huyo ni Fundi Sadifu mwenzangu (*technician*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niendeleo kwenye suala la lugha ya kufundishia. Nimesema naongelea mambo mawili tu; kwa ufundi nafikiri niishia hapo, lakini nijikite hasa katika suala la lugha ya kufundishia. Suala hili limo katika Sera ya Elimu na limeelezwa vizuri sana katika sura ya tatu ambayo inahusu mambo ya maazimio na malengo na lugha ya kufundishia. Ninayo Sera ya Elimu hapa ya mwaka 2014 ukurasa wa 38 inasema: "lengo ni kutumia lugha ya Kiswahili katika kufundishia."

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako maelezo, lakini muda sina, ila wenye sera hii wakasome sura tatu ukurasa wa 37

mpaka 38. Sasa naomba ni nukuu: “lengo la kutumia lugha ya Kiswahili katika kufundishia.” Tamko, nasoma kipengele cha 3, 2 na 19. “Lugha ya Taifa ya Kiswahili itatumiwa kufundishia na kujifunzia katika ngazi zote za elimu na mafunzo na Serikali itaweka utaratibu wa kuwezesha matumizi ya lugha hii kuwa endelevu na yenye ufanisi katika kuwapatia walengwa elimu na mafunzo yenye tija Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo tafiti zaidi ya 30 kwa muda wa miaka 45, zote zinasema: “mtoto yeyote ataelewa masomo vizuri kama atafundishwa kwa lugha ya kwanza au ya pili ya mtoto huyo.” Tafiti zote zimesema Kiswahili ndiyo lugha ya kwanza au ya pili kwa Watanzania wote. Kwa hiyo Kiswahili ndiyo lugha pekee inayofaa kufundishia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hilo, kipo kipengele kidogo cha mistari mitatu kimechomekwa hapa, naomba nikisome. Ni kipengele cha 3.2.20: “Serikali itaendelea na utaratibu wa kuimarisha matumizi ya lugha ya Kiingereza katika kufundishia na kujifunzia, tena katika ngazi zote za elimu na Mafunzo.” Hivi vipengele viwili vinagongana na matokeo yake, imeacha nchi nzima isieleweke tunatumia lugha gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hilo, napenda kusema yafuatayo: kwa kuwa tafiti zimeonyesha kuwa Kiswahili ndiyo lugha ya kwanza na inazungumzwa na Watanzania wote ikitumika kufundishia, kujifunzia elimu na maarifa mafunzo, yataeleweka zaidi kwa walengwa; kwa kuwa Kiswahili ndiyo lugha ya Taifa na Tunu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ipo haya ya kwenda kutumia Kiswahili; na tatu, kwa kuwa tafiti zaidi ya 30 zilizofanyika katika miaka zaidi ya 40 zimeonyesha kuwa Kiswahili ndiyo lugha inayofaa kwa Tanzania kufundishia na kujifunzia; na kwa kuwa nia ya mabadiliko ya lugha ya kufundishia na kujifunzia ni pamoja na kuimarisha mbinu za kufundishia Kiingereza...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*



**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie; na kwakuwa muda sasa wa kumuunga mkono Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa juhudi zake kubwa za kukithamini na kukikuza Kiswahili. Hivyo, kitumike Serikalini, Bungeni na kuwa lugha ya kufundishia na kujifunzia katika ngazi zote za elimu na mafunzo nchini. Serikali ilete Bungeni hoja...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maige.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea, Mheshimiwa Elias Masala atafuatiwa na Mheshimiwa Leah Komanya na Mheshimiwa Hongoli ajiandae.

**MHE. HASSAN E. MASALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hotuba ya Waziri wa Elimu. Naomba nizingumzie mambo makubwa matatu. Jambo la kwanza ni kuipongeza Serikali, kuwapongeza watendaji pamoja na watumishi wote wa Wizara hii wakiongozwa na mama yetu, Mheshimiwa Ndalichako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mambo mengi sana ambayo yamefanyika, kwangu binafsi kwa niaba ya wananchi ambao ninawawakilisha hapa, nitakuwa mtovu wa fadhala kama sitatambua kazi kubwa ambayo wameifanya ndani ya Jimbo la Nachingwea hasa katika eneo hili la elimu. Uko uboreshaji mkubwa wa Chuo cha Walimu Nachingwea umetumia gharama kubwa sana na sasa hivi mazingira yamekuwa ni yakuvutia sana watu kuendelea kupata elimu katika eneo lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niunganishe na ombi moja kwa moja hapo hapo, pamoja na jitihada zile bado tunaomba pia tupate fedha kwa ajili ya kukarabati nyumba za watumishi katika eneo lile au katika taasisi ile Chuo cha Uwalimu Nachingwea. Nyumba zilizopo bado siyo nzuri na

hazivutii, lakini gharama yoyote ambayo mtakuwa mmetusaidia, basi mtakuwa mmeyaweka mazingira yale yawe ya kuvutia zaidi na hivyo kutoa elimu ambayo tunaikusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo pia nilitaka nipongeze ni suala zima la ajira mpya kwa walimu. Tunaishukuru sana Wizara, tumepata mgao wa walimu ingawa bado hawatoshi na changamoto kubwa tunayo katika eneo la walimu wa sayansi. Walimu ambao tumepatiwa kwa mahitaji ilikuwa ni 30 lakini tuliopokea ni chini ya asilimia 50. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri na wataalam wakeo hebu walione hili ili waweze kutusaidia tupate walimu wa kutosha ambao wataenda kutoa maarifa kwa vijana wetu katika shule zetu za Wilaya ya Nachingwea na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo nilitaka nichangie kupitia hotuba hii linalohusu namna ya kuwaendeleza walimu. Ukiangalia kada mbalimbali za Utumishi, ipo mifumo ambayo inawa-*favour* watumishi tofauti na kada ya walimu. Katika *level* za *Form Four* ambazo wamekuwa wanatumia vyeti kupata elimu ya ngazi ya cheti, wenzetu wa kada nyingine wamekuwa wanatumia vyeti hivyo kwa ajili ya kupata Diploma na Degree, lakini kwa upande wa walimu, nafikiri kwa wale walimu watakubaliana name; tumekuwa na changamoto kutoruhusu walimu wetu kutumia vyeti vya *Form Four* au vyeti vya *certificate* kutoka *Grade A* mathalani kwenda kupata ngazi nyingine ikiwemo Diploma au *Degree*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu wataalam wa Wizara ya Elimu wakae walione namna bora ambavyo tunaweza nayo pia tuka-*switch* na tukatengeneza utaratibu ambao utasaidia walimu au wale wanaojiendeleza na ualimu kutumia *certificate* kwenda ngazi nyingine za juu ili kuondoa urasimu ambao kwa sasa hivi upo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua imefanyika hivi kutokana na umuhimu wa kada ya elimu na labda lengo

lake ni ku-*impart knowledge* zaidi kwa walimu ili waweze kuwa walimu wazuri, lakini bado naamini mafunzo na mitaala ambayo wanaitumia kupata elimu yao, bado inaweza ikasaidia walimu hawa kujiendeleza na kupata elimu ya juu zaidi ya vyeti ambavyo wamekuwa navyo katika wakati tulionao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu ambalo nilitaka nichangie katika hotuba hii ni suala zima linalohusu gharama za uendeshaji katika vyuo vyetu. Serikali imefanya kazi kubwa ya kuboresha mazingira ya vyuo na sasa hivi vyuo vingi vikongwe vinapata huduma muhimu. Hata hivyo, bado zipo changamoto za kuhakikisha vyuo hivi vinajienda vyenyewe. Vyuo vingi sasa hivi wana changamoto ya kupata fedha kwa ajili ya kulipia umeme; vyuo vingi sasa hivi vinapata changamoto kubwa sana kwa ajili ya kupata fedha kwa ajili kugharamia na hata kulipia bili za maji. Yote haya ni kwa sababu Serikali kupitia kukusanya maduhuli, ikiwemo ada na vitu vingine, gharama hizi zote zimekuwa zinaenda Serikali. Kwa hiyo, mgao ambao wanarudisha katika vyuo vyetu haukidhi mahitaji ya vyuo vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kwa heshima na taadhima Mheshimiwa Waziri pamoja na wataalamu wake hebu walione hili, badala ya kuendelea kuwakatisha tamaa Wakufunzi ambao wako katika vyuo hivi vya kati au Vyuo hivi vya Ualimu, tuone namna tunavyoweza kurudisha sehemu ya gharama ili waweze kumudu gharama mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia hili kwa *experience* ya chuo ambacho nimekitaja, mara nyingi nimekuwa nawasiliana nao, nimeona namna wanavyohangaika kulipia sehemu ya gharama ambazo kimsingi zamani ilikuwa moja kwa moja wao vyuo ilikuwa na mamlaka ya kukusanya na kuweza kutumia moja kwa moja. Kwa hiyo, niliona hili nalo niliwasilishe kama sehemu ya changamoto na pia nipendekeze kwa Serikali ione namna bora ya kuweza kuliangalia hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la mwisho ambalo nilitaka nichangie katika Wizara hii ni suala nzima linalohusu gharama kwa ajili ya wanavyuo walioko katika hivi Vyuo vya Ualimu. Kwa mwaka sasa hivi wanafunzi wanalipa siyo chini ya shilingi 600,000/=. Nia njema ya Serikali kutoa elimu bure ambayo tunaiunga mkono na imeleta mafanikio makubwa sana, imeanza katika ngazi ya shule za msingi, tumekwenda mpaka sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipato cha Watanzania hawa ambao tumekuwa tunawapa elimu bure kuanzia msingi kwenda sekondari, bado kumekuwa na changamoto ya namna wanafunzi wanavyoweza kugharamia sehemu ya malipo kwa ajili ya kulipia hii Elimu ya Ualimu. Kwa hiyo, nimefanya utafiti kwenye baadhi ya vyuo, wanafunzi wengi wanashindwa kugharamia hizi gharama na imekuwa inaleta usumbufu kidogo katika kukamilisha mafunzo au masomo ambayo wamekuwa wanayapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pamoja na Serikali kuwa na mzigo mzito wa kukopesha wana vyuo katika ngazi mbalimbali za *Degree* na Shahada mbalimbali naomba nitoe ushauri kwa watu wa Wizara waone kama kuna uwezekano pia wa kuwaangalia hawa Watanzania ambao kwa sehemu kubwa wamenufaika na elimu bure mpaka wanavyofika katika ngazi hii ya elimu ya kati ambayo tukiweka masharti nafuu ya kuweza kuwafanya hawa wamalize vyuo vyao, basi tutakuwa tumejikuta tume-*groom* walimu wa kutosha ambao watakwenda kutoa elimu moja kwa moja katika maeneo yetu na hivyo tatizo la walimu litaenda kupungua kwa kiasi kikubwa sana. Jitihada hizi za Serikali ambazo zinafanyika, sisi tunaendelea kuziunga mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mwisho kabisa, nizungumzie suala linalohusiana na mgawanyo wa hawa walimu ambao tulikuwa tunawatawanya. Ukienda kwenye maeneo ya Sekta za Utalii, watu kama wa Kilimanjaro huwa wananufaika kwa sehemu kubwa sana na mgao ambao umekuwa unapatikana na vyanzo vile vya utalii na vitu mbalimbali. Hata hivyo, katika maeneo ambao kumekuwa

na vyuo ndiyo maeneo ambayo yamekuwa yanaongoza kwa kutokuwa na walimu wa kutosha. Wilaya kama Nachingwea mathalani, ni jambo la ajabu sana kukosa walimu hasa katika *level* za shule za msingi. Hapa tuna upungufu mkubwa sana, lakini walimu wengi wanazalishwa pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa namwomba Mheshimiwa Waziri, najua hivi vyuo ni vya Kitaifa na tunazalisha hawa walimu kwa ajili ya kuhudumia Taifa zima. Naomba tufanye upendeleo wa makusudi katika maeneo ambapo vyuo vipo, basi angalau tuone tunanufaika kwa kiasi kikubwa. Kwa hili, naomba nilete ombi kwa Mheshimiwa Waziri aiangalie Wilaya ya Nachingwea, mgao ambao tumepatiwa safari hii bado hauakisi idadi ya shule tulizonazo na wingi wa shule ambazo tunazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii imetupa changamoto ya namna kutoa elimu ambayo kimsingi tumekuwa tunaikusudia. Kwa hiyo, ebu tutumie chuo kile kilichopo Nachingwea kutupendelea kidogo ili tuweze kupata walimu ambao watatoka moja kwa moja pale na hasa wale ambao wametoka katika shule jirani kutoka maeneo yale ya Chuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatufanyi hivi kwa maana ya kuwabagua watu wengine, lakini ni ukweli ambao utakubaliana name, lazima moto unapodondokea kwenye mkono, basi yule ambaye umemdondokea aanze kujitoa yeye mwenyewe kabla ya mtu mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliomba nichangie hayo kwa ufupi sana ili kuweza kuboresha bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Masala kwa mchango wako na kwa kuokoa muda. Mheshimiwa

Komanya, atafuatiwa na Mheshimiwa Hongoli na Mheshimiwa Kigola ajandae.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba nianze kwa kuipongeza Wizara ya Elimu kwa kazi nzuri wanazozifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi naona juhudi za Mheshimiwa Waziri pamoja na wasaidizi wake, kwa kuendelea kuongoza vizuri Wizara ya Elimu. Nianze kwa kuishukuru Serikali kwa kuendelea kuboresha mazingira ya kufanya kazi Wakaguzi wa shule, yaani wadhibiti elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuamua kuwajengea Ofisi katika Wilaya 100 ambazo zitawasaidia kuwa na mazingira mazuri ya kufanyia kazi. Nashukuru katika Wilaya 50 zinazoanza, Wilaya ya Meatu imo na tayari Wilaya hizo 50 zimeanza kuletewa fedha za kujengea Ofisi zao. Naamini muda wowote pia Wilaya ya Meatu nayo itaingiziwa fedha tayari kwa kuanza kujenga Ofisi ya Wadhibiti ubora wa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa hatua ya makusudi iliyochukua kuweza kunusuru maboma yaliyokuwa yameanzishwa na wananchi ili nguvu za wananchi zisipotee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali kwa makusudi ya hatua ilichukua ya kuweza kunusuru maboma yaliyokuwa yameanzishwa na wananchi ili nguvu za wananchi zisipotee, binafsi nishukuru kwa Mkoa wa Simiyu tumeletewa Sh.1,337,500,000 kwa ajili ya kukamilisha madarasa ya sekondari 107. Naishukuru sana Serikali kwa hiyo nguvu za wananchi hazitapotea bure. Hata hivyo, binafsi nikupongeze wewe binafsi huwezi kujisemea kwa kazi nzuri unazozifanya Jimboni kwako kwa fedha zako binafsi kwa kuanzisha maboma na hatimaye leo umepewa maboma 54 yakiwa kwa Halmashauri ya Bariadi DC na *Bariadi TC* hiyo ni juhudi yako ndiyo maana umeletewa mengi. *(Makofi)*

Pamoja na hayo Serikali inatoa fedha nyingi sana kwa ajili ya elimu ikiwepo elimu bila malipo. Kwa makusudi Serikali imeamua kuifanya elimu ya sekondari kuwa elimu ya lazima. Pamoja na fedha nyingi zinazotolewa na zinatumiwa kama zilivyokusudiwa nilikuwa nina wazo moja la kuweza kuboresha ili fedha zitumike kama zilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo changamoto kubwa katika sheria. Sheria ya kuhakikisha mwanafunzi akianza sekondari ya kumbakisha mpaka anamaliza, zipo sheria ambazo zinasema mtoto haruhusiwi kupata ujauzito au kuoa au kuolewa lakini sheria ya kumbakiza shuleni haipo. Naomba Wizara ione iweze kuleta sheria ili tuweze kuipitisha ili Walimu wasiwe na matatizo, wale wanafunzi wanaokatisha masomo waweze kuchukuliwa hatua na hatimaye warejee mashuleni.

Mheshimiwa mwenyekiti, lakini Mkoa wetu wa Simiyu unayo changamoto kubwa tatizo la mimba kwa wanafunzi bado ni kubwa kwa mwaka 2017 tulikuwa tunamimba 196, mwaka 2018 mimba 187 lakini kwa makusudi wananchi wameanza kujenga hosteli kwa ajili ya watoto wa kike.

Ombi langu kwa Serikali ni ku-*support* nguvu za wananchi ili mabweni yale yaweze kukamilika na yanufaishe watoto wao. Manufaa si tu kwa ajili ya kupunguza mimba za wanafunzi, bali pia itawaweka pamoja wanafunzi wawe na mawazo pamoja wawapo shuleni na kuondokana na mawazo ya mtaani, lakini pia itaongeza ufaulu hususan kwa watoto wa kike kwa kuwa maeneo yetu yanafahamika hamna maeneo ya kuishi inabidi wakae kwenye majumba ya ndugu na jamaa na unavyojua tabia zetu sisi ukikaa mahali lazima ufanye kazi huwezi kukaa tu kwa ajili ya kusoma, lazima ufanye kazi katika familia unayokaa lakini hii pia inapunguza pia kiwango cha ufaulu kwa watoto wa kike. Pia mabweni haya yatapunguza ule utoro kwa wanafunzi, wanafunzi wamekuwa wakiacha masomo kwa sababu ya kutembea umbali mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jamii yetu pia ni wafugaji, kwa hiyo kuwepo na mabweni kutawasaidia

wanafunzi wale wabaki mashuleni. Binafsi niipongeze Wilaya ya Meatu kwa juhudi zake binafsi kwa kuanzisha shule maalum ya makao kwa ajili ya watoto wa wafugaji ili waweze kubakia pale. Niiombe Serikali iweze kuwasaidia juhudi waliyofikia. Wamekamilisha madarasa manne, wamejenga maabara mawili yanahitaji kukamilishwa, wamejenga bwalo moja linatakiwa kukamilisha. Namwomba Waziri mgawo utakaopatikana waone pia Shule ya Sekondari Makao ambayo iko katika Kata ya Mwangudo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, toka nianze Ubunge wangu hapa nilikuta shule ya *High School* ya Nyalanja ina madarasa sita ambayo hayafanyi kazi kwa kuwa hawana bweni. Shule ile ni ya bweni upande wa *High School* na *O-level* ni shule ya kutwa. Naomba basi ili kuwepo na thamani ya fedha yale madarasa sita yapatiwe bweni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa mara nyingi namfuata Waziri pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, naomba basi katika bajeti hii waisaidie *High School* ya Nyalanja ipate bweni tuweze kupata mchepuo mwingine ambao pia utawaleta watoto wa kutoka mikoa mingine. Sambamba na hilo pia inawasaidia wanafunzi wa shule ya kutwa wa *O-level* kuweza na wenyewe kuvutiwa kupata matamano na wenyewe waweze kufika kama wenzao walivyofikia.

Mheshimiwa mwenyekiti, lakini niseme changamoto moja ambayo niliona wakati wa ziara tukikagua *LAAC*, ni gharama kubwa ya kuweka umeme katika shule. Shule inaomba kuwekewa umeme inapohitaji kuweka *transformer* *TANESCO* inaiagiza shule ilipie, wakati huo shule haina uwezo wa kulipia gharama hizo kubwa kama milioni 12. Naamini kwamba *transformer* ile ikienda itasaidia pia kijiji kwa sababu katika yale maeneo kuna taasisi nyingine za Serikali pamoja na kijiji kwa hiyo haitafanya kazi tu kwa ajili ya Sekondari. Niiombe sasa Serikali itoe zile fedha zenyewe badala ya kuiagiza shule itoe zile fedha.



Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naomba kuunga mkono hoja na nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Leah Komanya kwa mchango wako mzuri na kwa maneno mazuri uliyosema kwa niaba ya Mbunge wa Bariadi. Tunaendelea Mheshimiwa Hongoli, nilisema atafuatiwa na Lutengano Kigola na Mheshimiwa Sikudhani Yasini Chikambo ajjandae.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia kwenye hotuba ya Waziri. Nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa namna anavyosimamia suala la elimu na idadi ya wanafunzi wameongezeka kutokana na uamuzi wake wa msingi kabisa kuhakikisha kwamba wanafunzi wote wanasoma bure hasa elimu ya msingi kuanzia awali mpaka kidato cha nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze sana Profesa Ndalichako, Waziri wa Elimu, Naibu Waziri wake, Naibu Waziri wake Mheshimiwa Ole Nasha, Katibu Mkuu wa Wizara hii ya Elimu na Manaibu Katibu Wakuu wote na watendaji wote kwa namna wanavyofanya kazi kwa weledi lakini pia kwa kujituma kuhakikisha kwamba kiwango cha elimu kinaongezeka nchini, niwapongeze sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie kidogo kuhusu suala la kwanza juu ya mikopo ya wanafunzi hasa mikopo ya elimu ya juu, kuna tatizo kubwa sana sasa hivi pamoja na kwamba wigo wa mikopo umeongezeka wanafunzi wengi wanapata mikopo lakini bado kuna idadi kubwa ya wanafunzi wengi wanakosa mikopo na hatimaye wengine kuacha kabisa kuendelea na masomo ya Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wengi wanaotoka vijijini maeneo ya vijijini wanakuwa wamedahiliwa, lakini wakifika Chuoni, kutokana na masharti yaliyopo au vigezo vilivyopo basi wanakosa na mwisho wa siku wanarudi tu vijijini na kuendelea na maisha pengine kufanya shughuli nyingine kuacha kabisa kuendelea na masomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Wizara lakini pia nishauri Serikali, nafikiri sasa tuanzishe utaratibu, kwa kuwa wanapewa mkopo na wanapewa na unaitwa mkopo siyo kwamba wanapewa bure tu, ni hela ambazo wanatakiwa warejeshe baada ya kumaliza masomo yao. Hivi ni kwa nini sasa tusiwe na utaratibu kwamba kama mwanafunzi amedahiliwa kwenda kuanza Chuo Kikuu apewe tu mkopo kama tunavyosema mkopo, akimaliza basi abanwe alipe na kwa kuwa sasa tunaona hata makusanyo ya mkopo yanaongezeka kutokana na jitihada zao, basi tuombe sasa tuwape mikopo wote wanafunzi ambao wanakuwa wamedahiliwa kwenda Chuo Kikuu, kuliko ilivyo sasa hivi, utakuta kwamba watoto wengi wa maskini, sisi tunaotokea maeneo ya vijiji Wabunge tunajua, tunajua namna gani watoto wanavyohangaika huko, kila siku watoto wamejaa milangoni, wanaomba tuwasaidie namna ya kusoma Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe sana Serikali yangu, tuamue tu kwamba sasa mikopo itakuwa kwa wanafunzi wote wanaoenda Chuo Kikuu mradi tu wamechaguliwa. Kama haiwezekani kuwasomesha watoto wote kwa kuwa wanafunzi ni wengi wanaosoma Chuo Kikuu, basi tuanzishe utaratibu kwamba kama tumeamua *division one*, *division two* ndiyo watakaopata mikopo, basi iwe hivyo ili mwanafunzi ajue mapema kwamba mimi nimepata *division three* au nimepata *points* ambazo haziruhusu kupata mkopo, basi aanze utaratibu pengine wa kujiunga na vyo vingine kuliko kuruhusu mtoto anadahiliwa anaenda Chuo Kikuu, anakosa mkopo mwisho wa siku wengine wanajiingiza kwenye tabia ambazo au mienendo ambayo haifai katika nchi yetu. Kwa hiyo niombe sana Mheshimiwa Profesa Ndlichako wakae huko ndani Serikalini washauriane namna gani ya kuwasaidia Watanzania hawa wanaotaka kuendelea na masomo ya elimu ya juu.

Mheshimiwa mwenyekiti, jambo la pili ni juu ya lugha ya kufundishia, tumekuwa *in dilemma* siku zote, ukiangalia hata sera yenyewe ya elimu unakuta kule ndani kuna *contradiction*, sehemu moja inafuatana sikumbuki sehemu

gani kama siyo 3.2 to nine inasema kwamba elimu ya kufundishia sasa itakuwa Kiswahili, lakini ukienda chini yake pale inasema kwamba elimu tutaendelea na kufundishia maana elimu ya sekondari kwa lugha ya Kiingereza sasa ni vizuri tukaamua, kwa sababu hawa watoto tunawachanganya wanapokuwa shule ya msingi wanasoma Kiswahili, wanapofika *form one* wanaanza Kiingereza kwa hiyo kwao inakuwa ni lugha ya pili sasa na kitaalam ni kwamba ili mwanafunzi asome vizuri ni vizuri atumie lugha yake ya kwanza. Hiyo Walimu wote tunajua na sisi wote Walimu tunajua kwamba lugha ya kwanza ndiyo inamwezesha mtoto ku-*acquire* maarifa kivizuri zaidi na aki-*acquire* vizuri kwa sababu uelewa wake ni mzuri ataendelea vizuri na mwisho wa siku atakuwa na ufaulu mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana ukiangalia matokeo, ukiangalia matokeo ya shule ya msingi, shule ya msingi wanafaulu sana watoto wakifika sekondari wanaanza kufeli. Kwa hiyo ukiangalia wanaoshindwa kuendelea na masomo ya kidato cha tano sekondari ni wengi zaidi ukilinganisha na walioanza pale *form one*. Ukichunguza ndani lugha ya Kiingereza ni shida Tanzania. Kwahiyo tuamue vizuri, tuamue kwamba tunaamua kufundishia Kiingereza, toka darasa la kwanza ama toka awali mpaka Chuo Kikuu au tunafundisha Kiswahili toka awali mpaka Chuo Kikuu. Kwa hiyo niombe tusibaki na *dilemma* hii itatusumbua kwa hiyo ni vizuri tukae tuamue kwamba ni lugha gani sasa tunaenda kufundishia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni juu ya udhibiti wa ubora. Niipongeze Serikali nipongeze hatua zilizochukua kuhakikisha kwamba zinaanza kujengwa ofisi, lakini pia tunaanza kuwanunulia magari. Tatizo la magari imekuwa ni changamoto kubwa sana ukienda kwenye halmashauri nyingi magari wanayotumia Wadhibiti Ubona yamechoka na siyo magari tu hata mafuta ya kwenda kufanyia ukaguzi hawana utakuta mara nyingi wanaenda kukagua shule binafsi zisizo za Serikali kwa sababu wale wanalipa ada wanatumia zile fedha kwa ajili ya kuwajazia mafuta na posho, lakini shule za Serikali imekuwa tatizo kwa

sababu wakati mwingine hawapati posho wanategemea halmashauri yenyewe iweze kuwachangia mafuta ili waweze kukagua na hili ndiyo jicho la Serikali kwenye upande wa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Wizara ya Elimu iwawezeshe Wakaguzi, Kitengo cha Ukaguzi ili muda wowote wanapooona kuna dalili za mwenendo kwenye shule fulani hauendi vizuri au taaluma haiendi vizuri waweze kwenda kukagua muda wowote ambapo anaweza akafanya hiyo kazi, kuliko wanavyokuwa na bajeti ndogo ya mafuta na magari yenyewe hawana ya kutosha, kwa hiyo inakuwa shida kwenda kukagua mpaka wasubiri wawezeshwe. Kwa hiyo hii sasa inazorotesha ubora wa elimu kwenye shule zetu. Hivyo, nimwombe sana ndugu yangu Profesa Ndalichako, yeye ni mtaalam wa elimu, lakini wote pia ni wataalam awawezeshe hawa Kitengo cha Udhhibiti Ubora ili waweze kupata fedha za kutosha kwa ajili ya kuendelea kufanya kazi zao vizuri ili tuweze kuboresha ubora wa elimu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme pia juu ya elimu ya ufundi, nilishauri mara kadhaa hapa, ni vizuri turudishe ule utaratibu wa zamani kwamba tuwe na shule za misingi za ufundi, kila kata kuwe kuna shule mojawapo ambayo itakuwa na mchepuo wa ufundi, lakini pia kwenye tarafa au kwenye halmashauri tuwe na Sekondari moja ya ufundi ili tuanze kuwazalisha mafundi michundo wengi. Iliyoye sasa hivi, mpaka mtu amalize *form four*, amefeli ndiyo anaanza kutafuta fursa ya kuajiriwa anakwenda kusoma Chuo cha VETA. Kwa hiyo tukianza huko chini kwanza tutakuwa na mafundi wa kutosha kuanzia shule za misingi, hata kama amemaliza la saba amefeli, hajaendelea na masomo ya sekondari ana uwezo wa kujitegemea kwa sababu ana *skills* ambazo zitamfanya aweze kujajiri yeye mwenyewe. Hivyo hivyo anayemaliza *form four* badala ya kusubiri ajira nyingine anaweza akaanzisha shughuli na mwisho wa hizo shughuli hizo ndogo ndogo zitafanya watu wengi waweze kuajiriwa kwa mfano kwenye useremala, kwenye umakenika mdogo kwenye ufundi uashi na ufundi mwingine, mwingine mwingi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe Serikali yangu tuanze kuanzisha huo, pamoja na kwamba tunaanzisha vyuo na tunaziboresha hizi *Focal Development Colleges*, hizi tuziwezeshe ni kweli, lakini pia tuangalie shule za msingi ambazo tunaweza tukaanzisha kwenye kila kata, lakini pia kwenye kila tarafa au halmashauri kuwe na shule ya ufundi na mwisho wa siku tutakuta kwamba tumepata wataalam wa kutosha kuliko ilivyo hivi sasa hivi. Kwa hiyo nimwombe sana Mheshimiwa Profesa Ndlichako na Mheshimiwa Ole Nasha na wataalam wengine wa Wizara, hebu wajifungie ndani waweze kuangalia namna gani tunaweza tukafanya haya mambo yote yaweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nikushukuru sana kwa nafasi hii na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hongoli kwa mchango wako mzuri. Tunaendelea na Mheshimiwa Kigola, Mheshimiwa Chikambo na Mheshimiwa Amina Makilagi wajiandae.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia. Nianze na kuipongeza Serikali, tumeona mambo mengi kwenye elimu imefanya vizuri, Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wake kazi inaonekana ni nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina machache tu ya kushauri; kwanza nipongeze kwa elimu bure, elimu bure ni kitu kizuri sana kwa Taifa letu na sasa hivi kuna ongezeko kubwa sana la watoto kuanza shule za awali, shule za msingi mpaka sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri sana na wazazi wamelielewa hilo na kufuatana na ongezeko la watoto, kuna shule nyingi sana sasa hivi zinajenga madarasa kwa ajili ya ongezeko la watoto, lakini na wazazi wako tayari kujenga madarasa kuhakikisha watoto wanasoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema elimu bure, wazazi walio wengi sasa hivi wameanza kupata uelewa, lakini zamani uelewa ulikuwa mdogo sana, walikuwa wanajua elimu bure ni kila kitu huruhusiwi kuchangia, lakini sasa hivi elimu waliyoitoa kwa wazazi nawashukuru sana wameanza kuelewa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watoto wanamaliza *form four*, bahati mbaya hawaendi *high school* wanaishia *form four*, sasa wale wanaoishia *form four* kwa kwenda sasa hivi hakuna na wale watoto kwa sababu bado hawajitimiza miaka 18 hawawezi kuajiriwa mahali popote, kwa hiyo basi Serikali ili kuwanusuru wale watoto ni kuhakikisha kwamba inajenga Vyuo vya VETA katika kila wilaya kama sera inavyosema. Kuna wilaya nyingine hazina VETA kabisa, kwa hiyo Serikali lazima ijikite kuhakikisha kwamba wale watoto wanaomaliza *form four* hawajachaguliwa kwenda *high school* waweze kwenda kwenye vyuo vya VETA, ili waweze kupata ujuzi na wakimaliza huko VETA waweze kuajiri wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni suala la msingi sana, tulienda Arusha kwenye Kamati yetu ya Bajeti, tukatembelea viwanda pale, bahati nzuri tukakuta watoto waliomaliza VETA wamepata ajira pale, ni mafundi wazuri sana mpaka tukajifunza kwamba kumbe watoto wakipitia VETA wanaweza kupata ajira bila matatizo hata akiwa hajafika *form four* na anaweza akafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuboresha elimu, tukisema tunataka kuboresha elimu siyo kwamba kubadilisha mitaala kila wakati. Sasa hivi *Open University* – Chuo Kikuu Huria Walimu wengi sana wanapenda kujiendeleza kwa kusoma vyuo vikuu, lakini chuo kikuu rahisi kabisa ni Chuo Kikuu Huria ambao tunasema *Open University*. Sasa nataka niishauri Serikali ili kuongeza wingi wa Walimu wasomi na tumesema kwamba Walimu kuanzia Diploma, mpaka *degree* mpaka *Masters*, sasa hivi Walimu wenye *degree* wanafundisha shule ya msingi na hilo tumeliona na huko ndiyo kuboresha elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali tuseme elimu bure kwa Walimu, yaani Walimu wapewe elimu bure, Mwalimu anayejitolea kwenda chuo, anaenda kufanya degree kwenye *Open University* asome bure kwa sababu yeye akimaliza ni faida ya Taifa, anaenda kufundisha watoto katika shule zetu. Kuna Walimu wengine kufuatana na mshahara kuwa mdogo wanashindwa kujiendeleza kusoma *degree*, kwa sababu mshahara ni mdogo. Kwa hiyo, tukifanya hivyo, tutakuwa tumemsaidia sana Mwalimu kujiendeleza. Tunabadilisha mitaala kila wakati haitusaidii kama hatuboreshi elimu kwa Walimu wetu, hii itatusaidia sana. Kwa hiyo nasisitiza kwenye hilo na nawapongeza Walimu wale wanaopenda kusoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu kuna jambo lingine ambalo siyo zuri sana, Mwalimu anamaliza *Masters*, anamaliza *degree* anarudi kufundisha shule, anakuja kupitwa mshahara na Mwalimu mwenye *certificate*, inamkatisha tamaa Mwalimu aliyesoma. Kwa hiyo ni lazima tuweke *grading system* ikae vizuri ili ku-*motivate* Walimu. Tumesema wafanye *degree*, wafanye *diploma* na ukiweka elimu bure na akimaliza shule aongezewe mshahara kufuatana na elimu yake, lakini anamaliza *degree* unampeleka shule ya msingi na mshahara ni mdogo, basi Mwalimu anakata tama, sasa hapo bado tutakuwa hatujaboresha. Nimeona hili niliongee kwa msisitizo sana kwa sababu kuna Walimu wengi sana wanapenda sana kusoma soma, nami nawapongeza ili kuhakikisha kwamba Walimu wanakuwa katika mazingira mazuri kwenye elimu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine kuna hizi *private school*, Mheshimiwa Waziri siku moja alisema wataleta kiwango cha ada. Kuwa na *private school* ni jambo zuri sana na elimu bora kwenye *private school* ipo tunaiona, wanafundisha vizuri, lakini ada ni kubwa sana. Wewe unaweza ukaona ada ya *private school* mtoto analipa milioni kumi, milioni nane, jamani hicho ni Chuo Kikuu, ni shule ya sekondari, ni shule ya msingi. Wengine wanasema kama unaona mtoto wako huwezi kupeleka huko, peleka shule ya Serikali, ndiyo watu wanajitetea, lakini hiyo ni elimu na

tunavyoongea hivi lazima tupime maana mtoto anataka apeleke kuzuri na mzazi anataka ampeleke mtoto wake kuzuri ili apate elimu nzuri, lakini lazima kuwe na *grading system* ya ulipaji wa ada. Sasa kwa mfano, shule ya msingi mtu analipa milioni 12 unaweza kuona pale sawa ni lugha na elimu, sawa ni nzuri lakini lazima kuwe kuna *fairness* kwa watoto na kwa wazazi.

## TAARIFA

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Goodluck Mlinga, taarifa kwa ndugu yako.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nataka nimpe taarifa kaka yangu Mbunge anayezungumza kuwa hata kwenye mahoteli, kuna *guest house* Sh.15,000 mpaka Sh.2,000,000. Kwa hiyo, chaguo ni la kwake hawajatulazimisha, tupo nchi ya kidemokrasia hii. Kwa hiyo, kama mtoto wako unaona akasome St. Kayumba mpeleke zipo shule za *private* ada kuanzia Sh.300,000 mpaka hiyo Sh.10,000,000. Kwa hiyo, chagua ni lako. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kigola unaonaje hapo, patamu eeh?

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna siku moja nilikuwa naongea nikasema hizi taarifa tunazozitoa tuwe makini maana unaweza ukatoa mfano ambao hauendani na elimu. Sasa wewe unatoa mfano wa gesti na elimu wapi na wapi, nashangaa, hizi taarifa tuwe makini sana. *Academics* na vitu vya biashara kama gesti haviingiliana hata siku moja. Hivyo Mheshimiwa hapo inabidi ujjipime mwenyewe na taarifa yako. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni uboreshaji wa mazingira ya walimu kufundishia. Walimu lazima waishi



kwenye mazingira mazuri. Kwa mfano, kuna shule nyingine unaweza kuona mwalimu ana nyumba yake pale lakini nyumba haina jiko.

Mimi nimeona kwenye jimbo langu, siwezi kuongea kitu ambacho sijaona. Kwa hiyo, tunaposema tunajenga nyumba za walimu tuhakikishe nyumba ina jiko na choo safi. Miundombinu ya nyumba ikakaa vizuri basi mwalimu anayefundisha shule ile atajisikia vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tumesema nyumba zote za walimu ziwe na umeme, hilo ni jambo nzuri sana. Kama nyumba ina umeme ataandaa masomo jioni na atakaa vizuri lakini kama mazingira ni magumu unampa ugumu mwalimu kufanya maandalio. Kwa hiyo, hilo nalo ni suala la msingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo la walimu wa sayansi, shule nyingi sana za sekondari walimu wa sayansi hakuna. Kuna siku moja tuliongea tukasema tutoe motisha kwa walimu wa sayansi, wale wanaosoma digrii ya sayansi wapewe mkopo asilimia 100, watu wengi watakimbia kuchukua masomo ya sayansi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Jimbo langu pale Mgololo mwekezaji amejenga shule nzuri sana. Bahati nzuri sana namshukuru Makamu wa Rais alikuja pale na alikubali kwamba ile shule itakuwa ni *high school* iatakuwa ni sayansi tupu. Sasa ikiwa ni sayansi tupu, wale wanafunzi wanaomaliza, kwa mfano mtu amesoma *PCB, PCM* akimaliza anaenda kusoma *engineering* au digrii ya ualimu wapewe mkopo asilimia 100. Sasa utaona mwanafunzi amesoma masomo ya sayansi magumu anaenda chuo kikuu mkopo hapati basi wanafunzi wanakwepa yale masomo, wanasema si nafuu tusome masomo mepesi tuendee na maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni msisitizo ingawa lina *connection* na TAMISEMI ni upandaji madaraja walimu, walimu wanalalamika. Mwalimu alimaliza mwaka 2012 mpaka leo hajapanda daraja, kwenye jimbo langu wapo.

Kuna mwalimu mwingine amemaliza mwaka 2014 hajapanda daraja mpaka leo. Kuna mwingine amemaliza 2014 amepanda daraja, wa mwaka 2012 hajapanda daraja. Sasa yule aliyeanza kuajiriwa hajapanda daraja aliyekuja kuajiriwa baadaye amepanda daraja, tayari yule ambaye hajapanda daraja inakuwa ni shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vibali vya kupandisha madaraja vitolewe. Ikitokea ongezeko la mshahara lazima yule aliyekuja kuajiriwa baadaye atapata mshahara mkubwa zaidi kwa sababu ndiye aliyeanza kupanda daraja yule aliyeajiriwa mwanzoni anakuwa na mshahara mdogo, kwa hiyo, inaleta shida kwa walimu.

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Sikudhani Yassini, Mheshimiwa Makilangi na Mheshimiwa Ester Mahawe wajandae.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijalia kusimama katika Bunge hili na kupata fursa ya kuchangia katika Wizara hii ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi lakini nimpongezee Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote katika Wizara hii kwa kazi nzuri wanazofanya. Nimesikiliza vizuri hotuba ya Waziri jinsi gani wamejipanga kuhakikisha wanaweka miundombinu salama kwenye suala la elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze ukurasa wa 8 wa hotuba ya Waziri ambapo amezungumzia Vyuo vya

Maendeleo ya Wananchi. Katika ukurasa huo amezungumzia Chuo cha Mbinga na Chuo cha Nandembo kilicho katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru. Kama nitakuwa na kumbukumbu sahihi, Chuo kile cha Nandembo majengo yake yalijengwa mwaka 1947, majengo yale yalikuwa ya *mission* lakini yalikabidhiwa Serikalini kwa maana ya kuanzisha chuo mwaka 1978.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshawishika kusimama na kukiongelea chuo kile kulingana na mazingira magumu yalikuwepo pale. Waziri amesema kwamba anafikiria kutenga pesa kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu. Nimesimama kwa ajili ya kutaka kumkumbusha Mheshimiwa Waziri kwamba katika mwaka wa fedha 2017/2018 chuo kile walikitengea shilingi milioni 700 kama sijasahau kwa ajili ya kujenga karakana lakini mpaka leo nimesimama hapa pesa zile hazijanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la kuanzisha vyo hivi ni kwa sababu siku za nyuma shule za sekondari zilikuwa chache. Watoto wanapomaliza darasa la saba walikuwa wanapelekwa kwenye hivi vyo kwa ajili ya kupata stadi mbalimbali za kazi ikiwepo useremala, ufundi magari, cherehani, mapishi na mambo mengine mbalimbali. Cha ajabu na ambacho kinachonisikitisha naona sana kipaumbele si kwa vile vyo, hatuwasaidii watu wale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia chuo hiki ambacho nakizungumzia majengo yake ni chakavu. Mheshimiwa Waziri siku za karibu alikuja Mkoa wa Ruvuma kwa ziara Mheshimiwa Rais lakini nimwombe aje rasmi atembelee Halmashauri zetu za Mkoa wa Ruvuma ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru ili ajionee mazingira yaliyopo. Katika chuo kile walimu wanaotakiwa ni 17 lakini tuna walimu watatu (3), hivi kweli tunakusudia kuwasaidia watoto kwenye lengo letu lile ambalo lilifikiriwa na Serikali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli tuna dhamira ya dhati ya kutaka kuwasaidia watoto wetu kupata stadi

mbalimbali ni vizuri tukaona umuhimu wa kutenga hata hao walimu ili kuwapeleka kwenye maeneo haya waendeleo kusaidia. Pia itapendeza zaidi kuweka miundombinu na kujenga hizo karakana ambazo zitasaidia sana wanafunzi ambao watakuwa katika shule hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala ambalo wenzangu wamelizungumza la watumishi mbalimbali katika Wizara hii na hususani walimu. Nimeona hivi karibu Mheshimiwa Waziri Jafo akisema kwamba wameajiri walimu na amesisitiza walimu wale waende katika shule zile ambazo wamepangiwa. Sina hakika kama wameangalia matatizo yaliyopo kule. Kama kweli wameangalia matatizo yalipo kule sina shida lakini wamezungumza Wabunge wenzangu kuhusiana na suala la walimu na mimi naomba nisisitize kwamba mpaka hivi tunavyozungumza kwenye shule zetu walimu ni wachache, kwa hiyo, ni vizuri Serikali ikaongeza spidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kwanza kabla ya kuangalia wale walimu ambao walikuwa na vyeti feki na walimu hewa lakini siku za nyuma pia tulikuwa na upungufu wa walimu, kwa hiyo, tuna mapengo hayo ya kuhakikisha tunayaziba. Kwa hiyo, niombe hii Serikali ya Chama cha Mapinduzi, Serikali sikivu kupitia Waziri, Mheshimiwa Profesa Ndalichako hakikisheni jambo hili la kuajiri walimu linapewa kipaumbele. Hata sisi tulioko humu ndani kama siyo walimu tusingeweza kufika hapa.

Kwa hiyo, jambo hili ni jema katika kuhakikisha tunapanga walimu katika shule zile. Ukienda kwenye shule nyingine inasikitisha, shule inatakiwa walimu 10, 15 unaweza ukakuta walimu 2, hatuwasaidii watoto. Kwa hiyo, naomba sana tuzingatie hilo kupitia Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nizungumzie suala nyumba za walimu, wenzangu pia wamesema na mimi naomba niseme walimu wetu walio wengi wanaishi katika mazingira magumu sana. Mazingira pia ya kufundishia yanashawishi pia mwalimu kuwa mzuri katika eneo

analofanyia kazi. Niombe sana Mheshimiwa Prof. Ndalichako suala la nyumba za walimu na madarasa lipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wetu wa Ruvuma, sina hakika ns maeneo mengine lakini mpaka hivi ukienda unaweza ukakuta madarasa ambayo yameezekwa kwa nyansi. Ndiyo maana nimemuomba Mheshimiwa Waziri akimaliza bajeti hii afike kule aone hali halisi ili haya tunayozungumza Waheshimwa Wabunge kupitia vikao hivi basi hata yeye ataenda kuona uhalisia. Darasa moja watoto wa darasa la tano wanaangalia ubao upande mwingine, watoto wa darasa la sita wanaangalia upande mwingine. Unaweza ukaona ni kitu cha ajabu lakini hivyo vitu vipo katika maeneo yetu mpaka hapa tunapozungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni jukumu la Serikali kuhakikisha tunaondoa hizo changamoto. Yapo mambo mengi mazuri yanafanyika lakini palipo na mambo mengi mzuri lazima kuna changamoto na changamoto lazima kuzibaini na kuzitafutia ufumbuzi wake. Mheshimwa Waziri hali za elimu kule ni ngumu, nasisitiza sana mama yangu mpendwa uje mkoani uone si tu ukikaa pale ukitembelea Kigoma unakuta umemaliza mkoa njoo na Ruvuma uone hali ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la Wakaguzi wa Shule. Suala hili Waheshimiwa Wabunge wenzangu wamelisema na mimi naomba nisisitize jambo hili. Wakaguzi hawa wa Shule wana mazingira magumu. Kwenye Halmashauri zetu sisi Wabunge ni Madiwani unaona jinsi gani Wakaguzi hawaendi kwa mujibu wa ratiba kutembelea zile shule na kuangalia mwenendo mzuri wa elimu yetu. Nikuombe ipo haja sasa ya kuhakisha Wakaguzi wanapatiwa magari, mafuta na wanawezeshwa kwa namna moja au nyingine ili wafike kwenye maeneo mbalimbali ili tupokee taarifa zilizo sahihi vinginevyo tunaendelea kupokea taarifa zinazopikwa kila mwaka kwa sababu hawana uwezo wa kufika kwenye maeneo yale. Nalisisitiza hili naamini kabisa ni sehemu ya kuboresha elimu yetu, elimu ya msingi pia ya

sekondari, nasisitiza sana Wakaguzi wana hali ngumu katika Halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la kupandishwa vyeo walimu, nina hakika ni haki ya mtumishi kwamba anapostahili apate lakini wengi wamekuwa wakilalamika na hawapati fursa hizo. Nimwombe Mheshimiwa Waziri toa maagizo katika maeneo yanayohusika inapofika wakati mwalimu anastahili kupandishwa daraja, apandishwe kwa sababu ni haki yake. Katika maeneo mengine walimu wamekuwa wakilalamika kwamba anatakiwa kupandishwa daraja lakini hapandishwi, tunawakatisha tamaa walimu wetu kufanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la uhamisho wa walimu. Naamini Wizara hii inategemeana na Wizara ya TAMISEMI. Tunalo tatizo, walimu wengine na hasa maeneo ya vijijini wanakaa kule kana kwamba ni adhabu. Mwalimu anamfundisha mama mtu, mtoto mtu, mjukuu mpaka anazeeka kwenye shule ile ile. Inafika mahali inaonekana kama kuna upendeleo fulani katika uhamisho wa walimu. Niombe tuzingatia na tuwaangalie wale walioko vijijini, tutoe motisha kwa walimu wetu ili waendeele kufanya vizuri. Inapoonekana kwamba nay eye anatakiwa apate uhamisho basi ni vizuri ahamishwe aende maeneo mengine lakini anakaa anamfundisha mama/baba mtu, mtoto mpaka mjukuu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga nkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya, umeeleweka. Tunaendelea na Mheshimiwa Amina Makilagi, Mheshimiwa Ester Mahawe na Mheshimiwa Grace Tendega wajiandae.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Naomba nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu na nikushukuru wewe kwa kuniwezesha kusimama na kuweza kutoa mchango wangu katika sekta hii muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja hii iliyo mbele yetu. Naiunga mkono kwa sababu Wizara ya hii ya Elimu ukilinganisha na tulipotoka kazi kubwa na nzuri inafanyika katika sekta hii. Naomba kabisa nimpongeze Waziri Mheshimiwa Prof. Ndalichako; Naibu Waziri, Mheshimiwa Olenasha; Katibu Mkuu na watendaji wake na timu nzima ya Wizara ya Elimu kwa kazi njema na kubwa mnayoifanya ya kuhakikisha sekta ya elimu sasa inaleta tija kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Mheshimiwa Prof. Ndalichako Mungu akubariki sana, ni mama usiyejikweza, unafanya makubwa ukisaidiana na wenzako. Leo wakati unawasilisha ulikuwa unatuonyesha kwenye picha, kwa kweli umetushangaza, tumeona maghorofa yanavyojengwa mikoani mpaka Nyasa na maeneo mengine. Wote huo ni ubunifu wako pamoja na watendaji wenzako, mimi na wenzangu tunakuunga mkono. Niungane na Mheshimiwa Rais alipokuwa kule Mtwara alitamka bayana kwamba anafurahishwa na kazi yenu, chapeni kazi na muendeleo kusonga mbele, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba asitokee mtu yeyote kuwakatisha tamaa kwa sababu Waswahili wanasema vizuri vyajiiza na vibaya vyajitembeza. Maana watu wamezoea akifanya kidogo kashatoka kwenye *media* siyo Mheshimiwa Prof. Ndalichako na wenzake, wanafanya vitu vikubwa vinajitangaza vyenyewe. Hongereni sana, endeeleni kuchapa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niungane na maoni ya Kamati yangu ya Huduma za Jamii. Kwa mujibu wa taarifa iliyowasilishwa hapa Serikali inafanya kazi nzuri sana ya kupeleka fedha katika sekta hii. Unaona fedha ya miradi

ya maendeleo karibu asilimia sitini na kitu imekwenda, *OC* zaidi ya 37%, mishahara ni karibu 100%. Hata hivyo, naomba niungane na maoni ya Kamati kusema kwamba fedha inayopelekwa hailingani na kazi ya sekta hii. Naomba niishauri Serikali na Waziri wa Fedha kama yupo anisikilize, sekta hii naomba ipelekewe fedha 100% kama iliyopangwa ili miradi ya maendeleo itekelezwe na fedha za *OC* siweze kufanya kazi yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya ziara sisi kama wana Kamati, tumetembelea chuo cha *DUCE* tumeona kazi nzuri sana iliyofanywa na Serikali, fedha zaidi ya shilingi milioni 500 zimekwenda. Ukiangalia kuanzia taarifa ya Waziri na ya Kamati fedha zilizotengwa hazikwenda zote matokeo yake mradi hakuna kinachoendelea. Tumekwenda Chuo cha Mwalimu Nyerere pale Kigamboni, kuna fedha iliyotengwa kwa ajili ya mradi mpaka tunakwenda kukagua hakuna fedha iliyokuwa imekwenda. Naomba sana na bahati nzuri Waziri wakati tunaongea nawe kwenye Kamati ulituhakikishia kwamba kwa sababu bado miezi inaendelea itatafutwa fedha na kupelekwa, naomba nami nisisitize hilo kwa sababu hii ni fedha ambayo tulitenga kwenye bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha ya *OC* ndiyo inakwenda kulipa Wahadhiri wetu. Kwa mujibu wa taarifa iliyowasilishwa na tulizozipata tena kupitia kwa Wenyeviti wa Bodi, Wahadhiri wetu wana madai yao ya kodi ya nyumba. Mhadhiri ni kiongozi, ni mtumishi, ameaminiwa, anafanya kazi kubwa lakini hana uhakika wa kuishi. Naiomba Serikali yangu Tukufu na sikivu hebu pelekeni hizi fedha za *OC* ziende kulipa madeni ikiwepo na fedha za watumishi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba nitoe ushauri, kazi nzuri tuliyoiona pale Mwalimu Nyerere na *DUCE* kupitia vyanzo vya ndani wameweza kujenga miundombinu. Naomba nitoe ushauri, vyo vingine na kama ambavyo Kamati tumesema igeni mfano wa vyo hivi, kwa sababu vyanzo vya mapato vya ndani vipo lakini wakati mwingine havitumiki vizuri wote tunasubiri Serikali Kuu. Naomba tuwaige



hawe *DUCE* na Mwalimu Nyerere ili na vyuo vingine viweze kutengeneza miundombinu kwa kutumia vyanzo vya ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nivishauri vyuo vyote nchini vikiwepo vyuo vikuu na vyuo vya ufundi kubuni vyanzo vingine vya mapato. Sisi kwenye Kamati tuliona kuna uwezekano wa kubuni ambavyo vitafanya vyuo vijijendeshe bila kutegemea ruzuku kutoka Serikali Kuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye Chuo cha Julius Kambarage Nyerere cha Sayansi ya Kilimo ambacho kwa mujibu wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambaye na mimi ni mdau niliyeshiriki kuiandika na kutafuta maoni ya wananchi, tulipofika Mkoa wa Mara na kwa Watanzania walituambia wanataka mawazo ya Mwalimu yatimie. Mwalimu Nyerere na wenzake walitoa eneo bure kwa Serikali, walijinyima wakatoa zaidi ya heka karibu 450 kwa ajili ya kujenga chuo. Mwalimu Nyerere akajenga miundombinu ikiwemo Bwawa la Kialando, bwawa la mfano ili kesho na kesho kutwa kijengwe chuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chuo hiki kiliwekwa kwenye Ilani, ukurasa wa 101, Ibara ya 52, kifungu cha K, kifungu cha pili kidogo kinaeleza bayana kwamba, endapo CCM itachaguliwa 2015 – 2020, Chuo cha Mwalimu Nyerere Butiama kitajengwa. Nimefurahishwa na kazi inayoendelea kwa ajili ya ujenzi wa chuo hiki. Tumeona mipango kwa ajili ya kutafuta hati miliki.

## T A A R I F A

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Getere.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** *Okay.*

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nilitaka kumpa taarifa mzungumzaji kwamba kwenye ukurasa katika Chuo kilichozungumzwa hapa cha Mwalimu Nyerere kinachozungumzwa pale ni kwamba Chuo kijiandae kufundisha wajasiriamali kiangalie watu wanaokamua na kuangalia kuku, sio kufundisha wanafunzi waliokuwepo hapa. Kwa hiyo, mambo mengine yaliyoandikwa humu ni kwamba nataka kumpa taarifa kwamba aendeleo kuona kwamba hiki Chuo ni muhimu sana na wanaohusika wakione kama Chuo cha Mwalimu Nyerere sio kwenda kufundisha kuku. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, taarifa naipokea kwa sababu Mbunge Getere ni Mbunge mwenzangu wa Mkoa wa Mara, na hivi karibuni tulikuwa kwenye kikao cha RCC. Moja ya agenda zetu ilikuwa pia ni kuzungumzia Chuo cha Mwalimu Nyerere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapongeza kwa haya yaliyofanyika, nimeona mmehangaika kutafuta hatimiliki, sasa tunataka tujue hivi mmeishia wapi, kwa sababu, suala la upatikanaji wa hatimiliki hata kwa mtu wa kawaida. Siku hizi kwa sababu Serikali ya CCM imerahisisha miundombinu, na tumeletewa Ofisi iko katika Kanda ambayo Ofisi yetu iko Simiyu wiki mbili unapata hati. Inakuwaje leo Chuo cha Mwalimu mpaka leo hati haijapatikana, changamoto ni nini? Tunapongeza mambo yanayofanyika kuna maandiko yameandikwa, kuna mafunzo yanaendelea pale kwa ajili ya kuanzisha hiki Chuo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nijue Mheshimiwa Prof. Ndalichako mama ninaye kuamini, na mama ninaye kupenda, na kwenye Kamati pia nilikuuliza kwenye Randama yako nimeona umetenga bilioni moja, nilitaka nijue ni za nini?. Nataka kujua hizi fedha kwa ajili ya kujenga Chuo, na hasa kwa kuzingatia kwamba tunaelekea mwaka 2020 mwisho wa Ilani hii ya CCM ambayo tuliiahidi kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujua fedha kwa ajili ya ujenzi wa Chuo hiki, ziko wapi? Na ningependa kujua chuo kinaanza lini? Kwa sababu Serikali imeshawekeza, Mbunge wetu mpendwa, Mzee wetu, Mzee Mkono na Mungu ampe Wepesi apona, arudi Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, amejitahidi kujenga majengo na akayatoa bure kwa Serikali ilikuwa ni shule ya *High School* tukawaondoa watoto, majengo yapo na pa kuanzia palikuwepo kuna Chuo cha Kisangwa ambacho tulisema itakuwa ni sehemu ya Chuo Kikuu kile. Kuna maeneo ya Chuo cha Bweri, maeneo ya kule Rorya, tulisema yote yatakuwa ni sehemu ya Chuo, wakati tukijandaa kujenga miundombinu. Ningependa kujua hivi Mheshimiwa Waziri, Mkakati ni nini kutekeleza ndoto za Mwalimu alizozitoa akiwa hai, na kama kweli tuna lengo la kumuenzi Baba wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujua Mheshimiwa Waziri na timu yako, hivi ninyi mnaonaje, mmeshaajiri wafanyakazi tena wenye weledi, yuko Profesa pale Mkuu wa Chuo, mpaka amestaafu yule anayekaimu sasa ndiyo amekuwa Mkuu wa Chuo. Analipwa mshahara pamoja na watendaji wenzake zaidi ya kumi na nne, leo hakuna kinachoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda Mheshimiwa Waziri, hebu utakaposimama hapa, Watiamu, narudia tena Watiamu, akiwemo Baba wa Taifa aliyetangulia mbele ya haki. Ninapozungumza Watiamu naongelea Wazanaki wa Butiamu, walio kuwa na dhamira hiyo ya kujenga Chuo, wanataka leo wakusikie kauli yako, Chuo kitajengwa na Chuo kitafunguliwa na lini, ndiyo walichotuma leo nilete hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie ujenzi wa miundombinu ya shule ninapongeza sana Serikali yangu Tukufu ya Chama cha Mapinduzi, imefanya kazi nzuri ya kujenga miundombinu ikiwemo Vyuvo vikuu na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze kama mama...

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, liko tatizo Mheshimiwa Waziri kwenye suala la miundombinu na hasa katika mabweni katika Vyuo Vikuu watoto wetu wa kike wanakaa katika maisha...

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa,

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wanapanga kwenye majumba matokeo yake wanakuwa ni wake wanaolewa na watu.

**MWENYEKITI:** Muda wangu sio rafiki.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wanakosa kodi za kulipa wanatembea masafa marefu...

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na hata Vyuo vya Dar es Salaam kwenda kutafuta hiyo huduma. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Muda wangu sio rafiki.

**MBUNGE FULANI:** Naam...

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Waziri Ndalichako utakapokuja hapa..

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Baba alikuwa anatoa taarifa huku.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mmejipangaje, kujenga miundombinu kwa ajili ya hosteli ya wasichana, Chuo cha DUCE, Chuo cha Mwalimu Nyerere, Chuo cha Ardhi na Vyuo vyote nchini tumejiandaaaje ili kuwanusuru watoto wetu wa kike ambao wanaingia kwenye dhahama ya kulipa kodi kiwango ambacho ni kigumu, na sio kwa watoto wa kike peke yake...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Makilagi.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naongelea na VETA, kuna VETA hapa zinajengwa nchini naomba na Kisangwa iliyoko Mkoa wa Mara hebu ipe kipaumbele kwa sababu majengo pia yapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. *(Makofi)*

Mheshimiwa Ester Mahawe, Grace Tendega na Pascal Haonga ajiandae.

**MHE. ESTER A. MAHAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii, ya mimi nami kuweza kutoa mchango wangu, katika Wizara hii ya Elimu, naomba ku-*declare interest* ni mdau wa shule binafsi na mwalimu kwa taaluma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuweka tu rekodi vizuri, kwa mchango wa Kaka yangu Kigola, ninaomba ndugu zangu Watanzania, tutofautishe *English Medium Schools* na *International Schools* hivi ni vitu viwili tofatuti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *English Medium Schools* ni hizi ambazo hakuna *English Medium Schools* Tanzania

ninayoifahamu ambayo ina-charge zaidi ya 4.5 million, hakuna hata moja, hata moja, zingine zote zinazo-charge above that ni International Schools. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu mjadala tulishaufunga ni uchaguzi huria, kama ilivyo hoteli kama ilivyo huduma nyingine yoyote, nadhani ifike mwisho mambo ya kujadili ada elekezi na vitu vya namna hiyo kwa sababu mtu halazimishwi.

**MBUNGE FULANI:** Tuongeele humu ndani.

**MHE. ESTER A. MAHAWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, amlete shuleni kwangu ada ya *day* ni laki nane na nusu kwa mwaka, milioni mbili kwa mwaka kwa bweni, mwambie aje kwangu, hiyo nayo itamshinda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuweka hiyo rekodi sawa, ninaomba sasa nimpongeze sana Mheshimiwa Prof. Ndalichako, kwa kazi nzuri inayofanyika ya kuinua Elimu katika nchi hii. Naibu wako Mheshimiwa Ole Nasha, Dkt. Akwilapo, Katibu Mkuu, Mama Ave Maria Naibu Katibu kwa kweli watu hawa wanaipeleka elimu yetu mahali pazuri pamoja na kwamba changamoto ndogo ndogo zipo nina hakika nia ya dhati na njema ipo ya kuhakikisha tunamaliza changamoto hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo ninaomba kwa vile mengi yatasemwa na wenzangu, nijikite kwa yale ambayo sisi tulioko kwenye *field* ndiyo tunayapitia na hakuna mwingine wa kuyasema isipokuwa sisi tulioko huko. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba hili lisichukuliwe kwamba tumekuwa humu ndani kwa sababu ya maslahi binafsi, ninaweza kufa kesho na kesho kutwa, lakini Watanzania wapo, vizazi vyetu vitabaki, tunachotaka ni kuboresha elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Elimu, ni uwekezaji, tunazungumzia Uwekezaji wa vitu vingi, Rais amekuwa

akipigania kuhakikisha wawekezaji wanakuja kuwekeza Tanzania ili kuweza kupata fedha za Kigeni, na hatimaye Watanzania wapate ajira na vitu vya namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba nimuombe Rais, aangalie suala zima la Uwekezaji kwenye Elimu. Tunaweza tukawekeza kwenye Viwanda, ikiwa hatujawa-*train* watu wetu vizuri, inavyotakiwa bado uwekezaji wetu katika maeneo mengine unaweza usiwe wa tija sana. Nikizungumza hili ninajua Mheshimiwa Dada yangu Angella Kairuki, sasa umepewa nafasi ya uwekezaji, kusimamia uwekezaji katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuomba sana tuwekee dirisha la wawekezaji wa Elimu Tanzania, maana hawa ndiyo wanaowajenga wataalamu wetu watakao iendesha nchi hii kesho na kesho kutwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikisema hivi ni kwa sababu ya gharama kubwa ya uendeshaji wa shule hizi, ujenzi wake na vitu vya namna hiyo. Niliwahi kusema Uganda, ukifahamika tu wewe unataka kujenga shule, wanakuondolea *VAT* kwenye *constructions material* zote, zote unaondolewa, kwa sababu wanajua unakwenda kuwekeza kwa ajili ya jamii ya kwetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo na sisi tuangalie, namna ambavyo tutaweza kupunguza gharama zingine kwa wamiliki na waendeshaji wa hizi shule, tunapitia wakati mgumu sana. Niliwahi kusema ukiwapima waendeshaji wa shule, wengi wana *pressure* na sukari kwa sababu ya changamoto ya uendeshaji wa hizi shule. Nikisema hivi changamoto, mojawapo kwa mfano, vitabu, suala la vitabu, mwaka juzi tulizungumza hapa na vile vitabu vikaondolewa kwenye *system*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu la vitabu kutunga, kuvihakiki, kuvisambaza na kazi zingine zote imepewa *TET* au *TA* lakini kwa bahati mbaya tu naomba Bunge lako Tukufu

lifhamu ya kwamba *TET*hawajawahi kututungia vitabu watu wa *English Medium schools* mpaka leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa pata picha hawa watoto wanafundishwaje na ni watanzania na wako kwa mujibu wa Sheria? Ninapozungumza hivi ni pamoja na kutokuwa na mtaala wa lugha ya kiingereza, pamoja na kutokuwa na vitabu, hii inaleta mno changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia jambo lingine ni *TET*hawa hawa wamepewa *I mean, mandate* ya kuhakikisha wanatoa ithibati kwa waandishi wa vitabu vya ziada, jambo ambalo mpaka sasa, kuanzia 2015 hakuna mwandishi wa vitabu vya ziada aliyepewa ithibati na *TET*na watu wa *English Medium* wamekuwa wakitumia vitabu hivyo hivyo vya waandishi vya ziada visivyo na ithibati ndivyo vinavyotumika kufundishia, pamoja na kwamba bado hizo shule zinajitahidi kujikongoja kufanya vizuri katika mitihani hii ya mwisho ya kitaifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwaombe sana Mheshimiwa Prof. Ndalichako, naomba ufatilie suala *TET, TET* wanakuangusha, wao ndi wenye mujibu wa kutoa hivyo vitabu na mihutsari na mitaala. Tunaomba basi waangalie na hawa watu wa *English Medium* kwa jicho la huruma. Kama vile haitoshi, walimu wa shule za Serikali wamepatiwa mafunzo ya jinsi ya kutumia huo mtaala mpya wa Kiswahili uliotoka, lakini kwa bahati mbaya sana, walimu wanaofundisha *private schools* hawajapewa mafunzo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na juzi, wametoa barua *TET* ya kwamba ukitaka ku-*train* mwalimu kupata elimu ya huu mtaala mpya kila mwalimu anatakiwa alipiwe shilingi laki tatu. Hawa walimu wanawafundisha wa-Nigeria au ni watanzania? Kuna vitu vingine sijui kama hata Rais anavifahamu ama Wizara inavijua kwa *style* hiyo. Hebu pata picha tuna walimu zaidi ya 40,000 wa *private schools*, 40,000 mara 300,000 ni *over 12* Bilioni wanazifanyia nini? Hizi pesa? Wakati *TET* iko pale, kwa ajili ya kutoa na kusimamia Elimu mitaala na miongozo, hii haiko sahihi tunaomba watu angalie



na sisi ni watanzania, tunafundisha watoto wa Kitanzania, ndiyo wako humu wengine wamesoma wakina Mlinga hawa wamesoma *English Medium* leo ni Wabunge wazuri kama mnavyo waona wasingesoma huko, wasingekuwa hivyo kwa hiyo *TET* tunaomba watu angalie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kingine kwa haraka mwaka juzi Waziri alifuta kodi ya zimamoto humu ndani, nilipongeze hilo Jeshi letu, linafanya kazi vizuri, wamekuja hapa juzi wametupa Elimu ya namna ya kuzima moto sisi Waheshimiwa Wabunge. Lakini cha kusikitisha kodi hiyo imerudishwa kwa mlango wa nyuma, ukaguzi wa masuala ya zima moto unalipia *Certificate* shule, laki 500,000 lakini ile elimu ya kuja kupambana na habari ya kuzima moto, kila mwanafunzi anachajiwa shilingi 20,000 ina maana shule ikiwa na wanafunzi 500 unalipa shule yako milioni 10, kwa nini inaonekana kama vile kwenye *private schools* ndiyo mahali pekee pa kuchukulia pesa? Kwa nini, kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi sisi Wabunge tumefundishwa hapa, ni ile ya kuweka tu petroli pale na kuzima ule moto, wanafunzi wa *private* wanatakiwa walipe 20,000 kila kichwa, tunakoelekea ni wapi? Yaani *private schools* zimekuwa ni vyanzo vya kutafutia pesa kweli? *This is not fair?* (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna swali liliulizwa juu ya watoto yatima hapa na watoto wa mitaani, na vitu vya namna hiyo, naomba nitoe mapendekezo kwa Serikali yangu, tunafundisha watoto, nimemsikia hata mwenzangu, Mheshimiwa Shangazi akizungumza hizi shule za Mkanisa, ndiyo zinasaidia yatima, *on board* shuleni kwangu nenda leo wako 50 over 200 wamemaliza shule watoto yatima waliokuwa mtaani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *on board* wako 50, lakini bado pesa kama hizi unatakiwa uzitoe kweli, mngetuacha tuwasomeshee watoto hawa mtaani, kupunguza haya majanga? Na watu wa *private* pia wameomba ikiwezekana hata wapangiwe idadi kadhaa ya wale watoto kila mkoa,

kulingana na shule zilizoko, wachukue wale watoto yatima na watoto mtaani, wawasomeshe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, waachwe kufatwa fatwa na hivi vitu vingine kama mara kodi *fire*, mara *rent*, sijui *land rent* na vitu vingine visivyo na tija. Kwa hiyo, nilifikiri *private schools* ni mahali peke yake ambako watoto hawa wa mtaani wanaweza kuwa *absorb* na wakasaidiwa na tukamaliza janga la watoto wa mtaani katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tunapata *dialogue* nzuri sasa hivi, nimpongeze sana Mheshimiwa Prof Ndalichako, pamoja na Katibu Mkuu *at least* wanatushirikisha kwenye baadhi ya mambo mengi sasa kuhakikisha kwamba kunakuwa na *fair play* katika uendeshaji wa hizi shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema mambo haya ya msingi kabisa, hasa suala la vitabu tunaomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja atuambie ni lini *TET* watatoa vitabu kwa ajili ya hizi shule za kiingereza na lini hasa tutapata mitaala na lini hasa na ni kwa nini wanachaji shilingi 300,000 kwa kila mwalimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukipeleka huyo mwalimu kwenye hiyo kozi kumbuka unamlipia gharama za usafiri, chakula, malazi, ina maana mwalimu mmoja ana-*cost* shule zaidi ya shilingi milioni moja, haya kuna shule zina walimu mpaka 400, 450 huyo mwenye shule anazipata wapi hizo pesa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutamkamua huyo mzazi anayesomesha watoto wake kwenye hizi shule mpaka lini? Naomba kuunga hoja mkono lakini mama Ndalichako, ukija hapa tunaoamba utuletee majibu ya haya. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hilo la malipo ya zimamoto, hebu msaidie Mheshimiwa Waziri umletee ushahidi huo, kama ni GN gani tuone wote maana uamuzi wa Bunge hauwezi kwenda kupindwa pembeni. Tunaendelea Mheshimiwa Grace Tendega.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahsante sana, kwa kunipa nafasi na niweze kuchangia katika hoja iliyoko mbele yetu ya Wizara ya Elimu. Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii leo pia naunga mkono asilimia mia hotuba ya Kambi ya Upinzani yote ambayo yamo mule, ninaunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie katika masuala matatu nikianza na suala la kwanza, la kupungua kwa bajeti ya Wizara hii ya Elimu. Awamu ya Nne ya Serikali yetu ilikuwa ikienda kila mwaka ikipandisha bajeti ya Elimu, lakini toka tumeingia Awamu hii ya Tano, tunaona kuna mserereko wa kupungua kwa bajeti ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukianza mwaka 2016/2017 na chanzo cha takwimu hizi ni haki elimu, wanasema toka mwaka 2016/2017 imepungua bajeti kutoka trilioni 4.770 hadi kufikia trilioni 4.706 kwa mwaka 2017/2018. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona pia kwa mwaka 2018/2019 pia imepungua mpaka kufikia trilioni 4.628. Pamoja na hayo, tukiangalia uwiano mkubwa wa bajeti ya Serikali pia, tunaona kwamba imepungua kutoka asilimia 16.1 mwaka 2016/2017 mpaka 2018/2019 asilimia 14. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inapingana kabisa na azimio ambalo tumeridhia sisi la nchi za kusini mwa jangwa la sahara kwamba tufikie asilimia 20. Sasa tunavyopunguza bajeti ya Wizara ya Elimu, athari zake ni kubwa mno, mnaona Waheshimiwa Wabunge karibu wengi wanazungumza hapa wakilalamika jinsi ambavyo Wizara hii imekuwa haipati fedha kwa ajili ya kutatua changamoto zilizoko huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu iliyoko katika shule zetu, vyuo vyetu, ina mashaka makubwa mwaka huu kumekuwa na ongezeko la asilimia 17 ya wanafunzi wanaoingia shule za msingi, tofauti na miundombinu ambayo tunakwenda kwa asilimia moja. Sasa ukiona, miundombinu *vis-a-vis* hao wanaoingia mashuleni unakuta kwamba kuna

wanafunzi wameingia kidato cha kwanza mwezi wa tatu, kuna wengine wameingia mwezi wa nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalalamika nini hapa kwamba hawa watoto wanatoka hawajui kusoma na kuandika wakati wameingia mwezi wa tatu mwezi wa nne na mtaala unataka waanze mwezi Januari.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti,

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Nimekataa taarifa kwa sababu hazinisaidii sana, kwa muda wangu.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** *Yah (Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kumpa taarifa kwamba.

**MWENYEKITI:** Hapana nimekataa. *(Kicheko)*

Endelea!

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii tunavyozungumzia ni changamoto kubwa ambayo ipo katika jamii yetu, kwa Wizara hii kupunguza hiyo bajeti ya Wizara ya Elimu. Kuna upungufu wa vifaa maabara nyingi ambazo wananchi wamejenga, na Serikali haijamaliza kuna upungufu wa kemikali zinazotakiwa kwenye maabara zetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tunapunguza bajeti ya Wizara ya Elimu, tuna uhaba pia wa vifaa vya ufundishaji, na kufundishia, unakuta kwamba kuna walimu wengi wanalalamika kuna somo linaitwa stadi za kazi, mwalimu amepewa kitabu chake cha kiongozi, anaambiwa chukua

msumeno na ubao onyesha wanafunzi waanze kukata. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu mwalimu ambaye mshahara hamumuongezi? Huyu mwalimu ambaye madaraja yake hayapandi, hana pesa, lakini anatakiwa awe na vifaa darasani, wanafunzi wamezuiwa wasichukue vifaa majumbani wanasema tumesema elimu bure. Sasa mwalimu anafundishaje huyu? Hivi vifaa vinatakiwa kwa ajili ya mwanafunzi kupata ujuzi wa vitendo katika kazi zake. Zamani sisi tunavyosoma tulikuwa tunaambiwa katika masomo ya sayansi kimu mwingine aje na mafuta, mwingine aje na mchele, mwingine aje na sijui na chumvi, mwingine aje na kile. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi mnakaa darasani mwalimu anawafundisha kupika, mnapika, sasa hivi walimu wanashindwa kufanya hivyo? *Capitation grands* ambazo tulitaka zienda mashuleni zile 10,000 kwa shule za msingi na 25,000 kwa shule za sekondari kwanza haziendi, pili ziko chini hazitoshelezi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwanza napendekeza Mheshimiwa Waziri, hizo *capitation grands* ziende mashuleni kama zinavyohitajika kuna shule nyingi sana, ambazo hawapati, na hawapati wengine kwa wakati, lakini pia ni ndogo kama tulivyosema kwa dola, sasa dola inapanda, na sisi tumebakia na kiasi kile kile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba ipandishwe kwa *primary school* iwe angalau shilingi 20,000/= na kwa shule za sekondari iwe shilingi 50,000/=. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende katika suala la utekelezaji wenye mashaka sana wa bajeti katika fedha zetu za maendeleo kwa Wizara hii ya Elimu. Unakuta katika bajeti ya elimu, fedha za maendeleo zilizotengwa karibia nusu, shilingi bilioni 857 zilizotengwa katika maendeleo, shilingi bilioni 427 ndizo zinakwenda katika Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Hizi fedha ni nyingi, zinakwenda kule lakini tunakuta Wizara

hii inabakia na pesa kidogo ambayo ndiyo tunasema Wizara imepata pesa nyingi. Hii Wizara haipati pesa nyingi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Waziri wa Fedha awaongeze fedha Wizara ya Elimu kwa sababu kile kiasi kinachobaki ni kidogo. Miradi ya maendeleo karibu 40 haijapata fedha. Nikianza huu mradi huu wa Kitengo cha Kudhibiti Ubora. Mwaka 2017/2018 walitengewa shilingi bilioni moja mwaka 2018/2019 walitegewa shilingi bilioni 1.5 lakini miaka yote hii hawakupata fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge mnajua, hiki ni kitengo muhimu sana ambacho kinakagua jinsi ambavyo wanafunzi wetu au vijana wetu na walimu wetu wanatakiwa wafanye kazi, lakini hawatengewi fedha za kutosha; na tunajinasibu kwamba tunakusanya fedha nyingi, lakini fedha hazijaenda, hawa hawafanyi kazi ya ukaguzi, hawa watu wetu wa udhibiti ubora hawakagui shule zetu, lakini shule binafsi wanatoa pesa wenyewe kwa hawa Wadhibiti Ubora ndiyo maana wanaenda kukaguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona katika shule kumi bora huwa zinaongoza shule binafsi na shule za Serikali hazipo. Sasa mimi nasema hivi, *if you fail to plan, you plan to fail*. Wekezeni vya kutosha katika elimu. Namwomba Mheshimiwa Waziri, tuwekeze vya kutosha katika elimu, tuweke *foundation* ya kutosha katika msingi, twende sekondari ndio tutapata watu wazuri katika vyuo vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko vyuo vikuu tunakuta Wahadhiri wanalalamika kwa sababu hatujawekeza vizuri katika sekta hizi chini. Utaona tunazungumzia hapa, lakini tukisema elimu imeshuka Waziri haangalii Waziri wa TAMISEMI, unaangaliwa Waziri wa Elimu. Kwa hiyo, nawaomba mkae pamoja muone jinsi ambavyo mnaweza mkaboresha msingi ili huku juu tuwe na ubora unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja klatika suala la Taasisi ya Elimu Tanzania. Tunalalamika kuhusu vitabu hapa, lakini Taasisi ya Elimu Tanzania ilitengewa shilingi bilioni 40. Katika

shilingi bilioni 40 miaka miwili mfululizo hawakupata fedha, wamepata mwaka huu shilingi bilioni nne ambayo ni asilimia 10. Sasa asilimia 10 tunalalamika lakini asilimia 10 Mheshimiwa Waziri mnaowapelekea inatosha kufanya kazi zote hizo za kuandaa vitabu, kiongozi cha mwalimu na kufanya kazi zote ambazo zinatakiwa pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara iangalie Taasisi ya Elimu, kama wana shida ya kufanya elimu hii iwe bora. Taasisi ya Elimu iboreshwe lakini naomba mshirikiane na sekta binafsi *PPP* ili...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Unga mkono hoja hiyo. Mheshimiwa Haonga atafuatiwa na Mheshimiwa Yosepher Komba na Mheshimiwa Alfredina Kahigi, ajiandae.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. nami naomba kuchangia hii Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Leo nitakuwa nachangia pole pole sana lakini nitamwomba pia Mawaziri watakapokuwa wanahitimisha, nao wajibu pole pole wala wasi-*panic* na wala wasiwe na mpango wa kuvua nguo kama Waziri mmoja alivyosema atavua nguo. Naamini watajibu vizuri. Nataka twende vizuri kabisa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na hoja ya kwanza kamba wanafunzi wanaohitimu darasa la saba kila mwaka, kwa takwimu ambazo tunazo wanakadiriwa kuwa milioni moja, lakini wanaojiunga kidato cha kwanza kwa maana ya shule za Serikali na shule za *private* wanakadiriwa kuwa 300,000 tu. Wanafunzi 700,000 na kitu inaonekana wanabaki nje, hawako *private* wala *Government*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapozungumzia wanafunzi 700,000 ni wengi sana na kwa lugha nyepesi uchukulie ule uwanja wa Taifa ambao unajaa watu 60,000 mara 12 hawa

watu wote wanabaki nje, hatujui wanakokwenda ni wapi.  
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo inawezekana na inajulikana kabisa kwamba watoto wanaohitimu darasa la saba wengi wao wana umri mdogo sana. Wengi ni chini ya miaka 14, wengine 12, 13 wakizidi sana ni miaka 14, lakini hawa wengi wanabaki nje kama 700,000 na kitu hivi. Sasa kwa nini Serikali isitafute utaratibu wa hawa angalau waanze kurudia mtihani kwa utaratibu maalum tu, ambao ni maalum kabisa, kwamba waruhusiwe kurudia mtihani wa darasa la saba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini hata hapa wako Wabunge wengi, hata baadhi ya Mawaziri ambao walirudia mtihani wa darasa la saba kwa majina ya watu wengine. Hatuwezi kuwataja majina, lakini wapo kwa utaratibu ambao siyo maalum. Sasa kwa nini Serikali isihalalishe suala hili liwe ni suala ambalo ni maalum kabisa kabisa ili kusudi wanafunzi hawa wengi wasibaki mtaani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunahangaika, kwa mfano, wapo baadhi ya makundi yanaibuka nchini tunasikia panya *road*, sijui nani; ni watoto wadogo sana hawa. Sasa kwa nini Serikali isianzishe utaratibu ambao ni maalum waweze kurudia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, kwa sababu idadi hii ni kubwa sana, kwa nini Serikali isianzishe utaratibu waende kwenye Vyuo vya *VETA* kupata mafunzo ya ufundi umeme, ushonaji na mafunzo mengine ili Serikali iweze kutoa mikopo kwa wanafunzi hawa kama ambavyo inatoa mikopo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu? Kwa nini wasifanye hivyo? Kwa sababu tunaamini kwamba vyuo vyetu vya *VETA* viko vingi sana nchini, kwa hiyo, wanafunzi hawa wanaomaliza darasa la saba wanaweza wakapelekwa huko *VETA* Serikali ikawapa mikopo na wakalipa, kwa sababu mkopo unalipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iweze kuliangalia hili. Mheshimiwa Ndulichako nimekwambia



kwamba leo nitakushauri polepole na baadaye ujibu vizuri polepole kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu mishahara pamoja na motisha kwa Wahadhiri pamoja na Wakufunzi wa Vyuo. Juzi wakati nachangia Wizara ya Mambo ya Ndani nilizungumza na leo pia naomba niseme tu kwamba bado Waheshimiwa Wabunge tusiwe na utamaduni wa kulalamika. Yaani wananchi wametupa kura, hiki ndiyo chombo kinachofanya maamuzi, linapokuja suala la kujadili bajeti ya Wizara fulani Wabunge huwa tunajifanya wazalendo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa nini Wizara hii ya Elimu pamoja na kwamba Wabunge wengine wamechangia na Wabunge wa Chama cha Mapinduzi na ninyi mko wengi sana, anzisheni utaratibu mzuri tu tuweze kuongeza mishahara kwa Wahadhiri wetu. Sisi upande huu tutawaunga mkono. Ninyi ndio wengi. Utaratibu, wakati mwingine Mabunge huko nyuma wamewahi kurudisha bajeti isipitishwe. Bunge limewahi kuamua miaka ya nyuma huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unafahamu wakati huu tunapozungumzia bajeti ya Wizara ya Elimu tunazungumzia makusanyo pamoja na matumizi. Kwa hiyo, tunaweza ndio wakati muafaka huu. Wabunge wa Chama cha Mapinduzi mko wengi sana, ninyi ndio mnaopitisha akidi ya kila kitu. Kwa hiyo, hili pia tunaweza tukalijadili, sisi wa upande huu hatuna shida. Hata nikiwauliza Wabunge wa upande huu nyoosheni mikono ambao mnasema tuongeze mishahara kwa Wahadhiri; wengi sana.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walinyoosha mikono)*

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Unaona! Wako wengi sana; lakini nikisema nyoosheni kule, hata mmoja hatanyoosha. Kwa hiyo, niseme tu kwamba hili liko mikononi mwa Wabunge wa CCM na mishahara ya Wahadhiri iweze kuongezwa pamoja na stahiki zao mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ninapozungumza na wewe Wahadhiri kwa taarifa tulizozipata, wameanzisha mgomo wa chini chini, kwa sababu hata zile fedha za nyumba ambayo ni stahiki yao hazipelekwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tutaenda kupata wanafunzi wa aina gani? Mhadhiri anaamua kumkamata mwanafunzi...

**MWENYEKITI:** Acha uchochezi wewe, Mheshimiwa!  
*(Kicheko)*

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mhadhiri wa leo anaenda kumkamata mwanafunzi wakati mwingine kwa sababu tu yule mtu ana *stress*, ana msongo wa mawazo kwa sababu hela za nyumba zao hizo hajapewa na ni stahiki yao. Sasa mambo kama hayo Serikali iweze kuangalia. Shida ni nini? Wapeni hela zao, waongezeni mishahara, boresheni mambo yao yaweze kwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni suala la utegemezi wa miradi ya maendeleo kwenye fedha za wahisani. Imekuwa ni kawaida, Wizara hii ya Elimu kuomba fedha nyingi kutoka kwa wahisani kuliko fedha zaa ndani. Natoa mfano mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2018/2019 bajeti hii ambayo tunaimaliza sasa, yaani fedha za maendeleo kati ya shilingi bilioni 502 fedha ambazo tulikuwa tumeomba kwa wahisani ni shilingi bilioni 311 sawa na asilimia 62. Hizo zilikuwa ni fedha za nje. Fedha za ndani zilikuwa ni asilimia 38 tu, ndio zilikuwa za kwetu za ndani. Fedha hizo za wahisani ambazo zilikuja hadi sasa ni shilingi bilioni 111 kati ya shilingi bilioni 311.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niulize. Kwa mfano, unapoenda kuomba fedha aidha kwa mtu mwingine, unataka labda kujenga nyumba au kufanya jambo lolote la maendeleo, unaomba nyingi au unaomba kidogo, au wewe

unazo nyingi unatakiwa uongezewe? Sasa Serikali yetu tunaomba kwa wahisani shilingi bilioni 311 sawa na asilimia 62, halafu sisi eti asilimia 38. Hii ni aibu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu ndiyo tunaenda kuonesha utegemezi wa hali ya juu sana. Mwaka huu katika fedha za maendeleo shilingi bilioni 413, tunaomba kwa wahisani shilingi bilioni 279 sawa na asilimia 68. Fedha za ndani mwaka huu ni asilimia 32 tu, lakini wakati huo huo hawa wahisani ndio mmekuwa mkiwaita mabeberu. Yaani mnapoomba fedha mnasema ni wahisani, wanapowashauri namna ya kuendesha nchi na mambo kwenda vizuri, mambo demokrasia, mnasema mabeberu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri, ukiangalia kule nyuma kabisa ukurasa wa mwisho kabisa kule amewashukuru hawa ambao tunawaita wahisani hawa, lakini wakati mwingine mnawaita mabeberu. Inabidi mwaombe msamaha. Kwa mfano, Mheshimiwa Waziri anasema, napenda pia kushukuru baadhi ya mashirika yaliyochangia kufanikisha Programu za Elimu, Sayansi na Teknolojia ambayo ni pamoja na Benki ya Dunia, *DFID, SIDA, Umoja wa Nchi za Ulaya, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Jumuiya ya Madola, Global Partnership in education, United Nations, International children's, (UNICEF)...*

**WABUNGE FULANI:** Mabeberu.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani pale mmetaja wengi, *UNESCO, USAID...*

**WABUNGE FULANI:** Mabeberu.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Sasa wote hawa wanapokuwa wanatuchangia tunasema ni wahisani...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado dakika mbili.

**MWENYEKITI:** Hapana. Ahsante sana. Wewe mwenyewe ndio unawaita mabeberu, siyo Serikali. Ndiyo maana Hotuba ya Waziri iko *very clear*, inashukuru nchi zote na taasisi zote za Kimataifa ambazo zinatunga mkono. Tusipotoshe Watanzania. (*Makofi*)

Tunaendelea, Mheshimiwa Yosepher Komba, Mheshimiwa Kahigi, Mheshimiwa Rukia Kassim na Mheshimiwa Desderious Mipata wajiandae.

**MHE. YOSEPHER F. KOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kupata nafasi nami nichangie kwenye Wizara hii. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya afya njema anayonijalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nakishukuru chama changu kwa namna ambavyo kinaendelea kuniamini kutekeleza majukumu yangu. Kwa namna ya pekee namshukuru Mwenyekiti wetu na ninamwombea kila la heri katika mapambano haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja ya Kambi ya Upinzani. Maoni ambayo wameyatoa ni maoni ambayo Serikali inatakiwa isikilize na kuyachukulia maanani. Ni maoni ambayo ukiangalia hata hotuba ya mwaka 2018 na miaka iliyopita, kuna mambo yanajirudia. Kwa hiyo, inaonekana bado Serikali haijawa sikivu vya kutosha, kuna baadhi ya hoja zinajirudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati namsikiliza mama yangu Waziri Mheshimiwa Prof. Ndalichako akisoma hotuba yake ya mwaka huu, ni hotuba ambayo ukiisikiliza ina ladha sana. Baada ya kumsikiliza nikasema ili niweze kumhukumu vizuri au ili niweze kusema vizuri kwenye hotuba hii, nikajaribu kupitia hotuba ya mwaka 2018. Nimepitia hotuba ya mwaka 2018 nikafananisha na hotuba ya mwaka huu. Kuna baadhi ya mambo nimeyagundua. Mambo haya yanafanya hotuba

ya mwaka huu isionekane bora kwa sababu ya historia ya hotuba ya mwaka 2018. (Makofi)

Mheshimiwa mwenyekiti, ukiangalia suala zima la bajeti, wameongea wenzangu, bajeti ya Wizara ya Elimu inaendelea kushuka. Mwaka 2018 kulikuwa na shilingi trilioni 1.4, mwaka huu imetengwa shilingi trilioni 1.3, inashuka. Inashuka katika mazingira ambayo bajeti kuu ya Serikali inaongezeka; inashuka kwenye mazingira ambayo tunasema wanafunzi wanaongezeka kwenye shule za msingi na sekondari, inashuka katika mazingira ambayo vyuo vikuu wanafunzi wanazidi kuhitaji mikopo, lakini bajeti ya elimu inazidi kushuka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, nimeangalia kwenye matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo. Pamoja na bajeti kushuka, matumizi ya kawaida yameongezeka lakini matumizi ya maendeleo yameshuka. Kwa hiyo kuna athari nyingi za hii bajeti kushuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia kwenye suala la walimu na wataalamu. Wataalamu tunajua wanasaidiwa na Kitengo cha *COSTECH* lakini ukiangalia mwaka wa fedha uliopita, walikuwa na shilingi trilioni 1.6 wametengewa, lakini hawajapelekewa hata shilingi, ambapo wao ndio wanashughulikia masuala ya tafiti na sayansi. Hata shilingi hajapelekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu wametenga, hatujui kama itaenda. Kama ya mwaka 2018 haikwenda, ya mwaka huu hatujui. Kwa hiyo, hivyo ndivyo namna ambavyo mnaihudumia Wizara hii kwa watafiti na wataalam ambao wangeweza kutusaidia hiyo nchi ya viwanda tukaifikia kwa haraka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikisalia hapo, kuna suala la *capitation*, lipo kwenye fungu la maendeleo. Tunafahamu *capitation* mmesema mtakuja na kikokotoo kipya; mtakuja na utaratibu mpya wa namna ya kuandaa hii *capitation* ili wale wahusika wapate nafuu. Kwa sasa hivi mmefanya tafiti

kwenye shule moja tu ambayo ina wanafunzi 444, wao kwa mwezi wanapewa shilingi laki moja na themanini na saba na *point*. Shilingi 187,000/= uigawanye kwa kila mwanafunzi, kila mwanafunzi anapata chini ya shilingi 500/= kwa mwezi. Hiyo ndiyo *capitation* ambayo mnahubiri hapa elimu bure, elimu bure, elimu bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwashauri na niwaombe, mnaposema kitu ni bure, inatakiwa kiwe bure kweli. Elimu siku zote ni mchakato, elimu siyo suala la mara moja, ni mchakato. Nawaomba msemi elimu bila ada, siyo elimu bure. Haijawa elimu bure kwenye nchi hii bado. Wako wazazi ambao wanapangishia watoto wao vyumba ili wasitembee umbali mrefu, huwezi kumwambia yule mzazi mwanaye anasoma bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako wazazi ambao wanalipia boda boda na usafiri mwingine watoto wao kwenda shule kila siku, huwezi kusema ile ni bure. Wako wazazi wanachangia majengo. Siku hizi majengo kama alivyosema Mheshimiwa Tendega, mwezi wa Tatu watu wanaenda shule, wanachangia. Wazazi wanaitwa, nyie wazazi wenye watoto waliofaulu, changieni madarasa yakamilike; huwezi kumwambia yule mzazi mwanaye anasoma bure. Kwa hiyo, hiyo ni elimu bila ada, lakini bado wazazi wana mzigo mkubwa wanaolipia kwenye suala la elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu lingine nataka kuongelea siasa vyuoni. Bahati nzuri nimekuwa mwanafunzi, nimekuwa mwalimu na sasa hivi ni mwanafunzi, kwa hiyo, ninachokiongea nakifahamu. Kumekuwa na tatizo kwenye vyyo vyetu vikuu. Vyyo vingi sasa hivi kumekuwa na mkanganyiko; imekuwa ni kosa la jinai kujihusisha na siasa au kuonekana una mrengo fulani wa siasa, imekuwa kosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa Upinzani, wale ambao wanaonekana wana misimamo dhidi ya Uongozi wa Chuo au ya Serikali, ndio hao wanaopatishwa shida kwenye vyyo; lakini tunaona CCM, UVCCM wanafanya vikao kwenye Vyyo vya *DUCE*, Mwalimu Nyerere, wanafanya vikao.

Inapokuja kwenye Vyama cha Upinzani inakuwa shida. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu, Viongozi na Wasimamizi wa Vyuo vyetu wamekuwa wanaingilia chaguzi za wanafunzi kinyume na taratibu. Wakishaona anayegombea ana mrenge fulani, uongozi wa chuo utashirikiana na Polisi kuharibu ule uchaguzi bila sababu ya msingi; na mara nyingi wanakuwa wanatumwa na Chama Kikuu cha Siasa chama ambacho kinatawala. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Waziri wa Elimu atakapokuja kuhitimisha hapa atuambie, kama kweli ni marufuku kwa watu ambao wanasoma vyuoni ambao ni watu wazima, wengine wametoka makazini, wengine wametoka sehemu mbalimbali kufanya siasa, iwe marufuku kwa wote isiwe na *double standard*. Watu hao mnaowapa marufuku ni watu ambao wanajua siasa vizuri sana, wengine wanaisomea wanatafutia *degree*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la changamoto za watoto wa kike; naomba hapa nianze na suala la *pad*. Tunafahamu Serikali kwenye bajeti iliyopita ilitoa VAT kwa ajili ya kufanya hili suala la *pad* lishuke bei, lakini Mheshimiwa Waziri ni shahidi, hakuna badiliko lolote lililotokea. Kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Waziri kushirikiana na TAMISEMI, kushirikiana na Wizara ya Fedha waone namna ambavyo suala la *pad* wanaweza wakaliingiza kwenye *capitation fee*. Watoto kuanzia darasa la tano mpaka la saba wanaweza wakawa na utaratibu wamewawekea waweze kupata *pads* bure, tukiliacha hivi halitakuwa na maana yoyote kwa wanafunzi wetu ambao wanaendelea kupata shida, ambao wanaendelea kupata hii changamoto na kukosa kuhudhuria masomo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nigusie suala ambalo liko kwenye Wilaya yangu ninayoishi, Wilaya ya Muheza, tumeongea mara nyingi sana kuhusu changamoto za Walimu. Changamoto ambazo zinawafanya Walimu washindwe kutimiza majukumu yao, changamoto ambazo

zinawafanya Walimu wanakosa *morale* ya kufundisha na kuwasaidia watoto wetu. Kwenye Wilaya ya Muheza tulikuwa na shida hiyo ya Walimu katika baadhi ya maeneo, tukaamua kwenye Baraza kwamba baadhi ya Walimu wahamishwe kwenye Kata moja kwenda nyingine na kiutaratibu Walimu wanapohamishwa kuna ile tunaita *disturbance* wanatakiwa walipwe, lakini mpaka sasa hivi ninavyoongea walikuwa Walimu 86 waliotakiwa kulipwa, lakini wamelipwa Walimu 20 tangu mwaka jana mwezi wa Nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimwombe Mheshimwa Waziri aliangalie hilo, wale Walimu wamekosa *morale* kwa sababu *disturbance fee* yao hawajalipwa, mpaka sasa hivi zaidi ya mwaka, wanadai zaidi ya Walimu 66.

Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri alichukulie maanani hilo alifanyie kazi ili kuongeza *morale* ya walimu ambao wanafundisha kwenye maeneo yetu ili waweze kuona na wao ni wafanyakazi kama wafanyakazi wengine ambao wanathaminiwa na ambao wanatoa mchango mkubwa kwenye Taifa hili ili kuongeza masuala ya elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee fedha za mikopo kwa ufupi sana. Tumeona hapa fedha za mikopo ziko kwenye Fungu la Miradi ya Maendeleo, ambazo zinachukua asilimia kubwa kuliko miradi ya maendeleo yenyewe. Sisi tunashauri kupitia hata hotuba ya Kambi imesema, hizi fedha zitengewe Fungu Maalum ili tuweze kujua jinsi zinavyotoka na jinsi zinavyorudi, lakini hizi fedha zikiwa na Fungu Maalum tutajua fedha halisi zitakazobakia kwenye maendeleo mengine ya elimu kuanzia shule ya msingi mpaka sekondari kwa sababu kwa kuziacha humu, inaonekana kwenye maendeleo kuna fedha nyingi, lakini kwenye uhalisia nusu ya fedha au zaidi ya nusu zimeenda kwenye Bodi ya Mikopo ambapo watu wanaenda kulipia ada, chakula na malazi, kitu ambacho tunawaacha wanafunzi wetu wanakaa chini, wanakaa nje na wanakosa huduma muhimu kwenye mashule kwa sababu fedha nyingi.... *(Makofi)*



*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nitakuongezea muda ukiunga mkono hoja, Mheshimiwa Kahigi, atafuata Mheshimiwa Rukia.

**MBUNGE FULANI:** Mwambie nimeshaunga.

**MHE. YOSEPHER F. KOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Kambi ya Upinzani. *(Makofi)*

**MHE. ALFREDINA A. KAHIGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Nianze na Wizara ya Elimu, Wizara ya Elimu mimi nitaanza na Walimu. Walimu ni kioo cha jamii lakini Walimu kuanzia mavazi, kuja maadili, kuja na mahusiano na jamii Walimu wana upungufu. Kwa mfano mavazi, Walimu hapo zamani tulikuwa tunawaona ndiyo watu ambao wanafundisha watoto, kujipenda, kuvaa vizuri, kuwa wasafi lakini Walimu wa sasa hivi wanasikitisha mavazi wanayovaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Walimu wa kike, baadhi siyo wote wanavaa nguo ambazo hazina heshima yoyote, nguo ambazo ni fupi kiasi kwamba wanafunzi hawajifunzi kitu chochote kwa mavazi wanayovaa. Niombe Wizara ya Elimu katika suala hilo la mavazi iliangalie sana iwape mwongozo kusudi wawe wanavaa nguo ambazo wanafunzi wataona kwamba na sisi tujifunze kutoka kwa Walimu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwa watoto wa kiume wanavaa ma-*jeans* tisheti, *jeans* hilo akilivaa wala kulinyoosha halinyooshi utadhani ng'ombe amelitafuna amelitema ndiyo anakuja amelivaa mwanafunzi akiona namna hiyo kwa kweli halleti ustaarabu wa aina yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka katika mambo ya mavazi, nije katika maadili. Sisi ambao tumetoka vijijini Walimu wa vijijini wanasikitisha, baadhi lakini siyo wote. Wanalewa, wanakunywa pombe yaani Mwalimu anakuta wanacheza

ngoma na yeye anafunga kanga anacheza ngoma na wanafunzi wanamwona, kwa kweli haiteti heshima yoyote. Mwalimu ni kioo kama nilivyosema, hapaswi kunywa pombe akalewa mpaka na wanafunzi wale ambao anawafundisha wakamwona kesho yake akija darasani watajifunza kitu gani, ni aibu tupu. Niombe Wizara ya Elimu, wajaribu kuwakanya, wajaribu kujjeshimu ili watoto wetu waweze kuchukua maadili mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye mahusiano ya Walimu na jamii. Kuna baadhi ya Walimu wanajifanya Miungu watu. Nimshukuru Mheshimiwa Waziri, Profesa Ndalichako na uongozi mzima kwa kitendo ambacho walitufanyia watu wa Kagera kwa mtoto yule aliyepigwa mpaka akauwawa lakini walisuza nyoyo za Wanakagera au na wazazi wote Tanzania nzima kwa yule Mwalimu aliyempiga na ameadhibiwa kutokana na makosa yake, lakini bado baadhi ya Walimu wana tabia ambayo si nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juji juji niliangalia kwenye *WhatsApp*, kuna Mwalimu sehemu za Mbeya amepiga mtoto wa miaka nane, alimfunga miguu juu, kichwa chini mtoto wa miaka nane, eti ameshindwa kufanya hesabu, akampiga mpaka akamvunja uti wa mgongo. Mheshimiwa Waziri nitapenda hilo alifuatilie sana, tujue matokeo ya huyo mtoto. Sisemi vitu vya longolongo nasema vitu ambavyo nimeviona, amenisikitisha mno hata angelikuwa ni mtoto wako ungelia, mimi nilisikitika sana sana. Amempiga, wazazi wake wamemshughulikia yule mtoto mpaka hela zimewaishia, sasa hivi wamelipeleka mpaka kwa Mkuu wa Wilaya. Naomba Mheshimiwa Profesa Ndalichako alifuatilie hilo suala awasaidie wale wazazi wana masikitiko makubwa na mtoto wao. Bado kuna Walimu ambao ni wakorofi, wanajifanya ni Miungu watu, huyo Mwalimu nasikia wamemtoa kwenye hiyo Kata ameenda kwenye Kata nyingine aendeleze na ubabe wake huo, naomba afuatiliwe mpaka apatikane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za msingi ambazo hazina uzio. Mheshimiwa Waziri, niombe Serikali washughulikie kuwajengea walau shule ambazo ziko mijini, uzio siyo wa

matofali hata ukiwa wa senyenge kusudi kile kipindi cha *break* ambacho wanatoka madarasani kwenda nje, wasizurure hovyoy hovyoy yaani ndiyo kipindi ambacho wanatoroka, wengine wanaenda kuvuta bangi, wengine wanaenda kufanya mambo ambayo ndivyo sivyo. Niombe walau zile shule ambazo ziko mjini, wajaribu kuwawekea uzio wawe wanakaa shuleni hapo wana-*discuss* na wenzao muda ukifika wa kurudi nyumbani waende nyumbani, siyo kuzurura zurura. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoke huko nije kwenye suala la Mitaala, suala la Mitaala kuna shule Serikali na shule za binafsi. Shule za Serikali wanafunzi kuanzia awali wanajifunza Kiswahili tu, Kiingereza ni kidogo mno mpaka darasa la saba, lakini shule za watu binafsi wanajifunza Kiingereza kuanzia shule za awali mpaka juu. Kwa hiyo tumekuwa na matabaka ya hawa watoto, watoto wa shule za binafsi wanajiona ni bora zaidi kuliko hawa wenzao na hawa watoto wanapenda nao kujifunza Kiingereza lakini wazazi wao hawana fedha za kuwapeleka kwenye shule za Kiingereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiingereza ni muhimu, sisemi Kiswahili siyo muhimu, Kiswahili ni lugha yetu ya Taifa, ni lugha nzuri sana na mimi naipenda lakini na Kiingereza ni lazima na watoto nao wajifunze. Kama ni kusoma lugha zote mbili, Kiingereza na Kiswahili watoto wote wasome lugha hizo kusudi waweze wote kuwa *uniform*. Naomba Wizara hilo na lenyewe waliangalie na wengine wameshaliongelea zaidi na mimi nimeliongelea hivyo hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye motisha; Walimu nawapenda sana, japokuwa wanafanya mambo ya ndivyo sivyo hao ambao nawasema lakini wengi wanajituma wanafanya kazi nzuri. Naomba Serikali iwaangalie, mishahara yao ni midogo sana, kuanzia shule za chekechea mpaka kwenye vyuo. Sijui maprofesa labda wao wanakula mishahara mizuri sana sijui, lakini hawa Walimu wengine wanakula mishahara mdogo sana. Serikali iwaangalie Walimu

iwaongezee mshahara, japokuwa wafanyakazi wote wanalia lakini Walimu wanafanya kazi ngumu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani walikuwa wana-*teaching allowance* sijui zilienda wapi. Naomba Serikali wafanye mpango zirudi kusudi waweze kukimu mahitaji yao angalau madogo madogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mengi ya kusema mengine nitayaandika, lakini yangu ni haya. Nashukuru sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Alfredina Kahigi, tunashukuru sana kwa mchango wako. Mheshimiwa Rukia, Mheshimiwa Desderius Mipata na Mheshimiwa Rose Tweve wajandae.

**MHE. RUKIA AHMED KASSIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nami kuweza kupata nafasi hii ya kuchangia katika Wizara hii ya Elimu. Naanza na Mitaala ya Elimu. Mitaala yetu ya elimu bado ni tegemezi, haioneshi ni namna gani mwanafunzi anapomaliza shule anaweza kujitegemea mwenyewe kimaisha. Mwanafunzi pengine anamaliza anakuwa na *degree* ya *engineering* lakini akitoka pale hana uwezo wa kutengeneza hata baiskeli. Wanafunzi wanakuwa si wabunifu, elimu wanayopata inakuwa ni ya *theory* zaidi kuliko elimu ya vitendo. Kwa hiyo, nashauri Serikali ihakikishe kuwa, wanafunzi katika vyuo wanapata zaidi elimu ya vitendo kuliko *theory* ili wanapotoka pale wanafunzi wetu waweze kujitegemea wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa Mwalimu Nyerere kulikuwa na Elimu ya Ujamaa na Kujitegemea, ilikuwa ikifika *time* kuna vipindi wanafunzi wanatolewa darasani wanakwenda kufundishwa namna gani ya kulima. Wanafundishwa kutengeneza mbolea, kutengeneza pengine shamba linakuwa kutoka pengine mche wa mgomba mpaka kufikia mwingine pana urefu wa mita ngapi, wanatengeneza mashimo yanakuwa na ukubwa gani, wanaweka mbolea mpaka kima gani, mwanafunzi anapomaliza shule anakuwa

ni mkulima mzuri sana na anaweza kujitegemea. Kwa hiyo nashauri tuige mambo ya namna hii ili wanafunzi wetu wanapotoka vyo waweze kujitegemea wenyewe siyo tena wawe bado ni tegemezi kwetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nataka kuchangia kuhusu shule za *private*. Shule hizi za *private* tunazipenda sana na zinatuseaidia sana lakini kwa kweli baadhi ya shule watoto wengi wanaharibika hasa watoto wadogo. Kunakuwa na ulawiti mkubwa katika shule hizi za *private*, hasa shule ambazo zinachukua watoto wadogo, watoto wanaharibiana wao wenyewe kwa wenyewe. Kwa hiyo, nashauri Mheshimiwa Waziri awaite hawa walio na shule za *private*, wamiliki wa shule za *private*, wawape elimu wajue kama wanafunzi wanaowachukua ni wadogo kwa hiyo watoto wanapokuja pale wengi wao wanakuwa na tabia tofauti katika majumba yao. Baadhi ya wazazi wanakuwa wale watoto wameshawashinda kule nyumbani, kwa hiyo mtu anaamua bora nimpeloke *boarding*. Anapokwenda kule anakutana na watoto wengine wana tabia nzuri, lakini kwa sababu wale wana tabia mbaya wanaanza kuwaharibu na wenzao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nawashauri walio na mashule haya ya *private* wahakikishe kila bweni, kuwe kuna mtu ambaye analala nao watoto anawaangalia. Watoto wanaharibiwa usiku wanapokwenda chooni, watoto wakubwa wanawasubiri, wanawaharibu wadogo. Tutakuja kuzalisha watoto sisi tunaona watoto wetu wanakwenda kujifunza, kumbe wanajifunza mambo mengine ya ajabu. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri wa Elimu awaite watu walio na shule za *private* wahakikishe watoto wanawawekea ulinzi wa hali ya juu watoto wasiharibiane. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nitakwenda kwenye mishahara ya Walimu. Mheshimiwa Waziri asishangae kutuona kila anayenyanyuka anazungumzia suala la mishahara ya Walimu. Kama kuna watu ambao wanaishi katika maisha ya umaskini basi ni Walimu, Mwalimu anafikia kustaafu hana pa kukaa. Mwalimu

siku zote anakaa katika nyumba ya kupanga, ikikaribia Januari Mwalimu kichwa chake hakifanyi kazi anafikiria ni namna gani atapata hela ya kwenda kulipia kodi ya nyumba. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Walimu wetu tukiwaongezea mishahara na stahiki zao tukiwapa, kidogo akili zao zitaweza kutulia kwa sababu atakuwa hana wasiwasi wa mambo mengine, ataweza kusomesha vizuri na tutapata mafanikio mazuri. Walimu wengi ambao wanafanya kazi katika shule za *private*, wanalipwa vizuri na ndiyo maana tukaona wanafunzi wanaofaulu wengi wanatoka katika shule za binafsi. Kwa hiyo ingawa hawa walio na shule za *private* isije ikiwa ni ile tunayosema Mgema akisifiwa tembo atalitia maji, wakaja wakaona kama kweli wao wanawalipa vizuri wakawashusha, hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali stahiki za Walimu ziongezwe, tuwaongezee mishahara ili anapokuwa darasani asifikirie watoto wake watakula nini, wala asifikirie mke wake atapata wapi nguo ya kuvaa au atapata wapi fedha ya kwenda kulipia nyumba ili akiwa pale atulie kabisa aweze kutoa elimu nzuri kwa watoto wetu na tupate ufaulu mzuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa nitajielekeza kuhusu ajira ya Walimu. Katika vyuo vyetu wanamaliza pengine wanafunzi kama elfu thelathini ambao wote wale wanakuwa tayari ni Walimu, lakini kwenye ajira wanaajiriwa pengine elfu kumi, wengine wanabakia mitaani, utamkuta mtu ameshasoma vizuri, ana uwezo wa kufundisha lakini anakwenda kufanya kazi ya majumbani, kwa sababu hana kazi ya kufanya. Kwa hiyo nashauri Serikali iongeze ajira kwa Walimu ili katika madarasa iwe hakuna vipindi ambavyo hakuna Mwalimu wa kusomesha pengine *topic* fulani, hapana. Kwa hiyo nashauri tuongeze ajira kwa Walimu, watoto waliomaliza vyuo ambao wamesomea elimu waajiriwe ili tupate Walimu wengi katika vyuo na watoto wetu waweze kufanikiwa vizuri katika elimu zao. (Makofi)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. RUKIA AHMED KASSIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wangu umekwisha au bado. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilikuona karibu na eneo la Maganzo juzi, unaimarisha Muungano eeh! Mheshimiwa Rukia. Mmh! Nilikuona eneo la Maganzo.

**MHE. RUKIA AHMED KASSIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Naam!

**MWENYEKITI:** Maganzo, ulikwenda kufanya nini? Ni kwenu huko, Muungano ule! Haya tunaendelea Mheshimiwa.

**MHE. RUKIA AHMED KASSIM:** Maganzo nilienda kutembea.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Desderius Mipata, Mheshimiwa Rose Tweve na Mheshimiwa Silafu Jumbe Maufi wajiandae.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nipate kuchangia kwenye Wizara hii muhimu sana, Wizara ya Elimu. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na vile vile napongeza sana utendaji mzuri wa Serikali ya Awamu ya Tano kwa kazi zote wanazosimamia, Mheshimiwa Rais anatembea kwenye ahadi zake, lakini nimpongeze Waziri kwa uchapakazi wake, Waziri na wasaidizi wake bila shaka. Mheshimiwa Waziri amekuwa akitusaidia sana, ukimwona anakusaidia shida mara moja, lakini pia ametutembelea, ametembelea Rukwa, ametembelea Wilaya ya Nkasi na Jimbo letu ametembelea na kutokana na ziara yake tumenufaika. Nimeona hapa kwenye hotuba yake kunaanza ujenzi Chuo cha VETA Rukwa, ni jambo jema sana tunampongeza, tunaomba tu kasi ya ujenzi iwe nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kuanza kwa ukarabati wa Chuo cha Wananchi Chala ambacho kipo Jimboni kwangu na nimekuwa nikikisemea sana hapa, tunampongeza na tunashukuru sana. Naomba nishauri hapa, chuo hiki kikarabatiwe, kinapokarabatiwa ukarabati huu uelekezwe kwenye majengo ambayo wananchi waliyatoa maana yake eneo ambalo chuo kipo ni eneo la majengo ya Baba Askofu, Jimbo Katoliki la Sumbawanga na ameonesha nia ya kutumia majengo yale na wananchi walishaamua kujenga majengo mengine eneo la Isoma kwenye shule moja ya sekondari tunayotaka tuianzishe ya Isoma na tumekubali chuo kihamie pale. Kwa hiyo naomba huo ukarabati aliotutengea hapa uelekezwe hapo, atakuwa ametusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleo kukushukuru kwa kutenga fedha mwaka huu kuanza ukarabati wa majengo ya kuanzisha Chuo cha Ufundi Stadi – Nkasi. Mambo haya yatasaidia sana vijana wetu wanaomaliza darasa la saba na wale ambao wanashindwa kuendelea baada ya kumaliza *form four*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeomba pia pesa na umetusaidia, nishukuru Shule ya Sekondari Milundikwa umetupatia zaidi ya shilingi milioni 190 na Shule ya Sekondari ya Nkundi tumepata zaidi ya shilingi milioni 130 na Shule ya Sekondari ya Nduchi tumepata shilingi milioni 91, zote hizi ni za kujenga miundombinu ya sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile shule za msingi tumeweza kupata pesa katika Shule za Msingi Kasu na Chala. Tunaomba waendeleo kutusaidia, naomba Shule za Sekondari za Sintali, Kala, Kipande, Kate na Ninde zina hali ngumu sana ya miundombinu ya majengo, madarasa pamoja na maabara. Tunaomba utakapopata nafasi uweze kutusaidia katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuone umuhimu pia wa kusaidia katika maeneo ya Shule za Sekondari za Sintali, Kala



na Wampembe. Wizara inahimiza ubora wa elimu lakini katika kuhimiza ubora wa walimu, yapo maeneo katika jimbo langu ya mwambao wa Ziwa Tanganyika miundombinu ya elimu ni mibaya kabisa. Jimbo hili lina tarafa zaidi ya tano lakini Tarafa ya Wampembe miundombinu yake ni migumu sana na ni kandokando ya Ziwa Tanganyika. Kuna vijiji vipatavyo 23, katika vijiji hivi walimu wana hali ngumu sana ya ukosefu wa nyumba, madarasa ya kutosha na usafiri katika eneo lile ni mgumu sana, inafanya hata wakati mwingine wa mitihani vijana kuhama shule moja hadi shule nyingine kwenda kufanya mitihani, kwa hiyo, mazingira kwa ujumla ni magumu sana. Kwa hiyo, walimu wa eneo hili wakati mwingine wanatakiwa kuangalia kwa namna ya pekee maslahi yao. Ni hao ambao wanafuata mishahara yao umbali mrefu sana na hawana namna nyingine ya kuweza kuwasaidia kimaisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna shule chache ambazo tumezianzisha kwa sababu ya wingi wa wanafunzi, Shule za Loleshia, Itanga, Lusembwa, Lupata na Mkiringa. Shule hizi tumezianzisha baada ya kutembelea pale kukuta vijana wengi hawana namna ya kusoma na fedha zilizoanzisha shule hizo ni nguvu za wananchi na Mfuko wa Jimbo peke yake, hatujapata pesa za kutosha. Tunaomba watengewe pesa ili shule hizi ziweze kupata kasi ya kutoa elimu kama shule zingine vinginevyo tutapata shida kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kuhusu walimu. Walimu wetu wa shule za msingi wana shida kubwa mno. Shida kubwa ambayo tunaiona hapa ni maslahi pamoja na upandishwaji wa vyeo vyao. Unakuta mwalimu anakaa katika cheo kimoja muda mrefu sana na wakati mwingine hawapati uhamisho wa hapa na pale ili kubadili mazingira na kufanya kazi vizuri zaidi na kwa kufanya hivyo unakuta kazi zinaanza kufanywa kwa mazoea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba mageuzi katika suala zima la taaluma yaanze pia kwa watendaji wenyewe hawa ambao wako shuleni. Kitengo cha Ukaguzi kiimarishwe hasa katika shule za msingi. Kitengo hiki

kimeachwa bila vitendea kazi vya kutosha, hawana magari wala watumishi wa kutosha na kwa maana hiyo shule zote ambazo tunataja hapa hazitembelewi na hivyo huwezi kuona matokeo mazuri katika mitihani kwa sababu shule hizi haziangaliwi mara kwa mara na walimu wake sasa wanafanya kazi kwa mazoea. Kwa hiyo, naomba sana kitengo hiki nacho kiboreshwe sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo napenda kuchangia ni vijana ambao wanasoma elimu maalum maana yake watu wenye ulemavu, albino na watu wengine. Vijana hawa wanapata changamoto nyingi sana katika shule mbalimbali ambazo wanasoma, nyingi hazina miundombinu ya kuwasaidia lakini wanapomaliza hakuna mfumo unaoeleweka wa kuwaajiri vijana hawa japo inatajwa kwenye sera kwamba asilimia kadhaa katika nafasi zinazotolewa wawe wanaajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kuwe na ufuatiliaji (*cross check*) kuona katika ajira kadhaa zilizokwishatolewa, je, watu wenye walemavu wamezingatiwa kwa kiwango gani? Kama itakuwa tu ni sera lakini waajiri hawazingatii inakuwa haina maana sana. Naomba kila nafasi za ajira zinapotolewa kiwepo kitengo cha kuhakikisha kwamba watu hawa na wenyewe wanatengewa nafasi zao na tunahakikisha kwamba wamepewa lakini siyo kuacha tu kama sera ilivyo, inakuwa haitusaidii sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, nishukuru kwa mchango mzuri ambao umetolewa na wenzangu hasa katika shule za *private* kwamba shule hizi zina msaada mkubwa sana na kama kuna haja ya kutoa namna yoyote ya usaidizi hasa katika maeneo ambayo wameona kwamba ni changamoto waweze kufanya hivyo kwa sababu ni washika dau kama wengine, wanatoa elimu kama watu wengine. Kwa hiyo, ni wadau muhimu katika utoaji wa elimu katika nchi, isionekane kama ni wafanyabiashara tu pekee yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naona kama ni watu ambao wanasaidia kubeba mzigo mkubwa huo wa utoaji elimu katika nchi na kwa hivyo ni wadau muhimu sana na hii ndiyo inaweza ikatusaidia kwenda kwa pamoja. Kwa sababu tunasema PPP ni muhimu sana katika maendeleo ya Taifa letu bila kuimarisha sekta binafsi tukaiachia Serikali peke yake sidhani kama tutaweza kufikisha malengo ya Kitaifa yanayotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Rose Tweve.

**MHE. ROSE C. TWEVE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kutoa mawazo yangu kwa Wizara muhimu sana, Wizara ya Elimu. Awali ya yote, naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Mheshimiwa Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara kwa mchango mkubwa ambao mnautoa kwenye Wizara yenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Taifa tumekuwa na matamano sasa ya muda kuhakikisha nchi yetu inafikia uchumi wa kati. Ni imani yangu na ya Watanzania wengi kuwa Wizara ya Elimu ni kiungo kikubwa ambacho kitatusaidia sisi kuweza kufikia malengo hayo ya uchumi wa kati na ambayo yataendeshwa kwa viwanda na biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema haya? Wizara ya Elimu ndiyo iliyopewa jukumu la kuandaa Sera ya Elimu nchini, mitaala ambayo ita-reflect pale ambapo sisi Watanzania tunataka kufikia na kuandaa walimu ambao tunategemea watakuwa na hizi *skills* na *knowledge* ambapo wata-transfer kwa hawa watoto wetu ambao tunategemea waje waweze kuendesha hivi viwanda ambavyo tayari vimeanzishwa kwenye mikoja yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha hoja yake kesho angetueleza Wizara ya Elimu, Sera ya Elimu hapa nchini ni nini? Je, sera na mitaala ambayo tumeiandaa inaweza kuwasaidia hawa vijana kutimiza malengo yao? *Let's say* watoto ambao wata-*graduate* miaka mitano ijayo anaweza akatumia hizi *skills* na utaalim ambao amepata shuleni kufanya kazi kwenye viwanda hivi? Je, huu ujuzi alloupata anaweza akatumia fursa zilizopo akaanzisha biashara, akajikita kwenye kilimo chenye tija, akawa mfugaji badala ya sasa ambao asilimia kubwa ya vijana wanategemea kuajiriwa Serikalini? Hilo ni jambo la msingi sana Mheshimiwa Waziri, napenda ulitolee maelekezo ya kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya pili, nilitaka tujue sasa kama Wizara tumejiandaa vipi kuhakikisha hawa walimu ambao nimesema ndiyo nguzo muhimu wameandaliwa kuhakikisha wana utaalim wa kutosha kuweza kuwafikisha hawa watoto hapo ambapo tunataka wafikie. *I stand to be corrected*, nakumbuka kwenye hotuba ya bejeti ya mwaka 2018/2019 ilionyesha kabisa tuna upungufu wa walimu hasa shule za msingi, nakumbuka idadi ilikuwa zaidi ya 85,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali kuwa mwaka huu tumeweza kuajiri hao walimu 4,500 lakini ni wachache, hawawezi kukidhi shida ambayo tunayo sasa hivi na walimu wapo. Nakumbuka Waziri wa TAMISEMI alivyotangaza ajira hizi, zaidi ya walimu 90,000 walituma *application* kupata nafasi hizi za kazi.

Kwa hiyo, tushirikiane na Wizara ya TAMISEMI tuhakikishe tunaajiri walimu wa kutosha. Hali ya walimu kwenye maeneo yetu hasa Mkoa wa Iringa bado ni changamoto kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili walimu wetu wawe na ufanisi wa kufundisha lazima *workload* yao iwe ndogo, uwiano kati ya walimu na wanafunzi lazima uwe mzuri. Nitatoa mfano, kwa walimu wa shule ya awali inakadiriwa mwalimu mmoja

kwa wanafunzi 189, *in average* tunatakiwa tuwe na mwalimu mmoja kwa watoto 25. Kwa hiyo, tumeanza kuajiri ni jambo jema lakini tusiishie hapo, tuna jukumu la kuhakikisha tunaajiri walimu wa kutosha ili wawe na uwezo wa kufundisha hawa watoto wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *workload* waliyokuwa nayo tumeona inavunja *morale*. Hata hawa ambao sasa hivi wanakwenda kufundisha, wakifika kule kwa *workload* iliyopo ni vigumu wao kufanya *followup*, kuhakikisha hawa watoto wame-*grasp* hizi *concept* ambazo wanawafundisha darasani. Kwa hiyo, tunajikuta tuna walimu nusu, nadhani watu wa Hakielimu walionesha *last year, less than 40%* walimu wako *motivated* kufundisha darasani. Sasa tutapaleka hao walimu wako pale lakini kumbe zaidi ya nusu hawana *morale* ya kufundisha watoto wetu. Kwa hiyo, tunatakiwa tufanye jitihada za makusudi kuhakikisha jambo hili tunaliweka vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali utakuwa kama ufuatavyo. Kama nilivyosema walimu ni kiungo kikubwa sana sasa tuhakikishe *in-service training* tukishirikiana na Wizara ya TAMISEMI tunawaendeleza hawa walimu wetu. Kama Wizara mmekuwa mnatoa miongozo mbalimbali, tunabadilisha mitaala, je, hawa walimu wako *trained* kuhakikisha wanaenda na hiyo miongozo na mitaala mipya ambayo mmeileta? Kwa hiyo, tuhakikishe *in-service training* inakuwepo kwa walimu wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile *issue* ya *IT (Information Technology)*, ni lazima kama nchi tuanze hii *conversation*, hatuwezi kukwepa. Wenzetu wa Rwanda sasa hivi wameshaanza, Kenya wameshaanza haya majadiliano, najua ni gharama na itakuwa ni kazi kubwa lakini lazima tuanze. Hivi viwanda tunavyoanzisha lazima tuwe na vijana ambao wako *multiskilled*. Tutaanzisha viwanda tutaishia kuchukua *expert's* kutoka nchi za nje kuja kufanya kazi kwenye viwanda vyetu. Inasikitisha mtoto anakuja kuona *desktop* au *tablet* anapofika labda chuo, lazima hawa watoto wawe *exposed* kwenye hizi sayansi na teknolojia mapema. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama nilivyosema, *issue* ni kubwa, *we have to start somewhere at least* tuwe na *conversation*. Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa kuhitimisha atueleze tuone inakuwaje. Uzuri sasa hivi tuna umeme mpaka vijijini, kwa hiyo, tuna *access* ya kuweka hata *computer* moja moja kwenye shule ili watoto wawe *exposed* kwenye hizi *new technology*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua Mheshimiwa Waziri ana uwezo (*competent*) wa kututoa hapa tulipo kwa kutengeneza sera na mitaala yetu mizuri ili tuweze kufika pale ambapo tunataka kufika kwenye uchumi wa kati. Tuhakikishe tunaajiri walimu wa kutosha, tuwawezeshe, tuna uwezo wa kufika huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nimitakie kheri Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara katika utekelezaji wa bajeti hii. Nashukuru sana na naunga mkono hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** *Good!* Ahsante kwa mchango wako mzuri. Tunaendelea na Mheshimiwa Silafi Jumbe Maufi, atafuatiwa na Mheshimiw Eng. Amandus Ngonyani.

**MHE. SILAFI J. MAUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kuzungumza machache katika Wizara hii ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kunipatia pumzi na afya ya kuweza kusimama tena katika mwaka huu wa 2019 niweze kuzungumza haya yafuatayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, natoa pongezi za dhati kwa mdogo wangu Mheshimiwa Prof. Ndalichako, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wote wa Wizara ya Elimu kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kujituma na kujitoa kwa maslahi ya kuhakikisha kwamba elimu bora kwa Watanzania inapatikana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuzungumza hayo lakini napenda kumuarifu Waziri wa Fedha, Wizara ya Elimu ni vyema ikaangaliwa kwa jicho la namna yake la kuhakikisha ya kwamba ukomo wa bajeti unaongezwa. Nasema hivyo kwa sababu ina miradi mingi na mizito ya kutekelezwa ili kuiweka elimu katika hali inayotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia suala zima la miradi ya maendeleo. Fedha ya miradi ya maendeleo ya mwaka 2018/2019 haikuweza kutoka yote na vilevile nina wasiwasi hata mwaka wa fedha 2019/2020 zinaweza kutoka na kukidhi mahitaji katika maendeleo ya Wizara yetu ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia suala la maboma. Kuna maboma kadhaa ndani ya mikoa yetu ya madarasa, shule za msingi na shule za sekondari hali kadhalika nyumba za walimu. Maboma haya yamejengwa kwa nguvu za wananchi lakini Serikali yangu haijaongeza mkono wake katika kuhakikisha kwamba maboma yote yanakamilika ili watoto wetu waweze kupata nafasi ya kujifunzia. Kwa hiyo, tunaomba Wizara hii iongezewe ukomo wa bajeti ili waweze kuweka bajeti yao katika mahitaji yanayohitajika ili maboma yetu yaweze kukamilika yote pamoja na jitihada waliyofikia ya kukamilisha maboma hayo kadhaa. Kwa hiyo, tunaomba fedha za maendeleo ziweze kutoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nnapenda kuzungumzia suala la madarasa lakini shule ni choo, bila kuwa na vyoo vya kutosha kwa maana ya matundu ya kutosha kwa watoto wetu watapata maradhi mengi ya kuambukiza. Kwa hiyo, tunawaomba Wizara hii iwe na mpango mkakati wa kuhakikisha kwamba vyoo vya shule vinaendana na idadi ya wanafunzi waliopo hasa ukizingatia kazi nzuri aliyoifanya Rais wa Jamhuri wa Tanzania Dkt. Magufuli kuhusu elimu bure, ni dhahiri kusema kwamba wanafunzi wameongezeka katika shule zetu lakini vyoo vimebakia vilevile. Sasa hivi vyoo vingi vimejaa, tukiwaambia Mabwana Afya wakazungukie shule bila shaka nyingi zitafungwa kwa sababu vyoo vyao haviko sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Mheshimiwa Waziri aone namna ya kuweka mkakati maalum wa ujenzi wa vyoo vya watoto shuleni. Pia tunaomba waweke choo maalum kwa watoto wetu wakubwa wa kike hasa katika shule za sekondari kwani zimekuwa na matatizo makubwa. Hali kadhalika vyoo vinavyojengwa ni maji, tunaomba utaratibu wa kuweka miundombinu ya maji katika shule zetu uweze kupewa kipaumbele ili vyoo vyetu hivyo vitakavyojengwa viwe katika hali ya usafi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia suala la idadi ya wanafunzi. Idadi ya wanafunzi imeongezeka ndani ya madarasa yetu na kufikia walimu kufanya kazi ya ziada. Kwa kweli mimi napongeza sana kazi kubwa wanayoifanya walimu wetu pamoja na hali ngumu wanayofundishia lakini bado watoto wetu wanafaulu, wanakwenda sekondari, *high school* na vnyo vikuu lakini kazi ya walimu ni ngumu.

Katika kipindi hiki cha miaka mitatu cha ongezeko la wanafunzi katika madarasa yetu na mwalimu kujikuta ana watoto zaidi ya 60 ndani ya darasa lakini bado anaifanya kazi ile. Hata hivyo, mishahara yao haijaongezeka na ni midogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, karibuni kila Mbunge aliyesimama hapa amezungumzia mishahara ya walimu, kweli wamefanya kazi nzuri ndani ya hii miaka mitatu, tunaomba tuangalie madaraja yao na tuhakikishe ya kwamba tunawaongezea mishahara yao ili kuwatia morali walimu hawa waweze kufanya kazi nzuri zaidi na kazi iliyotukuka, pamoja na kazi hiyo ya kutukuka wanaifanya hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuzungumzia suala zima la kuhakikisha ya kwamba tunaongeza ajira, tunashukuru kwa hizo nafasi elfu nne, lakini nafasi elfu nne katika mahitaji ya milioni 60, kwa kweli haijafanyika kazi yoyote. Tunaomba tuongeze nguvu ya kutoa ajira kwa walimu, walimu wapo, wako kwenye mitaa yetu, hata kana kwamba walimu wengine wanashindwa kwenye maeneo



hayo kutokana na mazingira, lakini bado mazingira yale tuliyokuwa nayo sisi kule hasa mikoa ya pembezoni, vijijini, wako walimu waliomaliza vyuo wako mitaani, nao hawajaweza kupata nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba basi, kama wengine hawawezi kuja kwenye mazingira yale ya pembezoni, kule vijijini, basi walewalioko kule naomba wapewe kipaumbele waweze kupata ajira ya ualimu, kwa sababu wanazoea mazingira yale na wamo ndani ya mazingira yale, waendeleo kuwafundisha wenzao nao waweze kupata elimu iliyokuwa bora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba ongezeko la ajira ya walimu, bado tuko nyumba, tunaomba mshirikiane na ndugu wa TAMISEMI, tuweze kupata ajira ya kutosha kwa walimu kwani tunawahitaji sana, hasa sisi mikoa ya pembezoni. Ninasema sisi mikoa ya pembezoni, hata shule za *private* kule ziko ni chache, ziko mbili tatu, kwa hiyo, bado tunahitaji walimu, kwa hiyo, tunaomba walimu waweze kupatiwa kipaumbele waweze kuongezewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, nilikuwa nazungumzia upande wa watoto walemavu, kuna watoto walemavu maalbino, ambao wenye ufinyu wa uono, lakini wanahitaji kusoma, kuna baadhi ya wanafunzi albino, wamechanganyikana na wanafunzi wa kawaida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanapokuwa wanasoma katika kuandika ama wanapokuwa kwenye mitihani, wakati wa kuandika, wao wanakwenda taratibu mno, wenzao wanakwenda harakaharaka, kwa sababu hatuna shule maalum katika mikoa yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunawaomba kwamba ile mitihani wao wawekwe peke yao watu wa albino, halafu wale walemavu wakae pekee yao na wale wengine wawe peke yao na pia waongezwe mudu wa kufanya mitihani yao na wao waweze kufanya vizuri kama wanavyofanya wenzao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine lililokuwa napenda kuzungumzia ni kuhusu katika mkoa wetu wa Rukwa, katika Mkoa wetu wa Rukwa, tuna bahati ya shule kama tatu zina walemavu, wa mtindio wa ubongo, maalbino, viziwi na vipofu. Shule ya Malangali, Shule ya Katandara B, na Mwenge B, lakini walimu tunakuwa nao ni wachache ambao ni walimu wa taaluma, tunaomba walimu wa taaluma wapatikane katika shule hizo za Mkoa wetu wa Rukwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hawa watoto wanahitaji kupewa chakula mashuleni kwao, lakini bahati mbaya, Serikali yangu imetoa bilioni 22, chakula cha shule hizi, ambazo kwamba ni watoto kwa mwaka mzima. Wao hali halisi kwa maana ya Katandara, kwa maana ya Shule ya Mwenge B, na kwa maana ya Malangali, ni takribani bilioni 72, ndiyo hali halisia ya kuweza kupatikana kwa chakula kwa wale watoto. Lakini wanapata bilioni 22 ambazo kwamba hazikidhi mahitaji, tunaomba waongezewe ili watoto wale waweze kupata chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusiana na shule za stadi, shule za stadi, ufundi stadi wa mashule, tunazo shule kadhaa katika Mkoa wetu wa Rukwa Katandara, Mwaze, Matai na kadhalika. Lakini shule hizi wanafunzi wale hawana vifaa vya vitendea kazi, yaani vya kufundishiwa na vya kufundishika, hawana vitendea kazi. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba wapewe vitendea kazi, wapewe vitu vya kwenda kufundishiwa pale, wale ambao kwamba hawawezi kwenda sekondari kuendelea na masomo... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja, asilimia mia kwa mia, naomba tuangaliwe Mkoa wa Rukwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, *Eng.* Amandus Ngonyani, atafuatiwa na Mheshimiwa Angelina Malembeka.

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa hii ya kuongea leo, pili nikushukuru wewe kwa kunipa hii fursa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii, inayoongozwa na Mheshimiwa Prof. Joyce Ndalichako, kwa kweli sina maneno ya kusema, na wana Namtumbo wote hawana maneno ya kusema, ni furaha tu kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa mara ya kwanza, Tanzania inajenga vituo vya *VETA* katika ngazi ya wilaya na wameanzia Namtumbo, nawashukuruni sana. Nashukuru sana Mheshimiwa Rais amekuja na kukipa heshima kubwa zaidi kile kituo cha *VETA* cha Namtumbo kwa kukifungua, nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri, hakikisha kwamba yale yaliyobaki madogo madogo tuyamalize, ili mafunzo yaanze kutolewa katika kile chuo. Kile chuo kimejengwa pembeni kidogo na maeneo wanayokaa watu, kwa hiyo, wanafunzi wanahitaji mabweni, lakini vilevile walimu wanahitaji nyumba. Niombe sana tusaidiane hayo nayo yakamilike ili wana Namtumbo na watanzania wote kwa ujumla waweze kuanza kukitumia kile chuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu, katika sera ya kila kata kuwa na Sekondari, lengo la Serikali ilikuwa kwamba kila Sekondari, iwe ni ya *day*, iwe ni ya kutwa, na kisera tuko sahihi kabisa. Lakini tunapokuja kwenye utekelezaji, kuna baadhi ya kata zinaunganisha vijiji ambavyo viko mbalimbali sana. Nikitolea mfano, Kata yangu ya Magazine, kijiji hadi kijiji ni kilomita zisizopungua 20 na viko vijiji vitatu. Siyo hiyo tu, kuna Kitongoji ambacho kipo kilomita 26 kutoka kwenye makao makuu ya kijiji, cha mwisho kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika mazingira haya, hatutarajii sekondari hiyo isikose mabweni. Tunakubaliana kwamba sekondari zote za kata ni za kutwa, sisi hatuna tatizo na hilo, tatizo tulilionalo ni kwa idara hii ya udhibiti elimu

kutuzuia kujenga mabweni, ni sisi wenyewe tunaamua kujenga mabweni, na tunayahudumia wenyewe kwa sababu tunataka watoto wetu wale waliokusudiwa kuitumia hiyo shule ya sekondari, waweze kupata masomo, isitokee ni kile kijiji kimoja tu ambacho sekondari imejengwa na vijiji vingine vikakosa hiyo fursa kwa sababu ya umbali, umbali ni mkubwa sana na haiwezekani wakasoma kwa kutwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe, ni kata nyingi ambazo katika wilaya yangu zina mazingira hayo na kata zote zenye mazingira hayo zimeamua kujenga mabweni, wenyewe, na wenyewe wanahudumia! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna walaka umetolewa, na hii idara ya kudhibiti elimu inayokataza mabweni hayo yasifanye kazi na yasiendeleo kujengwa. Niombe sana hilo liangaliwe. Shule hizo ziendeleo kuchukuliwa kama shule za kutwa, lakini sisi wenyewe tulioamua kuhudumia wanafunzi wetu wanaosoma katika shule hizo kwa kujenga mabweni na kujenga eneo la kulia chakula na shuguli zote zile tunahudumia wenyewe, turuhusiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani siyo sahihi kutuzuia kwa sababu ukituzuia, maana yake unatuzuia fursa ya kutumia hizo shule za kutwa kupata elimu kwa watoto wetu. Niombe sana hilo liangaliwe kwa makini sana. Lakini ni utekelezaji mzuri sana wa hiyo sera kwa sasa kwa kweli ni kwa mara ya kwanza sisi Namtumbo napo tunapata wanafunzi wengi wanaomaliza kidato cha nne na wengine sasa wanaingia kidato cha tano kwa sababu kiwango kile cha ufaulu kimeanza kuongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niombe, kama ambavyo wengine wamesema, naomba hasa walimu wa sayansi, tunaomba sana muendeleo kutusaidia. Najua mnaendelea kuajiri, lakini kasi ya kuajiri ni ndogo sana, hata kama tatizo ni ukubwa wa bajeti ya mishahara ya Serikali kwa ujumla, naomba sana Serikali itoe kipaumbele kwa masuala ya elimu pamoja na afya kwa maana ya zahanati na vituo vya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hizi sekondari pamoja na shule za msingi, tutoe kipaumbele, tusijali sana ukubwa wa bajeti ya mishahara katika kuzuia kuajiri. Nikuombe sana Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) utusaidie kwenye hilo. Tunaomba walimu ili tuweze kupata ile elimu iliyokusudiwa kupitia hizi shule za sekondari za kata lakini vilevile shule za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vyuo vya walimu, hapa nilitaka tu kusema, kule kwetu Namtumbo, kilianzishwa chuo cha Walimu, kipo katika Kijiji cha Nahoro, kinamilikiwa na Chama Kikuu cha Ushirika cha Songea na Namtumbo, (SONAM). Chuo hiki kilianzishwa ili kujaribu kutatua changamoto za watoto wetu wengi wanaomaliza kidato cha nne lakini hawapati fursa ya kwenda kwenye vyuo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kilipoanza, kimedahili mara mbili kwa kutumia kile kibali cha muda, *(provisional registration)*. Sasa baada ya miaka miwili, mmetuziua tusiendeleo kudahili, ni sawa, ni suala la udhibiti, lakini kinachoshangaza ni kwamba, katika miaka ile miwili ya udahili, kile chuo kilikuwa ni kati ya vyuo bora Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ile miaka miwili, mitihani waliyofanya miaka ile miwili, hicho chuo kilikuwa bora kabisa na kikaanza kuvuta wanafunzi wengi kutoka maeneo, nje ya Namtumbo, nje ya Mkoa wa Ruvuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hatuelewi, kimezuiwa kweli ni kwa sababu hakijakidhi viwango kwa maana hawana jengo la kompyuta na mengine, au pengine ni kuzuia tu watu wasiende Namtumbo au na watu wa Namtumbo wasipate fursa ya kudahiliwa katika chuo hicho! Maana yake inawezekana tatizo tunaofanya kazi kwenye idara mbalimbali, unaweza ukafanya kitu sahihi kabisa, lakini *motive* yako ikawa tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwangu kwa mfano, nilifikiria, badala ya kukizuia, mngeweza kukisaidia kimalize zile changamoto kilizonazo ili wanafunzi waendeleo

kudahiliwa. Kwa sababu, tatizo halikuwepo katika ubora wa elimu inayotolewa, ubora wa elimu unaotolewa katika kile chuo ni *the best* na ndiyo maana katika ile miaka miwili kilikuwa kati vya vyuo bora Tanzania, kwa hiyo, hakukuwa na tatizo la ubora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kukizuia, inawezekana kweli ni kwa sababu ya hizo sababu ambazo Idara ya Udhhibiti wa Ubora wa Elimu imezitoa kwa kuzuia lakini sisi kule tunaona kama ni kutunyima fursa ya kukitumia kile chuo. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri, changamoto hizo, kama ni kweli ndiyo, *is it core or subsidiary*. Mimi nadhani, kama siyo *core reasons*, kile chuo kiendeleo kudahili, kwa sababu kinatoa mafunzo mazuri na kwa kweli, kinatoa walimu *the best* kati ya *the best* vyuo katika Tanzania. Nikuombe sana uliangalie hilo kwa makini na utusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli, nichukue fursa hii kuipongeza tena Wizara kwa kukiorodhesha Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Mputa, kati ya vyuo vitakavyofanyiwa ukarabati katika Awamu ya II, nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri, Umeendelea kutembea katika kivuli cha Mheshimiwa Rais, cha kuiona Namtumbo ambayo iko nyuma sana, ni kati ya wilaya ambazo ziko nyuma sana katika wilaya zile ambazo ziko Tanzania nyuma sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, na wewe unaanza kutembea katika kivuli cha Mheshimiwa Rais, cha kutuona sisi wana Namtumbo na kutusaidia. Nimefurahi sana na wana Namtumbo watafurahi sana kusikia chuo chao cha Mputa cha Maendeleo ya Jamii kinakwenda kukarabaitiwa... (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimwa.

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI:** Kimekuwa kikiishi kama chuo yatima...

**MBUNGE FULANI:** Muda umeisha, unga mkono hoja.

**MHE. EDWIN A. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia 100 na kwa kweli nashukuru sana, kama nilivyosema hatuna maneno juu ya Wizara hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Angelina Malembeka!

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia katika Wizara hii. Niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa Wizara hii pamoja na Taasisi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shukurani hizo, nitoe pia shukurani za pekee kwa Mheshimiwa Rais kwa kutimiza azma yake ya elimu bure kwa shule za awali mpaka sekondari, tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu imeweza kuwekeza katika elimu maalum katika shule nyingi katika nchi hii, karibu Mikoa yote ina vyuo vya kutolea elimu maalum, isipokuwa Mikoa mitatu ambayo ni Simiyu, Geita na Songwe, nafikiri kwa sababu ni mikoa mipya ni vizuri Mheshimiwa Waziri atakapokuja atuambie ni lini shule hizo zitafunguliwa katika mikoa hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shule hizo, nilitaka nichangie kuhusiana na mashine au vifaa vinavyotumiwa na walemavu. Tumekuwa tunazungumzia suala la masomo yao, vitendea kazi vyao lakini hatujazungumza kwa kina vifaa vyao wanavyotendea kazi au vinavyowasaidia. Mpaka sasa hivi, tuna mafundi 65 tu ambao wanashughulika na mashine za walemavu, kati ya hao sita tu ni wanawake na 59 ni wanaume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na idadi hiyo, fundi mtalaam mshauri, tunaye mmoja tu, ambaye yeye anafanya kazi Afrika Mashariki, Afrika ya Kati na Kusini mwa Afrika, ndugu Malim Kali, ambaye yuko pale Wizara ya Elimu, na msaidizi wake kidogo aliyekuwa anakuja kwa mbali,

niseme kwamba Mwenyezi Mungu amuweke mahali pema, alifariki mwezi wa tatu mwaka huu!

**WABUNGE FULAN:** Ooooh!

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hapo, mafundi waliokuwepo, wana mafuzo tu ya awali na wengine wamepata vyeti, hatuna walimu tena, au mafundi wa kutengeneza zile mashine. Sasa Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa, nataka aje aniambie, wana mpango gani angalu wa kutengeneza *program* maalum kwa ajili ya mafundi wa kutengeneza mashine za walemavu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, yule fundi aliyekuwa mtaalam mkuu, aliyekuwa anatengeneza mashine za viziwi, naye amestaafu, bwana Robert Lugeiyamu, amestaafu mwezi Machi, mwaka huu, ni vizuri basi Waziri atakapokuja atuambie katika walataam hao wa kutengeneza mashine hao wamejipanga vipi ili walemavu waendeleo kupata huduma zao pale vifaa vyao vinapoharibika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta hii ya elimu maalum, wamekuwa na ushirikiano mzuri sana baina ya Tanzania Bara na Visiwani, wamekuwa wakifanya kazi kwa pamojo na kwa ushirikiano mkubwa. Ni mara nyingi utakuta mafundi kutoka bara wanakweda Zanzibar na wengine wa Zanzibar wanakuja Dar es Salaam au Mikoa mingine ya huku kuja kujifunza au kufanya kazi. Sasa nilitaka kujua, ni lini mafundi hao watapata mafunzo, nchi nzima, bila kujali huyu Mzanzibar, au huyu Mbara ili waweze kuwatumikia walemavu katika nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna hizo shule kwa Pemba, tunazo tatu, Michakaweni, Mchangamdogo na Chakechake. Kwa Unguja, kuna Moga, Umoja, Uzini, Jambiani, Suza, *Haile Selassie*, CCK na Kisiwa Nduwi. (*Makofi*)



Mheshimiwa Mwenyekiti, Dar es Salaam, tunazo tatu, Uhuru Mchanganyiko, Msasani na Kibasila. Pwani ziko mbili, Lugoba Sekondari na Mwambao *Primary*, ambayo iko Bagamoyo. Tunayo Morogoro, Kilosa Sekondari na Mazimbu *Primary*, kwa Dodoma ziko nyingi kidogo, *Mpwapwa TC*, Mpwapwa Sekondari, Mvumi DCT, tuna Homboro *Primary* na Buigiri *Primary* Maalum. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanga tunazo, Lushoto Maalum, Kongwe na *Korogwe Grills*, kwa Kilimanjaro tunayo Same, tunayo Mweni, tunayo *Moshi Technical* na *Saint Francis*, lakini tunapokuja Arusha bado tunayo Temi, *Patandi TC*, Patandi Mazoezi, Lungido *Primary* na Longido Sekondari. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Manyara tuna moja, Kateshi *Primary*, lakini bado Mwanza, tuna Misungwi, Ukerewe, Kagera iko moja, Mugeza, ambayo iko Bukoba, lakini pamoja na hayo, Kigoma, wanayo Kabanga *TC* na Kabanga *Primary*. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haijajinyima, tukaenda Tabora tukakuta *Furaha Primary*, Shinyanga iko buhangija na *Shy-Bush*, ambako kuna Shinyanga Sekondari, Singida kuna Ikungi, kuna Singida Sekondari na kuna *Kizega Primary*. Kwa Iringa ipo Lugalo, ipo Makalale na Njombe kuna *Mundindi Primary*, hizo zote kwa ajili ya elimu maalumu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbeya tunayo *Katumba Two*, Katavi tunayo *Azimio Primary*, Rukwa tunayo *Malangale Primary*, Kantaramba pia, lakini Ruvuma tunayo *Ruhilo Primary*, *Ruhilo Sekondari*, *Songea Boys* na *Songea Girls*. Kwa Lindi tunayop *Nyangao Primary*, lakini pia na *Masasi Primary* na Ndanda ikafutwa! Waziri anapokuja atuambie, kwa nini Ndanda waliifuta. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo nimeeleza mwanzo, Simiyu hakuna, Geita hakuna, Songwe hakuna, Je, wale walemavu wa kule tunawapeleka wapi kusoma, ni vizuri

basi Serikali ijipange na ituambie lini itapeleka shule maalum katika maeneo hayo. (Makofi)

Pia nizingumzie kiwanda cha uchapaji kilichopo chini ya Wizara ya Elimu na Taasisi zake (*Press A na Press B*). *Press A* niwapongeze sana, wamefanya kazi nzuri katika mazingira magumo, vitabu hivi haa Wizara ya Elimu, Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Habari na Utamaduni vyote wamechapa wao. Mashine za kizamani, kazi ya kumaliza siku moja siku nyingine wanafanya siku mbili au tatu, siku nyingine wanalala huko huko, basi Waziri akija atuambie mashine zile wana mpango nazo gani, sambamba na mashine za uchapaji za *Press B* kwa ajili ya wasioona. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, nizingumzie kidgo khusiana na suala lauwekaji wa viwango kwa walimu, viwango vya ushindishaji. Nafikiria labda viwango hivi wanaviangalia kwa watanzania, kuna baadhi ya shule za binafsi, walimu hao wapo wanaojiita walimu, lakini hawana sifa za ualimu, wanafikiria kuongea kingereza ndiyo sifa ya kuwa mwalimu. Tumefika baadhi ya shule tumeenda, tunakuta mtu, tena wanatoka nchi jirani, mwingine hana kibali cha kukaa nchini, mwingine hana kibali cha kufanyia kazi, hana sifa yoyote ya ualimu, lakini amepewa hiyo kazi, ninaomba mpite kwenye hizo shule mkakague. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wakati huohuo nitoe pongezi zangu za dhati kwa wamiliki na wenye shule wote wa *private*, ambao wamekuwa watiifu na wanafanya kazi vizuri, kuisaidia Serikali kuboresha elimu katika nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo mengi mazuri yamefanywa katika Wizara hii ya Elimu, lakini kuna madogomadogo ambayo yameguswa inabidi yafanyiwe kazi na kuwekwa sawa. Katika mambo hayo, kuna masuala ya rushwa ya ngono katika vyuo na vyuo vikuu yametajwa, kuna masuala ya wizi wa mitihani, kuna masuala ya upendeleo katika usajili wa vyuo uliophelekea kusajili vyuo ambavyo havina sifa na hatimaye kuwapa wanachuo shida

ya kuacha shule mapema au kuondolewa, halafu chuo kinafungwa, wanapata tabu, ni vizuri watuambie, wamejipanga vipi kudhibiti hali hiyo ya rushwa kwenye vyuo, upendeleo kwenye usajili na wizi wa mitihani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kabla sijamaliza, bado kuna suala lingine la kuzungumzia kuhusiana na elimu kwa redio...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante sana.

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja asilimia mia kwa mia, na mwisho nasema siasa kwenye chama zinaendelea kwa sababu tunaanza chini tunakwenda juu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge, huyo ndiye alikuwa mchangiaji wetu wa mwisho kwa siku ya leo, mliona nilikataa kuchukua maombi ya taarifa kwa sababu nilitaka nitende haki kwa orodha ya makundi yote ambayo iko mbele hapa. Tumeimaliza yote na ndani ya muda wetu. Kwa hiyo, niwashukuruni sana Waheshimiwa Wabunge mliopata fursa ya kuchangia hoja hii kwa maoni yenu, ushauri wenu kwa Serikali kupitia Wizara hii muhimu.

Sina la ziada, mkataba wangu na ninyi kwa siku ya leo unaishia hapa, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho siku ya Jumanne Tarehe 30, Aprili, 2019, saa tatu asubuhi.

*(Saa 1. 45 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne Tarehe 30 Aprili, 2019 Saa Tatu Asubuhi)*